# UHUSIANO WA SILIKA NA UTENDAJI WA WAHUSIKA WA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI: UCHUNGUZI KIFANI WA *NGOMA YA MIANZI* NA *SAFARI YA PROSPA*

**SAUMU SAIDI MKOMWA**

**SHAHADA YA UZAMIVU**

**CHUO KIKUU CHA DODOMA**

**SEPTEMBA, 2023**

# UHUSIANO WA SILIKA NA UTENDAJI WA WAHUSIKA WA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI: UCHUNGUZI KIFANI WA *NGOMA YA MIANZI NA SAFARI YA PROSPA*

NA

SAUMU SAIDI MKOMWA

TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMIVU

CHUO KIKUU CHA DODOMA

SEPTEMBA, 2023

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, **Saumu Saidi Mkomwa**, natamka kwamba tasinifu hii inatokana na mawazo yangu halisi; na kwamba, haijawahi kuwasilishwa sehemu yoyote ile kwa ajili ya kutunukiwa Shahada yoyote ile, au kama mradi wa utafiti.

Saini…………………………………

Hairuhusiwi kunakili, kufasiri, kupiga chapa, wala kuiga sehemu yoyote ya tasinifu hii, kwa namna yoyote ile, pasipo ridhaa ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Dodoma.

## ITHIBATI

Waliosaini hapa chini wanathibitisha kwamba wameisoma tasinifu hii inayoitwa '**UHUSIANO WA SILIKA NA UTENDAJI WA WAHUSIKA WA FASIHI YA WATOTO YA KISWAHILI: UCHUNGUZI KIFANI WA *NGOMA YA MIANZI* NA *SAFARI YA PROSPA***', na kuthibitisha kwamba ni kazi halisi ya Saumu Saidi Mkomwa. Hivyo, wanapendekeza ikubaliwe kwa minajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Saini:………………………… Tarehe: 06 Septemba 2023

Dkt. Athumani Salum Ponera

Msimamizi

Saini…………………………… Tarehe 06 Septemba 2023

Dkt. Zuhura Abdallah Badru

Msimamizi

## SHUKURANI

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, muumba wa mbingu na ardhi, kwa kunipa afya njema na kunilinda kipindi chote cha kuiandaa tasinifu hii. Pia, shukurani za pekee ni kwa Mtume Muhammad (rehema na amani zimfikie) kwa kupokea kitabu kitakatifu (Quran) kinachotuongoza katika matendo yote hapa duniani na kutuandaa kwa ajili ya akhera.

Ninawashukuru wazazi wangu, Mzee Iss’haka Saidi Mkomwa (Allah amrehemu) na Bi. Amina Ally Kimweri kwa kunizaa, kunilea, kunisomesha, na kunipatia mahitaji yote muhimu yaliyoniwezesha kusoma kuanzia elimu ya msingi hadi nilipoweza kujitegemea.

Shukurani nyingine za dhati ni kwa mume wangu kipenzi, Bwana Abbas Juma Kambi, na watoto wangu wapendwa Said na Fatuma, kwa kunivumilia kipindi chote nilichokuwa nafanya kazi hii. Hawa walikuwa washauri wangu wa karibu, na mara zote walinipa nguvu pale nilipoelekea kulegalega.

Ninawashukuru wasimamizi wa utafiti huu, Dkt. Athumani Salum Ponera na Dkt. Zuhura Abdallah Badru, kwa kunishauri, kuniongoza, na kunisukuma pale nilipoonekana kuchelewa au kuwa nyuma ya wakati. Hawakusita kunipa ushirikiano kila nilipohitaji msaada wao, na walikuwa wepesi kunisaidia na kunikumbusha wajibu wangu.

Pia, ninaushukuru uongozi wa Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo, chini ya mtendaji mkuu, Dkt. Herbet Makoye, pamoja na Mkuu wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini, Profesa Hosen Mayaya, kwa kunipa ruhusa kufuatilia kazi yangu kila ilipobidi. Kwa hakika, walinifaa mno. Kwa upekee, ninawashukuru Dkt. Getruda Shima na Dkt. Aginiwe Sanga kwa kusoma na kuhariri kazi hii na kuonekana kama ilivyo. Ushauri wao ulijenga na kuimarisha maudhui ya kazi hii. Mungu awabariki sana. Shukurani nyingine ni kwa uongozi wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kwa kuniruhusu kutumia makavazi ya Taasisi hiyo kwa ajili ya kutafuta marejeleo katika kipindi chote nilichokuwa Chuoni hapo kwa ajili ya kukusanya data.

Shukurani za mwisho ni kwa watafitiwa, hususani waandishi wa riwaya teule, wataalamu wa Fasihi ya watoto, wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dodoma, pamoja na mwalimu wa Shule ya Msingi Mbezi. Hawakusita kurekebisha ratiba zao za siku ili kunisaidia kupata data nilizozihitaji.

# TABARUKU

Tasinifu hii ni tabaruku kwa wanangu: Said na Fatuma, ambao walinivumilia kipindi nilichokuwa masomoni. Walikosa mapenzi ya mama na kulelewa na walezi wasio mama. Ninawapenda sana wanangu. Mwenyezi Mungu awakuze katika kumjua Yeye na awajaalie wafikie elimu ya juu zaidi, Amiin.

# IKISIRI

Tasinifu hii ni zao la utafiti uliofanyika kuhusu uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Utafiti uliofanyika uliongozwa na malengo mahususi matatu: Kufafanua namna mbalimbali za utendaji wa wahusika wakuu wa riwaya teule za Fasihi ya watoto, kuchambua aina za silika za wahusika wakuu wa riwaya teule za Fasihi ya watoto, na kutathimini athari za uhusiano baina ya utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto na sifa za silika zao. Ili kufikia malengo hayo, uchunguzi kifani wa riwaya za *Ngoma ya Mianzi* na *Safari ya Prospa* ulizingatiwa. Utafiti ulifanyika katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam. Tasinifu hii imetumia mkabala wa kitaamuli kwa sababu utafiti ulijikita zaidi katika kuchunguza tabia, hisia, na uzoefu wa wahusika. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu za usaili, usomaji matini, na majadiliano ya vikundi lengwa. Nadharia ya Saikochanganuzi ilisaidia kufikia malengo haya. Nadharia hii imebainisha nafsi na misingi mbalimbali ambayo ilitusaidia katika mchakato mzima wa utafiti uliofanyika. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa wahusika hutenda mambo mbalimbali ili kushauri, kutoa taarifa, kuonya, kudanganya, kushawishi, na kudadisi. Pia, kila mhusika ana silika yake ambayo humtofautisha na mhusika mwingine. Prospa amebainika kuwa na silika ya melankoli na Sara ana silika ya sangwini. Kwa upande mwingine, Mbumi amebainika kuwa na silika ya koleriki na Chulu ana silika ya melankoli. Silika za wahusika zimewasaidia kufikia malengo yao, kwa sababu zimeepusha msuguano kati yao. Vilevile, utafiti ulibaini kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya utendaji na sifa za aina za silika, kwani, ili kutambua silika ya mhusika, ni lazima kuona matendo yake. Pia, silika ndiyo inayomsukuma mhusika kutenda kila akitendacho. Hivyo, tasinifu hii ina umuhimu mkubwa katika uga wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili kwa kuwa inaleta chachu kwa watunzi na watafiti kutunga kazi zao kwa kuzingatia aina za silika na kuangalia uhusiano uliopo baina ya Fasihi na saikolojia. Mwisho, tasinifu inatoa mapendekezo kwa serikali, watunzi wa kazi za Fasihi na watafiti. Inapendekeza kuwa serikali ihakikishe inasisitiza usomaji wa vitabu vya ziada ili kukuza usomaji wa kifasihi na kuwawezesha wanafunzi kutambua silika zao kupitia wahusika watakaowasoma. Waandishi, wahakiki, na wataalamu wa Fasihi wafanye ufaraguzi wa kazi hizi ili ziweze kuigizika jukwaani. Hii ni kwa sababu, mambo yote yanayohitajika kwa ajili ya kuigiza yapo katika kazi hizi, kama vile maleba, mandhari, wahusika, na uhusika wao. Kwa hiyo, kupitia uigizaji, watazamaji, hususani watoto watatambua silika zao na za watu wengine wanaowazunguka. Hali hii itasaidia kupunguza migongano na migogoro kwa watoto na jamii kwa jumla.

## YALIYOMO

IKIRARI NA HAKIMILIKI ........ i
ITHIBATI ........ ii
SHUKURANI ........ iii
TABARUKU ........ iv
IKISIRI ........ v
YALIYOMO ........ vi
ORODHA YA MAJEDWALI ........ x
ORODHA YA VIAMBATISHO ........ xi
UFUNGUO WA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ........ xii

**SURA YA KWANZA ........ 1**
**UTANGULIZI WA JUMLA ........ 1**
1.1 Utangulizi ........ 1
1.1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu ........ 1
1.1.1.1 Utendaji ........ 1
1.1.1.2 Silika ........ 1
1.1.1.3 Wahusika ........ 2
1.1.1.4 Mtoto ........ 3
1.1.1.5 Fasihi ya Watoto ........ 4
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 5
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ........ 9
1.4 Malengo ya Utafiti ........ 10
1.4.1 Lengo la Jumla ........ 10
1.4.2 Malengo Mahususi ........ 10
1.5 Maswali ya Utafiti ........ 11
1.6 Manufaa ya Utafiti ........ 11
1.7 Mawanda ya Utafiti ........ 11
1.8 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ........ 12

**SURA YA PILI ........ 13**
**MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA YA UTAFITI ... 13**
2.1 Utangulizi ........ 13

2.2 Mapitio ya Maandiko ... 13
2.2.1 Maandiko Kuhusu Utendaji katika Kazi za Fasihi ... 13
2.2.2 Maandiko Kuhusu Silika ... 14
2.2.3 Maandiko Kuhusu Wahusika katika Kazi za Fasihi ... 17
2.2.4 Maandiko Kuhusu Fasihi ya Watoto ... 18
2.2.5 Mapengo Yaliyotakiwa Kuzibwa na Utafiti ... 20
2.3 Kiunzi cha Nadharia ... 21
2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili ... 23

**SURA YA TATU ... 24**
**METHODOLOJIA YA UTAFITI ... 24**
3.1 Utangulizi ... 24
3.2 Usanifu wa Utafiti ... 24
3.3 Mkabala wa Utafiti ... 24
3.4 Eneo la Utafiti ... 25
3.5 Walengwa wa Utafiti ... 25
3.5.1 Wango Tafitiwa ... 26
3.5.2 Mbinu ya Usampulishaji ... 26
3.5.3 Sampuli Iliyotumika ... 27
3.6 Ukusanyaji wa Data ... 28
3.6.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data ... 28
3.6.1.1 Njia ya Usaili ... 28
3.6.1.2 Njia ya Usomaji Matini ... 29
3.6.1.3 Njia ya Majadiliano ya Vikundi Lengwa ... 29
3.6.2 Mchakato wa Kukusanya Data ... 30
3.7 Uchanganuzi wa Data ... 31
3.8 Maadili katika Utafiti ... 31
3.9 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti ... 31
3.10 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake ... 32
3.11 Muhtasari wa Sura ya Tatu ... 33

**SURA YA NNE ..................................................................................................... 34**

**UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI ................... 34**

4.1 Utangulizi ................................................................................................. 34

4.1.1 Muhtasari wa Riwaya Teule ................................................................... 34

4.1.1.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* ............................................ 34

4.1.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Safari ya Prospa* ............................................. 37

4.2 Utendaji wa Wahusika Wakuu wa Fasihi ya Watoto katika Riwaya Teule......... 40

4.2.1 Utendaji wa Kuhoji .................................................................................. 41

4.2.2 Utendaji wa Kushawishi .......................................................................... 49

4.2.3 Utendaji wa Kuonya ................................................................................. 53

4.2.4 Utendaji wa Kudadisi ............................................................................... 59

4.2.5 Utendaji wa Kudanganya ......................................................................... 63

4.2.6 Utendaji wa Kutaarifu .............................................................................. 65

4.2.7 Utendaji wa Kushauri ............................................................................... 73

4.2.8 Hitimisho ................................................................................................. 79

4.3 Ufafanuzi Kuhusu Aina za Silika kwa Jumla ............................................... 79

4.3.1 Makundi ya Silika .................................................................................... 80

4.3.1.1 Melankoli .............................................................................................. 81

4.3.1.2 Flegmatiki ............................................................................................. 82

4.3.1.3 Sangwini ............................................................................................... 82

4.3.1.4 Koleriki ................................................................................................. 84

4.3.2 Aina za Silika za Wahusika Wakuu katika Riwaya Teule ............................. 86

4.3.2.1 Silika ya Prospa ..................................................................................... 87

4.3.2.2 Silika ya Sara ......................................................................................... 98

4.3.2.3 Silika ya Mbumi .................................................................................... 109

4.3.2.4 Silika ya Chulu ..................................................................................... 122

4.3.3 Hitimisho ................................................................................................ 128

4.4 Uhusiano Baina ya Utendaji wa Wahusika Wakuu na Sifa za Aina za Silika ... 128

4.4.1 Uhusiano Baina ya Utendaji na Sifa za Aina za Silika katika *Safari ya Prospa* ................................................................................................ 128

4.4.2 Uhusiano Baina ya Utendaji na Sifa za Aina za Silika katika *Ngoma ya Mianzi* ................................................................................................ 142

4.4.3 Hitimisho ................................................................................................ 154

4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne ........................................................................ 154

**SURA YA TANO ...................................................................................... 156**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO........................................ 156**

5.1 Utangulizi.......................................................................................................... 156

5.2 Muhtasari wa Tasinifu........................................................................................ 156

5.3 Hitimisho.......................................................................................................... 158

5.3.1 Mchango Mpya wa Tasinifu ............................................................................ 158

5.3.2 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika ............................................................. 159

5.3.3 Maoni Kutokana na Utafiti Uliofanyika ......................................................... 160

5.4 Mapendekezo ................................................................................................... 160

5.4.1 Mapendekezo kwa Waandishi, Wahakiki, na Wataalamu wa Fasihi.............. 160

5.4.2 Mapendekezo kwa Watafiti ............................................................................ 161

5.4.3 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu.............................................................. 161

**MAREJELEO ............................................................................................ 163**

**VIAMBATISHO ........................................................................................ 171**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na 1: Mgawanyo wa Silika na Majira ya Mwaka.......................................... 80

Jedwali Na 2: Muhtasari wa Aina za Silika na Sifa zake........................................... 85

## ORODHA YA VIAMBATISHO

Kiambatisho Na 1: Zana za Ukusanyaji wa Data ..................................................... 171
Kiambatisho Na 2: Taarifa za Watafitiwa ............................................................... 175
Kiambatisho Na 3: Vibali vya Utafiti ..................................................................... 177

## UFUNGUO WA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

| | |
|---|---|
| AD | *Anno Domini* (Miaka ya mazazi ya Masihi) |
| BAKILIT | *Bachelor of Arts in Kiswahili Literature* |
| BED ECE | *Bachelor of Education in Early Childhood Education* |
| *CODE* | *Canadian Organization for Development Though Education* |
| Dkt | Daktari wa Falsafa |
| Ht | Hakuna tarehe |
| Htpp | *Hyper text transfer protocal* |
| IFAMU | Idara ya Fasihi Mawasiliano na Uchapishaji |
| Juz. | Juzuu |
| Ke | Mwanamke |
| Khj | Kama hapo juu |
| Ltd | *Limited* |
| Me | Mwanaume |
| Na. | Namba |
| Rev. | *Revised* |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TPC | Tanganyika Planting Company |
| TPH | Tanganyika *Publishing House* |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| USA | *United States of America* |
| Vol. | *Volume* |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii inafafanua istilahi muhimu, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti, pamoja na mawanda ya utafiti.

### 1.1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu

Sehemu hii inafafanua istilahi muhimu zilizotumika katika tasinifu hii. Istilahi hizi zimefafanuliwa kwa sababu uga wa insia na sayansi za jamii hupokea fafanuzi mbalimbali kwa dhana ileile moja. Hivyo, istilahi hizi mahali pengine zinaweza zikawa na maana ya mbali na ilivyo katika tasinifu hii. Istilahi hizo ni utendaji, silika, wahusika, mtoto, na Fasihi ya watoto.

#### 1.1.1.1 Utendaji

Utendaji ni ufanyaji wa jambo. Hii inajumuisha namna linavyofanyika, mahali linapofanyika, na nani anayelifanya. Kifasihi, utendaji ni mchakato wa uwasilishaji wa tukio linalohusu maisha ya binadamu kwenye jukwaa au mahali popote pa kuigizia mbele ya hadhira. Unajumuisha kile ambacho wahusika wanasema, wanatenda, wanafikiria, na, wakati mwingine, hata kile wanachoshindwa kukifanya (O'Quinn, 1981; Mlaga, 2017; Munyioki, 2018). Mlaga (khj) anafafanua kuwa sanaa tendaji imeegemezwa zaidi katika vitendo. Kwa hiyo, ufundi katika aina hii ya sanaa nje ya uwasilishaji wake wa kimaneno unapatikana katika vitendo vinavyojitokeza. Ufafanuzi wa Mlaga ni wa muhimu katika kufafanua utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili katika riwaya teule. Kwa maana hiyo, utafiti uliofanyika unafafanua utendaji kuwa ni uwasilishaji wa tukio kwa lugha ya mazungumzo baina ya wahusika na masimulizi ya kiutendaji yanayokwenda sambamba na mazungumzo hayo.

#### 1.1.1.2 Silika

Wanasaikolojia wanabainisha kuwa silika ni sifa za mtu binafsi ambazo zina msingi wa kibiolojia na, kwamba, huamua maoni ya kibinafsi, makini na utendaji katika hali mbalimbali. Silika huchipua kabla ya masuala ya utambuzi kwa mtoto mchanga (Mills, 2005; Rothbart na Bates, 2007; Shiner, 2012; Spinelli, 2018). Kwa hiyo,

silika ni hali ambayo mtu huzaliwa nayo, lakini huimarika au kufubazwa kutokana na makuzi yake. Kwa mfano, elimu ya baba na mama inaweza kuimarisha silika ya mtoto wao, wakati mazingira yanayomzunguka mtoto nyumbani na shuleni yanaweza kufubaza silika yake. Pamoja na athari zote hasi na chanya, ukweli unabaki kuwa silika haiwezi kubadilika. Flaskerud (2012) anafafanua kuwa kila binadamu ana kiasi fulani cha aina nne za silika (melankoli, flegmatiki, koleriki na sangwini), ijapokuwa mojawapo huweza kujitokeza kwa kiasi kikubwa kuliko nyingine. Kwa maana hiyo, hakuna mtu aliye na aina moja pekee ya silika, bali wengi wanayo moja yenye nguvu kuliko nyingine. Kila aina ina udhaifu na ubora wake, na hakuna silika iliyo bora kuliko nyingine. Silika zote zinahitajika ili dunia iwe mahali pazuri pa kuishi. Kwa hiyo, kila mtu ni wa kipekee, hakuna watu wawili wanaofanana kwa kila kitu. Hata hivyo, katika utafiti uliofanyika, dhana ya silika imetumika kwa muktadha wa kifasihi kurejelea tabia, sifa au haiba za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto ambazo huwatofautisha wahusika hao.

#### 1.1.1.3 Wahusika

Wahusika ni watendaji wakuu wa kazi ya Fasihi. Wanaweza kuwa binadamu, wanyama, ndege, wadudu, mimea, mawe, upepo, na kadhalika. Husawiriwa kisanaa na mwandishi ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za maisha katika jamii. Wahusika wana sifa za kimaadili, kitabia, kiitikadi, na kifalsafa ambazo hutambulishwa na wanayoyasema na wanayoyatenda, na huwa ni sehemu ya kazi nzima, yaani kutoka mwanzo hadi mwisho (Mbunda, 1992; Wamitila, 2002; Lyimo, 2014; Mulokozi, 2017). Vilevile, wahusika ni kiini cha masimulizi, maana wao ndio huibua na kutengeneza mgogoro. Wahusika wa kazi ya sanaa huwa na tabia zinazotofautiana kati yao kutegemeana na lengo la mwandishi, aina ya kazi, jinsi walivyosawiriwa, kuaminika kwao, uhusiano wao, uwakilishi wao, na majina yao (Madumulla, 2009). Kutokana na utafiti uliofanyika, wahusika pia huweza kutofautiana kutokana na silika zao. Kwa mujibu wa Mlacha (1985), wahusika ni watu ambao msanii mwenyewe huwabuni kutokana na maisha ya jamii yake kulingana na kile anachotaka kukifafanua. Anaongeza kuwa uchunguzi wa wahusika wake ndio hasa unaomuwezesha kuijenga hadithi yake. Kwa hiyo, katika kazi yoyote ya kifasihi, wahusika ni wawakilishi wa tabia za watu katika maisha waliyoumbwa

kisanaa. Hata hivyo, tasinifu hii inamjadili mhusika kama binadamu anayesawiriwa kisanaa na mwandishi ili kuwakilisha dhana fulani aliyoikusudia.

#### 1.1.1.4 Mtoto

Mtoto ni mwanadamu mwenye umri mdogo, asiye mtu mzima. Kwa kawaida, kuna tofauti katika tamaduni mbalimbali kuhusu umri ambapo mtoto hutafsiriwa kama si mtoto tena. Mara nyingi, miaka kabla ya balehe hutazamwa kuwa ni kipindi cha utoto, na mtoto akiuvuka umri huu huitwa kijana. Kwa mujibu wa Bakhresa (1992), mtoto ni binadamu ambaye hajakua au hajakomaa; ni kiumbe kidogo. Hapa, amezingatia kigezo cha ukuaji ambacho, hata kwa macho, kinaweza kumtofautisha mtoto na mtu mzima. Kukua kunajumuisha kiwango cha kuelewa na kupevuka mwili. Kwa kawaida, mwili wa mtoto huwa tepetepe, ilihali wa mtu mzima huwa na ukomavu. Madumulla (2001) anafafanua dhana ya mtoto kuwa ni mtu wa umri wa kwenda shule ya chekechea hadi kufikia anapohitimu elimu ya msingi, yaani darasa la saba. Kwa tarakimu, kipindi hiki katika maisha ya binadamu, hususani Tanzania, ni kati ya miaka mitatu hadi kumi na mitano. Kisheria, mtoto ni mtu au kijana ambaye ana umri chini ya miaka kumi na minane (Gerard na Sanjay, 1992; Bakize, 2013; Chama cha Wanasheria Tanganyika, 2016; Mulokozi, 2017). Fasili hii imejengwa kwa kuzingatia sheria ya mtoto ya mwaka 2009, na mkataba wa kimataifa wa haki za mtoto.

Tasinifu hii inamtambua mtoto kama ni yule binadamu mwenye umri kati ya siku moja hadi miaka kumi na minane. Hata hivyo, watoto walengwa katika tasinifu hii ni wenye umri wa miaka kumi na mitano hadi kumi na minane. Kundi hili ni la watoto ambao wapo katika umri wa mwisho wa utoto. Kwa mujibu wa Herman (2012) kwa kujikita katika kigezo cha umri, Fasihi ya watoto ni ile inayowahusu watu walio chini ya umri wa miaka 18. Kundi analolitaja Herman ni kubwa sana, hivyo utafiti uliofanyika ulijikita katika kundi la mwisho la utoto. Watoto hawa inaaminika kuwa wamekomaa zaidi kiakili, hivyo wanakuwa na utambuzi wa mambo kuliko watoto wa makundi mengine. Watoto hawa, kwa muktadha wa Tanzania, mara nyingi huwa katika elimu ya sekondari.

#### 1.1.1.5 Fasihi ya Watoto

Fasihi ya watoto ni ile ambayo walengwa wake wakuu ni watoto; yaani, ni Fasihi iliyotungwa kwa ajili ya kutendwa au kusomwa na watoto (Madumulla, 2001; Ngugi, 2014). Kazi hizi mara nyingi huwa ni sahili, zenye rangi za kuvutia, zinazohusisha vitendo vingi, zenye mwisho wenye furaha na kutohusisha uonevu uliopitiliza. Pia, zinapaswa kuwa na mada inayovutia, pamoja na njia bora ya uwasilishaji inayozingatia maana na tajiriba za watoto husika (Nodelman na Reimer, 2003). Fasihi ya watoto humsaidia mtoto kujua mazingira ya nyumbani, jamii yake, na ulimwengu kwa jumla. Kama ilivyo Fasihi ya watu wazima, Fasihi ya watoto ina dhima ya kuelimisha, kuonya, kuburudisha, kuadibu, kurithisha amali za jamii, na kupanua maadili ya kijamii. Ngugi na wenzake (2014) wanabainisha kuwa dhima hizi ndizo zilizoibua Fasihi ya watoto kwa umahususi wake ili mtoto ambaye ndiye mlengwa mkuu aweze kupata kile ambacho alikuwa anakikosa hapo awali. Wanaongeza kuwa, hapo awali watoto hawakuwa na umuhimu wa kusoma kazi za kifasihi. Hata hivyo, kwa kusoma kazi za Fasihi ya watoto humbadilisha mtoto kifikra, kimtazamo, na wakati mwingine kimatendo. Jambo hili linatiliwa mkazo na Ngugi (khj) anaposema kuwa kama ujumbe wa kwenye hadithi utakuwa unamhusu mtoto, unaweza kumsaidia katika maisha yake kwa kudhibiti hisia mbalimbali, kubadilisha mienendo fulani, na hata kupata taarifa fulani itakayomsaidia maishani. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, mambo anayoyasema Ngugi yana ukweli, kwa sababu watoto hufyonza mambo yakawakaa kwa haraka kutokana na vichwa vyao kutokuwa na mambo mengi. Kwa mantiki hii, Fasihi ya watoto ina umuhimu mkubwa katika makuzi ya watoto. Amukowa (2018) anaonesha umuhimu wa sayansi na teknolojia uliovumbua vyombo vya kielektroniki na kufanya Fasihi ya watoto kupata mwamko mpya, hivyo kuwavutia zaidi. Mtafiti huyu alitolea mfano wa kibonzo cha *Kirikuu* ambacho kimetokea kupendwa sana na watoto. Kwa kupitia vibonzo, watoto hufuatilia matukio kwa umakini, na hivyo, hujifunza kwa haraka sana. Kwa mujibu wa tasinifu hii, Fasihi ya watoto ni ile inayotungwa na watoto au watu wazima. Wahusika na hadhira yake ni watoto, wakati maudhui yake ni ya kuelimisha na kuburudisha.

### 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Fasihi ya watoto huhusisha kazi za kifasihi ambazo walengwa wake wakuu ni watoto. Utanzu huu una sifa sawa na tanzu nyingine za Fasihi, hasa katika matumizi ya lugha, ingawa mara nyingi hutumia lugha nyepesi ili iwe rahisi kueleweka kwa hadhira lengwa. Crippen (2012) anabainisha kuwa Fasihi ya watoto ni muhimu sana kwa sababu inawapa watoto uwezo wa kujifunza, kuukubali, na kuupenda utamaduni wao na wa wengine. Kuupenda na kuuthamini utamaduni wao kutawasaidia katika maendeleo binafsi na ya jamii. Pia, Fasihi ya watoto inakuza fikra na ubunifu, na inaeneza Fasihi na dhamira zake toka kizazi kimoja hadi kingine.

Kwa mujibu wa Bingham (1970), Fasihi ya watoto ulimwenguni ilichipuka kutoka katika hadithi zilizokuwa zikisimuliwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Historia inaonesha kuwa masimulizi ya kwanza katika maandishi yaliyoitwa *Pachatantra* yalipatikana India ambayo yanakisiwa kuandikwa miaka ya 200 *AD.* Bingham (khj) anasisitiza kuwa kwa kuwa bara la Ulaya lilikuwa kitovu cha utamaduni wa dunia, maandishi ya kuelekeza watoto yaliongezeka kama vile vitabu vya alfabeti na vitabu vya kuabudu katika miaka ya 1400. Vitabu hivi vilikuwa na picha zilizotengenezwa kwa vipande vya mbao. Mnamo miaka ya 1920 vitabu vya picha vya watoto vilianza kuzalishwa kwa wingi. Baadhi ya vitabu katika mwongo huo ni pamoja na *Wanda gag's Millions of Cats* (1928), *The Little Engine that Could* (1930), *Babar* (1931), *Madeline* (1933), na *Nacurious Neorge* (1941).

Hata hivyo, Bakize (2020) anasema kuwa chimbuko la Fasihi ya watoto bado ni tata, hasa tunapoangalia ni wapi ilipoanzia. Fasihi hii ilichipuka kutokana na uhitaji au maendeleo. Watoto walikuwa wanarejelewa katika Fasihi, isipokuwa walikuwa wanajumuishwa na wahusika wengine. Wakati mwingine kulikuwa na vimaudhui vichache vilivyokuwa vinawarejelea. Kwa maana hiyo, hakukuwa na Fasihi mahususi kwa ajili ya watoto, bali ilikuwapo kwa namna tofauti kama vile, mbazi za kufunza vijana na watoto. Anasisitiza kuwa tunapoangalia chimbuko la Fasihi ya watoto tusifananishe na gonjwa fulani lililolipuka, kwamba lilianzia mahali fulani, mwaka fulani, eneo fulani na kadhalika. Pamoja na umuhimu wake, utanzu huu haukupewa kipaumbele kwa miaka mingi katika maandishi ya tahakiki nchini Tanzania. Kazi nyingi za kihakiki zilishughulikia zaidi Fasihi ya watu wazima kwa imani kuwa Fasihi ya watoto haikustahili kuchunguzwa kwa sababu inahusu ngano

za chura na sungura (Wamitila, 2008). Mtazamo wa jamii ya wasomi kuhusu watoto ndio unaoathiri namna unavyoiangalia Fasihi hii. Bakize (2015) anafafanua mitazamo ya jamii ya wasomi kuwa wengi walikuwa wakiinasibisha Fasihi hii na mambo ya kitoto ambayo ni rahisi na yasiyohitaji uchunguzi wa kina.

Mulokozi (2017) anaeleza kuwa kabla ya mwaka 1991 nchini Tanzania, riwaya za watoto katika Kiswahili zilikuwa chache. Uandishi wa Fasihi za watoto kwa Kiswahili umeanza kupewa umuhimu baada ya mwaka 1960, ukapamba moto kidogo miaka ya 1970 na 1980, na kushika kasi zaidi miaka ya 1990 (Mulokozi, ametajwa). Riwaya hizo ziliongezeka baada ya kuanzishwa kwa mradi wa vitabu vya watoto Tanzania (*Children Books Project* - CBP) mwaka 1991 uliowawezesha waandishi, wachapishaji na wachoraji wa vitabu vya watoto kufanya kazi za Fasihi ya watoto kwa weledi na kasi zaidi. Aidha, mradi ulifungua maktaba katika shule zilizo chini yake na kusambaza vitabu vilivyochapishwa kwa ajili ya usomaji wa ziada. Hadi kufikia mwaka 2015, mradi ulikuwa umechapisha na kusambaza zaidi ya vitabu 350 mashuleni (Madumulla, 2009).

Mulokozi (khj) anaendelea kufafanua kwamba ziko riwaya ambazo zinamchora vizuri na kumjenga kichanya mhusika mtoto kiasi cha kuacha taathira njema katika nadhari ya msomaji. Baadhi ya riwaya na hadithi za watoto na vijalunga[1] ni pamoja na *Moto wa Mianzi* (2015) na *Ngome ya Mianzi* (2006) za Mulokozi, *Safari ya Prospa* (Lema, 2004), *Kipofu Mwenye Miwani Myeusi* (Mtobwa, 1997), *Vijana Jasiri* (Shija, 1980) na *Mashujaa wa Kazakamba* (TPH, 1978).

Kwa mujibu wa Mbuthia (2018), vitabu vya watoto katika lugha ya Kiswahili vimeongezeka sana katika siku za hivi karibuni kutokana na mashirika ya uchapishaji kuanza kutazama sana aina hii ya Fasihi. Ijapokuwa hapo awali utanzu huu haukupewa kipaumbele, baadhi ya wataalamu waliona kwamba aina hii ya vitabu inaweza kuwasaidia wasomaji wadogo kuelewa mazingira yao na kupanua maoni kuhusu dunia. Mbuthia (khj) anafafanua kwamba waandishi wa vitabu wanaweza pia

[1] Kwa mujibu wa Mulokozi (2017), kijalunga ni kijana wa kike au kiume mwenye umri wa kubalehe, yaani kati ya miaka 12-21. Vijana hao huandaliwa vitabu maalum vinavyolingana na umri wao na vyenye kuzingatia mahitaji na maendeleo yao. Kijalunga hajatajwa katika sheria ya Tanzania, bali yeye ameona wana umuhimu wa kuainishwa. Katika tasinifu hii, tunashughulikia watoto wenye umri kati ya miaka kumi na mitano hadi kumi na minane.

kuwasaidia watoto kuelewa lugha, jamii yao, pamoja na kujenga maoni yao ya ulimwengu kutokana na kile wanachokisoma.

Fasihi ya watoto, kama zilivyo aina nyingine za Fasihi, hutegemea wahusika kama msingi muhimu katika matukio yanayoisukuma hadithi tangu mwanzo hadi mwisho. Wahusika hukusudiwa wawasilishe dhana, fikra, au tabia za watu (Mbunda, 1993). Wahusika wakuu ndio wanaobeba mawazo ambayo mwandishi hudhamiria kuyapeleka kwa hadhira husika. Maudhui ya kazi ya Fasihi huwa yanamzungukia, na hata kutolewa, na mhusika huyo zaidi kuliko wahusika wengine. Hivyo, wahusika wamekuwa midomo na vipaza-sauti vya watungaji (Senkoro, 2011). Mhakiki analazimika kuuelewa uhusika wa kila mhusika katika kazi ya Fasihi. Wahusika wanaweza kuumbwa kinafsi, kiakili, na kimwili. Ujenzi huu wa kinafsi na kimwili huonesha wasifu wake wa ndani na nje au huweza kuonesha mabadiliko yake kila anapokutana na hali isiyo ya kawaida. Mabadiliko haya huathiriwa na nguvu za kiutamaduni, kisiasa, na kiuchumi (Muhando na Balisidya, 1976).

Pamoja na athari hizo, utendaji wa wahusika ndio msingi katika Fasihi yoyote ile. Kwa kawaida, utendaji wa wahusika hudhihirika kwa maneno yanayoambatana na matendo au kwa masimulizi. Mlaga (2017) anasema kuwa utendaji ni sanaa. Anaigawa sanaa ya utendaji katika makundi mawili: Fasihi simulizi kwa upande mmoja, na tamthiliya au drama kwa upande mwingine. Pia, anaifafanua sanaa kwa namna mbili: kwanza, ufundi wa mtu kuwasilisha mawazo yaliyo katika fikra ili yadhihirike katika sura mbalimbali kama uchoraji, uchongaji, uhadithiaji, na ufuaji. Pili, sanaa ni kitu kilichotengenezwa kwa ufundi na uzuri ili kuwavutia watu. Hii inaweza kuwa katika maandishi, maongezi, ushonaji, uchongaji, ufumaji, na kadhalika. Utendaji unaoshughulikiwa ni sanaa ya maandishi katika riwaya za watoto.

Suala la utendaji katika riwaya linathibitishwa na Mulokozi (2020) anaposema kuwa utendaji huu unatofautiana na wa Fasihi simulizi, kwani unahusisha usawiri wa wahusika, uhusiano wao, na yale wanayoyatenda ili kusukuma mbele hadithi. Yeye anaamini kuwa utendaji ndio unaosababisha kupata muundo na msuko ambao unaakisi mgogoro. Hii ina maana kuwa watendaji wanakuwa na pande mbili au tatu ambazo zinagongana na kusukuma mbele hadithi, na hatimaye, kufika kileleni

ambapo ujumbe uliokusudiwa unakuwa umefika. Utendaji huu unakuwa ni wa wahusika ndani ya masimulizi, lakini ni wawakilishi wa watu waliopo katika ulimwengu wa nje ya hadithi. Wahusika hao wanahusiana na wanatendaji na kuibua mambo fulani. Kwa kuwa Fasihi ya watoto ni kazi ya sanaa, kwa mintarafu ya tasinifu hii, utendaji unatambuliwa kwa lugha ya mazungumzo baina ya wahusika na masimulizi ya mwandishi yanayokwenda sambamba na mazungumzo hayo.

Zipo namna anuwai ambazo waandishi huwajenga na kuwachora wahusika wao kwa kuonesha uthubutu wao katika mambo mbalimbali. Wapo wanaokuwa wanyonge, wanaoonewa na kubaguliwa; vilevile, wapo ambao huthubutu kufanya mambo mbalimbali, tena ya hatari, ambayo yangeweza kufanywa na watu wazima. Kwa mujibu wa Mudhihiri (2019), kuthubutu ni silika ya binadamu tangu kuzaliwa kwake. Binadamu huthubutu ili kuutawala na kuumiliki ulimwengu. Kwa kurejelea mawazo ya Mudhihiri, ni dhahiri kuwa hata wahusika huthubutu kufanya mambo mbalimbali ambayo mwandishi amedhamiria, kwa kuwa wahusika ni wawakilishi wa binadamu wa kawaida. Mambo hayo hudhihirika kupitia wanayoyasema na wanayoyatenda au kutendewa. Mlacha (1985) anaeleza kuwa kutokana na mazungumzo ya ndani ya mhusika, pamoja na fikra zake, msomaji anaweza kumfahamu na kujua sababu za matendo yake. Pia, anaweza kufahamu mawazo yake kuhusu watu wengine, matendo yake, na mahusiano na wengine. Haya yote huifafanua tabia yake na namna alivyoumbwa. Kwa hiyo, silika ni jambo la muhimu katika kuzisoma na kuzielewa kazi hizi. Hata hivyo, suala la silika halijatafitiwa kwa kina na upekee wake katika Fasihi ya watoto.

Kwa mtazamo wa tasinifu hii, Fasihi ya watoto ina umuhimu mkubwa kwa kuwa inaruhusu ujenzi wa msingi katika utu wa mtu na tabia yake. Athari yake huweza kuwa kubwa, kwani watoto wana sifa ya kufyonza mambo yakawakaa na kuwaathiri tangu wakiwa watoto mpaka wanapokuwa watu wazima, hivyo, kuathiri jamii yote. Pamoja na umuhimu huu, kazi hizi zinasomwa kwa kiasi kidogo sana; na wale wanaosoma wanakuwa na uelewa hafifu. Katika utafiti jaribizi, ilionekana kuwa watoto hawazisomi riwaya hizi, isipokuwa wanasoma zaidi vitabu vya kiada kwa ajili ya kujibia mitihani. Hata kazi hizo za kiada wapo ambao hawazisomi, bali husoma tahakiki tu kwa shabaha hiyohiyo. Bakize (2018) anatoa ithibati ya jambo hili kwa kutaja sababu mbili: moja, wanaosoma kazi hizi ni wale tu waliopo katika

mradi wa vitabu vya watoto; pili, watoto wanapenda zaidi kuangalia runinga na sinema kuliko kusoma vitabu. Pamoja na hayo, Lyimo (2017) anafafanua kuwa, pamoja na kutofautiana kwa Fasihi ya watoto na ile ya watu wazima, bado dhima ya Fasihi inabaki ileile, ya kuonya, kufundisha, kuadibu, na kurithisha amali za jamii. Hivyo, ni dhahiri kuwa Fasihi ya watoto inahitaji kuchunguzwa, kwani nayo ni kazi ya sanaa yenye umuhimu kwa mtu mmojammoja, na jamii nzima kwa jumla kama zilivyo kazi nyingine.

Hata hivyo, kutokana na umuhimu wa Fasihi ya watoto na ongezeko la vitabu vya watoto kwa lugha ya Kiswahili, ni dhahiri kwamba watafiti mbalimbali wamechochewa kutafiti katika uga huu, kama vile, Ashmun (2010), Shima (2012), Rothbart (2012), Bakize (2013), Ngugi (2014) na Keen (2018). Watafiti hawa walijikita zaidi katika maudhui ya Fasihi ya watoto na athari zake kwa mtoto. Katika Fasihi andishi, fani na maudhui ni sawa na pande mbili za shilingi, kiasi kwamba haziwezi kutengwa. Hata hivyo, kuna mambo ambayo hayako wazi, ambayo kwayo yalituhamasisha kufanya utafiti. Kwa mfano, uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili haujadadavuliwa kwa kina. Kutomakinikiwa kwa suala hili, imebainika ndiyo sababu ya watoto kutopenda kusoma kazi zilizoandikwa kwa ajili yao, hususani riwaya za *Ngoma ya Mianzi* na *Safari ya Prospa*. Endapo suala hili lingemakinikiwa, watoto wangefurahia kusoma riwaya zilizoandaliwa kwa ajili yao na kuzielewa vizuri zaidi. Pia, riwaya hizo zingewajenga kisaikolojia, kwa kuwa wangekuwa miongoni mwa wahusika kwa kufuatilia hadithi hizo. Hivyo, utafiti uliozalisha tasinifu hii uliona haja ya kuchunguza suala hilo kwa kina na kwa upekee kwa kutumia riwaya teule za Fasihi ya watoto ili kushughulikia tatizo hilo.

### 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Wataalamu mbalimbali wamejihusisha na kutafiti au/na kuhakiki juu ya masuala mbalimbali yanayohusiana na Fasihi ya watoto na wahusika. Miongoni mwao ni Muthubi (2005), Wambua (2008), Njue (2010), Mulewa na Kawika (2011), Bakize (2013), Mutua, Lyimo na Ngugi (2014), Ngugi, Karanja na Mzee (2015), Mrikaria na Moh’d (2017), pamoja na Mbuthia (2018). Baadhi ya wataalamu hawa wameonesha namna mhusika wa kike anavyosawiriwa katika kazi mbalimbali za kifasihi, hasa Fasihi ya watu wazima. Pia, wamebainisha changamoto zinazoikabili Fasihi ya

watoto ya Kiswahili na kuangalia maendeleo yake katika nchi za Tanzania na Kenya. Kwa upande wa utendaji, umefanyika zaidi katika tamthiliya au drama na Fasihi simulizi, ingawa wapo wataalamu kama vile Munyioki (2018) waliofanya tafiti zao katika utendaji wa wahusika wa riwaya, lakini si riwaya za watoto. Masuala ya uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika, hususani kwenye riwaya za watoto, yalikuwa hayajachunguzwa kwa upekee wake. Kwa mtazamo wa utafiti uliofanyika, jambo hili lingeachwa pasipo kushughulikiwa, lingeendelea kuathiri wasomaji waliolengwa katika kazi hizi. Hii ni kwa sababu wangeshindwa kuzielewa silika zao kutokana na kutobainishwa kwa aina za silika, kutofafanuliwa kwa utendaji wa wahusika na kutotathminiwa kwa uhusiano wa utendaji na sifa za aina za silika. Hii huweza kufubaza utamaduni wa kujisomea kazi hizo, na hivyo, kushindwa kujenga maono ya kiulimwengu. Kwa kuwa wasomi wengi ndio wazazi na walezi wa watoto waliolengwa na utafiti uliofanyika, inaaminiwa kuwa wakiisoma tasinifu hii, watasaidia kuwaelimisha watoto na kuzijua silika zao. Kwa hiyo, mtafiti aliona haja ya kumakinikia wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto, kwa kuangalia silika na utendaji wao, kwa kuwa wao ndio msingi mkuu wa kueleweka kazi zenyewe, na ndio kipaza sauti cha mwandishi.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti uliozalisha tasinifu hii ulikuwa na malengo ya namna mbili, lengo la jumla na malengo mahususi.

### 1.4.1 Lengo la Jumla

Utafiti uliofanyika ulilenga kuhusianisha silika na utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

a) Kufafanua namna mbalimbali za utendaji wa wahusika wakuu wa riwaya teule za Fasihi ya watoto;
b) Kuchambua aina za silika za wahusika wakuu wa riwaya teule za Fasihi ya watoto; na
c) Kutathimini uhusiano baina ya utendaji wa wahusika wakuu wa riwaya teule za Fasihi ya watoto na sifa za aina za silika zao.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

a) Utendaji wa wahusika wakuu wa riwaya teule za Fasihi ya watoto ni wa namna gani?
b) Ni aina gani za silika zinabainika kwa wahusika wakuu wa riwaya teule za Fasihi ya watoto?
c) Utendaji wa wahusika wakuu wa riwaya teule za Fasihi ya watoto unahusianaje na sifa za aina za silika zao?

## 1.6 Manufaa ya Utafiti

Tasinifu hii inatarajiwa kuleta tija za kitaaluma, kijamii, kitafiti, na kisera. Kitaaluma, itaonesha mtagusano mkubwa baina ya nyuga mbili za Fasihi na saikolojia; kwamba, Fasihi haiwezi kujitenga na nyuga nyingine za kitaaluma, kupanua taaluma ya Fasihi kwa jumla na Fasihi ya watoto kwa upekee wake, pamoja na kuongeza stadi, ari, na hamu ya usomaji wa kifasihi. Kijamii, itakuza utambuzi binafsi wa kisilika na kuwa na uwezo wa kujitofautisha na wengine, hivyo kuboresha utendaji wa jamii. Martin na Bobgan (1992) wanasema kuwa kila binadamu ameumbwa na baadhi ya maumbile yasiyotabirika, pamoja na yale ya kurithi ili kumfanya aonekane alivyo na atende kwa namna fulani. Tija nyingine ya kijamii ni kusaidia watoto kuzisoma na kuzielewa riwaya hizi na nyingine zilizoandaliwa au zitakazoandaliwa na kuandikwa kwa ajili yao, kwa kuwa watunzi na wahakiki watatunga na kuhakiki kazi zao kwa kuzingatia makundi ya silika. Kitafiti, itatumika kama rejeleo kwa watafiti wengine ambao watafanya tafiti zao katika uga huu wa Fasihi ya watoto, na kuhamasisha watafiti wengine wafanye utafiti mwingine utakaofanana na utafiti huu. Mwisho, itawasaidia watunga sera katika kutunga sera za watoto zinazoendana na aina nne za silika.

## 1.7 Mawanda ya Utafiti

Utafiti uliofanyika ulichunguza wahusika wa Fasihi ya watoto katika riwaya teule. Ijapokuwa riwaya hizi zina wahusika wengi, tulichunguza wahusika wakuu tu ili kukidhi haja ya malengo ya utafiti. Kupitia wahusika wakuu, data kuhusu utendaji wao zilibainika, na hivyo, zilihusianishwa na sifa za silika zao. Wahusika wengine walichukuliwa kama sehemu ya kuongeza maarifa kwa mtafiti, lakini hawakuhusishwa katika mjadala wa matokeo, isipokuwa katika sehemu ambazo wanafanya mazungumzo na wahusika wakuu. Pamoja na mawanda haya, matarajio

ya matokeo ya utafiti hayajaathiriwa kwa namna yoyote. Hivyo, matokeo yanaweza kutumika katika vipera vingine vya Fasihi. Pia, tulitumia kazi nyingine, hususani tafiti tangulizi, ili kupata data fuatizi za kujaliza katika data kuu.

## 1.8 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii imejadili utangulizi wa jumla ambapo dhana muhimu zilizotumika katika utafiti zimefafanuliwa. Dhana hizo ni utendaji, silika, wahusika, Fasihi ya watoto, na mtoto. Pia, usuli wa tatizo la utafiti umeelezwa na kuonesha umuhimu wa kufanya utafiti katika uga huu. Jambo jingine ni tamko la tatizo la utafiti ambalo limeonesha kuwa masuala ya silika bado hayajachunguzwa kwa upekee wake katika Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Pamoja na hayo, malengo ya utafiti yamebainishwa ambayo ni kufafanua utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto, kuchambua aina za silika za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto, na kutathimini uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili katika riwaya teule. Malengo haya yameambatana na maswali ya utafiti. Zaidi, sura imebainisha manufaa ya utafiti huu; ambayo ni kitaaluma, kijamii, kitafiti, na kisera. Mwisho, mawanda ya utafiti yamebainishwa.

Sura inayofuata inajadili kuhusu mapitio ya maandiko yaliyotumika katika utafiti uliofanyika, pamoja na kiunzi cha nadharia.

# SURA YA PILI

# MAPITIO YA MAANDIKO NA KIUNZI CHA NADHARIA YA UTAFITI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii imeyapitia na kuyafafanua maandiko mbalimbali yaliyoshabihiana na utafiti uliofanyika ili kupata mwanya uliohitaji kuzibwa. Maandiko hayo, kwa kiasi kikubwa yalikuwa ni tafiti tangulizi. Pia, sura hii imefafanua nadharia iliyotumika katika utafiti huo.

## 2.2 Mapitio ya Maandiko

Maandiko yaliyoshughulikiwa tuliyagawa katika sehemu kuu nne: maandiko kuhusu utendaji, maandiko kuhusu silika, maandiko kuhusu wahusika, na maandiko kuhusu Fasihi ya watoto kwa jumla. Mwisho, mapengo yaliyojitokeza ambayo yalimsukuma mtafiti kufanya utafiti uliozalisha tasinifu hii yamebainishwa.

### 2.2.1 Maandiko Kuhusu Utendaji katika Kazi za Fasihi

Munyioki (2018) amebainisha vipengele vya utendaji vilivyowezesha kutathimini kuigizika kwa riwaya teule. Vipengele hivyo ni matumizi ya lugha ya majibizano ilivyotumika na utendaji wa wahusika, masimulizi ya kiutendaji na taswira za kifilamu, na utendaji wa kidrama. Katika kuchunguza lugha ya majibizano, anabainisha majukumu ambayo lugha hiyo imepewa itekeleze kama vile kuhoji, kupasha habari, kushawishi, kuliwaza, kuhamasisha, na kuendesha mashitaka. Andiko lake limebainisha mambo ya msingi ambayo yalisaidia katika utafiti huu kama vile, vipengele vya utendaji. Kwa upande mwingine, andiko hili liliacha mwanya wa kufanyika kwa utafiti mwingine, kwani halikuonesha uhusiano baina ya vipengele hivyo na silika.

Soyinka (1988) ameona kwamba matumizi ya jukwaa yana athari chanya katika utendaji, kwa kuwa yanaathiri hadhira kisaikolojia na kimwili. Athari hizi hudhihirika zaidi pale utendaji unapofanyika kwenye jukwaa, huku hadhira ikingoja kwa hamu kuona ikiwa mhusika mkuu ataepuka matatizo anayokumbana nayo kutokana na mpinzani wake, au la. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, utendaji siyo lazima uwe jukwaani, bali unaweza kufanyika mahali popote. Jambo hili la kufanyika mahali popote linashadidiwa na wa Thiong'o (1986) anaposema kuwa utendaji ni sehemu ya maisha ya binadamu, na siyo lazima ufungamane na ukumbi

wa maonesho. Kwa hiyo, andiko la Soyinka lilitusaidia kujua athari za utendaji kwa hadhira, lakini halikutuonesha uhusiano wa utendaji huo na sifa za aina za silika za wahusika. Hivyo, utafiti uliofanyika ulikusudia kuziba mwanya huo kwa kutathimini uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wakuu wa kazi teule.

Mlacha (1985) amefafanua kuwa riwaya yoyote ile inatawaliwa na matendo ya wahusika kufuatana na maono ya msanii katika utendaji wa kinathari. Msanii naye anatawaliwa na mazingira. Kwa hiyo, katika matendo ya wahusika, msanii anaweza kusisitiza kile kilichopo katika jamii yake, au kile anachotaka kukionesha. Kwa kuwa wahusika ni kiwakilishi cha watu halisi, matendo yao yanaibua athari ya moja kwa moja. Andiko la Mlacha limedokeza matendo ya wahusika na athari yake, lakini, halijabainisha uhusiano wa matendo hayo na silika za wahusika hao. Kutobainishwa huko kuna athari kwa walengwa wa kazi hizi, kwani hawataweza kutambua silika walizo nazo. Jambo hili lilisababisha kuhitajika utafiti mwingine ambao ungeonesha uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Naye, Schechner (2013) amefananisha utendaji na tabia ya mwigo ambayo hutofautiana na tabia halisi ya mtu mwenyewe. Katika mwigo, mtu huambiwa afanye kama kwamba yeye ni mtu mwingine. Kwa kawaida, mwigo hujumuisha aina nyingi za matendo. Kwa hiyo, tabia na matendo yote huwa yameigwa, yaani yalishafanywa awali. Kuna wakati wanyama au vitu huiga matendo ya binadamu kutegemeana na dhamira ya mwandishi. Andiko hili lina manufaa kwa mintarafu ya utafiti wetu, kwani linaonesha umuhimu wa matendo ya wahusika katika kuwasilisha ujumbe uliodhamiriwa na mtunzi. Pamoja na manufaa hayo, bado utafiti huu uliacha mwanya wa kufanyika kwa utafiti wenye kuchunguza uhusiano wa utendaji wa wahusika na silika zao.

### 2.2.2 Maandiko Kuhusu Silika

Mills (2005) ametofautisha silika na tabia. Anasema kuwa silika inatokana na uumbaji; yaani, muundo asilia wa maumbile ya mtu ya kihisia, wakati tabia ni haiba inayoathiriwa na maisha ya mtu ya kila siku. Kwa hiyo, tabia ya mtu ni zao la haiba yake, mafundisho ya wazazi, shule, marafiki, mazingira, jamii, uzoefu wa maisha, tofauti za kibaiolojia baina ya mwanamke na mwanaume, na historia ya mtu husika. Mawazo ya Mills yalitusaidia katika utafiti uliofanyika kwa kutofautisha silika na

tabia, kwa kuwa dhana hizi zinaingiliana. Tulijikita katika silika kwa kuangalia sifa za silika za kila mhusika mkuu na kuzihusianisha na utendaji wake.

Gerard na Sanjay (1992) wanafafanua kuwa jamii inapohukumu juhudi za mtu kwa kuegemea katika viwango vya jamii husika, hiyo huitwa tabia. Kwa hiyo, tabia ya mtu hutokana na silika na haiba yake. Pia, tabia ni tathmini ya haiba. Hivyo, silika ya mtu ina mchango mkubwa katika tabia yake. Kwa kuwa tabia hutokana na silika, utafiti wao ulitusaidia kufafanua utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto, kwani wahusika hutenda kutokana na tabia zao.

Shiner (2012) anaonesha namna watoto wachanga wanavyotofautiana kutokana na maumbile ya kuzaliwa na uzoefu wa mazingira. Anabainisha kuwa sifa za upole za watoto zinaundwa na mchanganyiko wa mambo ya maumbile na ya mazingira. Vilevile, anabainisha asili ya mifumo ya tabia kwa kina zaidi, hususani kuhusu silika za nafsi zinazojidhihirisha kwa watoto, jinsi wanavyokabiliana nazo, na zinavyowajenga katika matokeo muhimu ya kijamii na utendaji wa akili. Pia, anaona kuwa katika umri wa miaka mitatu, watoto huanza kutofautiana katika mitazamo yao na namna ya kushirikiana na wengine. Mitazamo hiyo huweza kuwa hasi au chanya kuhusu suala husika. Kwa hiyo, elimu kuhusu silika inahitajika kwa walezi wa watoto ili waweze kuwalea vizuri. Andiko hili ni muhimu, kwani limebainisha umuhimu wa silika katika utendaji wa akili, na hivyo, kutoa hamasa ya kulichunguza suala hili katika Fasihi ya watoto.

Spinelli (2018) amefafanua kuwa uhusiano wa wazazi na watoto, hasa katika kipindi cha mwaka wa kwanza tangu azaliwe, humsaidia mtoto kujifunza lugha, kwa sababu hiki ni kipindi ambacho silika ya mwanzo hujitokeza. Hii ina maana kuwa silika ni suala ambalo linaathiri sana watoto katika kukabiliana na mazingira na kushirikiana katika kupata ujuzi mpya. Andiko la Spinelli lina mwanya uliohitaji kushughulikiwa kwa mnasaba wa utafiti uliofanyika. Matokeo ya utafiti kuhusu umuhimu wa malezi ya wazazi katika kujifunza lugha ni muhimu sana, kwa sababu wameonesha namna silika za mwanzoni zinavyoweza kumuathiri mtoto. Hili ni jambo zuri. Hata hivyo, katika andiko hili silika zimebainishwa kwa ujumla wake kutokana na malengo ya utafiti husika. Jambo hili linawafanya watoto, watunzi wa Fasihi ya watoto, na jamii kwa jumla, kutojua aina za silika na matokeo yake katika utendaji. Endapo jamii

itajua aina za silika, itaepusha migogoro na migongano isiyokuwa ya lazima, na hivyo, kuimarisha amani katika jamii. Katika mazingira haya, utafiti mwingine ulihitajika ili kuchunguza aina za silika za wahusika wa Fasihi ya watoto.

Mudhihiri (2019) analinganisha silika na kuthubutu; yaani, mja kuvaa ujasiri katika kufanya uamuzi na kutenda jambo. Anafafanua kuwa kuthubutu ni silika ya mwanadamu tangu kuzaliwa kwake. Ndani ya kuthubutu, mwanadamu hubeba dhamira ya kumiliki ulimwengu na kunufaika katika mahitaji yake. Mudhihiri (khj) anaamini kuwa kuthubutu kunasababishwa na ujasiri, kwa sababu ya utayari wa mtu kuyapokea matokeo ya dhamira yake, hata kama yatakuwa yameenda kombo. Masuala yaliyojadiliwa na Mudhihiri yalikuwa muhimu katika utafiti uliofanyika kwa sababu yamethibitisha kuwa silika humfanya mtu kutenda jambo fulani ili kuumiliki ulimwengu. Kwa hiyo, maelezo hayo yalitusaidia katika kuonesha uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika.

Mlacha (1985) anaeleza kuwa kutokana na mazungumzo ya ndani ya mhusika, pamoja na fikra zake, msomaji anaweza kumfahamu na kujua sababu za matendo yake. Pia, mawazo ya mtu kuhusu watu wengine na matendo yake katika uhusiano na wengine, huifafanua tabia yake na namna anavyoumbwa. Kwa kuwa mtu huzaliwa na silika zake, inaweza kusemwa kuwa silika za wahusika hutengenezwa na mwandishi kukidhi lengo lake. Hivyo, tulichunguza silika hizo na kuona uhusiano baina yake na utendaji wa wahusika.

Abulizi (2017) anaonesha umuhimu wa elimu kuhusu silika. Anabainisha kuwa elimu hii huwasaidia walezi wa watoto, walimu, na wazazi kutambua kwamba tabia za watoto na hisia siyo tu ni matokeo ya kijamii, bali, watoto wa umri mdogo hutofautiana katika kuonesha hisia zao na kanuni ya kujitegemea na wanaweza kufuata mielekeo tofauti kwa matokeo endelevu. Hivyo, anawashauri walezi kukubali na kuthamini kila sifa pambanuzi za mtoto. Matokeo ya sifa hizo yanaweza kurekebishwa moja kwa moja kwa juhudi ya kuzuia na kuingilia kati tabia zao. Andiko hili lina pengo lililohitajika kuzibwa kwa mintarafu ya utafiti uliofanyika. Limebainisha umuhimu wa elimu ya silika kwa wazazi na walezi, lakini halikuweka wazi uhusiano wa silika hizo na matendo ya watoto hao. Hili ni tatizo lililoleta haja

ya kufanyika kwa utafiti mwingine. Kutokana na hilo, tulichunguza uhusiano wa matendo ya wahusika na silika zao.

### 2.2.3 Maandiko Kuhusu Wahusika katika Kazi za Fasihi

Ali (2015) anaonesha namna mhusika mwanamke alivyosawiriwa katika kazi za kifasihi. Anataja vipengele vya ulezi wa watoto na familia, chombo cha starehe, kujiamini, huruma, kiumbe duni, ukatili, uchoyo, ufitinishaji, pambo, usaliti, uroho, ushiriki katika harakati, na ushawishi ambavyo amesawiriwa mhusika huyo. Pamoja na ubora wa utafiti huu, suala la namna silika zinavyoweza kuathiri wahusika na usawiri wao halikushughulikiwa. Pia, andiko la Ally limeshughulikia wahusika katika Fasihi ya watu wazima. Kutokana na hilo, utafiti wake umetoa hamasa ya kufanyika utafiti ambao unashughulikia uhusiano wa utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto na silika zao, kwani wahusika huwasilisha ujumbe wa riwaya husika kama alivyodhamiria mwandishi, hivyo humuathiri msomaji ambaye ni mtoto..

Mulewa (2011) anathibitisha kuwa wahusika katika hadithi fupi za Kiswahili huwa wakamilifu na watoshelevu, kinyume na madai ya wahakiki wengi wa hapo awali. Mhusika mkamilifu ni yule anayeingiliana vilivyo na vipengele vingine vya hadithi. Pia, waandishi wa hadithi fupi hutumia mbinu mbalimbali ili kuwapa wahusika wao sifa pana na zinazoonesha utoshelevu wa aina yake. Andiko hili limekuwa chachu katika utafiti uliofanyika na kuzaa tasinifu hii, kwani limedokeza sifa za wahusika ambazo kwazo zimehusianishwa na utendaji wao.

Kawira na Kisurulia (2018) wamedhihirisha kuwa waandishi wa kazi nyingi za Fasihi ya Kiswahili wameonekana kujibidiisha kuyapa majina ya wahusika wa kazi zao majukumu mapana zaidi yanayovuka mipaka ya mbinu ya majazi. Watunzi hutumia majina ya wahusika kama njia ya kueleza muonoulimwengu wao kuhusu hali mbalimbali zinazojitokeza katika jamii wanazoziandikia. Pia, wahusika wanafanya kazi ya kujitambulisha, na wakati huohuo wanafanya kazi ya kupitisha ujumbe wa mwandishi. Matokeo ya utafiti wao ni muhimu katika utafiti huu kwa sababu wameonesha wahusika wanavyojitambulisha na kupitisha ujumbe wa mwandishi. Haya ni mambo yaliyochunguzwa katika utafiti uliofanyika na kuhusianishwa na silika zinazotawala utendaji wa wahusika.

Mohamed (2017) amelinganisha tabia za wahusika wakuu na dhamira katika riwaya za *Utengano* na *Kusadikika.* Ameonesha kuwa wahusika wamesawiriwa katika namna mbili: tabia mbaya na nzuri. Anawashauri watafiti wengine wafanye utafiti kuhusu wahusika wakuu wa Fasihi. Andiko lake ni muhimu sana, kwani anabainisha tabia mbaya na nzuri za wahusika. Kwa kuwa silika za mtu hudhihirika kwa kupitia tabia yake, ilionekana haja ya kufanya utafiti mwingine wa kubainisha silika za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto.

Shepard (1962) katika andiko lake, amechunguza namna wahusika walivyosawiriwa na waandishi katika vitabu vyao kwa kutumia jumla ya vitabu kumi na sita. Miongoni mwa mambo aliyoyachunguza, ni pamoja na faida na hasara za utaifa, rangi, na kiwango cha uchumi. Anahitimisha kwamba mashujaa wote wameoneshwa kama wasafi, wenye afya na watanashati, na ni watu wa daraja la kati; hivyo, wamekwezwa sana. Kwa upande mwingine, wale wa daraja la chini wameoneshwa kinyume chake. Utafiti huu umeacha mwanya wa utafiti mwingine, kwani haukuzingatia nafasi ya silika katika usawiri wa wahusika hao, pamoja na tabia walizopewa na watunzi waliowasana. Utafiti uliofanyika uliona umuhimu wa kuzingatia tabia walizopewa wahusika, kwani ndizo zinazomfanya mhusika atende jambo fulani. Kutokana na matendo hayo, ndipo tunapata aina za silika. Jambo hili limefanyiwa kazi katika utafiti huu uliofanyika kwa kubainisha aina za silika za wahusika wakuu katika riwaya teule.

### 2.2.4 Maandiko Kuhusu Fasihi ya Watoto

Bakize na Senkoro (2019) wamemwangalia shujaa wa kike katika bunilizi za kihistoria. Katika mjadala, wanasema kuwa waandishi wa bunilizi wana fursa ya kuumba ulimwengu wao wanaoutaka kupitia bunilizi hizo. Wanaamini kuwa, ili suala la ujenzi wa taifa lifanikiwe kwa haraka, wanawake na wanaume wanatakiwa wapewe majukumu sawa bila kubagua jinsia zao. Wanazungumzia kuhusu kuibadili jamii kwa mtazamo wa kijinsia bila kumdunisha mwanamke kwamba ni suala la muhimu katika zama hizi. Utafiti wao una msaada mkubwa katika utafiti huu, kwani wameonesha ushujaa wa mtoto wa kike ambao ni sifa mojawapo ya silika za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Hata hivyo, huwa ni vigumu kuijua silika ya mhusika kama hajatenda. Hivyo, utafiti mwingine ulihitajika

kuonesha uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto. Kwa hiyo, utafiti uliofanyika ulitarajiwa kuziba mwanya huo.

Naye, Gatwiri (2015) anatathimini hadithi za watoto katika mtandao. Anazitaja hadithi hizo kuwa ni visasili, hekaya, hurafa, na hadithi zinazotokana na methali. Pia, anaona kuwa mtandao unaweza kutumika kama maktaba ambapo watoto wanaweza kuzisoma hadithi. Andiko lake limebainisha kuwa hadithi za watoto kwa lugha ya Kiswahili hazitumiwi Kenya tu, bali hutumika katika ulimwengu mzima. Kazi hii ilikuwa ni ithibati ya kuwapo kwa hadithi nyingi mtandaoni. Hata hivyo, kazi yake haikushughulikia wahusika ambao ni kiungo muhimu katika hadithi ili kupeleka mbele maudhui ya hadithi. Kwa hiyo, utafiti mwingine ulihitajika kuchunguza uhusiano wa utendaji na sifa za silika za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto katika riwaya teule.

Herman (2012) anazungumzia mbinu ya fantansia. Anaeleza kuwa ina dhima za kujenga msuko wa matukio na taharuki kwa wasomaji, kuibua migogoro ya hadithi na dhamira, na kuvuta usikivu wa hadhira. Kwa hiyo, anashauri kuwa mtindo huu uendelee kutumika, kwani si lazima mambo yote yaelezwe kiuhalisia. Kazi hii ni muhimu, kwa sababu inaonesha mambo yanayoibuliwa na fantasia. Hata hivyo, suala la silika lilihitajika, kwa sababu ili kuvuta usikivu kwa hadhira ni lazima msomaji aijue silika yake na za watu wengine. Kwa hiyo, tulichunguza aina za silika za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto ili kuziba mwanya huo.

Ngugi (2014) anabainisha vipengele vya msingi vinavyomotisha hamu ya kusoma miongoni mwa watoto. Vipengele hivyo ni ujengaji wa shauku, umuhimu wa kuelewa makundi mbalimbali ya watoto, suala la uhalali na ukweli katika Fasihi ya watoto na kanuni za uwasilishaji wa kazi za watoto. Hata hivyo, ili kuongeza motisha ya usomaji kwa watoto, hawana budi kufahamu aina za silika na sifa zake, kwani itawasaidia kufuatilia masimulizi na kujihusisha na wahusika hao. Hivyo, utafiti uliofanyika ni muhimu katika kuziba mwanya huu.

Bakize (2013) anazitaja changamoto zinazoikabili Fasihi ya watoto nchini Tanzania. Changamoto hizo ni pamoja na: Kazi nyingi kuandikwa na watu wazima, kazi za watoto kupata hadhira ndogo, kuegemeza uandishi katika aina moja ya kazi za

Fasihi, kutokufanyika kwa uchambuzi na uhakiki wa kutosha wa kazi za watoto, pamoja na kuchelewa kutambulika kwa kundi la watoto kifasihi. Hivyo, anapendekeza Fasihi hii kuangaliwa upya kwa umakini. Kutokana na changamoto zilizoibuliwa na Bakize, pamoja na mapendekezo aliyoyatoa, mtafiti alipata hamasa kufanya utafiti uliopendekeza kipengele cha silika kupewa umuhimu wake katika uhakiki wa Fasihi ya watoto. Kwa kumakinikia suala la silika katika uhakiki, litaibua hamasa ya usomaji kwa watoto ambao ndio walengwa wakuu wa kazi hizo.

Greenlaw (1970) amechunguza iwapo kazi za kubuni za Fasihi ya watoto za kisayansi zinaakisi athari ya teknolojia kwa binadamu. Katika uchunguzi wake, anatumia sampuli ya vitabu 133 vilivyoandikwa na waandishi 15 kwa ajili ya watoto wa umri kati ya miaka tisa na kumi na mitano, na vilivyochapishwa kati ya mwaka 1945 hadi 1970. Matokeo aliyoyapata yalibainisha kwamba vitabu vya kubuni vya watoto vya kisayansi vinajumuisha masuala ya watu binafsi, pamoja na matatizo yatokanayo na teknolojia ya kisasa, kama vile, nguvu ya nyuklia, na vinaweza kutumika katika kufundishia sayansi za jamii, sayansi asilia na historia. Andiko hili ni muhimu sana, kwani linabainisha umuhimu wa Fasihi ya watoto na namna kazi hizo zinavyoweza kuathiri watoto na jamii kwa jumla. Kwa kuwa Fasihi ya watoto ina umuhimu mkubwa kama huu, ilionekana haja ya kufanya utafiti mwingine hususani wenye kuonesha uhusiano baina ya utendaji wa wahusika na silika zao.

### 2.2.5 Mapengo Yaliyotakiwa Kuzibwa na Utafiti

Baada ya kupitia maandiko yanayohusiana na mada ya utafiti uliofanyika, tulibaini mambo kadhaa ambayo yalileta hamasa ya kuufanya utafiti huu. Mosi, wahusika wakuu katika Fasihi ya watoto bado hawajaangaliwa kwa undani wake, kwani maandiko mengi yanayohusu wahusika yamejikita zaidi kwa wahusika wa Fasihi ya watu wazima, hasa wanawake. Pili, maandiko kuhusu silika yamehusu zaidi uga wa saikolojia na sosholojia. Maandiko haya yameonesha umuhimu wa elimu kuhusu silika kwa wazazi na walezi katika kukabiliana na silika za awali. Kwa kutambua mchango mkubwa wa saikolojia kwa wahusika, ilionekana haja ya kufanya utafiti changamani wa kuhusisha Fasihi na saikolojia, hususani kwa kuangalia aina za silika za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto. Tatu, suala la utendaji limeandikwa zaidi katika Fasihi simulizi na tamthiliya. Kwa wale walioandika katika riwaya, hawakuchunguza riwaya za watoto. Aidha, uhusiano baina ya utendaji wa wahusika

wakuu na sifa za aina za silika zao haujashughulikiwa. Kutokana na hayo, lilikuwapo hitaji la kufanyika utafiti ambao ungeshughulikia kwa kina suala la silika kwa kuzingatia aina, sifa, pamoja na uhusiano wake na utendaji wa wahusika hao. Utafiti uliofanyika umerejelea mifano ya wahusika wakuu kutoka katika riwaya za *Ngoma ya Mianzi* na *Safari ya Prospa*.

### 2.3 Kiunzi cha Nadharia

Utafiti uliofanyika ulitumia Nadharia ya Saikochanganuzi ambayo iliasisiwa na mwanasaikolojia wa Ki-Austria, Sigmund Freud (1856-1939). Mulokozi (2017) anabainisha kuwa Saikochanganuzi huibua hisia na silika zilizohifadhiwa kutoka katika ung'amuzibwete (*unconsciousness*) kuingia katika hali ya umaizi (*consciousness*). Katika Fasihi, hisia na silika hizo huweza kumhusu mwandishi au wahusika wake.

Kwa mtazamo wa Freud, lugha huakisi michakato ya akilini inayojibainisha katika ndoto, misemo, na usemaji. Hali kadhalika, nafsi hubeba mahusiano hai yenye kudokeza ukinzano. Aidha, alibainisha nafsi tatu ambazo ni: nafsi ya kiwango cha msingi (*Id*) ambayo ni nafsi ya kisilika na matamanio bila urazini, hali ya unyama, kitovu cha misukumo ya kisilika kama ushari na ashiki dhidi ya dhamiri. Nafsi ya pili ni ya kiwango cha kati (*Ego*) ambayo ni nafsi ya utashi, urazini, na tafakuri inayoongoza maamuzi ya busara. Mwisho, ni nafsi ya kiwango cha ukomavu (*Super-ego*) ambayo ni nafsi ya kidhamira, ya kimaadili, inayochunguza uadilifu wa tendo, wema na ubaya wake, kabla ya kulitenda. Kwa mujibu wa Freud, tabia ya binadamu ni muingiliano baina ya nafsi hizi tatu zinazopatikana katika ubongo (Mbarouk, 2009).

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) Nadharia ya Saikochanganuzi ina misingi mitatu iliyobainishwa na Freud: mahitaji, matamanio, na wasiwasi. Mahitaji ni mambo ambayo yakikamilishwa humfanya mtu aishi vizuri. Mambo hayo ni chakula, mavazi na sehemu ya kulala. Matamanio hurejelea starehe, hasa za kingono. Wasiwasi ni mashaka na dukuduku kuhusu maisha kuwa mtu atafanikiwa, au la. Kati ya mambo haya matatu, nafasi kubwa huchukuliwa na matamanio. Kwa hiyo, kila binadamu hufanya jitihada kuhakikisha anakamilisha matamanio yake. Wakati mwingine, jitihada za kukamilisha matamanio hayo huumiza watu wasiokuwa na hatia.

Pia, Freud anafananisha Fasihi na ndoto. Kwa kuwa Fasihi andishi ni kazi bunifu, kazi hizi zinalandana na ndoto. Usanii ni njozi zinazoashiria matumaini na matamanio ya mwandishi. Pia, wahusika wanaosanwa na mwandishi ni wanadamu wanaoishi katika ndoto zake. Vilevile, Freud anaona kuwa fani na maudhui ni ndoto inayoweza kumliwaza anapoamua kuisoma kazi hiyo. Hali hii inaleta athari kubwa kwa msomaji, ijapokuwa anayoyapitia ni mambo ya ubunifu. Ndoto imewekewa msisitizo, kwa sababu katika jamii kuna miiko na makatazo mengi yanayomfanya mwanadamu ashindwe kuwasilisha kile alichonacho katika nafsi yake. Kwa hiyo, mtu hukiuka miiko hiyo kwa kupitia ndoto na kukamilisha mahitaji yake bila kukatazwa na mtu yeyote (Vice, 1990 na Mulokozi, 2017).

Kutokana na mawazo ya Freud, msomaji na mhakiki wanatazamiwa kuwaona wahusika kuwa tamathali fiche ambazo hutokana na mambo aliyoyapitia mwandishi zamani katika kukua kwake. Pia, msomaji anaweza kujiona katika kazi anayoisoma (Wamitila, 2003). Kutokana na hilo, nafsi ya msomaji inaweza kufurahi au kuchukia. Freud anaamini kwamba ndoto zote husheheni maana na ukweli kuhusu maisha ya mtu. Maana na ukweli kuhusu ndoto hizo vingejulikana kama vingefasiriwa.

Katika utafiti uliofanyika, tulitumia nafsi na misingi hiyo kama mwongozo katika mchakato mzima wa utafiti. Mawazo na matamanio yaliyopo katika akili za binadamu hujitokeza katika nafsi tatu zilizobainishwa. Nafsi hizo humsukuma mtu kutenda jambo fulani na kuacha jingine kutokana na mila na desturi za jamii husika.

Nadharia hii ilitusaidia katika utafiti uliofanyika kwa namna zifuatazo: Mosi, tulitumia misingi mitatu hasa msingi wa matamanio kufafanua namna mbalimbali za utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Matamanio ya wahusika husukumwa na nafsi tatu za ki-Feud ambazo humfanya mhusika atende au asitende jambo fulani kutokana na mila na desturi za jamii husika. Katika muktadha huu jamii ni ile iliyoandikiwa kazi hizi. Kila jamii ina makatazo ambayo humfanya mhusika asitende mambo fulani ili asiende kinyume na mila na desturi hizo.

Pili, tulitumia nafsi tatu zilizobainishwa kuchambua aina mbalimbali za silika na kuonesha jinsi zinavyomtofautisha mhusika mmoja na mwingine. Silika hizi ziliweza kuchambuliwa na kutambua sifa za kila silika baada ya wahusika kutenda kwa

namna mbalimbali, na matendo yao yalisukumwa na nafsi tatu zilizobainishwa. Sifa hizi za silika zilibainika kutokana na mhusika kusukumwa na matamanio yake na nafsi tatu zilizosababisha atende kwa namna anavyotenda. Katika uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti, nadharia hii ilitoa mwongozo katika kufafanua na kuweka wazi uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wakuu kwa kujiegemeza katika riwaya teule.

### 2.4 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii imepitia maandiko mbalimbali ambayo yalihusiana na mada ya utafiti uliofanyika. Mapitio hayo yalihusu utendaji, silika, wahusika, na Fasihi ya watoto, kisha mapengo yaliyotokana na maandiko hayo yalibainishwa kwa kueleza ni kwa namna gani utafiti huu ungeweza kuyaziba. Pia, nadharia iliyoongoza utafiti imefafanuliwa. Nadharia hiyo ni ya saikochanganuzi. Nadharia hii imebainika kuamiliana na malengo mahususi matatu ya utafiti huu.

Sura inayofuata inafafanua vipengele mbalimbali vya methodolojia iliyotumika kuendeshea mchakato wa utafiti uliofanyika.

# SURA YA TATU

# METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii imefafanua methodolojia iliyotumika katika mchakato wa utafiti. Methodolojia imegawanyika katika vipengele vya usanifu wa utafiti, mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti na njia za ukusanyaji na uchanganuzi wa data. Vipengele vingine ni maadili katika utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, mawanda ya utafiti, pamoja na changamoto zilizojitokeza, na utatuzi wake.

## 3.2 Usanifu wa Utafiti

Katika utafiti uliofanyika, usanifu kifani ulitumika ili kupata data tulizozihitaji. Usanifu kifani ni aina ya usanifu ambao mtafiti huteua mahali au kitu maalumu atakachokishughulikia kwa kina katika utafiti wake. Ni mbinu nzuri ambayo humuwezesha mtafiti kutumia muda wake vizuri, kwa kuwa tayari anakuwa ameshateua kitu cha kushughulikia (Robson, 2007). Kwa hiyo, hatapoteza muda mwingi kushughulikia mambo ambayo hayahusiki katika utafiti wake. Sambamba na hilo, Creswel (2009) na Ponera (2019) wanafafanua usanifu kifani kuwa ni uchunguzi wa kina wa tatizo moja ili kutumia matokeo ya uchunguzi huo kama kiwakilishi cha kuonesha hali ilivyo katika sehemu nyingine kama hiyo. Hivyo, tasinifu hii ilichunguza kwa kina na kumakinikia silika na utendaji wa wahusika wakuu katika riwaya za *Safari ya Prospa* na *Ngoma ya Mianzi*, na hivyo, kukusanya data zilizohitajika. Usanifu huu ni unafaa kutokana na mkabala wa utafiti uliofanyika ambao ni wa kitaamuli. Pia, hutumia usampulishaji usio nasibu wa kipekee katika kupata watafitiwa wa kutoa data zilizokusudiwa kwa kuamini kuwa wana sifa za kipekee za kuchaguliwa. Pamoja na hayo, usanifu huu ni muafaka kwa usaili kama mbinu mojawapo ya kukusanyia data ambayo ilitumika kwa waandishi wa riwaya teule na wataalamu wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili.

## 3.3 Mkabala wa Utafiti

Utafiti uliofanyika ulitumia mkabala wa kitaamuli. Kothari (2004) anasema kuwa mkabala wa kitaamuli huchambua data kwa mfumo wa maelezo, pasipo kufuata utaratibu wa kitakwimu. Mtafiti alitumia maelezo katika kubainisha aina za silika zinazojitokeza kwa wahusika wakuu, utendaji wa wahusika hao, na uhusiano baina ya matendo na sifa za aina za silika, mambo ambayo aliamini kuwa yangekidhi

mahitaji ya utafiti wake. Mkabala huu ulitumika kutokana na mwelekeo wa utafiti ambao ulihusisha maelezo kwa kiasi kikubwa. Dawson (2002) anasisitiza kuwa tafiti zinazotumia mkabala huu hujiegemeza zaidi katika kuchunguza tabia, hisia, na uzoefu. Kwa kurejelea mawazo hayo, utafiti uliofanyika ulichunguza silika na utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto, kwani silika hudhihirika kupitia mambo hayo.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Utafiti ulifanyika katika mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam. Mikoa hii iliteuliwa kama kiwakilishi cha mikoa mingine kwa jumla. Hata hivyo, kimahususi, Dodoma ilihusika kwa sababu ndipo walengwa wa utafiti wanapopatikana. Mathalani, kuna Chuo Kikuu cha Dodoma ambacho kinatoa Shahada za Awali katika Elimu ya Awali, Shahada ya Umahiri, na Shahada ya Uzamivu katika Kiswahili. Kwa hiyo, ilikuwa rahisi kwa mtafiti kupata watafitiwa na marejeleo muhimu kwa utafiti uliofanyika. Dar es Salaam ilihusika kwa sababu kuna Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho ni kikongwe, hivyo ilitarajiwa kupata wabobezi wa Fasihi ya watoto, pamoja na waandishi wa riwaya teule. Kwa mujibu wa Bakize (2018), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ndicho cha kwanza kuanzisha kozi ya Fasihi ya watoto na vijana (KF 203) ambayo inawawezesha wanafunzi kupata maarifa na mbinu za kuhakiki na kuchambua Fasihi ya watoto na vijana. Pia, mtafiti alitumia maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na makavazi ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) katika kusoma maandiko mbalimbali yaliyosaidia kupata mapengo ya utafiti. Sehemu nyingine iliyotumika ni kampuni ya uchapishaji ya E & D ambapo ndipo ilipo ofisi ya mwandishi mmojawapo wa riwaya teule, Bi. Elieshi Lema. Jambo hili linawekewa mkazo na Ponera (2019) anaposema kuwa eneo la utafiti huthibitishwa kwa upatikanaji wa watafitiwa na upatikanaji wa maktaba kwa ajili ya kupata nyaraka za kusomwa. Data zilizopatikana katika maeneo tajwa ni za msingi kwa kiasi kikubwa.

### 3.5 Walengwa wa Utafiti

Utafiti uliofanyika ulihusisha walengwa walio katika makundi mawili, wango na sampuli tafitiwa.

### 3.5.1 Wango Tafitiwa

Wango ni jumla ya watu au vitu vyote vinavyofaa kutafitiwa kadiri ya mwelekeo wa mada ya utafiti husika (Ponera, khj). Wango la utafiti uliofanyika limegawanyika katika makundi manne: riwaya za watoto, waandishi wa riwaya za watoto, wataalamu wa Fasihi ya watoto, wanafunzi wanaosoma Shahada ya Awali katika Kiswahili, Shahada ya Awali katika Fasihi ya Kiswahili na wanafunzi wanaosoma Shahada ya Awali ya Ualimu wa Elimu ya Awali. Makundi haya yaliteuliwa kwa kuamini kwamba yangetuwezesha kupata data ambazo zingekidhi haja ya malengo ya utafiti uliofanyika: riwaya za watoto zina wahusika watoto ambao wamechunguzwa silika na utendaji wao, waandishi wa riwaya hizo wana ujuzi kuhusu riwaya zao, wataalamu wa Fasihi ya watoto wamebobea katika uga huo, na hivyo, tuliamini kuwa wanajua mengi kuhusu Fasihi ya watoto. Kwa upande mwingine, wanafunzi waliteuliwa kwa sababu wanasoma fasihi ya Kiswahili na Saikolojia, hivyo tuliamini wana ujuzi wa wahusika na silika kwa ujumla.

### 3.5.2 Mbinu ya Usampulishaji

Usampulishaji ni kitendo cha kuteua sampuli ambayo itawakilisha watafitiwa wote wanaotarajiwa katika utafiti utakaofanyika (Creswell, 2009). Utafiti uliofanyika ulitumia mbinu za usampulishaji nasibu bahatishi kwa sampuli ya wanafunzi na usampulishaji lengwa wa kipekee kwa sampuli ya riwaya teule, waandishi wa riwaya teule, na wataalamu wa Fasihi ya watoto ili kupata data zilizotarajiwa. Usampulishaji nasibu ni aina ya usampulishaji ambao kila mshiriki katika kundi lengwa anakuwa na fursa sawa ya kuchaguliwa. Katika mbinu hii, wanafunzi walitakiwa kuhesabu namba, kisha wale wenye namba inayogawanyika kwa mbili waliteuliwa kuwa sampuli ya utafiti. Usampulishaji huu ulitumika kwa sababu sampuli ya wanafunzi ilikuwa kubwa, hivyo ilionekana haja ya kupata wawakilishi ambao walikuwa na fursa sawa ya kuchaguliwa na kutupa data tulizozihitaji. Usampulishaji lengwa ni aina ya usampulishaji ambapo mtafiti huteua sampuli kwa sababu ya kuwa na sifa za kipekee za kumpatia data (Kothari, 2004). Sababu za kutumia usampulishaji huu ni kutokana na sampuli lengwa kuwa na sifa zilizokidhi haja ya kupata data za utafiti. Hivyo, tulitumia aina hizi za usampulishaji ili kutupatia sampuli tuliyoihitaji.

### 3.5.3 Sampuli Iliyotumika

Sampuli ni viwakilishi ambavyo huteuliwa kutoka katika kundi kubwa la wango ili kutoa data ambazo zitawakilisha kundi zima (Robson, 2007). Hivyo, sampuli ya utafiti uliofanyika ni vitabu viwili (2) vya riwaya za watoto ambavyo ni *Ngoma ya Mianzi* (Mulokozi, 2018) na *Safari ya Prospa* (Lema, 2004). Waandishi hawa wameandika riwaya mbalimbali za watoto, lakini tulichagua riwaya mbili tu ili kukidhi malengo ya utafiti, ambapo data kuhusu silika na utendaji wa wahusika zilizingatiwa. Pamoja na hayo, tulichagua riwaya hizi kwa sababu ya uwakilishi sawa wa kijinsi, kwani kimoja kimeandikwa na mwanaume na kingine kimeandikwa na mwanamke. Pia, kila riwaya ina wahusika wakuu wawili, wa kike na wa kiume. Suala la jinsi limezingatiwa kwa sababu kila mwandishi ana tofauti katika uandishi wake kutokana na jinsia yake. Pia, utendaji hutofautiana kati ya mwanamke na mwanaume. Mulokozi (keshatajwa) anasisitiza suala la jinsia kwa kusema kuwa unapowaumba wahusika wako ni lazima uzingatie uwiano wa kijinsia, yaani wasiwe wanaume tu au wanawake tu, bali makundi yote mawili yaonekane katika kazi husika. Suala la jinsi limeshadidiwa pia na Matundura, Kobia, na Mukuthuria (2013) wanaposema kuwa kutumia vitabu vya waandishi wa jinsia tofauti kutaleta matokeo yasiyo na upendeleo. Sampuli hii ilipatikana kwa mbinu ya usampulishaji lengwa wa kipekee, kwa sababu sampuli lengwa ilikuwa na sifa za kipekee za kuchaguliwa. Pia, sampuli hii iliaminiwa kukidhi haja ya malengo ya utafiti uliofanyika.

Sampuli nyingine ni waandishi wawili wa riwaya zilizoteuliwa. Uhusika wao ulitokana na wingi wa maarifa waliyonayo kuhusu vitabu vyao. Hivyo, tulitaraji wangetueleza kwa undani juu ya wahusika na utendaji wao. Pia, wataalamu watatu wa Fasihi ya watoto ambao wamehakiki na kutafiti Fasihi ya watoto walihusika kutupatia data zilizohusiana na Fasihi ya watoto kwa jumla na wahusika kwa kuwa ni weledi katika uga huu. Kigezo kilichotumika ni wingi wa kazi zao zinazohusiana na uga huu. Sababu ya kuteua waandishi hawa ni uzoefu wao katika uandishi na utafiti katika uga huu. Hivyo, tuliamini kuwa wangekuwa na maarifa ya kutosha kuhusu wahusika na uhusika wao. Sampuli hizi pia zilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa wa kipekee.

Sampuli nyingine ni wanafunzi wanaosoma Shahada ya Awali katika Elimu ya Awali ambao wanasoma Saikolojia na Fasihi. Wanafunzi hawa tulitarajia watupatie

data za kutosha kuhusiana na silika na utendaji wa wahusika. Sampuli nyingine ilihusisha wanafunzi wanaosoma Shahada ya Awali katika Kiswahili ambao wanasoma Fasihi ya watoto kama kozi mojawapo na wanafunzi wa Shahada ya Awali katika Fasihi ya Kiswahili. Sampuli ya wanafunzi ilipatikana kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa, lakini kutokana na wingi wao, usampulishaji nasibu wa kubahatisha ulitumika, ambao ulitoa fursa sawa ya kutafitiwa kwa kila mtafitiwa. Mtafiti aliwaomba wanafunzi hao kuhesabu namba kadiri ya idadi yao. Kisha wale waliohesabu namba inayogawanyika kwa mbili walihusishwa katika mjadala. Kwa kuwa utafiti uliofanyika ni wa kitaamuli, sampuli haikuwa na idadi maalumu, bali kilichozingatiwa ni utoshelevu wa taarifa zilizopatikana.

### 3.6 Ukusanyaji wa Data

Kipengele hiki kinafafanua mbinu, zana, pamoja na mchakato mzima wa kukusanya data za utafiti uliofanyika.

#### 3.6.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data

Kothari (2004) anaeleza kuwa njia za kukusanyia data ni namna ya kukusanya taarifa zinazohitajika katika utafiti, ambazo hutumiwa katika kutolea matokeo ya jumla ya utafiti. Kwa kawaida, hakuna mbinu moja toshelevu; kwa hiyo, mtafiti anashauriwa kutumia mbinu zaidi ya moja ili kupata data toshelevu kwa ajili ya utafiti wake (Cohen, Manion na Marrison, 2000). Katika utafiti huu, njia zifuatazo zilitumika: Usaili, usomaji matini, na majadiliano ya vikundi lengwa.

##### 3.6.1.1 Njia ya Usaili

Usaili ni mazungumzo yanayoambatana na maswali anayoulizwa mtu na mtu mwingine au jopo maalumu lililoandaliwa ili kudadisi taarifa fulani zinazohitajika kwa kazi iliyokusudiwa (TATAKI, 2013). Mazungumzo yanaweza kufanyika ana kwa ana, au kwa kupitia simu (Kothari, 2004). Mazungumzo ni muhimu katika kupata mawazo mbalimbali na yanaweza kuwa yamepangwa rasmi au ya kushtukiza tu (Mbunda, 1993). Mbinu hii ilitumika kwa waandishi wa kazi teule ambao ni Mulokozi na Lema, na wataalamu mbalimbali ambao wamefanya tafiti zao katika uga wa Fasihi ya watoto ambao ni Bakize, Lyimo, na Shima. Kupitia njia hii, tulitarajia kupata data zinazohusiana na wahusika na utendaji wao ili kukamilisha lengo la kwanza la kufafanua namna mbalimbali za utendaji; na lengo la tatu

lililokusudia kutathimini uhusiano baina ya utendaji na sifa za silika. Njia hii ilichaguliwa kwa sababu humsaidia mtafiti kupata ufafanuzi wa ziada pale unapohitajika. Kutokana na ufafanuzi, watafitiwa hupata nafasi ya kujieleza kwa mapana, na hivyo, humsaidia mtafiti kupata taarifa nyingi zinazohitajika. Katika mchakato wa kukusanya data, watafitiwa walipata nafasi ya kufafanuliwa kile ambacho hawajakielewa. Pia, walipewa nafasi kueleza kwa undani kuhusu jambo husika. Katika mchakato huo, zana zilizotumika ni mwongozo wa usaili (kiambatisho Na. 1 a na b), simu kwa ajili ya kupanga miadi na kurekodia majibu ya watafitiwa waliofanyiwa usaili.

#### 3.6.1.2 Njia ya Usomaji Matini

Mbunda (khj) anabainisha kuwa mtafiti husoma kwa mapana na kufanya uchunguzi juu ya yale anayohitaji kuyatumia katika uhakiki wake. Usomaji matini humpa msomaji fursa ya kusoma andiko husika kwa utulivu na umakini, halafu akaweza kubaini data ambazo anazihitaji (Kombo na Tromp, 2006). Kwa mujibu wa Kothari (2004), mbinu ya usomaji matini ni nzuri na isiyopoteza muda katika ukusanyaji wa data. Mbinu hii ilitumika kusoma riwaya za *Ngoma ya Mianzi* na *Safari ya Prospa* ili kupata data za msingi. Data hizo zilihusu utendaji wa wahusika ambao ulisaidia kuzijua silika zao, kisha tulitathimini uhusiano wa vyote viwili. Pia, vitabu na tafiti tangulizi za saikolojia zilisomwa kwa ajili ya kupata maarifa ili kujaliza na kukamilisha utafiti huu. Vitabu na tafiti hizo zilihusu utendaji, Fasihi ya watoto, wahusika, na silika kwa jumla. Zana zilizotumika katika mchakato huo ni mwongozo wa usomaji (kiambatisho Na. 1 d), kompyuta mpakato, kijidaftari cha kuandikia na kalamu.

#### 3.6.1.3 Njia ya Majadiliano ya Vikundi Lengwa

Hii ni njia ambayo watafitiwa hutoa mitazamo yao katika masuala mbalimbali ambayo huongozwa na mada zilizoandaliwa na mtafiti (Creswell, 2007). Njia hii huhitaji idadi ya watu kadhaa ambao hutafitiwa kwa wakati mmoja, hivyo, huokoa muda, pamoja na gharama. Njia hii ilitumika kwa sampuli ya wanafunzi. Katika mbinu hii, tulitarajia kupata data kuhusu aina za silika na uhusiano wake na utendaji ili kufafanua namna mbalimbali za utendaji wa wahusika wakuu, kubainisha aina za silika; na kutathimini uhusiano baina ya utendaji na sifa za aina za silika. Mbinu hii ilisaidia kupata mitazamo tofauti ya watafitiwa kuhusiana na mada husika. Zana

iliyotumika katika mchakato huu ni mwongozo wa majadiliano wa vikundi lengwa (kiambatisho Na. 1 c).

### 3.6.2 Mchakato wa Kukusanya Data

Mchakato ulianzia maktabani kwa kusoma riwaya teule kwa muda wa mwezi mmoja. Hili lilitangulia, kwa sababu utafiti wetu ulikuwa ni wa maktabani kwa kiasi kikubwa. Huko, zilipatikana data za msingi na fuatizi zilizohusu utendaji wa wahusika ambao ulisaidia kubainisha aina za silika. Kisha, safari za kwenda uwandani zilifuata kwa ajili ya kupata data nyingine za msingi. Tulianza na usaili na waandishi wa vitabu teule kwa siku kumi. Kisha, ulifuata usaili na watafiti wa kazi za Fasihi ya watoto, uliofanyika kwa siku kumi na mbili. Kabla ya kufanya usaili, mtafiti alipiga simu kwa watafitiwa ili kupanga miadi. Alitambulisha shabaha ya utafiti wake na kukubaliwa. Siku ya usaili, mtafiti alifika kwa wakati sehemu ya miadi na kujitambulisha. Kisha, aliomba ridhaa ya watafitiwa ili awarekodi kwa ajili ya kutunza kumbukumbu. Baada ya kukubaliwa, zoezi la usaili lilianza. Mwisho, mtafiti aliwashukuru watafitiwa kwa kumpa ushirikiano.

Mchakato wa kukusanya data ulimalizikia kwa kufanywa kwa majadiliano ya vikundi lengwa kwa siku tatu. Mtafiti aliongoza majadiliano kwa kutumia mada zilizoandaliwa. Kila kikundi kilikuwa na wanafunzi watano ili kuongeza ufanisi katika majadiliano. Jumla, kulikuwa na vikundi viwili kwa kila sampuli iliyotumia mbinu hii. Pia, kila kikundi kilikuwa na kiongozi mmoja ambaye alikuwa na jukumu la kuchukua nukuu ya mambo yanayojadiliwa. Mtafiti alikuwa msimamizi wa majadiliano, ambapo alichokoza majadiliano, kisha waliendelea wenyewe. Ili kuzifanya nukuu ziwe na ufanisi, mtafiti alitumia simu ya mkononi kurekodi majadiliano hayo. Hili lilifanyika baada ya kuomba ridhaa yao na kuwaeleza umuhimu wa kila neno watakalolitamka. Majadiliano yalifanyika kwa kupishana dakika 15 kwa kila kikundi. Mara baada ya majadiliano kumalizika, data zilizorekodiwa zilihamishiwa katika kompyuta mpakato kwa ajili ya usalama na kumbukumbu ya baadaye. Pia, viongozi wa vikundi walitumia kalamu na karatasi kunukuu hoja za wanakikundi. Hivyo, mchakato wa uwandani ulifanyika kwa siku ishirini na tano.

### 3.7 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ni kitendo cha kupanga, kuchagua, kulinganisha, na kutolea maelezo data zilizokusanywa ili ziweze kujibu maswali ya utafiti yaliyokusudiwa (Young, 1949). Utafiti uliofanyika ulitumia mbinu ya mwegamo wa kimaudhui kwa sababu ni wa mkabala wa kitaamuli. Katika uchanganuzi wa data, hatua zifuatazo zilizingatiwa: mosi, data zote zilizokusanywa. Pili, tulioanisha mada kuu na mada ndogo zilizokusudiwa kutumika katika uchanganuzi wa data. Tatu, tulizipangilia data kwa kuziweka pamoja zinazofanana; na mwisho, tulizitolea maelezo data zilizokusanywa ili kujibu maswali ya utafiti. Kwa kutumia mwegamo wa kimaelezo, namna mbalimbali za utendaji wa wahusika wakuu zilifafanuliwa, aina mbalimbali za silika zilibainishwa, na uhusiano wa utendaji wa wahusika wakuu na sifa za aina za silika zao ulitathminiwa. Data zilipangwa kulingana na malengo matatu ya utafiti, kisha kutolewa maelezo ya kina. Hivyo, kila lengo limetumika kama sehemu ya mjadala. Data na matokeo ya utafiti uliofanyika, vimewasilishwa kwa njia ya maelezo, madondoo, na majedwali.

### 3.8 Maadili katika Utafiti

Mchakato wa utafiti ulifanyika kwa kuzingatia maadili ya utafiti kwa mtafiti kufuata kanuni za maadili zilizopendekezwa na Chuo Kikuu cha Dodoma, pamoja na tafiti zote kwa jumla. Ponera (2014) anafafanua kuwa maadili ya utafiti hujengwa na masuala kama vile uombaji wa ridhaa ya watafitiwa, utunzaji wa siri za taarifa, na ufichwaji wa majina ya watoa taarifa kadiri ya matakwa ya watafitiwa. Katika utafiti uliofanyika, maadili yalizingatiwa ikiwa ni pamoja na kuomba barua ya utambulisho wakati wa kwenda kukusanya data za uwandani. Pia, kupanga miadi na waandishi wa riwaya teule kwa ajili ya kuzungumzia riwaya zao na mada ya utafiti kwa jumla. Maadili mengine ni pamoja na mtafiti kutohusisha hisia zake na mtazamo wake juu ya matokeo ya utafiti na aliwasilisha yale tu ambayo aliyapata katika mchakato mzima wa kukusanya data.

### 3.9 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uhalali wa matokeo ya utafiti ni namna ya kuyafanya matokeo ya utafiti yawe na vigezo vinavyopima mambo yaliyotakiwa kupimwa katika utafiti huo. Uthabiti wa utafiti ni namna utafiti unavyoweza kutoa matokeo yanayofanana na tafiti nyingine za baadaye zinazolingana nao. Uthabiti hupatikana hata kama utafiti kama huo

utafanywa sehemu nyingine, na mtu mwingine, na hata kwa kutumia njia nyingine za kukusanyia data. Matokeo yake yatakuwa na uwiano sawa na utafiti uliotangulia. Uhalali na uthabiti ni vipengele vinavyohusiana na kutoshelezana katika utafiti; na hivyo, ni vigumu kuwa na utafiti wenye matokeo yaliyo thabiti, lakini yasiwe na uhalali (Kothari, 2009). Kutokana na uhalali na uthabiti, matokeo yanakuwa ni ya kuaminika.

Kwa mujibu wa Ponera (2010), uhalali wa matokeo ya utafiti huthibitishwa kwa mambo yafuatayo: Kwanza, kupitia kuyabainisha malengo ya utafiti, pamoja na mipaka yake. Pili, kupitia matumizi mazuri ya njia za kukusanyia data zinazotoa matokeo ya utafiti kwa kiwango cha uthabiti kinachoridhisha. Tatu, kupitia matumizi ya lugha nyepesi na rahisi kufahamika kwa watafitiwa juu ya kinachotafitiwa ili kupata majibu yanayolingana na malengo ya utafiti husika. Hivyo basi, utafiti ulifanyika kwa kuegemea katika misingi hii ili kuweza kujenga uhalali na uthabiti wa matokeo yake. Uthabiti uliongezwa na matumizi ya mbinu zaidi ya moja za kukusanyia data zilizozalisha data za kina, thabiti, na halali. Kwa msingi huo, matokeo ya utafiti uliofanyika yanaaminika kuwa thabiti na halali.

### 3.10 Changamoto za Utafiti na Utatuzi Wake

Katika mchakato mzima wa kufanya utafiti uliohusu uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili, changamoto zifuatazo zilijitokeza:

Mosi, kuibuka kwa janga la UVIKO 19. Wakati mtafiti yupo katika hatua ya kukusanya data, Serikali ya Tanzania ilitoa tamko la kufungwa kwa asasi zote za elimu kuanzia tarehe 17/03/2020 hadi ilipotangazwa tena kufunguliwa tarehe 01/06/2020. Kutokana na tamko hilo, zoezi la kukusanya data kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lilisimama kwa muda. Hata hivyo, baada ya vyuo kufunguliwa, ratiba ya kuonana na wanafunzi ilikuwa ngumu kutokana na kubinywa na ratiba zao zilizokusudia kufidia muda uliopotea wa masomo. Changamoto hii ilitatuliwa na mtafiti kwa kuomba kuonana nao katika siku za mwisho wa juma ambapo huwa na ratiba binafsi. Pia, katika mjadala, tahadhari muhimu za kukabiliana na janga hili zilichukuliwa, ikiwa ni pamoja na kunawa mikono na kukaa kwa umbali usiopungua mita moja.

Pili, uhaba wa fedha za kuendeshea utafiti. Hii ilitokana na uhamisho alioupata mtafiti na kupelekwa kituo kingine cha kazi. Kwa kuwa mtafiti alikoma kuwa mtumishi wa asasi ya awali, asasi hiyo ilijitoa katika udhamini. Zaidi ya hayo, mwajiri mpya hakuwa na fungu la kudhamini wafanyakazi walio katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu. Hali hiyo ilisababisha mchakato wa utafiti uliokuwa katika hatua ya pendekezo, kusuasua. Kikwazo hiki kilitatuliwa na mtafiti kwa kutumia vyanzo vyake binafsi.

## 3.11 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii imefafanua methodolojia ya utafiti. Vipengele vya methodolojia vilivyofafanuliwa ni usanifu wa utafiti, mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, na ukusanyaji data. Vipengele vingine ni uchanganuzi na uwasilishaji wa data, maadili ya utafiti, na changamoto za utafiti.

Sura inayofuata inawasilisha data zilizopatikana katika utafiti uliofanyika, pamoja na kujadili matokeo ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha na kujadili data zilizopatikana katika utafiti uliofanyika. Kabla ya kuwasilisha na kujadili data hizo, imeonekana haja ya kuzijua riwaya teule kwa ufupi ili kuleta muwala na kufanya tasinifu hii ieleweke kwa wasomaji. Sura hii ina sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza inatoa utangulizi wa sura na kueleza muhtasari wa riwaya teule. Sehemu ya pili inajadili utendaji wa wahusika wakuu katika riwaya teule. Sehemu ya tatu inachambua aina za silika kwa jumla, pamoja na makundi ya silika hizo. Kisha, inabainisha aina za silika za wahusika wakuu katika riwaya teule. Sehemu ya nne inaonesha uhusiano uliopo baina ya utendaji wa wahusika wakuu na sifa za aina za silika zao. Sehemu ya tano, inatoa muhtasari wa sura yote ya nne. Sehemu ya pili hadi ya nne zinahusu mada zinazoendana na malengo ya utafiti. Sehemu hizi zimepangwa kulingana na malengo na maswali ya utafiti uliofanyika ili kuleta muwala na kufanya matokeo ya utafiti kueleweka kwa msomaji wa tasinifu hii.

### 4.1.1 Muhtasari wa Riwaya Teule

Kama ilivyobainishwa katika sura zilizotangulia, utafiti uliozaa tasinifu hii ulitumia riwaya mbili za watoto ambazo ni *Ngoma ya Mianzi* na *Safari ya Prospa*. Kwa kuwa data za utafiti huu, kwa kiasi kikubwa, zilitoka katika riwaya hizo, imeonekana haja ya kueleza kwa ufupi yale yaliyomo katika riwaya hizo ili kuleta muwala na kufanya tasinifu hii ieleweke. Pia, kuwajua wahusika wake wakuu ambao watahusika katika mjadala kwa kiasi kikubwa. Muhtasari huo unabainishwa kama ifuatavyo:

#### 4.1.1.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Ngoma ya Mianzi*

*Ngoma ya Mianzi* imeandikwa na Mulokozi ambaye ni Profesa mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na ni mwandishi wa riwaya za vijana, tamthiliya, na mashairi. Pia, ni mwalimu na mwanazuoni aliyebobea katika taaluma ya historia na Fasihi ya Kiswahili. Riwaya hii ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1991 na *Tanzania Publishing House*, Dar es Salaam; na kisha, chapa hii ya mwaka 2018, mchapishaji akiwa ni KAUTTU, Dar es Salaam. Ni riwaya ya kihistoria ya mapambano ya Wahehe na Wasagara dhidi ya Wadachi mnamo mwaka 1891. Riwaya hii ni muendelezo wa masimulizi ya masaibu ya Mbumi na Chulu baada ya

kurejea kwao kutoka Bagamoyo walikokwenda kuwatafuta wazazi wao waliotekwa na kupelekwa pwani, utumwani. Vijana hawa ni mapacha wenye umri wa miaka kumi na sita. Safari hii, Mbumi na Chulu hawaendi Bagamoyo, bali wanakwenda Iringa kupeleka ujumbe wa siri wa mbiu ya mapambano kwa Mutwa Mukwava (Mkwawa) baada ya Wadachi kuivamia Usagara na kuanza kuinyemelea Uhehe (Mulokozi, 2018). Lengo kuu lilikuwa Wahehe na Wasagara washirikiane kupinga ukoloni. Katika safari yao, walikumbana na masaibu mengi, ikiwa ni pamoja na kutembea umbali mrefu usiku na mchana, kuvuka mito, milima na mabonde, na kushuhudia vifo vya ndugu zao na vya Wadachi, ambao waliwavamia Wasagara. Pia, walifanikiwa kumuua Nyundo, Jemedari wa Wadachi. Hatimaye, wanafanikiwa kuwasilisha ujumbe wao wa haraka kwa Mutwa na kutangazwa kuwa mashujaa. Katika riwaya hii, mwandishi amewapa majukumu sawa mtoto wa kike na wa kiume na kuachana na kasumba ya waandishi wengi wanaomtweza mtoto wa kike na kumkweza wa kiume.

Mulokozi (khj) anasema kuwa lengo kuu la kuandika riwaya hii lilikuwa ni mpango wa kuandika riwaya za kihistoria ulioratibiwa na Bi. Elieshi Lema, wakati huo akiwa ni mmojawapo wa wahariri katika kampuni ya TPH, miaka ya themanini. Waandishi mbalimbali waliteuliwa, akiwemo yeye mwenyewe, hayati Euphrase Kezilahabi, Richard Mabala, Elieshi Lema, na Amandina Lihamba. Waandishi hawa walikusanywa ili washirikiane kuandika mfululizo wa vitabu vya riwaya za kihistoria ambao uligharamiwa na Shirika la Maendeleo ya Elimu la Canada (CODE). Shirika hili lilisimamia uandishi na uchapishaji wa riwaya hizo, kisha kuzisambaza katika shuke zilizokuwa katika mradi.

Katika kuandika vitabu vya kihistoria, Mulokozi alisema kuwa waligawana kazi kwa kuangalia historia ya Tanzania kwa kuanzia biashara ya watumwa mwishoni mwa karne ya 19, vita vya kupinga ukoloni, na vita vya majimaji. Hivyo, walipeana kazi kama ifuatavyo: mambo ya utumwa alikuwa aandike Amandina, yeye Mulokozi alipewa kazi ya kuandika juu ya upinzani dhidi ya ukoloni, Mabala naye juu ya upinzani, lakini ajielekeze Uchagani kwa akina Mangi, na Kezilahabi alielekezwa kwenye vita vya majimaji. Kazi hii ilipoanza, Amandina aliandika *Wimbo wa Sokomoko* ambayo mandhari yake ilikuwa Kwailosa (sasa Kilosa) ambapo watu walikuwa wanatekwa na kupelekwa pwani, utumwani. Katika utekaji huo, mama yao

Mbumi na Chulu alikuwa ametekwa. Hivyo, walianza kumtafuta Bagamoyo, bila mafanikio. Kwa hiyo, Mulokozi alianzia hapo kwa kuwatumia wahusika haohao, ambapo Mundewa (chifu wa Kwailosa) aliwapa ujumbe watoto hao wapeleke kwa Mukwava. Ndipo hadithi ilipoanzia. Lengo kuu lilikuwa Wahehe na Wasagara washirikiane kupinga ukoloni. Mulokozi anasema kuwa riwaya zake ziliandikwa kwa ajili ya vijana kuanzia miaka 13-20, ambao kwa sasa wanaitwa vijalunga (*adolescents*).[2] Umri unaoshughulikiwa katika utafiti huu umo ndani ya umri alioutaja Mulokozi, yaani miaka 15-18.

Riwaya hii ina wahusika wakuu wawili, wa kike na wa kiume. Wahusika hawa ni ndugu, mapacha, ambao wanasafiri kupeleka ujumbe wa siri wa mbiu ya mapambano baada ya Wadachi kuivamia Usagara na kuanza kuinyemelea Uhehe. Mwandishi amewavika uhusika wa kihistoria katika mapambano dhidi ya wakoloni wa Kidachi. Utafiti umebaini kuwa mwandishi amewaumba wahusika wake kwa kuzingatia zaidi mazingira yao, yanayosababisha watende kutokana na misukumo ya kijamii na kiutamaduni inavyoingiliana, na kusababisha kijana alazimike kuwa shujaa hata kama hajafikia umri wa utu uzima. Yote haya yanatokana na muktadha fulani wa kihistoria. Wahusika hao ni hawa wafuatao:

Mhusika wa kwanza ni Mbumi. Huyu ni binti mwenye umri wa miaka kumi na sita, Mwanasokomoko aliyetumwa kuipigania jamii ya Wasagara dhidi ya wakoloni wa Kidachi. Ana uwezo mkubwa kiakili na, mara nyingi, huwaongoza wengine kwa ushauri ambao huzaa matunda chanya. Binti huyu, pamoja na kaka yake, walifanikiwa kupeleka ujumbe wa siri wa mbiu ya mapambano baada ya Wadachi kuivamia Usagara na kuanza kuinyemelea Uhehe. Ni binti jasiri sana ambaye matendo yake hayaendani na umri wake. Kutokana na umri wake, hata maadui walipomwona hawakudhani angeweza kuwa na madhara.

Mhusika wa pili ni Chulu. Huyu ni pacha wa Mbumi ambaye ana umri wa miaka kumi na sita. Mhusika huyu alishirikiana na dada yake katika kila hatua baada ya kutumwa kupeleka mbiu ya siri ya mapambano dhidi ya Wadachi. Ni kijana mwenye

---

[2] Mahojiano kati ya mtafiti na Mulokozi yaliyofanyika katika iliyokuwa ofisi ya Mulokozi katika jengo la TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mnamo tarehe 10/02/2020. Mulokozi alikuwa Mhadhiri Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mwandishi wa kazi mbalimbali za Fasihi na tahakiki.

huruma, lakini ni hatari akutanapo na adui. Mara nyingi humtii dada yake, licha ya tofauti zao za kijinsia. Wakati mwingine, anakuwa na mfumo dume, hasa katika mazingira ambayo mwanamke haruhusiwi kufanya jambo fulani. Kwa mfano, walipokuwa safarini baada ya giza kuingia waliamua kupumzika, ilibidi walale kwa zamu kwa ajili ya usalama. Ilipofika zamu ya Chulu kulala, alilala na mkuki wake mkononi, kwa sababu aliamini kuwa wanawake hawaruhusiwi kuushika mkuki huo (uk. 32). Huu ni mfumo dume, kwani, hakuna madhara yoyote kwa mwanamke kushika mkuki, hasa katika hali ya mapambano. Hata hivyo, utafiti umebaini kuwa baada ya kuona ujasiri wa Mbumi, Chulu hatimaye alikubali kumpa mkuki. Mwandishi anafafanua hili katika ukurasa wa 106 anaposema, "Chulu alimpa Mbumi mkuki kimyakimya. Mbumi aliupokea Mkuki-wa-Mianzi[3] kwa mshangao kidogo, lakini hakusema neno."

Pamoja na riwaya hii, Mulokozi pia ameandika kazi nyingine za kifasihi ambazo ni *Mashairi ya Kisasa* (pamoja na K. K. Kahigi) (1973), *Malenga wa Bara* (pamoja na K. K. Kahigi) (1976), *Mukwava wa Uhehe* (1979), *Utenzi wa Nyakiiru Kibi* (1997), *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (pamoja na K. K. Kahigi) (1982), *Ngome ya Mianzi* (1992), na *Moto wa Mianzi* (1996).

#### 4.1.1.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Safari ya Prospa*

Riwaya ya *Safari ya Prospa* imeandikwa na Elieshi Lema ambaye ni mmiliki mwenza wa kampuni ya uchapishaji ya *E & D Limited*. Lema ni mwandishi wa mashairi, riwaya, na Fasihi ya watoto. Riwaya hii ilipigwa chapa na *Book Printing Services Ltd* ya Mauritius mwaka 1995. Riwaya hii ilitolewa tena mwaka 1997, 2001 na 2004. *Safari ya Prospa* inahusu kutoweka kwa Merisho, mtoto mwenye umri wa miaka minne, mpwa wa Prospa na mtoto wa pekee wa mwalimu Josefina. Merisho anapotea katika mazingira ya kutatanisha sana. Prospa anaamua kutoa taarifa katika kituo cha polisi ili wamsaidie katika kumpata mpwa wake. Juhudi zote za mama yake na polisi zinagonga mwamba. Kwa hiyo, Prospa anajitosa kwenye ulimwengu wa upelelezi na kuamua kwenda kumtafuta Merisho. Katika safari yake,

[3] Aina ya mkuki ambao ni chuma kitupu, bamba na mpini ambao Mukwava aliupokea kutoka kwa baba yake Munyigumba, na Munyigumba aliupokea kutoka kwa baba yake Kilonge wakati huo ukiitwa Lisala. Inasemekana kuwa mkuki huo Mukwava aliutumia kuwashinda Waarabu, wateka utumwa ambao walikuwa wakitumia mianzi inayotema moto, hivyo ukapewa jina hilo.

anaongozana na Sara aliyekutana naye Same na kujitolea kumsaidia. Safari yao inakumbwa na vikwazo vingi, lakini hawakati tamaa.

Watoto hawa wanaingia katika jiji la Dar es Salaam wakiwa hawajui lolote kuhusu jiji hilo. Katika mizunguko yao, wanakutana na Petro (kaka yake Prospa) na kumwelezea sababu ya ujio wao. Ijapokuwa Petro hafurahii ujio wao, lakini anawasaidia mahali pa kulala na kuwawezesha kufika Zanzibar kumtafuta Merisho. Huko, hawafanikiwi na kuamua kurudi Dar es Salaam wanapokutana na changudoa na kuanza maisha mapya ya mitaani. Watoto hawa wanaishi maisha ya kuombaomba na kufanya vibarua ili kukidhi mahitaji yao ya kila siku. Baada ya mizunguko mingi, wanakutana na Feliksi, mjomba wake Prospa, ambaye anawapeleka nyumbani kwake na kukutana na Uzuri, mfanyakazi wa ndani wa Feliksi. Watoto hawa wanajenga urafiki na Uzuri kwa kupitia Sara. Uzuri anafunguka mambo mengi ambayo yanasaidia kujulikana mahali alipo Merisho, ambapo, hatimaye, wanafanikiwa kumpata akiwa salama nyumbani kwa mzee Mchau.

Kila mwandishi huwa na shabaha yake anapoandika kazi ya Fasihi. Kwa upande wa Lema, alizama katika jamii na kuangalia shida wanazozipata watoto, na kisha kuwaonesha wanajamii kuwa watoto wadogo wana uwezo mkubwa kiakili. Pia, anaonesha mgongano wa kijamii kuhusu uzazi wa watoto wa jinsia moja, jambo ambalo watu wengi hawalikubali. Kwa hiyo, kutokana na mgongano huo, ndiyo sababu Merisho aliibwa na yule mama ili ampelekee mtoto wake ambaye alikuwa na watoto wa kike tu.[4]

Riwaya hii ina wahusika wakuu wawili: Prospa na Sara. Prospa ni mtoto mwenye umri wa miaka kumi na miwili ambaye anaishi na dada yake, Josefina, katika kota namba tatu za wakata miwa za TPC - Moshi. Anasoma katika shule ya msingi TPC. Prospa alipendelea kucheza mpira na watoto wenzake katika kiwanja cha gofu cha TPC. Ana uwezo mkubwa kiakili na mara nyingi aanzapo jambo halikatishi hadi alimalize. Prospa alikosa imani na askari polisi na kuamua kuanza kumtafuta Merisho, mtoto wa dada yake, ambaye alipotea wakati yeye akicheza mpira na wenzake. Mwandishi anasema:

[4] Mahojiano kati ya mtafiti na Bi. Lema yalifanyika katika ofisi yake iliyopo katika kampuni ya uchapishaji ya E & D, Africa-sana, jijini Dar es Salaam mnamo tarehe 17/02/2020.

> “Prospa aliondoka kituoni akiwa hana raha. Merisho alikuwa bado hajapatikana. Askari alikuwa anauliza maswali tu. Atauliza maswali mpaka lini? ... Prospa alikata shauri kufanya uchunguzi wake mwenyewe utakaokuwa na matendo kuliko askari” (uk. 15).

Hivyo, aliamua kufunga safari kutoka Moshi kuelekea Dar es Salaam. Katika safari yake, alikumbana na vikwazo mbalimbali, akavivuka na kufika mwisho wa safari yake. Hatimaye, alifanikiwa kumpata Merisho kwa kusaidiana na Sara na watoto wengine wa mtaani aliokutana nao Dar es Salaam.

Prospa ni kijana mwenye upendo mkubwa kwa watu. Mwandishi ameudhihirisha upendo wa Prospa kwa kupitia Merisho ambaye alipotea. Prospa alikosa raha kabisa tangu alipogundua kuwa Merisho ametoweka nyumbani na alimhurumia sana dada yake. Katika ukurasa wa 15 mwandishi anasema kuwa baada ya Prospa kumsikia Josefina akilia chumbani, alijisikia uchungu na kujiona mwenye hatia. Hii ni kwa sababu kama asiingeenda kucheza mpira uwanjani, Merisho asingeibwa. Pia, Prospa alionesha upendo kwa Sara, kwani hata alipokuwa mbali naye alikuwa akimuwaza. Kwa mfano, baada ya kupewa chai na kuanza kunywa yeye na marafiki zake, alimuwaza Sara kama naye amepata chai, lakini mwenzake mmoja alisema kuwa aachane naye. Hivyo, Prospa aliweka maandazi mawili kwenye kila mfuko wa kaptula yake, halafu aliendelea kula (uk.119-120).

Mhusika wa pili ni Sara. Huyu ni binti wa rika sawa na Prospa ambaye alikutana na Prospa na kumuomba waende naye Dar es Salaam kumtafuta Merisho. Anakuwa msaada mkubwa sana katika safari ya Prospa kutokana na ujasiri wake. Ni binti mcheshi na mwepesi kumzoea mtu kwa haraka. Kwa muonekano wake wa nje, alikuwa na jicho ambalo mtu akimuangalia lilitisha sana. Kwa mujibu wa Aiello (2015), Sara ni msichana mpweke aliyebaguliwa kwa sababu ya jeraha baya katika jicho lake. Katika ukurasa wa 48, mwandishi anasema:

> Prospa hakujibu, aliendelea kustaajabia msichana ambaye jicho lake la kushoto lilikuwa bovu. Mboni ya jicho ilionekana kama iliyotoboka, ikapoteza rangi yake na kupata weupe kama maziwa. Isitoshe, jicho hilo lilikuwa kubwa kuliko la kulia.

Mwandishi ameelezea jinsi Prospa alivyostaajabishwa na jicho la Sara. Pia, kutokana na mambo yake, Prospa alimwona kama mchawi, mwandishi anaeleza kuwa:

> Prospa aliduwaa. “Msichana huyu ni mchawi, au ni mtoto wa mchawi.” Prospa aliwaza,“Sura yake inatisha, lakini yeye mwenyewe hatishi” (uk. 49).

Sara alisaidia Merisho kupatikana kutokana na udadisi wake, ucheshi, na ujengaji wa urafiki na watu. Mwandishi anasawiri namna Sara alivyojenga urafiki na Uzuri na kupata habari ambazo alizihitaji, zilizosaidia Merisho kupatikana. Ukiacha kazi hii, kazi nyingine za Lema ni pamoja na:*Parched Earth* (2001), *In the Belly of Dar es Salaam* (2011), *Mwendo* (1998), Upendo’s Dream (2004), *Cousin Lusu*: *A Graded Reader for Class Four* (2011) na *The man from Tanga: A Reader on HIV/AIDS for Standard Four* (2007).

**4.2 Utendaji wa Wahusika Wakuu wa Fasihi ya Watoto katika Riwaya Teule**

Sehemu hii imelenga kufafanua utendaji wa wahusika wakuu. Hoja yetu hapa ni kuthibitisha namna utendaji unavyoweza kudhihirishwa kwa mitindo mbalimbali ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Kama tulivyofafanua katika sura zilizotangulia, utendaji ni uwasilishaji wa tukio kwa lugha ya mazungumzo baina ya wahusika na masimulizi ya mwandishi yanayokwenda sambamba na mazungumzo hayo. Sehemu hii inaundwa na vijisehemu nane ambavyo vimetoka katika Riwaya ya *Safari ya Prospa* na *Ngoma ya Mianzi*: Utendaji kwa mtindo wa kuhoji, kushawishi, kuonya, kudadisi, kudanganya, kutaarifu, kushauri na hitimisho. Kama ilivyodokezwa katika sura zilizotangulia, kwa kiasi kikubwa, utendaji umekuwa ukijadiliwa katika tamthiliya na Fasihi simulizi. Hata hivyo, katika sehemu hii tunajadili utendaji katika riwaya teule za Fasihi ya watoto.

Wahusika hutenda kulingana na tukio linalowasilishwa, ambalo linaweza kuwa la furaha au la kusikitisha. Matendo huakisi aliwazalo mwandishi katika kazi ya Fasihi. Mlacha (1982) anabainisha kuwa, kwa kuwa wahusika ni watu halisi, matendo yao yanamwathiri msomaji moja kwa moja. Kwa kuyaangalia matendo hayo, mtu anaweza kujihusisha moja kwa moja na kujikuta yupo katika mazingira yake. Kutokana na mawazo ya Mlacha (khj), utendaji ndio unaosukuma mbele hadithi yoyote ile. Katika utafiti uliozalisha tasinifu hii, utendaji umefafanuliwa kwa kutumia mazungumzo baina ya wahusika wakuu wenyewe kwa wenyewe au wahusika wakuu na watu wengine ambao wamejitokeza katika masimulizi. Waandishi wengi hutumia lugha ya mazungumzo ili wasimchoshe msomaji ambaye,

kwa muktadha wa tasinifu hii, ni mtoto wa miaka kumi na mitano hadi kumi na minane. Lugha ya mjazo mara nyingi humchosha mtoto, lakini inapowekwa lugha ya mazungumzo, anakuwa miongoni mwa wahusika wa hadithi inayosimuliwa. Msokile (1993) anafafanua kuwa mazungumzo ya wahusika katika hadithi fupi hujaribu kuiga hali halisi ya maisha kimazungumzo kama ilivyo katika jamii. Kwa maana hiyo, hapa tunafafanua ni kwa namna gani utendaji huu unajitokeza katika riwaya teule za Fasihi ya watoto ya Kiswahili:

Utendaji katika riwaya hizi, kwa kiasi kikubwa, umeoneshwa kwa kutumia wahusika wake wakuu, Prospa na Sara katika *Safari ya Prospa*, na Mbumi na Chulu katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi*. Mwandishi amewapa namna mbalimbali za lugha ya mazungumzo wao kwa wao na, wakati mwingine, wao na wahusika wengine. Pia, ametumia masimulizi kuonesha matendo mbalimbali kama vile kuacha kucheza, kukimbia, kwenda, kuendelea, na kutembea. Masimulizi yanayotumika katika mjadala huu ni yale tu yanayoambatana na mazungumzo ya wahusika ili kufikia malengo ya utafiti huu. Utendaji katika riwaya hizi umebainika kupitia mitindo ya kuhoji, kushawishi, kuonya, kudadisi, kudanganya, kutaarifu, na kushauri kama ifuatavyo:

### 4.2.1 Utendaji wa Kuhoji

Utafiti umebaini kuwa utendaji unaweza kudhihirishwa kwa mtindo wa kuhoji. Katika mazungumzo hayo, kunakuwa na kusemezana kwa wahusika kwa kupokezana kama inavyojitokeza katika tamthiliya. Wahusika hwuliza au huulizwa maswali mbalimbali ili kupata taarifa ambazo zinaweza kuwasaidia katika 41aisha yao kama yalivyoumbwa na mwandishi. Maswali hayo huulizwa na wahusika wenyewe au watu wanaowazunguka. Mathalani, katika *Safari ya Prospa*, baada ya Prospa kuhisi kuwa Merisho anamwita, aliendelea kucheza mpira kwa muda, lakini baadaye aliacha na kwenda kumuangalia. Alipofika nyumbani, aliangalia kila mahali bila mafanikio. Jambo hili lilimpa wasiwasi, ikabidi awafuate watoto waliokuwa nje kwenye uwanja wakicheza ili ajaribu kuwahoji kama walimwona Merisho. Mahojiano yao yalikuwa kama ifuatavyo:

> "Merisho yuko wapi? Mmeshamuona Merisho?" Moyo ulikuwa ukimpiga kwa nguvu kifuani.
> Mtoto mmoja alimjibu, "Merisho alikufuata uwanjani."
> "Lini? Alifuata wapi?" Prospa aliuliza.
> "Uwanjani ulipokuwa unacheza mpira," Mtoto mwingine alisema bila kumtazama Prospa.
> "Mbona sikumwona?" Prospa alijiuliza. Alimwendea yule mtoto aliyemjibu bila kumtazama, akamshika shati na kumtikisa ili amsikilize vizuri. "Hebu niambie vizuri bwana," Prospa alimkazania. Mtoto huyo jina lake Mustafa alisimama, akamtazama Prospa, akasema, "Usinirarurie shati yangu." Alikaa tena akaendelea na shughuli yake ya kuunda gari ya bati na matairi yake ambayo alikata kutoka soli ya ndala iliyochakaa. "Mustafa niambie. Niambie basi," Prospa alimbembeleza.
> "Kamtafute uwanjani huko," Mustafa alisema… (uk. 3-4).

Kupitia dondoo hili, ni dhahiri kuwa Prospa alimhoji Mustafa ili kupata ukweli wa mahali alipokwenda Merisho. Kutokana na nafsi za Nadharia ya Saikochanganuzi, Prospa aliongozwa na nafsi ya kiwango cha kati inayoongoza maamuzi ya busara. Prospa aliona ni busara kumhoji Mustafa ili amfahamu mtu aliyemchukua Merisho. Mtafiti anaamini kuwa kutokana na kukosa mbinu nzuri ya mahojiano, Prospa alishindwa kupata taarifa alizozitaka, kwani alimtia hasira Mustafa akashindwa kutoa ushirikiano. Baada ya kuona hivyo, ilibidi atumie mbinu ya kubembeleza, lakini nayo haikufua dafu, kwani tayari Mustafa alikuwa ameshakasirika.

Mahojiano mengine yalikuwa baina ya Petro (kaka yake Prospa) na Prospa baada ya kukutana Manzese, jijini Dar es Salaam. Prospa alishangaa sana kumwona kaka yake. Alikuwa hajachana nywele, suruali yake ilikuwa chafu, shati lake la rangi ya buluu halikuwa limefungwa kifungo hata kimoja, na raba alizovaa miguuni zilikuwa zimechakaa. Petro naye alikuwa anamshangaa Prospa kafikaje jijini Dar es Salaam. Kwa hiyo, walikuwa wanashangaana. Hata hivyo, Prospa hakushangaa sana, kwani tangu anatoka Moshi alikuwa anafahamu kuwa kaka yake anaishi Dar es Salaam, sehemu inayoitwa Manzese. Baada ya kukutana, mazungumzo yao yalikuwa hivi:

> "Kaka Petro!" Prospa alimaka, "Sijakutambua!"
> "Mezea basi," Petro alisema. "Unafanya nini Dar?"
> "Tumefika sasa hivi. Kwa basi. Lo! Jamani, siamini bahati hii! Nilikuwa nataka kuulizia unakoishi. Nimekuja kumtafuta Merisho." Prospa alisema kila kitu kwa haraka, akiwa amefurahi sana.
> "He, unakuja kuulizia mtu jijini hapa? Unafikiria huku ni Kiboroloni?" Petro alisema, huku akiangalia huku na kule.

> Prospa alimtazama kaka Petro kwa mshangao, kama bado hajaamini kwamba macho yake yanamwambia kweli.
> "Habari za Moshi?" Petro aliuliza.
> Akili ya Prospa ilikuwa imetekwa nyara na habari za kupotea kwa Merisho, kwa hiyo alijibu, "Aliibwa, nimekuja huku kumtafuta."
> "Kumtafuta nani? Mimi?" Petro aliuliza akiwa anacheka.
> "Merisho. Merisho alipotea, yaani aliibwa kutoka nyumbani kule TPC." Prospa alijibu.
> "Aa ndiyo. Nilisoma gazeti la uhuru wasingeandika jina la Ringo, nisingeamini," Petro alisema. "Mpaka sasa hajapatikana tu."
> "Kumbe habari zilipelekwa gazetini?" Prospa alishangaa… (uk. 58-59).

Utafiti umebaini kuwa katika mazungumzo ya hapo juu, Petro alihoji ili kujua sababu ya Prospa kwenda Dar es Salaam. Pia, alishangazwa na Prospa alipomwambia kuwa alitaka amuulizie, kwani ni nadra mtu kumuulizia mtu mwingine katika jiji kubwa kama Dar es Salaam, lenye pilika na watu wengi. Kwa mujibu wa Nadharia ya Saikochanganuzi, nafsi ya Prospa iliakisi michakato aliyokuwa nayo akilini mwake kutokana na namna alivyoongea. Alionesha uchungu sana na kujihisi kuwa na hatia kuhusu kupotea kwa Merisho, kwani kama asingekwenda kucheza, Merisho asingepotea. Lema (keshatajwa) anasema kuwa:

> Prospa alimwambia Petro alitaka kumuulizia kwa kuwa alikuwa halijui jiji. Kwa kuwa Prospa alifika Dar es Salaam kwa mara ya kwanza alikuwa anawaza kuhusu sehemu ya kufikia. Hata hivyo, pamoja na kuwa alimshangaa kaka yake kutokana na alivyovaa, lakini alikuwa na hofu iliyochanganyika na matumaini. Matumaini yake ilikuwa ni kupata hifadhi kwa kaka yake.

Dondoo hilo linadokeza furaha aliyoipata Prospa baada ya kukutana na kaka yake. Katika mazingira ya kawaida, mtu yeyote angefurahia, kwa sababu sehemu ya ugenini kama huna mwenyeji na pesa, hofu huongezeka maradufu.

Utendaji wa mahojiano pia umetumika baina ya mjomba Feliksi na Prospa. Baada ya mahangaiko ya muda mrefu ndani ya jiji la Dar es Salaam, Prospa na wenzake walifanikiwa kumwona mjomba ambaye walikuwa wanamtafuta. Kilichowasaidia ni rangi ya gari pamoja na mguu wake ambao anapotembea huwa anauvuta. Walipomwona, wenzake walimwambia Prospa amfuate na kujitambulisha. Utafiti umebaini kuwa kutokana na msingi wa pili wa Nadharia ya Saikochanganuzi ni dhahiri kuwa matamanio ya Prospa ya kutaka kumwona mjomba wake yalitimizwa.

Pia, alipata mwanga mpya katika kumtafuta Merisho. Mjomba alihoji kutaka kujua kwanini wanamtafuta. Mwandishi anasema:

> Prospa aliendelea kusema, “Mimi nakaa na dada Josefina kule TPC. Unamfahamu dada Josefina ambaye ni mwalimu kule TPC? Siku ile ulipokuja ulimchukua kwenye gari yako mkaenda kanisani.”
> Mwanamume alimkazia macho zaidi. Halafu alisema, “Aa, ni wewe yule kijana mdogo aliyelilia gari mpaka nikampa hela akaacha kulia! Umetoka wapi huku?”
> “Ndiyo, ndiyo ni mimi,” Prospa alisema kwa furaha. Aliwaita wenzake waje halafu akamwambia mjomba wake, “Hawa ni rafiki zangu. Huyu ni Tofa na huyu ni Mansa. Tulikuwa tunakutafuta wote siku nyingi sasa.”
> Mjomba Feliksi aliuliza, “Mnanitafuta? Mnanitafutia nini? Na hawa ni rafiki zako? We kwanza ulikuja lini hapa mjini?”
> “Mtoto wa dada Josefina alipotea, sasa nikaja huku kumtafuta. Bado sijampata,” Prospa alieleza.
> “Mtoto alipotea? Lini? Mambo ya ajabu haya. Hebu twende nyumbani ukaoge kwanza halafu unieleze vizuri.” Mjomba Feliksi alisema…(uk. 130-132).

Nukuu hiyo inaonesha kuwa mjomba Feliksi alishangazwa na maelezo ya Prospa kwa sababu si jambo la kawaida mtoto kama yeye kwenda Dar es Salaam kumtafuta mtoto mwenziwe. Kukutana na Prospa pamoja na maelezo yake yote ulikuwa kama muujiza kwa mjomba wake. Ni kawaida kwa mtu mzima anapokutana na mtoto mdogo katika mazingira asiyoyatarajia kumwuliza sababu ya kuwapo kwake. Kwa kuwa Feliksi alimfahamu Prospa, ni wazi kwamba alitamani kujua sababu ya yeye kuja Dar es Salaam peke yake.

Mahojiano mengine yalifanywa na Sara dhidi ya Uzuri. Sara alikuwa katika harakati za kutaka kuwajua majirani wa Feliksi. Ijapokuwa mwanzoni Uzuri hakumpenda Sara, lakini Sara alijitahidi kuhakikisha kuwa anaendelea kumsemesha ili wazoeane. Michakato ya akilini mwa Sara ilibainika kutokana na misemo na usemaji wake. Alijitahidi kuwa mpole na kutii kila aambiwacho na Uzuri ili apate alichokitaka. Hili lilitokana na silika ya Sara. Sara alihoji:

> "Mama Mchau ana watoto wengi?"
> Uzuri hakujibu. Alikuwa anapima mchele na kuuweka kwenye ungo. Kabla hajajibu Sara alisema,
> "Eti hana mume amezaa watoto hivihivi?"
> "Nani tena mwenye umbea huo? Vivulana vya hovyo kweli hivyo. Ndugu zako hao wakoje? Waongo kama nini!" Uzuri alisema. Aliendelea, "Mama ana mume, tena mume hasa. Matayo Mchau, mzee wa watu ni mme mzuri."
> Sara aliuliza, "Eti umethema hiyo nyumba ina watu wengi?"
> Uzuri alisema, "Wala. Ni ndugu tu, na watoto wa kuletwa. Mama mwenyewe ana watoto wanne. Wote wa kike."
> "Hana mtoto wa kiume hata mmoja? Mathikini," Sara alisema kwa huruma.
> "He! Masikini. Masikini nini?" Uzuri alifoka. Sara alinyamaza hakutaka kumkasirisha uzuri.
> Basi yuko dada yake Mzee Mchau, anaitwa Awaichi Mchau, ana mawazo kama wewe hapo." Uzuri alimweleza Sara… (uk. 143-144).

Dondoo hili linaonesha kuwa Sara alikuwa makini sana kumhoji Uzuri ili apate anachotaka. Katika mahojiano yoyote ni lazima mtu anayetafuta taarifa awe makini, kinyume chake, hatopata taarifa hizo. Imebainika kuwa Sara alichagua maneno ya kuongea ili asimuudhi Uzuri, kwa sababu taarifa alizokuwa anazitoa zilikuwa muhimu katika zoezi lao la kumtafuta Merisho. Kutokana na nafsi tatu za Nadharia ya Saikochanganuzi, Sara aliongozwa na nafsi ya ukomavu inayoongoza maamuzi ya busara. Wakati mwingine, Sara aliona ni busara kuonesha huruma kwa mama aliyesimuliwa kuwa na watoto wa kike tu, lakini lengo lake lilikuwa kupata data zaidi zitakazowasaidia katika upelelezi wao wa kumtafuta Merisho.

Kwa upande wa *Ngoma ya Mianzi,* utendaji umetumika kuhoji ili kupata taarifa mbalimbali au kupata kitu fulani. Taarifa au kitu hicho ni muhimu kwa yule anayehoji. Kwa namna moja au nyingine, taarifa hizo huweza kuokoa mtu, jamii au taifa kwa jumla wake. Katika riwaya hii, mahojiano yamefanyika baina ya mhusika mkuu na wahusika wengine, au wahusika wakuu wenyewe kwa wenyewe. Mathalani, bibi yao Mbumi na Chulu alipoamshwa usingizini, baada ya kusikia ngurumo, alihoji ili kujua ni nini kilichotokea. Kwa kuwa alitoka usingizini, ni wazi kuwa alikuwa na mawenge, asingeweza kujua kilichotokea. Mwandishi anasema:

> Hakukawia zaidi. Aliruka kutoka kitandani, akamshika bibi na kumtikisa huku akisema kwa sauti ndogo, “Bibi amka! Kuna radi!” Bibi aliamka na kuketi kitandani, akauliza kwa sauti ya usingizi “Radi gani?” “Nasikia kishindo labda kuna tufani yenye ngurumo.” Hakutaka kumueleza bibi kuwa amesikia mshindo wa bunduki. “Kuna nini?” Bibi alimaka huku akijizoazoa kitandani. Alisikiliza. “Labda ni vita! La haula, mahoka wapishe mbali! Mateso tuliyopata hayajatosha tu?... Sijui kama ni vita. Lakini nadhani kuna jambo, nitakwenda kutazama.” Mbumi alianza kutembea gizani kuelekea mlangoni (uk. 4-5).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa bibi alihoji kutaka kujua muungurumo ni wa nini. Mbumi hakutaka kumwambia ukweli, lakini kutokana na utu uzima aliokuwa nao, bibi yao aliweza kubashiri kuwa huenda ni vita. Baada ya kuamshwa, alihoji kwanza ili kujua zaidi. Ubashiri wake ulikuwa sahihi, kwani baada ya muda, ngoma zilianza kusikika kuashiria taarifa ya hatari.

Mbumi naye alihoji kutaka kujua kwanini Chulu hamsaidii kukata kuni, ambapo wote walikuwa safarini, na moto utakaowashwa ungekuwa na faida kwa wote. Utafiti umebaini kuwa Chulu alikuwa ameshikilia mila za kwao zinazobagua kazi kutokana na jinsia. Mathalani, mwanaume haruhusiwi kukata kuni, bali kazi hiyo huchukuliwa kuwa ni ya wanawake. Huu ni mfumo dume, kwani suala la kuchanja kuni au kuokota, halichagui jinsia yoyote. Ni vyema watoto wakazoeshwa kufanya kazi zote, bila kujali jinsia. Hii itawaondolea suala la kibaguzi watakapokuwa wakubwa. Kwa mujibu wa Bakize (2020), Chulu aliendekeza mfumo dume na kujiona yeye hastahili kufanya kazi azifanyazo dada yake. Mwandishi anaonesha mahojiano hayo kama ifuatavyo:

> “Hunisaidii Chulu?” Mbumi alisema. “Mwanamume kuchanja kuni si mila yetu,” Chulu alisema. “Mambo ya mila yangesubiri tumalize matatizo kwanza; hatuna muda,” Mbumi alisema. “Hebu kanisaidie kukata tawi hilo hapo kwenye kichaka. Chulu hakutaka kuvunja mila, lakini wakati huohuo alitambua kuwa alipaswa kumsaidia dada yake ili kuwanusuru wote wawili. Mila ilimzuia lakini akili ilimsuta. “Potelea mbali!” Alisema huku akiuegemeza mkuki wake kwenye mgude, ambao shina lake la njano nyepesi lilikuwa limenyooka na linateleza kama sanamu ya mpingo. Alichukua mundu, akamfuata Mbumi kule vichakani kutafuta kuni. Punde walirejea na mizigo ya kuni na kuibwaga karibu na mgude… (uk. 29-30)

Kwa hiyo, kuhoji kwa Mbumi ndiko kulikosaidia kaka yake kutoa msaada wa kutafuta kuni na kuweka pembeni masuala ya mila na desturi. Kutokana na Nadharia ya Saikochanganuzi, Chulu alisukumwa na nafsi ya kiwango cha ukomavu ambayo huchunguza uadilifu wa tendo, wema na ubaya wake kabla ya kulitenda. Aliona kuwa kufuata mila na desturi wakati wa shida siyo sahihi. Hatimaye, walifanikiwa kuwasha moto kwa kutumia njia ya asili ya kupekecha vijiti, maarufu kama ulindi na ulimbombo.

Katika safari ya kuelekea Lugalo, Mbumi na Chulu waliongozana na Mpunza kama mwenyeji ambaye alikuwa na wajibu wa kuwapitisha njia fupi itakayowafikisha haraka. Mwandishi wa riwaya hii anasema kuwa kutokana na umri na ugeni wao, Mbumi na Chulu ilibidi wapewe mtu wa kuwasindikiza ili kufanikisha lengo lao. Anasisitiza kuwa katika jamii ya Wahehe, ni jambo la kawaida kupokea wageni na kuwasindikiza kama hawajamaliza safari yao. Katika safari hiyo, Mpunza alihoji kuhusu Wadachi kwa Mbumi na Chulu, kwa sababu walishawaona walipokwenda kuwatafuta wazazi wao Bagamoyo. Mahojiano yalikuwa kama ifuatavyo:

> "Mnasema Wadachi walikuwa wamekwishaikamata Bagamoyo?" Mpunza aliuliza.
> "Naam," aliitikiwa. "Walikuwa wanajenga boma."
> Inaelekea ni watu hatari!"
> "Wana silaha kubwa sana ziitwazo 'mizinga'. Mshindo wake kama radi."
> "Bado hawajakutana na wanaume," Mpunza alitamba huku akipunga lisala lake.
> Mbumi alimtazama Mpunza kwa makini na kusema, "Usiseme hivyo! Wale watu ni hatari. Wekundu kama vichuguu!"
> "Ala! Hivi mlipotoka Usagara mliwaacha wakijiandaa kuja Uhehe?"
> "Yaelekea hivyo."
> "Kwa hiyo wanaweza kufika huku wakati wowote? Na njia yao bila shaka itakuwa ni hii hii tunayopita sasa."
> "Kumbe!" Chulu na Mbumi waliitikia kwa pamoja.
> "Ndiyo njia fupi ya kufika Usagara. Nyinyi mlifuata njia ndefu kidogo; uzuri wake ni kwamba njia yenu ilipita vijijini."… (uk. 50-51).

Katika mahojiano ya hapo juu, tunathibitisha kuwa, pamoja na kupewa habari kuhusu Wadachi na silaha zao, Mpunza hakuonesha woga kabisa, naye alijitapa na lisala lake. Ni kawaida kwa vijana ambao wamekula kiapo kuilinda nchi kutokuwa

na woga na kuwa na utayari wakati wote. Kwa upande mwingine, Mbumi na Chulu walitawaliwa na wasiwasi kwa kuwa walikuwa wanazijua silaha wanazozitumia Wadachi.

Utendaji mwingine wa mahojiano ulibainika kati ya Chulu na Mpunza, kuhusu vita dhidi ya maadui, walipokuwa katika bonde la Lugalo wakijiandaa na vita. Baada ya kupata mbiu ya vita, watu wengi sana walikusanyika wakitokea pande zote za Uhehe. Hali hiyo ilimfikirisha sana Chulu kwa kuona kuwa silaha zao zilikuwa dhaifu zikilinganishwa na silaha za maadui, ambazo aliziona Bagamoyo. Kutokana na msingi wa tatu wa Nadharia ya Saikochanganuzi ambao ni wasiwasi, Chulu alikuwa na mashaka na dukuduku kuhusu vita kama watafanikiwa, au la, kwa sababu ya silaha zao. Mwandishi anasema:

> Chulu alimuuliza Mpunza, “Je, vita vitakuwa vikali?”
> “Labda, lakini tutashinda,” Mpunza alijibu huku akiipapasa na kuigonganisha mikuki yake miwili – lisala na mugoha. Hakuonesha wasiwasi.
> “Kwanini unasema hivyo?” Mbumi aliingilia.
> “Kwa sababu maadui watashtukizwa. Hawajui kuwa tupo hapa.”
> “Lakini watu wengi watakufa; maadui wana silaha kali sana,” Mbumi alieleza, akikumbuka zile silaha alizoziona Bagamoyo.
> “Hata sisi tunazo,” Mpunza alisema huku akipunga mkuki wake. Hakujua chochote kuhusu silaha za Wadachi (uk. 93-96).

Kupitia nukuu hii, ni dhahiri kuwa Mpunza hakuzifahamu vizuri silaha za maadui. Mazingira ya vita aliyoyazoea Mpunza ni tofauti na yale waliyoyaona Mbumi na Chulu, ndiyo maana walikuwa na wasiwasi wa vifo vingi kutokea.

Utendaji wa mtindo wa mahojiano umetumiwa pia na askari wa Kidachi dhidi ya Mbumi. Baada ya vita kuisha, Mbumi aliamua kwenda kupumzika mianzini. Hata hivyo, alisita baada ya kuona nyayo kubwa za binadamu zilizokuwa zinaelekea kule vichakani. Mbumi alipata wasiwasi na kuwa na shauku ya kujua ni nyayo za nani. Utafiti umebaini kuwa Mbumi alihisi zile zilikuwa ni nyayo za adui, kwa sababu wenzake alikuwa amewaacha. Wasiwasi wake ulikuwa sahihi, kwani nyayo hizo zilikuwa za askari wa wadachi, ambaye naye alikuwa amepumzika eneo hilo. Askari alishtuka kumwona Mbumi. Hivyo, alilazimika kumhoji:

> "Hujambo binti?"
> "Sijambo."
> "Unakwenda wapi?"
> "Nazunguka tu."
> "Watu wako wako wapi?"
> "Watu gani?"
> "Wa kabila lako."
> "Niko peke yangu. Askari wako mbali."
> Kusikia hivyo, askari huyo alitoka mafichoni, akamaka, "Afadhali! Unasikia mtoto mzuri? Usiwaambie kuwa nipo hapa."
> "Kina nani."
> "Wenzio."
> "Sitawaambia. Naona umechoka. Nikupe ulanzi?"
> "Ulanzi ndio nini?"
> "Kinywaji chetu cha kuburudisha."
> "A-ha! Kipo wapi? Basi nipe." (uk. 106-108).

Nukuu hii inaonesha kuwa askari wa Kidachi alimwamini Mbumi kutokana na udogo wake, na maneno aliyomwambia. Hivyo, alikubali kupatiwa kinywaji hicho, ambacho alikinywa kwa kasi kutokana na kiu aliyokuwa nayo. Unywaji wake wa kasi ulisababisha alewe sana. Kutokana na ulevi alioupata ilikuwa rahisi kwa Mbumi kumkamata mateka. Kwa hiyo, ilimsaidia katika kazi yake na kutangazwa kuwa shujaa. Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, askari alionesha udhaifu kwa kukubali kupewa kinywaji. Katika mazingira ya kawaida, ya kivita, askari haruhusiwi kula au kunywa kitu chochote kutoka kwa mtu asiyemfahamu, hata kama atakuwa na njaa au kiu kiasi gani.

Kwa hiyo, mahojiano husaidia mtu kupata taarifa au kitu anachokitaka. Hata hivyo, anayehoji akikosa mbinu nzuri za kufanya mahojiano, anaweza asifanikiwe. Wakati mwingine, mhusika inabidi atumie mbinu ya kubembeleza, kushawishi, au kuongea kwa upole ili kupata kile anachokitaka kama asemavyo Munyioki (khj) kuwa mahojiano hufanyika kwa lugha tofauti na ile ya kuamrisha. Anaongeza kuwa anayehoji lazima atumie mbinu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na lugha laini ili apate taarifa anazozitaka.

### 4.2.2 Utendaji wa Kushawishi

Utafiti uliozaa tasinifu hii umebaini kuwa utendaji unaweza kudhihirika kwa mtindo wa kushawishi ili kupata kitu fulani kama vile chakula, mavazi, na usafiri. Utendaji wa namna hii huhitaji mbinu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kulia, kuonesha sura ya

huruma, na hata kuongea kwa sauti ya chini, na kudanganya. Utendaji huu umedhihirika katika riwaya ya *Safari ya Prospa*. Kwa mujibu wa CKDA4 (2020):

> Utendaji unaweza kutumika kumshawishi mtu ili akupe kitu fulani ambacho ni muhimu katika maisha. Katika kushawishi unatakiwa uwe mjanja sana ili kuchota akili ya huyo mtu.

Suala alilolishadidia CKDA4 (khj) linathibitika katika riwaya ya *Safari ya Prospa* baada ya Prospa kupanga mipango yake ya kwenda Dar es Salaam kumtafuta Merisho. Alianza safari yake kwa kupitia geti la TPC. Alipokaribia, aliona gari aina ya *pick-up* likipakia majani, ambalo alifikiri anaweza kupata lifti kumtoa eneo hilo. Hivyo basi, alimsalimia dereva ambaye hakuitika, ila alimwuliza anachotaka. Prospa alimwambia kwamba anaomba lifti, huku moyo wake ukimwenda mbio. Dereva yule alimkatalia kwa kumwambia kuwa gari limejaa. Prospa aliendelea kumshawishi kwa kudanganya kuwa anauguliwa. Matamanio yake yalimwambia ni lazima atoke katika eneo hilo kabla hajaonekana na kuzuiwa. Prospa anasema:

> "Bibi anaumwa kaka nampelekea…"
> "We mtoto huoni gari imejaa? Hakuna nafasi"
> "Bibi anaumwa, nampelekea dawa" Prospa aling'ang'ania akawa ameshika gari kama vile ataweza kulikataza kuondoka…
> Dereva alipiga gari moto.
> Prospa aling'ang'ania gari "Kaka…," alisihi.
> "Shauri yako, panda," dereva alisema huku akiondoa gari… (uk. 21-22).

Kupitia nukuu hii ni dhahiri kuwa Prospa alimshawishi mwenye gari kwa kumdanganya na kushikilia gari ili aonewe huruma, hivyo, apewe lifti. Ijapokuwa mwenye gari hakuitikia hata salamu ya Prospa akijua kuwa anataka kumuomba kitu, lakini ushawishi wake ulimwezesha kupata lifti iliyomtoa katika maeneo aliyokuwa akifahamika. Hivyo, alijihisi yupo salama. Katika mazingira ya kawaida, watoto wa mitaani wanapotaka kitu, hutoa salamu inayoambatana na kuomba kitu. Mfano: "Shikamoo, dada naomba hela sijala tangu juzi". "Naomba nikusaidie kubeba mzigo." Watoto hawa huomba kusaidia kubeba mizigo ili wapate ujira wa kujikimu katika maisha yao ya kila siku.

Utendaji wa ushawishi pia ulitumika pale ambapo Sara alikuwa anaomba lifti kuelekea Dar es Salaam. Baada ya Sara na Prospa kukutana, Prospa alimweleza

lengo lake. Sara akajitolea kumsindikiza akimwambia kuwa alitamani kwa muda mrefu kwenda Dar es Salaam ili akasome *University*. Kwa kuwa Sara alipenda Prospa amwite Edison, Prospa alimpa masharti kuwa akiomba lifti atamuita jina hilo. Sara alijaribu kusimamisha magari lakini yaliwapita. Baada ya kujaribu kwa muda mrefu, gari moja lilisimama. Mwandishi anasema:

> Sara alimshika Prospa kwa nguvu na kumwambia, "Acha niombe mimi. Uthitheme kitu."
> "Usipoipata utanikoma," Prospa alimtishia.
> Sara alimwambia mwenye gari, "Baba, tunatembea mimi na mdogo wangu kwenda Darithalam. Tuthaidie."
> "Mnatembea? Mmetoroka nyumbani?" Mwenye gari aliuliza.
> Mkono mmoja wa Sara ulimfinya Prospa asije akasema kitu. Sara alisema, "Baba yetu yupo Darithalam, thatha mama ametukimbia, amemfuata baba. Nyumbani hakuna chakula."
> "Lo! Nyie watoto mnasema kweli?" Mwenye gari aliuliza.
> Prospa alidakia, "Hapana baba, ni kweli kabisa."
> "Ingieni," mwenye gari alisema akawafungulia mlango. Alafu aliwaambia, "Mnajua safari yenu ni ya hatari? Hapa katikati ya Same na Makanya kuna mbuga ya wanyama wakali. (uk. 51-52).

Dondoo hili linaonesha namna Sara alivyomshawishi dereva kwa kumdanganya kuwa Prospa ni mdogo wake, na walikuwa wanaelekea Dar es Salaam kwa wazazi wao. Kulingana na nafsi tatu za Nadharia ya Saikochanganuzi, nafsi ya kiwango cha ukomavu ilimsukuma kusema uongo, ijapokuwa alijua kusema uongo ni kosa. Lengo lao lilikuwa ni kupata lifti itakayowafikisha Dar es Salaam. Kutokana na uongo huo, dereva alishawishika na kuwabeba katika gari lake, ijapokuwa hakuwafikisha sehemu waliyoitaka.

Sehemu nyingine inayoonesha utendaji wa ushawishi ni pale Prospa alipokutana na kaka yake Petro, na kumtaka ampeleke anapoishi au kwa mjomba Feliksi. Ijapokuwa walikutana katika mazingira ya kutatanisha na kila mtu akiwa na mambo yake, Prospa hakulijali hilo. Nafsi ya kiwango cha kati ilikuwa ikimsisitiza ni lazima aondoke na kaka yake. Ilibidi atumie mbinu ya kumshika mkono kaka yake ili kumfanya apate kile alichokitaka. Hili linabainishwa na Prospa anaposema:

> “Sasa unaishi wapi kaka? Nakuomba unipeleke nyumbani basi,” Prospa alimsihi kaka yake. Alimshika mkono kama kumzuia asiondoke.
> “Yaani umekuja kwangu?” Petro aliuliza.
> “Nilikuwa nataka… Utanipeleka kwa mjomba Feliksi basi,” Prospa alisihi. “Mambo ya kushtukiza siyawezi mie,” Petro alilalamika.
> “Kaka Petro jamani,” Prospa alisema kwa sauti ya unyonge.
> “Agh! Balaa gani hii,” Petro alilalamika, akionesha kukasirika. “Basi twende,” alisema kwa ghadhabu. Waliondoka pamoja na kuelekea kwenye uchochoro mmoja katikati ya nyumba nyingi zilizosongamana (uk. 60).

Mazungumzo haya yalikuwa ni ya kumshawishi Petro awapeleke sehemu anayoishi. Ili kuonesha umuhimu wa suala hili, Prospa alionesha sauti ya unyonge ili Petro amhurumie. Ijapokuwa Petro alikasirika sana kutokana na kushtukizwa, lakini aliwapeleka. Hili linathibitishwa katika ukurasa wa 61 mwandishi anapofafanua kuwa Petro aliwafikisha kwenye nyumba iliyokuwa kwenye bonde, mwisho wa uchochoro. Aliwaingiza katika chumba kimoja kati ya vyumba vingi vya nyumba hiyo. Mtafiti anaamini kuwa matamanio ya Prospa yalitimia kwa kuwa alimpata kaka yake na alipata mahali pa kufikia. Jambo moja tu lilibakia, kumpata Merisho.

Mazungumzo ya ushawishi pia yalitumika kati ya Sara na Uzuri. Sara aliachwa na wenzake ili ajenge urafiki na Uzuri ili baadaye wapate taarifa ambazo zingesaidia kupatikana kwa Merisho. Uzuri hakumpenda Sara, lakini Sara alimshawishi kwa maneno mazuri ya kumsifia, pamoja na nyimbo. Katika kushadidia lugha ya ushawishi, Munyioki (ametajwa) anasema kuwa ni lugha yenye wingi wa ahadi na upole. Anaongeza kuwa lugha hii huambatana na matendo ya ukarimu kama aliyoyafanya Sara. Hata hivyo, Sara alichunguza uzuri na ubaya wa tendo kabla hajalifanya. Mwandishi anasema:

> Sara na Uzuri walikaa kimya. Sara alikuwa akifikiria jinsi ya kumwingia Uzuri bila kumkasirisha. Uzuri alikuwa anachambua mchicha… Hakutaka msichana huyu akae naye jikoni, kwani angechelewesha kazi yake tu. Mwishowe alimwuliza Sara, “Sasa wewe unasubiri nini hapa? Nenda ukakae na hao wazururaji wenzako.”
> Sara alitabasamu, mlango wa mazungumzo umefunguka, alijiambia kimoyomoyo. Sara akicheka uso wake hung’aa na kuonesha uzuri wake kamili. Meno yake yalikuwa meupe mithili ya mahindi mapya.

> Uzuri alimtazama, alivutiwa na tabasamu, na hapo hapo kabla Uzuri hajasema lolote, Sara alisema,
> "Wewe ni mthuri kama udi."
> Uzuri aliuliza, "Unasemaje?" "We ni mthuri kama udi." Sara alirudia.
> Uzuri alicheka. Alirudia tena kuchambua mchicha. Lakini kicheko kilimbana akaanza kucheka tena. "Mtoto we una mambo," alisema…
> Sasa wote wawili walicheka. Uzuri alimwambia Sara, "Nisaidie basi kuchambua mchicha." (uk. 141-143).

Utafiti umebaini kuwa kutokana na ushawishi wa Sara, aliweza kujenga urafiki na Uzuri, hivyo, akafikia hatua ya kumsaidia kazi za jikoni na kumsuka nywele zake. Maelezo katika dondoo la hapo juu yanadhihirisha namna Sara alivyomshawishi Uzuri kwa lugha ya upole, kumsifia na kutabasamu. Hatimaye, Uzuri alimwamini Sara na kuzungumza naye mambo mengi, ambayo yalihitajika kwa Sara. Kutokana na nafsi tatu za Nadharia ya Saikochanganuzi, Sara alisukumwa na nafsi ya kiwango cha ukomavu inayochunguza uadilifu wa tendo, wema na ubaya wake kabla ya kulitenda katika kushawishi. Suala la ushawishi linashadidiwa na Bakize (2020) anayesema kuwa:

> Ukimuangalia Sara na Prospa utagundua kuwa Sara alikuwa na ushawishi mkubwa sana, ndiyo maana Prospa aliweza kuambatana naye, ijapokuwa hakumuamini. Hii inaweza kutokana na silika yake. Hata ukiangalia sehemu mbalimbali walizokuwa wote, bado anaonekana kuwa na ushawishi.

Dondoo hilo linashadidia ushawishi wa Sara, ijapokuwa mtaalamu huyo alijaribu kumlinganisha na Prospa kwa sababu ndio wahusika wakuu katika riwaya ya *Safari ya Prospa*.

Hivyo basi, ni muhimu mtu kufanya lolote linalowezekana ili kupata kile anachokitaka kama kina umuhimu. Watoto hawa walikuwa wajanja na waliweza kucheza na akili za watu. Kwa mujibu wa nadharia iliyotumika katika utafiti uliofanyika, lugha ya Sara na Prospa imeakisi michakato ya akilini mwao ambayo ilijibainisha kwa misemo na usemaji wao.

### 4.2.3 Utendaji wa Kuonya

Kuonya ni kukataza mtu kufanya jambo fulani kwa kuhofia hatma yake (Bakhressa, 1992). Mara nyingi, mtoa onyo huwa na ujuzi wa matokeo ya kile anachokionya

kutokana na uzoefu katika maisha. Pia, muonyaji huelewa madhara yanayoweza kutokea iwapo jambo hilo litafanyika. Ni jambo la msingi kusikiliza na kuyatii maonyo ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea. Katika mjadala huu, maonyo yanatolewa kwa wahusika wakuu pale ambapo wanakwenda kinyume na taratibu mbalimbali. Sehemu nyingine wanapeana maonyo wao kwa wao ili kukumbushana kuhusu taratibu hizo. Lengo la onyo ni kumtahadharisha muonywaji kuhusu jambo fulani ambalo linaweza kutokea na kuleta madhara. Mathalani, katika riwaya ya *Safari ya Prospa*, Prospa alipanga kwenda Dar es Salaam bila kujua atafikaje. Katika mawazo yake, alikuwa anajua labda angeweza kufika hata kwa kutembea. Baada ya kukutana na watoto waliokuwa wanachunga ng'ombe na kukaribishwa kwao, wazazi wao walimuonya kutokwenda safari yake kwa miguu kwa kuhofia usalama wake. Mzazi anasema:

> "Sasa wewe mtoto usiondoke mpaka tutafute njia nzuri ya kukufikisha Dar es salaam. Unasikia?"
> Prospa aligoma kubishana naye. Alipanga kuondoka asubuhi hiyohiyo. Baba alipoona Prospa amenyamaza alimwambia, "Ukiondoka hapa utapata tabu sana njiani. Dar es salaam hakufikiki kwa miguu kijana. Halafu kuna wanyama wakali wanaokula watu huko njiani. Safari hii sio jambo la mchezo. Usiondoke."
> Prospa alisema, "Ndio baba." (uk. 43).

Pamoja na kuonywa na kuelezwa hatari ya kutembea kwa miguu, Prospa hakuzingatia maonyo hayo, kwa sababu matamanio yake yalikuwa kufika Dar es Salaam na kumpata Merisho. Alichunguza wema na ubaya wa lile aliloambiwa, akafanya maamuzi. Hivyo, alikaidi. Na baada ya wazazi wale kuondoka, Prospa alimhadaa binti aliyebaki naye na kumtoroka.

Prospa aliendelea kupata maonyo kwa kuwa lilikuwa ni jambo la hatari. Mathalani, baada ya kukutana na Sara, walifanya juhudi ya kuomba lifti. Walikuwa tayari kupanda gari lolote ili kutimiza matamanio yao ya kufika Dar es Salaam na kumpata Merisho. Baada ya kupata lifti, mwenye gari aliwapa onyo. Mwandishi anasema:

> "Ingieni," mwenye gari alisema, akawafungulia mlango. Halafu aliwaambia, "Mnajua kwamba safari yenu ni ya hatari? Hapa katikati ya Same na Makanya kuna mbuga ya wanyama wakali. Giza lingeingia kabla hamjafika popote, mngeweza kuliwa na simba." Wote wawili walinyamaza kimya. Mwenye gari aliendesha kasi. Prospa na Sara walishikilia viti walivyokalia ili wasigongane.

> Wakati mmoja, dereva alitingisha kichwa kama vile alikuwa akiwaza jambo la kusikitisha, halafu alisema, “Hatari tupu hii. Mnaona hamna kabisa maskani ya watu” (uk. 52).

Kupitia nukuu ya hapo juu, tunaona namna dereva wa gari alivyowaonya Prospa na Sara kuhusu safari yao, kuwa ni ya hatari. Dereva huyu alikuwa na ujuzi wa eneo hilo, lisilokuwa na makazi ya watu, na wakati mwingine huwa na wanyama wakali. Hata hivyo, katika mazingira ya kawaida, ni hatari sana kutembea kwa miguu sehemu zenye mbuga au misitu, kwa sababu huweza kuwa na wanyama wakali. Prospa na Sara hawakuwa na namna, kwa sababu walikuwa hawajui umbali wa sehemu waliyokusudia kwenda. Pia, walishajitoa mhanga kumtafuta Merisho. Kutokana na msingi wa matamanio katika Nadharia ya Saikochanganuzi, watoto hawa walisukumwa na matamanio yao ya kwenda Dar es Salaam kumtafuta Merisho, hivyo hawakujali namna ya kufika.

Onyo jingine lilitolewa na kaka yake Prospa, Petro, baada ya kusikia Prospa na Sara wamekuja mjini kumtafuta Merisho. Petro alikuwa na wasiwasi sana kuhusiana na ujio wao. Aliona wanaingilia kazi za polisi. Petro anasema:

> “Nyie balaa kabisa, mnapoteza nguvu zangu bure tu,” Petro alisema. “Mnataka kumpata huyo mtoto, ama hamtaki. Kwanza wewe Prospa ni wa kupelekwa polisi utiwe jela ya watoto. Umemtoroka dada yako, halafu umekwenda umemtorosha msichana wa watu, wazazi wake hawajui aliko, eti kwa kujitia wewe ni mpelelezi! Dada yako umemuona bwege kwa kuwaachia polisi mambo haya? Na msichana mwenyewe basi, nusu kichaa nusu mchawi! Agh, nakwenda zangu kulala.” Petro alitoka nje, akaacha mlango wazi, akaenda zake.
> “Utalala wapi?” Prospa aliuliza.
> Petro hakujibu (uk. 65).

Dondoo la hapo juu linatuonesha namna Petro alivyowaonya wadogo zake. Katika mazingira waliyokutana, Petro aliona siyo salama kwao, kwa sababu kazi ya kutafuta waliopotea ni ya polisi. Hata hivyo, Prospa na Sara hawakukata tamaa, waliendelea na juhudi zao za kumtafuta Merisho kwa sababu matamanio yao yalikuwa hayajatimizwa.

Utafiti umebaini pia Prospa na Sara walionywa kuhusu kulala hovyo mitaani. Hali hii ilitokea baada ya watoto hawa kutoka Zanzibar wakiwa mikono mitupu. Matarajio

yao yalikuwa wamkute Merisho Zanzibar. Baada ya kumkosa walirudi Dar es Salaam wakiwa wamechoka mwili na akili na kuamua kujipumzisha katika bustani. Kutokana na uchovu waliokuwa nao, walipitiwa na usingizi. Kwa kawaida, mtu akipitiwa na usingizi anakuwa hana fahamu, hivyo waliposhtuka waligundua wameibiwa kila walichokuwa nacho. Kilio chao kiliwashtua vijana wa mitaani, maarufu kama changudoo, na kufanya wawafuate ili kujua kinachowaliza. Baada ya kuelezwa kinagaubaga, kiongozi wao aliwaonya. Mwandishi anasema:

> …Ghafla mvulana msemaji mkuu alikatisha kicheko kwa kusema, "Sisi ni changudoo, watoto wa mjini, watoto wa barabarani. Tunalala barabarani tunaamkia hapohapo. Sisi ndio baba na mama, tunajilea wenyewe. Mambo ya kulialia na kulala ovyo hakuna tena. Mama ulishamwacha ukaja mjini. Sasa huu mji utakulea. Mnasikia?"
> Prospa na Sara walikaa kimya.
> Aliendelea, "Na ukishaingia kwenye kundi hutoki tena. Kundi lako ndilo litakulinda. Ukitoka tu utakaa peke yako, unakufa, utashikwa wizi upigwe ufe, au utashikwa na polisi uende ndani… (uk. 112-113).

Imebainika kuwa Sara na Prospa waliogopa sana wakati kiongozi huyo alipokuwa anaongea. Walishindwa kujibu chochote. Iliwalazimu watii kila wanachoambiwa kwa sababu jiji walikuwa hawalijui vizuri. Kutokana na nafsi ya tatu ya Nadharia ya Saikochanganuzi ambayo ni nafsi ya ukomavu inayochunguza wema na ubaya wa tendo kabla ya kulitenda, watoto hawa waliona ni busara kunyamaza na kutii ili jambo lao liweze kufanikiwa.

Prospa pia alionywa na Tofa kuachana na Sara, pale alipoonesha wasiwasi kama alikuwa amepata kifungua kinywa au la. Kutokana na mahitaji ya mwanadamu yeyote kama ilivyozoeleka, mara baada ya kuamka huhitaji kupata kifungua kinywa ili aweze kuishi na kushinda vizuri mchana kutwa. CKDOISJ2 (2020) anasema kuwa:

> Mazungumzo ya utendaji yanaweza kutumika kumuonya mtu asiyesikia kuachana na jambo fulani. Kama muonywaji hatosikia anaweza kupatwa na matatizo makubwa baadaye.

Dondoo hilo linadokeza umuhimu wa maonyo. Hata hivyo, mashaka ya Prospa yalikuwa sawa, kwani alitengwa na Sara wakati Sara ni dada yake aliyekuja naye

mjini kumtafuta Merisho. Tofa na wenzake walipoona Prospa anazidi kulalamika, ilibidi waachane naye, waendelee na mambo mengine. Masimulizi yanatanabaisha:

> Prospa alimwambia Tofa, “Tumpelekee Sara maandazi.”
> Tofa alisema, “Achana na huyo msichana bwana. Wana kazi zao hao. Wanapata chakula hukohuko.”
> “Sara ni dada yangu. Alinisindikiza kuja huku Darisalam kumtafuta Merisho. Nimeenda naye mapaka Zanzibar, siwezi kumsahau,” Prospa alisema huku akilalamika.
> Tofa na Mansa waliondoka na kumwacha Prospa akilalamika. “Shauri yake bwana.” Alimsikia Mansa akisema huku wakiwa wanatembea haraka.
> Moyo wa Prospa ulimsukuma kumtafuta Sara. Alitaka kufahamu alipo hata kama atakuwa amepata chakula kama walivyosema Mansa na Tofa (uk. 120).

Nukuu hii inadhihirisha kuwa Prospa alionywa kwa sababu wale watoto walijua Sara atakuwa ameshakula. Utafiti umebaini kuwa watoto hao wana utaratibu wao waliouzoea wa kutafuta chakula. Watoto wa kike na wa kiume hutafuta chakula na hula tofauti kutokana na jinsi zao. Pamoja na Prospa kuonywa na wenzake, hakusikia na akaondoka kwenda kumtafuta Sara. Hata hivyo, alizunguka tu huku na kule bila kumpata Sara, akaamua kurudi kwa wenzake akiwa na maandazi yake kwenye mfuko wa kaptura. Kwa hiyo, kama Prospa angesikiliza maonyo ya wenzake, asingehangaika kumtafuta Sara, kwa sababu alikuwa hajui mahali mahususi walipo Sara na wenzake.

Kwa mtazamo wa utafiti uliofanyika Prospa alikaidi mambo mengi aliyoonywa kutokana na silika na matamanio yake yaliyomsukuma kumtafuta Merisho hadi ampate. Hata hivyo, ni vizuri kufuata maonyo yanayotolewa bila kujali yanatolewa na nani na kwa wakati gani, kwa sababu siku zote anayeonya anajua madhara au matokeo ya kile anachokionya.

Katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* mwandishi pia amesawiri maonyo mbalimbali kwa wahusika wake. Kwa mfano, wakati Mundewa alipowaita Mbumi na Chulu kwa ajili ya kuwaagiza wapeleke ujumbe kwa Mukwava aliwapa onyo. Mundewa anasema:

> “Mkwava ametuma ujumbe wa urafiki. Sisi tunataka kuitikia ujumbe huo. Zaidi, tunataka kumtahadharisha kuhusu mwenendo wa maadui ambao mmewaona kidogo jana. Inavyoelekea wanakwenda Uhehe, japo wanatumia njia ya mzunguko - labda kupoteza lengo. Inabidi Mukwava azipate habari hizi haraka ili ajiandae kuwapokea kwa ukarimu wa kihehe! Je, mtaweza kupeleka ujumbe huu?”
> ”Tutaweza!”waliitikia kwa pamoja.
> “Vizuri. Nataka mfahamu kuwa hii ni safari ya hatari. Muwe waangalifu sana. Msifichue siri hata kwa dawa (uk. 22-23).

Dondoo hili linadhihirisha kuwa ijapokuwa Mundewa alidhamiria kuwatuma watoto hao, lakini alikuwa na wasiwasi dhidi yao, labda kutokana na utoto waliokuwa nao. Kwa hiyo, aliwaonya kuhusu safari hiyo. Katika hali ya kawaida, huwa ni vigumu kwa mtoto kutunza siri, anaweza kudanganywa kidogo au kutishiwa, akatoa siri zote. Mundewa alilitambua hilo kutokana na umri wake na uzoefu katika maisha, ndiyo maana aliwaonya.

Sehemu nyingine inayoonesha onyo alilopewa mhusika, ni wakati wanaelekea kwa Mukwava kupeleka ujumbe. Chulu alimuonya dada yake kuhusu nyoka kutokana na tabia yake ya kutembea akiwa anaburuza miguu. Mwandishi anasema:

> “Jihadhari na nyoka,” Chulu alimtahadharisha Mbumi. “Usikokote miguu kama kigori; kanyaga kwa kishindo kama jimama la Kisagara, Nyoka wakisikia watakimbia!” Mbumi aliitikia kwa kichwa. Siku hiyo alikuwa na maneno machache na mawazo mengi. Hakuhitaji ushauri wa Chulu.
> “Siogopi nyoka naogopa majoka,” alisema.
> Nadhani eneo hili halina chatu,” Mpunza aliwahakikishia. “Watakuwa kule bondeni Lugalo karibu na maji; au maeneo ya Ilundamatwe. Chatu hawakai milimani (uk. 53).

Kutokana na dondoo hilo, utafiti umebaini kuwa Chulu alikuwa na mapenzi ya dhati kwa dada yake, hivyo hakutaka kumpoteza, hasa katika kipindi kama hicho, cha mapambano. Katika mazingira ya kawaida, inasemekana kuwa wakati wa matembezi ya usiku miguu hupaswa kunyanyuliwa na kushushwa kwa kishindo ili wadudu wabaya kama nyoka wasiidhuru, na kusababisha maumivu au kifo.

Utendaji mwingine wa kuonya unadhihirika pale Chulu alipokuwa na dada yake mianzini. Aliona jambo la busara ni kutoka ili kujua mahali walipo maadui. Chulu

alimtahadharisha dada yake asimfuate ili aweze kumsaidia kama litatokea tatizo. Mwandishi anatanabahisha:

> "Sijui Wadachi wameondoka? Chulu aliuliza. "Hawawashi hata taa?"
> "Wakiwasha taa si wataonekana? Nadhani bado wapo."
> "Kweli. Hebu nisogee mbele kidogo niangalie. Wewe subiri hapa," Chulu alitamka huku akianza kusogea.
> "Nisikufuate?"
> "Wewe subiri hapahapa! Siendi mbali. Nateremka hapo chini kuangalia."
> Chulu alianza kuteremka kilima. Kabla hajafika mbali alisikia kitu kama kijiwe kinaviringika majabalini… (uk. 64).

Dondoo hili linadhihirisha namna ambavyo Chulu ameonesha ukomavu wa akili kwa sababu wangeondoka wote wangekamatwa, na angekosekana wa kuwasaidia. Bakize (2020) anasema kuwa maamuzi mengi wanayoyafanya watoto hawa hayafanani na umri wao, kwani wanafanya mambo makubwa yaliyostahili kufanywa na watu wazima. Anaongeza kuwa watoto hawa wamesawiriwa kama vile wamewahi kupelekwa katika mafunzo maalum ya ulinzi na usalama.[5]

Kwa hiyo, katika riwaya hii ya *Ngoma ya Mianzi*, utendaji umefafanuliwa kwa mtindo ambao umesaidia katika kujiandaa kwa vita, kupigana vita, na hata kusherehekea mafanikio baada ya vita.

### 4.2.4 Utendaji wa Kudadisi

Kudadisi ni hali ya kuchunguza ukweli wa kitu (TATAKI, 2013). Hii mara nyingi hutokea pale mtu anapoona kitu kwa mara ya kwanza na akahitaji kukijua kwa undani wake. Udadisi unaweza kuwa mawazoni mwa mtu pale anapofanya tafakuri kuhusu kitu au jambo fulani, au kwa kwuliza mtu mwingine ili amfafanulie. Utendaji huu umethibitika katika sehemu mbalimbali katika riwaya ya *Safari ya Prospa*. Mathalani, baada ya Prospa kushushwa kutoka katika basi, alijikuta ugenini kabisa pasipokuwa na yeyote anayemfahamu. Katika hali hii alijikuta anaanza kudadisi eneo hilo. Mwandishi anatanabaisha:

---

[5]Mahojiano kati ya mtafiti na Leonard Bakize yalifanyika katika ofisi ya mtaalamu huyu iliyopo katika jengo la TATAKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mnamo tarehe 12/02/2020. Bakize ni Mhadhiri Msaidizi na mbobevu wa kazi mbalimbali za fasihi, hususani fasihi ya watoto.

> Alijihisi kulegea miguu. Uchovu ulimwelemea mwili mzima. Akatazama huku na kule akitafuta mahali pa kukaa. Kando, kushoto kwake aliona mapipa yaliyokwisha tolewa lami yamelundikwa sehemu moja. Akatembea polepole, akatengeneza pipa moja vizuri ili lisiviringike, akakaa. Mbele yake, ng'ambo aliona ofisi ya C.C.M. Jengo dogo lililopakwa rangi nyeupe, milango na madirisha yamefungwa. Kulia kwake kulikuwa na hoteli ndogo. Nje ya hoteli, kijana mdogo kama yeye alikuwa anachoma mishikaki (uk. 33).

Katika dondoo hilo Prospa alikuwa akijaribu kudadisi mazingira hayo ili apate mahali pa kupumzika kwani ilikuwa usiku, naye alikuwa mgeni wa eneo hilo. Udadisi wake ulimsaidia kupata sehemu ambayo alikaa na kuendelea kusoma mazingira hayo.

Utendaji wa udadisi pia umedhihirika pale ambapo Sara na wenzake walifika nyumbani kwa Mchau kwa lengo la kumtafuta Merisho. Kutokana na kuaminiwa na wenzake, walimtuma aangalie katika vyumba vya nyumba hiyo kwa kupitia dirishani, kama atamwona Merisho. Wenzake walibaki wamejibanza mahali wakimtazama. Mwandishi anasema:

> Sara alianza kuchunguza nyumba ya uani. Alichungulia kila mahali. Kwa sababu ya joto mapazia yalikuwa hayakufungwa. Katika chumba kimoja kilichokuwa kinawaka taa, Sara aliona watoto wawili wamelala kitandani. Hakuweza kutambua kama ni watoto wa kike au wa kiume (uk. 158).

Katika dondoo hilo tunaoneshwa kuwa udadisi wa Sara ulisaidia kuona watoto ambao hakuweza kuwatambua jinsia yao. Sara anaonekana kumudu kazi ya upelelezi aliyoshirikishwa na Prospa kutokana na kujiamini na kuaminiwa. Nafsi ya kiwango cha ukomavu ilimsukuma kumsaidia Prospa hadi ampate Merisho kama alivyoahidi walipokutana Same.

Katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* wahusika pia wametenda kwa mtindo wa kudadisi. Mathalani, Mbumi alipofika nyumbani kwa Mutwa Mukwava alidadisi namna alivyo katika mawazo yake. Siku zote alikuwa akimsikia tu Mutwa kwa watu katika masimulizi mbalimbali, kwa hiyo, ili kupata ukweli ilibidi adadisi kwa macho yake. Mwandishi anasimulia:

> Mutwa Mukwava aliwasikiliza kwa makini bila kusema neno, mara kwa mara alitingisha kichwa kwa kuafiki. Mbumi kwa upande wake, alikuwa macho kayakaza chini sakafuni, japo kila alipopata fursa alijaribu kumwangalia vizuri Mutwa kwa kuibia. Kwa njia hiyo aliweza kupata picha kamili ya umbile la Mutwa. Aligundua kuwa Mutwa Mukwava alikuwa ni mtu wa makamo wa umri wa miaka kama arobaini. Hakuweza kuona nywele zake kwa sababu alikuwa amefunga kilemba kikubwa cheupe mtindo wa kihehe. Uso wake ulikuwa mweusi, mrefu wa kuvutia lakini ulioficha ukali na ujasiri. Shingo lilikuwa refu, lililosimikwa juu ya mabega mapana ya kiaskari. Alikuwa mrefu lakini hakuwa mnene. Alikuwa amevaa nguo nyeupe kiunoni na mgolole mweupe kwa mtindo wa Kihehe. Sime yake ilining'inia kiunoni. Mikononi na miguuni alivaa mabangili meupe ya pembe za ndovu (uk. 42-43).

Dondoo hili linaonesha namna udadisi wa Mbumi ulivyomsaidia kumfahamu Mutwa kwa umbile lake na mwonekano wa nje. Ni dhahiri kuwa Mbumi aliridhishwa na muonekano huo, ijapokuwa alitamani kuona nywele zake pia. Mwanafunzi CKDOH7 anabainisha tabia ya udadisi kwa watoto. Anasema:

> Watoto wanapenda kujua kila kitu ili kujifunza. Mara nyingi hutumia maswali ya udadisi, ambayo yakijibiwa, huibua swali jingine. Anaongeza kuwa, kama mtu una mambo mengi huenda akakerwa na maswali hayo.

Katika dondoo hilo, mtafitiwa anashadidia tabia ya udadisi kwa watoto ambayo huwasaidia kujifunza mambo mbalimbali. Mtafitiwa huyu amefafanua kutokana na maisha halisi tunayoishi ambapo watoto hupenda kudadisi hasa wanapoona jambo ambalo hawalijui.

Utafiti umegundua udadisi mwingine pale Mbumi na Chulu walipokuwa wanaelekea kwa Mutwa. Njiani walipita vijiji mbalimbali lakini walipokuwa wanakaribia Kalenga waliona idadi ya watu inaongezeka. Walipishana na watu waliotoka ngomeni na walioelekea Kalenga. Katika udadisi wao waligundua vitu walivyobeba. Mwandishi anasema:

> Baadaye Chulu na Mbumi waligundua kwamba mafurushi waliyokuwa wamebeba yalijaa vyakula vilivyokuwa vikipelekwa kuhifadhiwa ngomeni. Kadhalika waligundua kuwa wengi wa wanaume waliokuwa wakienda na kutoka huko huko walikuwa ni askari wa zamu wa kulinda ngome. Hapo wakajua kuwa kweli Uhehe ilikuwa imara, imejiandaa kwa vita (uk. 35-36).

Nukuu hii inathibitisha kuwa watoto hawa walikuwa wadadisi kwa kila walichokiona. Utafiti unaona kuwa mambo yote haya waliyafanya kwa lengo la kujifunza na kujua mengi kuhusu askari hao. Hata hivyo, Mbumi aliendelea na udadisi wake alipofika nyumbani kwa Munzagila kupeleka habari ya kukamatwa kwa Chulu. Baada ya kutoa taarifa, aliambiwa akapumzike ili siku itakayofuata wafanye juhudi za kumwokoa. Hivyo, Munzagila alimkonyeza kijana mmoja wa kiume amwongoze Mbumi kwenda kupumzika. Hapo ndipo Mbumi alipata nafasi ya kudadisi eneo hilo. Mwandishi anafafanua:

> Wakati wanakwenda Mbumi alilitazama boma hilo kwa udadisi. Lilikuwa pana sana. Aliweza kuhesabu nyumba kama kumi za tembe. Kila nyumba ilikuwa imejitenga kidogo, imezungukwa na miti ya kivuli na matunda kama mitowo, misasati na migohola na mipogolo. Katikati ya boma palikuwa na mti mkubwa wa aina ya mukwe ambao ulitandaza matawi yake pande zote kwa staha na mbwembwe. Aliutambua mti huo kutokana na vitu vilivyouzunguka ambavyo alihisi kuwa kwa vyovyote vilihusika na matambiko na masuala mazito ya kiukoo (uk. 71-72).

Nukuu ya hapo juu inadhihirisha namna Mbumi alivyofanya udadisi ili kujiridhisha na eneo hilo lililokuwa geni kwake. Ni kawaida kwa mtu yeyote mgeni, hususani askari au kijana aliyepitia mafunzo, kudadisi mazingira ili kuyajua, na kujiandaa kwa lolote litakaloweza kutokea. kutokana na misingi ya Nadharia ya Saikochanganuzi, Mbumi alisukumwa na matamanio yake kutaka kulijua eneo hilo. Mbumi alikuwa na mipango yake kichwani ya kumwokoa ndugu yake. Alidadisi eneo hilo ili kama atafanikiwa kutoka ajue namna ya kutoka kwa urahisi.

Katika harakati za kusubiri vita, baada ya kugundua makazi ya wavamizi, Mbumi na Chulu walidadisi kuhusu vita hiyo. Kwa kuwa ilikuwa mara yao ya kwanza kupigana, walijaribu kutengeneza taswira vichwani mwao kuhusu vita itakavyokuwa. Mpunza aliwasaidia kujua zaidi na kuwatoa wasiwasi. Mwandishi anafafanua:

> Chulu alimuuliza Mpunza, “Je, vita vitakuwa vikali?
> “Labda lakini tutashinda,” Mpunza alijibu huku akiipapasa na kuigonganisha mikuki yake miwili-lisala na mugoha. Hakuonesha wasiwasi.
> “Kwanini unasema hivyo,” Mbumi aliingilia.
> “Kwa sababu maadui watashtukizwa. Hawajui kuwa tupo hapa.
> Lakini watu wengi watakufa; maadui wana silaha kali sana,” Mbumi alieleza, alikumbuka zile silaha alizoziona Bagamoyo.

> “Hata sisi tunazo, Mpunza alisema huku akipunga mkuki wake. Hakujua chochote kuhusu silaha za Wadachi (uk. 95-96).

Nukuu ya hapo juu, inadhihirisha watoto hawa hawakuwa wakijua lolote kuhusu vita. Zaidi walijua silaha za maadui ambazo waliziona kabla. Mwenyeji wao aliwapa moyo kuwa watashinda, ijapokuwa hakuwa akifahamu kuhusu silaha kali za Wadachi. Ni dhahiri kuwa watoto hawa walikuwa na hamu ya kupigana ili kuikomboa jamii yao. Kutokana na msingi wa tatu wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu wasiwasi, Chulu alikuwa na mashaka na dukuduku kuhusu vita ikiwa watashinda au la.

### 4.2.5 Utendaji wa Kudanganya

Kudanganya ni kusema uongo. Mara nyingi watu husema uongo ili kupata kitu fulani cha muhimu. Wanaosema uongo wanakuwa na uelewa kuwa uongo ni kinyume cha maadili ya jamii husika, lakini huwa inawabidi kufanya hivyo ili kukidhi matamanio yao. Katika riwaya hii wahusika wakuu wamedanganya katika sehemu mbalimbali, lengo ni kufanikiwa katika kile wanachokitamani. Mathalani, Prospa alimdanganya dereva wa gari aliyekuwa anapakia majani ya ngombe katika *pick-up*. Mwandishi anasema:

> Alitembea chapuchapu. Mbele yake aliona pick-up inapakia majani, akakimbia ili awahi kabla haijaondoka. Alipofika alimwona dereva aliyevaa vizuri akiwa na vijana wengine wawili wachafu. Vijana hao walikuwa tayari wameingia kwenye gari. Prospa alimwendea dereva aliyekuwa amevaa vizuri akamwamkia.
> “Nini?” Dereva alimuuliza badala ya kupokea salamu.
> “Nakuomba lifti kaka,” Prospa alisema kwa heshima. Moyo wake ulianza kumwenda mbio.
> “Gari limejaa majani huoni? Dereva alisema. Aliwasha gari na kuingiza gia.
> “Bibi anaumwa kaka nampelekea…” Prospa alianza kukariri haraka.
> “We mtoto huoni majani yalivyojaa? Hakuna nafasi,” dereva alisema kwa sauti isiyokuwa na subira.
> “Bibi anaumwa nampelekea dawa,” Prospa aling’ang’ania… (uk.21-22).

Katika dondoo hilo tunathibitisha kuwa Prospa aliamua kudanganya kwamba anauguliwa ili dereva amuonee huruma. Lengo lake lilikuwa kuondoka katika eneo hilo la TPC ambalo alikuwa akifahamika hadi na walinzi. Kutokana na nafsi tatu za

ki-Freud Prospa alisukumwa na nafsi ya ukomavu iliyomfanya adanganye baada ya kuchunguza wema na ubaya wa tendo hilo. Kwa hiyo, kudanganya kwake kulimsaidia kupata lifti iliyomvusha katika geti la TPC na kuwa nje ya eneo hilo. Hivyo, alijihisi yupo salama.

Sehemu nyingine inayoonesha utendaji wa kudanganya ni pale Prospa alipokutana na Sara na kuamua kuomba lifti ili iwapeleke Dar es Salaam kumtafuta Merisho. Ijapokuwa magari mengi yaliwapita na kuwatimulia vumbi, baadaye msamaria mwema mmoja alisimamisha gari. Sara na Prospa walifurahi kuona gari limesimama, lakini waliwaza watamwambia nini dereva huyo. Katika mazingira hayo ilibidi wadanganye. Mwandishi anasema:

> Sara alimshika Prospa kwa nguvu na kumwambia, "Acha niombe mimi. Uthitheme kitu."
> "Usipopata utaniona," Prospa alimtishia.
> Sara alimwambia mwenye gari, "Baba tunatembea mimi na mdogo wangu kwenda Darithalam. Tuthaidie."
> "Mnatembea? Mmetoroka nyumbani?" Mwenye gari aliuliza.
> Mkono mmoja wa Sara ulimfinya Prospa asije akasema kitu
> Sara alisema, "Hapana baba. Baba yetu yupo Darithalam, thatha mama ametukimbia, amemfuata baba. Nyumbani hakuna chakula."
> "Loh! Nyie watoto mnasema kweli?" Mwenye gari aliuliza.
> Hapana baba, "Hapana baba, ni kweli kabisa."
> "Ingieni," mwenye gari alisema, akawafungulia mlango.

Dondoo hilo linaonesha jinsi watoto hao walivyomdanganya dereva wa gari ili awape lifti. Katika mazingira ya kawaida, watoto wengi hudanganya kwa madereva wanapotoroka majumbani kwao kwa lengo la kwenda kutafuta maisha Dar es Salaam kutokana na ugumu wa maisha. Hata hivyo, Sara na Prospa walisukumwa na matamanio yao ya kutaka kumtafuta Merisho hadi wampate.

Sehemu nyingine inayoonesha utendaji wa kudanganya ni pale walipofika Zanzibar kwa mzee Mohamed kwa lengo la kumtafuta Merisho. Prospa alihisi kuwa Merisho anaweza kuweko huko, kwa sababu alihisi kuwa jirani yao aitwaye Sofia ndiye aliyemchukua Merisho na kumpeleka kwa wazazi wake. Uhakika huu aliupata kutokana na maelezo ya yule mama aliyesema alimwona Merisho akipita na mama mmoja liyejitanda ushungi. Kwa hiyo, walipofika Zanzibar ilibidi wadanganye, kama mwandishi anavyotanabahisha uongo huo:

> Prospa alieleza kwamba Mohamed alikuwa amempa rafiki yake, mkata miwa mwenzake, ili amlete huku nyumbani Zanzibar kwa wazazi wake. Tangu hapo, hajasikia habari za mtoto kufika salama wala rafiki yake kurudi TPC. Jambo hili lilimsumbua sana Bwana Mohamed. Alimwandikia mzee Zinja barua, lakini hakupata majibu. "Kwa hiyo Mohamed ametutuma, yaani, amenituma mimi na Sara amenisindikiza. Tumekuja kuona kama mtoto aliletwa na kama hajambo. Amesema eti nirudi naye kwa sababu Mama Sofia ni mpweke sana bila mtoto" (uk. 90-91).

Dondoo hilo linatuthibitishia kuwa Prospa aliupanga uongo wake ukapangika na kuwa karibu na ukweli. Alichokuwa anafikiria yeye ni kumpata Merisho tu, hakujali madhara yatakayotokea kutokana na uongo wake. Akishadidia suala hili, Lema (khj) anasema kuwa uongo unaosaidia ni mzuri kuliko ukweli usiokuwa na msaada. Akaongeza kuwa Prospa alikuwa na uwezo mkubwa sana wa akili, kwa sababu yote aliyoyasema yalikuwa ukweli kwa wazee wale ambao walikuwa na hamu ya mjukuu kwa muda mrefu.

### 4.2.6 Utendaji wa Kutaarifu

Wakati mwingine, utendaji hufanyika ili kutaarifu kuhusu tukio fulani au jambo fulani. Taarifa hizo huwa ni muhimu katika kusaidia jamii, mtu, au kikundi fulani cha watu. Taarifa pia zinaweza kuikomboa jamii kutoka katika hali duni kwenda katika hali nzuri au kuokoa jamii kutokana na vita, njaa, na masaibu mengine. Taarifa hizi hutolewa na wahusika wakuu au wahusika wakuu hupewa na wahusika wengine. Utendaji huu umedhihirika katika riwaya ya zote mbili. Katika *Ngoma ya Mianzi* mwandishi anaeleza kuwa Mbumi na Chulu waliposhuhudia mtu akipigwa risasi mbele yao, walijawa na huruma, wakamnyanyua na kumketisha kitako. Yule majeruhi alipenda kujua wao ni akina nani, kisha aliwapa taarifa kuwa yeye anaitwa Mutandisi, ni mjumbe kutoka Uheheni, na aliomba kupelekwa kwa Mundewa ili afikishe ujumbe wake. Aliposhindwa kuinuka, aliamua kuwapa taarifa wale vijana, Mbumi na Chulu, akisema:

> "Mwisho wangu unakaribia. Lakini lazima ujumbe nilionao umfikie Mundewa. Mahoka wamenikutanisha na nyinyi vijana. Inabidi niwakabidhi mikoba hii… mutwa wetu Mukwava, kutokana na uchunguzi wake, amegundua kuwa wazungu wanapanga kuja kushambulia na kuyatawala maeneo yote ya Wahehe, Wasagara, Wakaguru, Wamasai na Wagogo… Mkakati wao ni kushambulia kabila moja baada ya jingine, ili tusipate nafasi ya kuungana na

> kuwa na nguvu ya kuwashinda…" Alishika mkuki wake akamkabidhi Chulu na kusema, "Pokea mkuki huu. Ndiyo mkoba wangu, na ndiyo sauti ya Mutwa…" (uk. 13-14).

Dondoo hili linaonesha kuwa Mutandisi alitamani kupeleka taarifa hiyo mwenyewe, lakini kutokana na hali yake kuwa duni, alishindwa. Kwa kuwa ujumbe ule ulikuwa ni muhimu, Mutandisi aliona busara kuwapa taarifa vijana wale kabla mauti hayajamkuta. Mbumi na Chulu walizipokea taarifa hizo na kuahidi kuzipeleka kama walivyoagizwa. Kutokana na nafsi za ki-Freud, watoto hawa waliongozwa na nafsi ya kiwango cha kati inayoongoza matendo ya busara, kufanya matendo yote hayo kwa busara.

Mwandishi pia anaeleza kuwa baada ya Mbumi na Chulu kumhudumia marehemu Mutandisi kwa kuuweka vizuri mwili wake, walikwenda kwa Mundewa ili kumpa taarifa kuhusu marehemu huyo, na kukabidhi mkuki wa Mkuu-wa-Mianzi. Mwandishi anafafanua:

> Walimlaza vizuri mle kichakani, wakamfunika kwa shuka lake, wakatoka pale kwenda kutoa taarifa kwa Mundewa na Wanasokomoko ili taratibu za mazishi na nyinginezo ziweze kufanywa…Mbumi alieleza, "Huyo mwenzio aliitwa Mutandisi. Amekufa kutokana na majeraha aliyoyapata. Kafia pale kwetu. Ila kabla hajafa, alituusia tuwasilishe ujumbe wake kwa Mundewa pamoja na mkuki huu." "Poleni," Mundewa na yule mgeni waliwafariji. "Maiti yuko wapi?" "Pale karibu na nyumbani. Tumeshawaarifu Wanasokomoko wamchukue na kumleta Ikulu," Chulu alieleza (uk. 15-17).

Maelezo katika dondoo hili yanaonesha namna watoto wale walivyofanikiwa kutoa taarifa kwa Mundewa, na kuukabidhi mkuki waliokabidhiwa na marehemu Mutandisi. Mundewa alizilinganisha taarifa hizi na alizopewa na Mwanyenza, akaona zinalingana. Akawasifu watoto wale na kuwaambia kuwa huenda mahoka wamewachagua kubeba mikoba ya Mutandisi.

Kwa upande mwingine, kiongozi wa Wanasokomoko aliwataarifu Mbumi na Chulu wafike Ikulu kwa Mundewa kwa ajili ya kupewa ujumbe wao. Walikuwa na utayari mkubwa wa kuitetea nchi yao na Sokomoko kwa jumla. Walipofika, walifanya maamkizi ya kawaida, kisha Mundewa aliwakaribisha wakae na kuwachunguza kwa makini. Kisha, aliwapa taarifa ifuatayo:

> "Tumekuiteni kwa sababu tunataka kuwatuma. Nchi yetu inakabiliwa na janga. Janga kubwa. Tunataka tuwatumeni katika nchi ya mbali kupeleka habari na kuomba msaada. Je mpo tayari?"
> "Ndiyo," wote waliitikia. Mbumi akaongeza, "Sisi ni wanasokomoko. Tumeapa kutimiza wajibu wetu kwa nchi yetu!"
> "Vizuri. Tumewateua nyinyi kwa sababu tunafikiri, baada ya safari yenu ya Bagamoyo, mnao uzoefu wa kutosha kuliko Wanasokomoko wengine. Aidha, yule marehemu Mutandisi kwa matakwa ya mahoka aliwakabidhi mikoba. Waaidha, Mwanyenza, mjumbe wa Mutwa, bado anaumwa sana; hawezi kufuatana nanyi. Itabidi aendelee na matibabu. Nyinyi bado ni watoto wadogo, lakini wenye upeo na uzoefu wa kiutu-uzima. Na hata lugha za misafara mnaziongea (uk. 20-21).

Dondoo hilo linashadidia na kudokeza umuhimu wa taarifa waliyopewa Mbumi na Chulu katika kipindi hicho walichokuwa nacho. Utafiti uliofanyika uligundua kuwa, katika zama hizo, njia pekee ya mawasiliano ilikuwa ni barua au ujumbe wa mdomo, ambao hupelekwa na watu kwa kutembea kwa miguu umbali mrefu. Ujumbe unapofika, kama ni wa watu wote, itapigwa mbiu ya wito na watu hukusanyika ili waarifiwe kuhusu ujumbe huo. Mwandishi anasema:

> "Mukwava ametuma ujumbe wa urafiki. Sisi tunataka kuitikia ujumbe huo. Zaidi, tunataka kumtahadharisha kuhusu mwenendo wa maadui ambao mmewaona kidogo jana. Inavyoelekea, wanakwenda Uhehe, japo wanatumia njia ya mzunguko – labda kupoteza lengo. Inabidi Mukwava azipate habari hizi haraka ili ajiandae kuwapokea kwa ukarimu wa Kihehe! Je, mtaweza kupeleka ujumbe huu?"
> "Tutaweza!" waliitikia kwa pamoja (uk. 22).

Nukuu ya hapo juu inatuthibitishia umuhimu wa taarifa katika jamii. Katika muktadha huo, taarifa ilitumika kuiweka tayari jamii ya wahehe katika kukabiliana na maadui. Hata hivyo, watoto hao walionesha utayari mkubwa kutekeleza yote waliyoambiwa kwa ajili ya nchi yao, hivyo walikubaliana na Mundewa. Kutokana na mazungumzo hayo, ilibainika kuwa safari hiyo ilikuwa ya hatari, lakini walionesha utayari wa hali ya juu. Hili lilitokana na matamanio ya nafsi zao na uzoefu walioupata walipokwenda Bagamoyo.

Utafiti pia umebaini kuwa baada ya Chulu kukamatwa na askari wa Wadachi kule vichakani, Mbumi alinusurika na kukimbia kwenda kwa Munzagila kumpa taarifa. Alitokwa na jasho jingi, ijapokuwa kulikuwa na baridi kali. Lengo lake lilikuwa ni

moja tu, kufikisha taarifa hii kwa Munzagila mapema sana kabla Chulu hajadhurika. Mwandishi anasema kuwa baada ya kufika na kukaribishwa, Chulu alitoa taarifa ifuatayo:

> "Mheshimiwa Munzagila, nimeleta habari muhimu. Mimi na mwenzangu Chulu tulikuwa njiani kupeleka ujumbe wa Mutwa huko kwetu Usagara, tukaona kundi la watu watokao mbali likiwa limeketi katika mianzi ng'ambo ya mto Lugalo. Tulipotaka kuondoka kuja kuleta taarifa wakatukimbiza. Mwenzangu Chulu wamemkamata lakini mimi nimewatoroka na kukimbilia hapa moja kwa moja kuleta taarifa." (uk. 70).

Kulingana na Nadharia ya Saikochanganuzi inayosisitiza kuwa lugha huakisi michakato ya akilini inayojibainisha katika ndoto, misemo, na usemaji, taarifa ya Mbumi iliakisi michakato ya akilini mwake kutokana na namna alivyoongea. Imebainika kuwa aliongea kwa shauku kubwa ili Munzagila aone umuhimu wa taarifa hiyo. Utafiti umebaini kuwa taarifa hiyo ilikuwa muhimu sana kwa Munzagila, kwani aligundua kuwa tayari maadui walikuwa wamekaribia katika himaya zao, hivyo walitakiwa kujiweka tayari kwa vita.

Sehemu nyingine inayothibitisha utendaji katika mtindo wa kutaarifu ni baada ya Mpunza kuondoka na kuwaacha Mbumi na Chulu mianzini. Kutokana na upelelezi wao, walitamani kujua maadui walipo. Kwa hiyo, Chulu alimwambia Mbumi abaki ili yeye akawaangalie. Hata hivyo, kwa bahati mbaya, Chulu alikamatwa. Mbumi akaamua kupeleka taarifa kwa Munzagila. Alipowasilisha taarifa hiyo, Munzagila alitaka kujua zaidi kile alichokiona. Mwandishi anasema:

> Munzagila alimuuliza Mbumi, "Umesema hao watu walionekana kuwa wageni?"
> "Ndiyo Munzagila"
> "Walikuwa wamevaaje?"
> "Wamevaa nguo zilizochukuana na maumbo yao, kofia, vitambaa miguuni na mifuko ya ngozi nyayoni."
> "Wamechukua nini?"
> "Wamechukua mianzi ya chuma."
> Munzagila na wenzake walitazamana. "Mh," Munzagila alimaka. "Wako kama wangapi?"
> "Wengi tu sikuweza kuwahesabu. Nadhani wanazidi mia."
> "Ni weusi kama sisi?"
> "Ndiyo. Wengine weusi kutuzidi."

> "Hukuona mtu mwenye rangi nyekundu, kama zeruzeru vile, miongoni mwao?"
> "Hapana. Sikuona." (uk. 70-71).

Mtindo huu wa kutaarifu katika dondoo la hapo juu, ulimsaidia Munzagila kujua kuwa watu hao ni askari wa Wadachi. Munzagila aligundua hilo kutokana na maelezo ya namna walivyovaa, kwani hapakuwapo na watu wengine wanaovaa kama wao. Hivyo, Munzagila aliwaambia wazee wenzake wajiweke tayari kwa vita. Mbumi alikuwa na kiu ya kumwokoa kaka yake, lakini Munzagila aliona kuwa siyo suala la haraka. Yeye alitaka watu wake wawe tayari kwa vita. Matamanio ya Mbumi kumwokoa Chulu yalikuwa yanahitaji kutimizwa ili awe na amani.

Utafiti umebaini kuwa taarifa ni za muhimu sana katika kipindi walichokuwa nacho na katika maisha yote kwa jumla. Taarifa zinaweza kuiokoa jamii kutoka katika shida mbalimbali zinazoikabili na kuwainua kiuchumi, kiutamaduni na kifikra. Mathalani taarifa aliyoitoa Chulu mara baada ya kuokolewa na dada yake iliyohusu yale yaliyomkuta baada ya kukamatwa na maadui, kwani zilimkumbusha alivyochapwa na mijeledi ya Wajerumani baada ya kutekwa. Mbumi alikuwa na hamu sana kuzipokea taarifa hizo. Chulu anaeleza:

> "Unajua Mbumi, hivi unavyoniona mgongo wote umevimba.
> "Kwanini?"
> "Kipigo cha Mdachi. Walitaka niwape habari za siri, lakini hawakupata chochote."
> "Uliwaambiaje?"
> "Niliwaambia mimi ni mwenyeji wa kijiji cha hapa karibu na nimekuja bondeni kugema ulanzi. Niliwaambia habari za Mukwava na nyendo zake sizijui, maana mi ni mtoto tu, si askari."
> "Waliamini?"
> "Yaelekea hivyo, maana hawakunipiga tena. Ila askari aliyenichukua pale kwa Mzungu kunileta kwenye boma la wapagazi alinitishia kuwa zile fimbo tano nilizoonjeshwa pale zilikuwa ni za makaribisho tu; kipigo chenyewe cha khamsa-ishirini[6] kingekuwa kesho" (uk. 88).

Dondoo hili linaonesha umuhimu wa taarifa alizozitoa Chulu katika kuwajua maadui. Pia, zinaweka wazi mbinu za Wanasokomoko walizofunzwa, kwamba ikitokea wamekamatwa hawaruhusiwi kutoa siri kwa maadui. Chulu alifaulu katika hili, licha

[6] Kwa mujibu wa Mulokozi (1991) khamsa-ishirini ni ishirini na tano; idadi ya viboko ambavyo Wadachi walikuwa na kawaida ya kuwachapa watu kwa makosa madogomadogo.

ya viboko alivyochapwa. Hata hivyo, uvumilivu na kujitoa kwa Chulu ndiko kulikosaidia kutoka mikononi mwa maadui.

Taarifa nyingine imetolewa na Chulu kwenda kwa Mbumi na Mpunza kuhusu yale aliyoyasikia alipokuwa amekamatwa na maadui. Kwa kuwa Chulu alikaa na maadui hao kwa saa kadha, aliweza kuwasikia wakisimuliana mambo mbalimbali yanayowahusu na yanayohusu kambi yao. Kwa hiyo, Chulu alijua siri za maadui kwa urahisi na bila kutarajia. Mwandishi anasema:

> Chulu aliwasimulia yale aliyoyaona na kushuhudia katika kambi ya maadui. Aliwaarifu kuwa alisikia wale wapagazi wakisema kiongozi mkuu wa msafara aliitwa Nyundo, na kuwa alikuwa mzungu mrefu na mkali sana. Aligundua pia kuwa wale askari weusi hawakuwa wenyeji wa eneo hilo, bali wengine walitoka nchi za mbali kabisa za Sudani na Afrika Kusini. Kilichowasisimua na kuwasikitisha zaidi ni maelezo yake kuhusu namna alivyotandikwa mjeledi; alisema baada ya askari mweusi kumaliza kumchapa viboko vitano vilivyouma sana, aliongeza kiboko kingine cha sita huku akisema kwa kiburi, “ Viboko vya Bwana tayari, hiki sasa ni changu!” (uk. 92).

Kupitia nukuu hii, ni dhahiri kuwa Chulu alikuwa na maumivu makali, lakini aliweza kuwapa taarifa zote zilizotokana na aliyoyasikia na kuyaona katika kambi ya maadui. Taarifa hizo zilikuwa muhimu katika kipindi hicho, kwani wenzake walifahamu namna maadui walivyokuwa wakatili na sehemu walizotoka.

Katika *Safari ya Prospa* mwandishi anatuonesha taarifa mbalimbali. Mathalani, baada ya Prospa kuhojiwa na polisi na kutoridhishwa na maswali yake, ilimbidi kwenda kutafuta taarifa nyingine kwa Mustafa. Prospa alihisi Mustafa atakuwa anamfahamu mtu aliyemchukua Merisho kwa kuwa alikuwa nje ya uwanja wakati yeye akicheza mpira uwanjani. Baada ya Prospa kuumuuliza Mustafa kuhusu mwanamke aliyemuona alifananaje, Mustafa alitoa taarifa ifuatayo:

> “Sikumtazama lakini alikuwa kama bibi hivi. Mzee kidodgo.” Mustafa aliendelea, “Kaja vile, kupitia barabara ya miguu. Aliuliza watoto pale, kwa Josefina Ringo ni wapi? Mtoto mmoja akamwonesha kwa kidole. Mtoto mwingine akamuita Merisho. Sijui alimwambia nini, lakini huyo mama na Merisho waliondoka pamoja” (uk. 16).

Katika dondoo hilo taarifa aliyoitoa Mustafa ilimsaidia Prospa katika kuanza upelelezi wake binafsi wa kumtafuta Merisho. Katika mawazo yake alifikiria wanawake wote waliokuwa wamezoeana na dada Josefina ili ajue wapi pa kuanzia. Kwa hiyo, Prospa aliamua kwenda Dar es Salaam kumtafuta Merisho.

Sehemu nyingine inayoonesha taarifa katika riwaya hii ni pale Prospa na Sara walipokutana na Petro. Walimweleza lengo lao la kwenda Dar es Salaam. Hata hivyo, Petro alitaka kujua wanahisi ni nani aliyemwiba Merisho. Prospa alitoa taarifa ifuatayo:

> Dada ana rafiki yake anayeitwa Sofia na mume wake anayeitwa Mohamed. Walimpenda sana Merisho. Mimi najua tu ni wao walimtorosha. Siku Merisho aliyopotea, mama Sofia hakuwa nyumbani. Polisi walipomuuliza kwamba alikuwa wapi, yeye alisema kwamba alienda mjini Moshi kununua kitambaa cha gauni. Polisi walipomwambia alete kitambaa, alisema hana. Nikajua tu hicho kilikuwa ni kisingizio” (uk. 63).

Dondoo la hapo juu linatuonesha namna Prospa alivyotoa taarifa. Kutokana na kumjua Sofia aliunganisha matukio ya upendo wa Sofia kwa Merisho na kuhisi kuwa kwa vyovyote yeye ndio atakuwa amemchukua. Kutokana na nafsi tatu za ki-Freud zinazotokana na Nadharia ya Saikochanganuzi, Prospa alisukumwa nafsi ya pili inayoongoza maamuzi ya busara kuona kuwa Sofia atakuwa mtuhumiwa wa wizi wa mtoto.

Taarifa nyingine katika riwaya hii ilitolewa na Petro aliporudi katika nyumba aliyopanga, ambapo alikuwa amewahifadhi Prospa na Sara. Baada ya Petro kusikia kuwa wamekuja kumtafuta Merisho, ambaye alikuwa ameibwa nyumbani kwao Moshi alitafuta mbinu itakayowasaidia kumpata. Kwa hiyo, katika mizunguko yake alikuja na taarifa ifuatayo:

> “Enhee. Leo asubuhi niliondoka hapa nikamtafuta huyo ndugu yake Mohamed wa TPC anayeishi Magomeni. Nikampata, kwa njia zangu mwenyewe. Nikamwambia bwana we, yule mtoto aliyeandikwa kwenye gazeti la uhuru kwamba kaibwa huko TPC, ni mtoto wenu. Ni mtoto wa Mohamed aliyezaa nje na msichana wa siri.
> Alaa, ndugu ya Mohamed akasema.
> Nikanogewa na hadithi. Hasa, nikasisitiza. Sasa? Yeye akaniuliza.

Mimi nikamwambia kwamba wazazi wake Mohamed walitaka wamuone mjukuu wao. Sasa, msichana alikuwa hataki kumuachia mjukuu wake. Hapo ndipo Mohamedi na mke wake walipofanya mbinu zao hadi wakamtorosha mtoto. Alaa, jamaa akasema.
Na yeye vile vile alianza kunogewa na mambo. Mimi nikamwambia kwamba kuna vijana hapa, wametumwa na mzee Mohamedi wakaangalie kama mtoto kafika. Lakini mambo ni siri kabisa, kwa sababu polisi bado wanafanya uchunguzi. Hivyo, tulikubaliana kwamba mwondoke mapema iwezekanavyo mwende Zanzibar kwa babu na bibi wa mtoto…"(72-73).

Kutokana na taarifa katika dondoo la hapo juu Prospa aliona mwanga mpya katika zoezi lake la kumtafuta Merisho. Ijapokuwa, katika mawazo yake, na kutokana na mahojiano yake na Mustafa, Prospa alijua kuwa Merisho ameibwa na mwanamke. Kwa upande mwingine Sara alimpa moyo kuwa ni lazima waende Zanzibar kwa kuwa alikuwa na uhakika na mahali alipo Merisho. Sara alisukumwa na nafsi ya pili ya ki-Freud inayoongoza maamuzi ya busara. Aliona ni busara waende Zanzibar, kwa sababu Petro alikuwa ameshawaandalia pasi za kusafiria.

Utendaji wa kutaarifu, pia umedhihirika Sara na Prospa walipofika Zanzibar. Kutokana na ugeni waliokuwa nao, walijikuta wanatembea tu bila kujua kwa usahihi wapi wanapokwenda. Walipofika kwenye magofu ya Kasri ya Sultani Barghash, bila kutegemea walikaribishwa na mzee ambaye alitaka kuwasaidia. Mzee aliwaeleza kuhusiana na Sultani na Masuria wake. Hata hivyo, Prospa na Sara walitaka kupata taarifa zaidi kuhusu Masuria. Mzee huyo aliwapa taarifa ifuatayo:

"Basi niwaelezeni. Uzuri wao ulisifika dunia nzima. Dunia nzima! Sultani aliwachagua kwa makini kama mkulima anavyochagua mbegu. Yenye doa ilibaki, kwani doa laweza kuleta kidonda. Mbegu ndogo isiyokuwa na matumaini ya kuota kwa afya, iliachwa. Aaa, afya ni kitu muhimu maishani, afya yavutia macho haswa, yavuta heri. Mkulima hutazama mbegu kwa makini wanangu, huchagua moja moja, zikiwa changa, kabla hazijaliwa na wadudu waharibifu au kukaushwa vibaya…"(uk. 85-86).

Katika dondoo hilo, taarifa waliyopewa Prospa na Sara iliwasaidia kujua mengi kuhusu Sultani Barghash na Masuria wake. Kwa hiyo, walijikuta wanasahau machungu ya kupotea kwa Merisho kwa muda, baadaye waliendelea na safari yao akili zikiwa na mtazamo mpya.

Sehemu nyingine inayodhihirisha utendaji huu ni pale Prospa na watoto wengine wa mtaani, maarufu kama changudoo walipomuomba Sara ajenge urafiki na Uzuri na kumdodosa kuhusu jirani yao. Sara alijitahidi na akawa rafiki mkubwa wa Uzuri, hivyo alipata taarifa nyingi ikiwa ni pamoja na nyumba anayoishi jirani yao huyo. Baada ya kuijua, Sara alikuja na taarifa ifuatayo kwa wenzake:

> "Lakini kila kitu ni thawathawa. Nyumba naifahamu, ndani na nje. Ni nyumba ya ghorofa, imepakwa rangi nyeupe. Chini kuna thebule, jiko, thehemu ya kulia chakula na chumba cha wageni. Kuna milango miwili inayotoka nje, mlango wa mbele na mlango wa uani. Tutatumia mlango wa uani. Ukiingia mlangoni mtu aliye jikoni atakuona" (uk. 146)

Dondoo hilo linaonesha umuhimu wa taarifa aliyoileta Sara kwa wenzake. Wote waliifahamu nyumba hiyo, hivyo ilikuwa rahisi kupanga mipango yao, ya namna ya kuingia katika nyumba hiyo. Watoto hao walipata mwanga katika upelelezi wao, na taarifa hiyo ilikuja muda muafaka, kwani Prospa alibakiza siku moja ili aondoke kurudi Moshi

### 4.2.7 Utendaji wa Kushauri

Kwa mujibu wa Bakhresa (1992), kushauri ni kupendekeza, kutoa maoni, rai, au nasaha. Kuna wakati mtu huomba ushauri au hutoa ushauri kwa mtu mwingine kuhusiana na jambo fulani. Mara nyingi, anayeshauri huwa ana ujuzi au upeo zaidi, na anayeshauriwa huweza kuwa katika mtanziko kutokana na maamuzi anayotaka kuyafanya. Pia, ushauri unaotolewa unaweza kuzingatiwa au kutozingatiwa kwa kupima faida na hasara zake. Katika riwaya hizi wahusika wakuu wameshauri ama kushauriwa kuhusu mambo mbalimbali, ambayo yamewasaidia katia kufanikisha safari zao. Mathalani, katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* baada ya Mbumi na Chulu kusikia mingurumo na kuona vimweka kwa mbali, waliamua kutoka nje bila kumuamsha bibi yao; lakini aliwasikia. Mbumi hakutaka bibi yao atoke nje, hivyo alimshauri arudi ndani ili kujihakikishia yanayojiri. Mbumi aliongozwa na nafsi ya kiwango cha ukomavu kupima faida na hasara za bibi yao kutoka nje; akaona ni bora asitoke kwa wakati ule hadi watakapohakikisha kile kinachojiri. Mwandishi anasema:

> Vipi mapacha wangu," Bibi alisema.
> "Rudi ndani bibi, kuna baridi huku," Chulu alimshauri.
> "Si baridi, ni moto," Mbumi alimsahihisha. "Nadhani kuna vita."
> "Labda ni wateka watumwa," bibi alisema kwa sauti ya hofu. Alikumbuka rabsha iliyosababishwa na wateka watumwa pale kijijini miaka michache iliyopita (uk. 6).

Katika dondoo la hapo juu tunaoneshwa namna Mbumi alivyomshauri bibi yake akihofia hali ya hewa na afya ya bibi yake. Ijapokuwa, Mbumi alimshauri bibi yake, lakini hakukubaliana naye kwa kuwa alihisi kuna hatari, jambo ambalo lilikuwa ni kweli. Hili linadhihirishwa na mwandishi anaposema kuwa mara walisikia vishindo na mayowe ya watu waliokuwa wakikimbia kutoka kijijini. Majeruhi kadha wa kadha walikuwa wakikimbia huku wakitokwa na damu. Baada ya kuona hali hiyo, Mbumi alitoa ushauri mwingine kwa kusema:

> "Bibi twende!" Mbumi alisema huku akimshika mkono bibi yake na kumvuta ndani. Haraka haraka walianza kukusanya vitu vyao vya thamani. "Wafungulie mbuzi Chulu," Bibi aliamrisha. Chulu aliwafungulia wale mbuzi wawili, halafu akatoka nje huku akiwashikilia kwa kamba. Bibi na Mbumi walikuwa wamekwishatangulia nje, wamesimama wakitazama watu waliokuwa wakikimbia kwa kasi kuelekea kusini kwenye maficho yao ya kijadi (uk. 7).

Ushauri wa Mbumi katika nukuu ya hapo juu ulikuwa na lengo la kuondoka eneo hilo na kurudi ndani ili wakusanye vile vinavyoweza kubebwa. Kutokana na misingi ya Nadharia ya Saikochanganuzi, Mbumi alisukumwa na matamanio ya kutaka kutoka katika eneo hilo ambalo tayari lilionesha hatari. Watoto hawa na bibi yao walitoka nje na kuelekea walikokuwa wanaelekea wanakijiji wengine, lakini ghafla waliona kwa mbali mtu anakuja upande wao akikimbia. Kwa namna alivyokimbia, alionekana kuwa ni majeruhi aliyekuwa anakimbizwa. Chulu alipatwa na shauku ya kumsaidia, lakini Mbumi alimshauri kutosimama kwa kuhofia kuonekana na maadui. Mwandishi anasema:

> Chulu alisema huku akiinuka, "Tumsaidie!" Mbumi alimvutia chini na kumaka kwa kunong'ona, "Usifanye pupa kaka!" Chulu alipoangalia kwa makini aligundua kwa nini Mbumi alikuwa amemzuia kusimama. Mbali kidogo kama mita mia moja nyuma ya yule mtu, watu wawili wenye bunduki walikuwa wakimkimbiza. Ingawa watu hao walikuwa ni weusi, lakini mavazi yao

yalimjulisha mara moja kuwa walikuwa ni askari wa wazungu (uk. 10).

Kupitia dondoo hili, imebainika kuwa Chulu alikuwa na pupa ya kumsaidia mtu huyo bila kuchukua tahadhari, lakini ushauri wa Mbumi ulimsaidia kuwa na subira ili asionekane na maadui. Mbumi alikuwa na maono sana katika mambo yake, lakini Chulu huwa na haraka bila kufikiria jambo kwa kina. Suala la vita linahitaji tahadhari kubwa sana, kwa sababu mara nyingi adui hjificha. Kwa hiyo, mtu akifanya kwa pupa, anaweza kuangamizwa na maadui.

Ushauri mwingine ulitolewa na bibi yao Mbumi na Chulu. Kabla ya kuanza safari ndefu ya kwenda Uhehe, watoto hawa walikwenda kumuaga bibi yao na kuchukua masurufu ya njiani. Kwa kawaida, mtu yeyote anayesafiri safari ndefu anahitaji masurufu ya njiani kwa ajili ya kujikimu. Walipofika kwa bibi, walipewa ushauri huo. Mwandishi anatanabahisha kama ifuatavyo:

> “Wanangu, safari kama hiyo yenu inahitaji ugali wa mtama au ulezi. Hauharibiki hata kwa wiki. Mtakuwa mnamega kidogo mnakula na hayo maziwa. Maji mtapata hukohuko njiani. Chukueni na nyama hii kavu ya mbuzi tuliyokuwa tumeihifadhi. Itawafaa. Tena nilitaka kusahau – kuna na hii mihogo…” (uk. 26).

Katika dondoo hilo, ushauri wa bibi ulikuwa mzuri sana kama mzazi au mlezi kwa wajukuu wake, kwani alitaka wasipate shida njiani. Hata hivyo, alisahau kuwa watoto wale walikuwa na safari ndefu ya kutembea kwa miguu, hivyo, wangeweza kuelemewa na mizigo. Kwa hiyo, walichukua vile tu walivyovimudu kuvibeba.

Vilevile, katika msafara wa kuelekea kwa Mukwava, watoto hawa waliongozana na Mpunza. Walipokuwa mianzini, waliwaona watu wengi, ambao kutokana na mavazi yao, walibaini kuwa ni askari wa Kidachi. Mpunza alitoa ushauri:

> “Tufanye hima. Muda ni mfupi. Mimi nitarejea Iringa sasa hivi kupeleka habari. Nashauri ninyi mrejee kule mianzini tulikokuwa, mjifiche humo hadi nitakaporejea. Nitarudi usiku huu … Mpunza aliwaaga, akashika njia kurejea Iringa (uk. 62).

Nukuu ya hapo juu inaonesha kuwa lengo la Mpunza kuwashauri watoto hao ni kujificha ili adui asiwaone, pamoja na kupumzika kidogo kutokana na safari yao kuwa ndefu. Baada ya Mpunza kuondoka, Mbumi na Chulu walirudi mianzini kama

walivyoshauriwa. Waliona ni busara kufuata ushauri wa mwenyeji wao, ambaye pia amewazidi umri. Hata hivyo, baada ya kukaa mianzini kwa muda mrefu wakimsubiri Mpunza, Mbumi alisukumwa na nafsi ya kiwango cha kati kutoa wazo. Alimshauri kaka yake watoke mianzini ili kujua walipo maadui. Mbumi anasema:

> "Kwanini tunaketi hapa kama mitungi?"
> "Unataka tufanye nini?" Chulu alimjibu.
> "Tunakuwa kama sio wanasokomoko?"
> "Eh?"
> "Kwanini tusitoke hapa mianzini tukaenda huko kilimani kuangalia adui anafanya nini?"
> "Ni wazo zuri," Chulu alimwitikia
> Waliondoka taratibu, kimyakimya, mle mianzini. Chulu alikuwa ametangulia ameshika Mkuki-wa-Mianzi na kiunoni amening'iniza sime yake. Mbumi alimfuata hatua chache nyuma akiwa na sime na kisu. Nje ya mianzi baridi iliyoandamana na upepo ilipenya hadi kwenye mifupa (uk. 63-64).

Dondoo la hapo juu linatufafanulia kuwa Mbumi hakuona busara kuendelea kukaa mianzini, wakati walikwenda kwa ajili ya kupigana. Pia, alitaka wafahamu mahali walipo maadui na jambo wanalolifanya kwa wakati huo. Hata hivyo, baada ya kutembea gizani kwa dakika kadha, Chulu aligundua kuwa kulikuwa na maadui karibu yao; na hivyo, alimsihi dada yake akimbie. Kwa hiyo, ushauri wa Mbumi ulisaidia kufahamu walipo maadui, ijapokuwa Chulu alikamatwa na kuwekwa mateka.

Utafiti pia umebaini kuwa, baada ya vita dhidi ya maadui kuanza, msafara wa Wadachi ulitawanywa na kusambaa maeneo yote. Wazungu kadha walionekana wakiwa na farasi wao. Macho ya kina Mbumi yaliwaona wakipotelea vichakani na kutokea upande wa pili, huku mikononi wakiwa na silaha zao ndogo za moto. Punde, vijana hawa waliona mzungu mmoja anakuja mbio na farasi wake upande wao. Mpunza aliwashauri Mbumi na Chulu kurudi mianzini ili wasionekane. Chulu alimtambua mzungu huyo kuwa ni yule aliyemtesa alipokamatwa. Mwandishi anasema:

> Punde waliona Mzungu mmoja, yule aliyekuwa akiongoza msafara, akiwajia mbio juu ya farasi wake, huku silaha yake ndogo kaiinua juu.
> “Nadhani anakuja upande wetu,” Chulu alisema kwa wasiwasi.
> “Bila shaka,” Mpunza alitamka. “Haraka, rudini mianzini asituone.” Walirudi mianzini na kuchuchumaa huku wakimchungulia yule mzungu.
> “Bado anakuja,” Mbumi alisema. “Akituona tumekufa.”
> “Tuwe tayari kwa lolote,” Mpunza alisema kwa sauti ya chini.
> “Ni Nyundo kamanda wao! Ndiye aliyenitesa!” Chulu alisema kwa sauti ya chini. “Leo atanikoma!”(uk. 99-100).

Ushauri wa Mpunza kwa vijana hawa uliwasaidia kuepuka kuuawa na askari huyo, ambaye alikuwa na silaha za moto. Mapambano yalikuwa makali sana, hatimaye yule mzungu aliuawa na vijana wa Kihehe waliokuwa na hasira kali. Kutokana na msingi wa pili wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu matamanio, ni dhahiri kuwa wapiganaji walifanya jitihada kuhakikisha kuwa wanamwua askari huyo, na hivyo, kukidhi matamanio yao ya kuikomboa Usagara na Wasagara wake.

Kwa upande wa *Safari ya Prospa*, wahusika pia wameshauriwa na kushauri kuhusu mambo mbalimbali. Baada ya Prospa kufanya uamuzi wa kwenda Dar es Salaam alikwenda kumpa taarifa Mustafa ambaye ni rafiki yake wa karibu, aliyezoea kucheza naye. Ijapokuwa Mustafa hakuliafiki suala hilo, Prospa alimhakikishia kuwa kuna ndufu zake wanaoishi huko, hivyo hatopata shida. Baada ya Mustafa kukubaliana naye na kumchangia nauli, Prospa alimpa ushauri ufuatao:

> “Naondoka kesho. Sasa wewe, kesho hiyohiyo mwambie dada Josefina kwamba nimekwenda Darisalam kumtafuta Merisho. Mimi sitamweleza chochote leo. Halafu Mustafa mfuatilia huyo askari.”
> “Agh, yule askari hovyo bwana,” Mustafa alisema.
> “Wewe mfuatilie tu.” Prospa alimsihi. “Mwambie unataka kumsaidia katika uchunguzi, halafu usikilize mambo yake. Usiseme kitu mpaka akuulize swali.”
> “Nitaona.” Mustafa alisema.
> Walikubalian na kushikana mkono wa kwaheri (uk. 17-18).

Katika dondoo hili Prospa alitoa ushauri huo kwa Mustafa kwa kuwa yeye alikuwa ameshafanya uamuzi wa kufanya upelelezi binafsi. Prospa alisukumwa na nafsi ya kiwango cha kati kuona kuwa ni busara kumfuatailia askari kwa sababu walishapeleka taarifa kituo cha polisi. Pia ushauri wa kumwambia dada yake kwamba yeye ameondoka ulikuwa ni sahihi, kwani kwa namna moja ama nyingine

ingempunguzia hofu ya kumtafuta. Kwa wakati huo Josefina alikuwa tayari na majonzi ya kupotelewa na mwanaye, Merisho, kwa hiyo haikuwa busara kumuongezea majonzi zaidi.

Sehemu nyingine inayoonesha utendaji wa kushauri katika riwaya hii ni pale Prospa alipoachwa nyumbani na msichana, ambaye wazazi wake walimkaribisha kwao. Ijapokuwa Prospa aliambiwa asiondoke hadi atakapotafutiwa namna nzuri ya kufika Dar es Salaam, na kuambiwa wachote na maji na kufua nguo zao, Prospa alikaidi. Kwa hiyo wazazi walipoondoka alitoa ushauri ufuatao kwa yule msichana:

> “Wewe nenda uchote maji, na mimi nitafua nguo.”
> Msichana alikubali. Prospa alifurahi.
> Msichana alipoondoka tu, Prospa alichukua mhogo wa kuchemsha walioachiwa kama chakula chao cha mchana, akaufunga kweye jani la mgomba alilolainisha na joto la moto. Prospa aliweka chakula kwenye mkoba ili ale njiani atakaposikia njaa. Akaondoka harakaharaka bila kuaga (uk 43-44).

Dondoo hilo linatuthibitishia namna ushauri wa Prospa kwa msichana aliyebaki naye nyumbani ulivyomsaidia kutoroka. Kwa kuwa Prospa alikuwa ameshaweka nia ya kwenda kumtafuta Merisho Dar es Salaam, hakutaka mtu yeyote akwamishe nia yake. Hivyo, kitendo cha kuambiwa abaki ili atafutiwe namna nzuri ya kufika Dar es Salaam, aliona kinamchelewesha. Prospa alifanya yote haya ili kukamilisha matamanio yake ya kumpata Merisho.

Utendaji wa ushauri mwingine umebainika pale watoto changudoo na Prospa walivyokuwa wanamuuliza sana maswali Sara kutokana na ukaribu wake na Uzuri. Watoto hawa walikuwa wanasubiri muda ufike ili wakaingie katika nyumba yam zee Mchau. Hii ilikuwa ni siri kubwa kati yao, kwa hiyo hawakutaka Uzuri agundue. Kwa hiyo, kila mara walikuwa wakimuita Sara na kumuuliza maswali mbalimbali wakihofia huenda akatoa siri. Sara alichoka, mwandishi anasema:

> Ilipofika saa tano, Sara alichoka kuulizwa maswali. Aliwaambia, “Nyie thatha mtanipa taabu. Nendeni mjini mtarudi thaa kumi” (uk. 149).

Katika dondoo hilo, watoto walisikia ushauri wa Sara na mara moja waliondoka. Sara alisukumwa na nafsi ya tatu ya ki-Freudi inayochunguza uadilifu wa tendo,

wema na ubaya wake kabla ya kulitenda. Aliona ni jambo jema wakaondoka ili muda uende kuliko kuendelea kuwepo na kumsumbua kwa maswali.

### 4.2.8 Hitimisho

Kwa jumla, sehemu hii imefafanua utendaji wa wahusika wakuu wa riwaya teule. Kupitia mjadala huu, imebainika mitindo mbalimbali ya utendaji kama vile kushauri, kutaarifu, kuhoji, kudadisi, kudanganya, kuonya na kushawishi. Mitindo hii ni ya kawaida, ambayo hata katika mazingira ya kawaida inatokea ili kufanikisha mambo mbalimbali. Kwa kuwa tumeshatambua utendaji wa wahusika, sehemu inayofuata inafafanua aina za silika kwa ujumla, kisha aina za silika za wahusika wakuu wa riwaya teule.

## 4.3 Ufafanuzi Kuhusu Aina za Silika kwa Jumla

Aina za silika zinahusishwa na mwanasaikolojia Hippocrates (460- 377 KK). Huyu alianzisha na kuendeleza tathmini ya zamani ya haiba za binadamu na silika kwa kutumia vimiminika ya aina nne: damu, nyongo ya kijani, nyongo nyeusi, na kohozi. Mwanasaikolojia huyu aliamini kwamba afya ya binadamu inategemea ulingano wa vimiminika hivi, na kuna uhusiano kati ya vimiminika hivi na majira ya mwaka. Kwa mfano, makohozi huongezeka kipindi cha baridi na kupungua kipindi cha joto. Sababu za ongezeko hili ni njia mojawapo ya mwili kukabiliana na baridi na mzio. Kwa kawaida, makohozi ni ute unaofanya kazi za kuulinda mwili dhidi ya maambukizi na kuusafisha kutokana na vitu vinavyosababisha mwako. Mwili ukipata baridi, pua na uwazi ndani ya fuvu unaowasiliana na mianzi ya pua zinakuwa hatarini kupata maambukizi ya bakteria (Asamoah, 2018).

Wanasaikolojia wamegawa tabia hizi kama ifuatavyo: moto, baridi, kavu na nyevunyevu. Tabia hizi ziliendelezwa na kuwa aina nne za silika ambazo ni: sangwini, koleriki, melankoli, na flegmatiki. Wanasaikolojia hao walihitimisha kwa kufafanua kuwa, kama mtu ni sangwini ambaye msukumo wake upo katika damu, atakuwa mchangamfu, mwenye upendo, nguvu, na asiye na woga, mwenye huruma na mpenzi wa starehe za kimwili, na huonekana popote alipo kutokana na uchangamfu wake. Kama ni flegmatiki, anasukumwa na makohozi, atakuwa mpole, hana hisia, asiyependa kushirikiana na watu wengine, na mtegemezi. Kama ni koleriki, basi anazalisha nyongo ya njano katika ini, kwa hiyo ataonesha tabia kama

hasira, chuki, na mihemko. Na, kama ni melankoli, basi atakuwa anaendeshwa na nyongo mbaya nyeusi kutoka katika ini, kwa hiyo, siku zote atakuwa hana furaha, mwenye mawazo mengi, mnyonge, na mwepesi kujiua (Larrimore, 2001; Nyongesa, 2004 na Asamoah, 2018). Ili kuyaelewa vizuri makundi haya na sifa zake, jedwali lifuatalo linatoa ufafanuzi kwa muhtasari:

**Jedwali Na 1: Mgawanyo wa Silika na Majira ya Mwaka**

| **Silika** | **Vimiminika** | **Majira ya Mwaka** | **Sifa** |
|---|---|---|---|
| Sangwini | Damu | Kuchipua | Vuguvugu na nyevu |
| Koleriki | Nyongo ya njano | Kiangazi | Vuguvugu na kavu |
| Melankoli | Nyongo nyeusi | Kupukutika majani | Baridi na kavu |
| Flegmatiki | Kohozi | Baridi | Baridi na nyevunyevu |

Mtafiti (2021) limeboreshwa kutoka Nyongesa (2004).

### 4.3.1 Makundi ya Silika

Kutokana na maelezo ya wataalamu hao, silika imegawanywa katika makundi makubwa mawili, ambayo nayo yamegawanyika zaidi katika makundi mawili mawili. Makundi hayo ni wandani (*introverts*) na wasondani (*extroverts*). Wandani, vichocheo vyao hutoka ndani, wana uwezo mkubwa kiakili, na wanatafakari mambo kwa kina. Kwa upande wa wasondani, vichocheo vyao hutoka nje kwa watu wanaowazunguka. Wasondani wana uwezo wa kawaida kiakili, na mara nyingi, huwa hawana aibu na hushirikiana katika kufanya kazi. Wandani wamegawanyika katika makundi mengine mawili: melankoli na flegmatiki. Pia, wasondani wamegawanyika katika makundi mawili: sangwini na koleriki. Kutokana na mgawanyo huo, kwa jumla, tunapata aina nne za silika (Martine na Bobgan, 1992; Larrimore, 2001; Nyongesa, 2004; Flaskerud, 2012; na Asamoah, 2018).

Martin na Bobgan (khj) wanasema kuwa kila silika ina tabia hasi na chanya. Chanya zinaitwa uwezo na hasi zinaitwa udhaifu. Kutokana na kujitambua na kutambua wengine, watu hurekebisha udhaifu wao na kuendeleza uwezo wao ili kuboresha mahusiano yao na wengine. Pia, kwa kuujua uwezo wa kila silika, itasaidia kujua msingi wa kisaikolojia wa tabia za watu. Hata hivyo, uwezo na udhaifu huu unaweza kufanana kwa baadhi ya watu, lakini upo unaojitokeza zaidi na kusaidia kujua silika ya mtu. Ufafanuzi wa silika hizo ni kama ifuatavyo:

#### 4.3.1.1 Melankoli

Kundi hili hujumuisha watu waliopo katika kundi la wandani. Watu hawa wana uwezo mkubwa kiakili ukilinganisha na aina zote za silika. Mtu mwenye silika ya Melankoli kama ilivyobainishwa hapo awali, huendeshwa na nyongo mbaya nyeusi kutoka katika ini, kwa hiyo, siku zote huwa hana furaha, mwenye mawazo mengi, mnyonge, na rahisi kujiua. Kwa mujibu wa Rakmanina na wenzake (2019) na Nazarov (2022), silika hii ina uwezo na udhaifu ufuatao:

Kiuwezo, ni watu wenye hisia za ndani kwa kiasi kidogo, lakini wana uwezo mkubwa katika kuchanganua mambo. Upendo wao ni wa dhati na wenye hisia kali. Pia, wana huruma sana na hawapendi kuona wengine wakionewa. Wapo radhi kujitolea kusaidia wale wasiojiweza na wanawajali sana wenye shida. Hali hii husababisha wawe na imani zaidi wakilinganishwa na makundi mengine. Siyo watu wa majungu, hupenda mambo yenye tafakuri za kina. Wana ushawishi mkubwa, hasa katika masuala ya kiimani. Hivyo, huwabadilisha watu wengi kutokana na mawaidha yao. Ni wepesi kuomba msamaha wanapokosa, na pia, huomba msamaha kwa ajili ya wengine. Watu wa kundi hili, pia, humudu masomo ya sayansi na hesabu, na mara nyingi, hufuata sheria na taratibu zilizopangwa bila kwenda kinyume. Ni wavumilivu sana hata wanapoonewa au kunyimwa haki zao za msingi. Wanapopata maumivu, huyapunguza kwa kulia, na wanapenda sana kutiwa moyo. Ni wasafi na hupanga vizuri vitu vyao. Kwa mfano, chumba chake mara nyingi huwa na mpangilio mzuri na kinavutia. Siyo wafuatiliaji wa masuala ya watu wengine bila sababu ya msingi.

Udhaifu wa melankoli ni kutojiamini. Mathalani, wawapo darasani, huwa wazito kunyosha mkono kujibu maswali. Mara nyingi, huhesabu kushindwa kuliko kufanikiwa. Mfano, akitaka kuanzisha biashara, anawaza, “itakuwaje kama nitaibiwa?”, badala ya kuwaza, “itakuwaje nikipata faida?”. Huwa ni watu wenye mawazo sana, kwa hiyo, huathiriwa sana na magonjwa ya shinikizo. Mioyo yao hujeruhiwa kwa urahisi, kwa sababu ya kulimbikiza mambo mengi yaliyopita. Ikiwa baba na mama ni wa kundi hili, watoto wao huwa na ndoto za kufanikiwa haraka, lakini wachache ndio hufanikiwa. Pia, wazazi wa kundi hili siyo wepesi kuadhibu, hivyo, husababisha watoto kuharibikiwa. Ni waoga kuanzisha jambo kama biashara, wakihofia kushindwa. Hivyo, wengi wao huishia kuwa masikini kiuchumi. Endapo

atakosolewa kwa kufanya jambo fulani, hukata tamaa, badala ya kujirekebisha. Pia wana aibu sana.

#### 4.3.1.2 Flegmatiki

Silika ya Flegmatiki hujumuisha kundi la wandani ambao wana uwezo mkubwa kiakili baada ya kundi la melankoli. Flegmatiki anasukumwa na makohozi, kwa hiyo, imesemwa hapo awali kuwa mara nyingi atakuwa mpole, asiyependa kushirikiana na watu wengine, na mtegemezi. Ni kundi lenye watu wachache sana ikilinganishwa na makundi mengine. Ali, Islam, na Hamdard (2007) wanasema kuwa watu wa kundi la flegmatiki wana uwezo na udhaifu ufuatao:

Kwa kuanza na uwezo: wana hisia za ndani za hali ya juu, ni watulivu na mara nyingi hupenda kujitenga. Wakilinganishwa na aina nyingine zote, kundi hili lina watu watulivu sana wenye kupenda amani na suluhu. Kutokana na sifa hii, wengi huwa viongozi wa dini, na hivyo, hutumika kuleta amani palipo na chuki. Hawa ni wazuri sana katika kujenga hoja. Hivyo, kama ni mtoto amekosa, ukimpa nafasi ya kujieleza, ni vigumu kuadhibiwa. Pia, wanapenda kukaa mbali na matatizo, na hawana hasira. Wana maisha ya kawaida, na ni wasikilizaji wazuri. Hili ni kundi lenye watu wasuluhishi wa migogoro mbalimbali katika jamii.

Kwa upande mwingine, udhaifu wao ni kupata shida katika kuzoea watu au hatua fulani za kufanya jambo. Hufanya kazi, lakini hupoteza muda mwingi kwa kukaa chini; na hivyo, huchelewesha kazi. Mara nyingi, hupenda kuahirisha jambo hata kama ni la lazima na muhimu. Pia, ni wakali sana wanapochokozwa. Udhaifu huu unawafanya wawe watu wa kujitenga mara kwa mara.

#### 4.3.1.3 Sangwini

Silika hii ipo katika kundi la wasondani wenye uwezo wa kawaida kiakili. Wen na wenzake (2019) wanabainisha kuwa kundi hili hutawaliwa na kichocheo cha *haimma* ambacho hupatikana katika damu. Kichocheo hicho husababisha damu kuwa na hewa nyingi, na hivyo, humfanya mtu kuwa na msisimko mkubwa. Hali hii husababisha kuwa mchangamfu, mwenye upendo, mwenye nguvu na asiye na woga, mwenye huruma na mpenzi wa starehe za kimwili, na huonekana popote alipo kutokana na kupenda sana kuongea na kila mtu. Kutokana na uchangamfu wao,

masangwini wengi huishia kuwa wanasiasa na wasanii. Kwa mujibu wa Crey (1981) na Howart (1988), uwezo mwingine wa sangwini ni huu ufuatao:

Ni watu wanaopenda kujichanganya na kuwazoea watu kwa haraka sana. Sangwini hujiamini na kuaminiwa kwa kila jambo hata kama analolifanya haliko sawa. Ni watu wenye matumaini katika maisha, hukasirika mara moja kisha hurudia katika hali yake ya kawaida kwa kipindi kifupi, hivyo, hawana vinyongo. Hujenga urafiki kwa haraka kutokana na uchangamfu wao, hivyo, hupata marafiki wengi na huwatunza wasipotee. Pia, humpendeza kila mtu kwa sababu mtu akikaa naye hawezi kuchoka.

Sifa nyingine ni kuwa na maamuzi ya haraka. Wanapopatwa na jambo lenye kuwaudhi au linalohitaji kufikiria sana, hufanya maamuzi ya haraka. Ni wasafi, nadhifu na muda mwingi hupenda kuvaa nguo zenye rangi za kung'aa. Kutokana na unadhifu wao, ndiyo maana hupenda kuonekana na kila mtu. Hawarubuniki kimapenzi, kwa sababu ni waongeaji sana. Hupenda sana kusaidia watu, lakini kwa kujionesha. Pia, wanadharau sana na hujiona wao ni bora kuliko watu wengine.

Udhaifu wao ni kuongea kwa sauti kubwa ili waonekane kwa wengine kwamba wapo, lakini hawatunzi kumbukumbu. Hawawezi kuzuia hisia zao. Wakikasirika ni rahisi kuwatambua, na wakipenda huonesha upendo, hufanya hivyo kwa haraka sana. Pamoja na upendo wao, wanaweza kuwa na uhusiano wa kimapenzi na mtu zaidi ya mmoja. Pia, hujisukuma kufanya jambo kwa kuwa mara nyingi hawapendi kufanya kazi, wanapenda kazi rahisi zisizoumiza sana kichwa kwa kufikiria. Wana kigeugeu, na hawana msimamo katika maamuzi yao. Anapoamua jambo, ni rahisi kubadilika endapo atashawishiwa japo kidogo. Mara nyingi, huanika mambo yao kwa watu wengine hata kama wamefahamiana kwa kipindi kifupi, na wakati mwingine, husema uongo. Kwa hali hii, siyo watunzaji wa siri, hivyo, huwa wasaliti. Wengi wao ni wavivu katika kufanya kazi, lakini wanapenda sana starehe. Huwa na ndoto za kufanikiwa kimiujiza. Wakikaa na watu hupenda kuzungumzia mafanikio, kwa mfano, kwenda nje ya nchi, au kumiliki gari zuri. Hata hivyo, huwa hawana bidii zozote za kutafuta kutokana na uvivu. Ni watumiaji wazuri sana wa pesa, na hivyo, hawajui kupanga bajeti. Kwa hiyo, matumizi yao huwa ni ya kiholela. Ni watu wasiokuwa na nidhamu, na wana hasira za karibu.

#### 4.3.1.4 Koleriki

Kundi hili lina watu ambao wapo katika kundi la wasondani. Tofauti na sangwini, watu wa kundi hili wana uwezo mkubwa kiasi kiakili. Koleriki huzalisha nyongo ya njano katika ini. Kwahiyo, huonesha tabia kama vile hasira, chuki, na mihemuko. Howart (1988) anabainisha uwezo na udhaifu wa kundi hili kama ifuatavyo:

Ni watu jasiri sana. Wanafaa sana kuwa viongozi, kwa sababu ya ushawishi walionao na kwa sababu hutawala wenzao muda wote. Kwa kuwa wanatoka katika kundi la wasondani, ni rahisi sana kukabiliana na mtu yeyote ili wamshawishi katika lile wanaloliamini na hawapendi kudharauliwa na watu wengine. Kutokana na tabia yao ya kupenda kuthubutu, wengi wao huwa matajiri. Ni watu wanaojitegemea katika mambo mengi. Pia, wana maono. Kwa mfano, wanaweza kutabiri kitu, kikatokea kutokana na maono yao. Mara nyingi wafanyapo jambo huwaza watafanikiwaje, na kama jambo halina mafanikio hawawezi kulifanya. Hutumia pesa zao nyingi katika kuwekeza kuliko kustarehe ukilinganisha na sangwini, ambao ni watu wa starehe sana. Panapotokea ghasia mahali, watu wa silika hii hutumiwa kuzizima au kuanzisha jambo lenye upinzani. Hii ni kutokana na ushawishi walio nao.

Uwezo wao mwingine ni kuwa watu wa vitendo kuliko maneno. Hujali sana hisia za watu. Wakifuatwa kwa ajili ya ushauri, maoni yao husikilizwa kwa makini, na wakati mwingine, hulivaa suala la mtu kupima anavyojisikia. Wanapenda mazingira yanayovutia. Hupanda miti na maua katika maeneo yanayowazunguka. Hata watembeapo, hupenda maeneo yenye mazingira mazuri na yanayovutia. Pia, hawapendi kushirikisha watu wengine mambo yao. Wana nguvu sana, hivyo, hutamani na hufanya kazi za nguvu hata kama zikiwa ni za kushtukiza, kwa sababu hawana muelekeo maalum.

Udhaifu wao hudhihirika katika mambo mbalimbali ambayo ni: siyo watu nadhifu sana ukiwalinganisha na sangwini, kwa sababu muda mwingi wanawaza kazi na kufanikiwa tu, na hawapendi starehe. Wanapofanya jambo, hata kama halipo sawa, hawataki kukosolewa; na hivyo, kama ni kiongozi, huwa ni dikteta kwa maana ya kuwa lile alisemalo, ndilo la mwisho. Hawapendi kupingwa wala kukosolewa. Hawana tafakuri za kina, kwa sababu uwezo wao kiakili ni wa wastani. Pia, ni

vigumu sana watu wa silika hii kuombwa suluhu. Hivyo, huishi kwa visasi na kinyongo katika maisha yao yote. Pia, siyo watu wa amani. Ni waonevu kutokana na ubabe walio nao. Hawana huruma wala unyenyekevu kwa watu wengine. Pia, wana hasira sana, na ni wajeuri. Hawapendi sana kusaidia wengine, kwa sababu wanaposaidia wanawaza watakirudishaje kile walichokitoa. Hawana hisia kali, hasa za mapenzi, na hawajui kubembeleza wala kuchekesha.

**Jedwali Na 2: Muhtasari wa Aina za Silika na Sifa zake**

| **Kipengele cha Uwezo na Udhaifu** | **Aina ya Silika** | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Melankoli** | **Flegmatiki** | **Sangwini** | **Koleriki** |
| Uchangamfu | XX | X | √√ | √ |
| Ukaidi | √ | √√ | XX | X |
| Kujenga urafiki | XX | X | √√ | √ |
| Ubinafsi | XX | X | √√ | √ |
| Kujiamini | XX | X | √ | √√ |
| Ufanisi | √ | √√ | **XX** | **X** |
| Kujionesha | X | X | √ | √√ |
| Kujitegemea | X | XX | √√ | √ |
| Kutulia mahala pamoja | √√ | √ | XX | X |
| Hasira | √√ | √ | XX | X |
| Upole | √ | √√ | XX | X |
| Unadhifu | XX | X | √√ | √ |
| Mabadiliko | XX | X | √√ | √ |
| Uoga | √√ | √ | **XX** | **X** |
| Uthubutu | X | XX | √ | √√ |
| Hisa ya akili (IQ) | √√ | √ | XX | X |
| Kuchanganua mambo | √√ | √ | XX | X |
| Majungu | XX | X | √√ | √ |
| Ujasiri | X | X | √ | √√ |
| Uvivu | XX | X | √√ | √ |

Mtafiti (2022).

Ufunguo:

√√ = Chanya sana
√= Chanya
XX= Hasi sana
X = Hasi

Kupitia jedwali la hapo juu ni dhahiri kuwa kila silika ina uwezo na udhaifu wake. Alama √√ ina maana kuwa uwezo wake ni wa kiasi kikubwa kwa silika husika. Alama √ina maana kuwa uwezo huo upo kwa kiasi kidogo katika silika hiyo. Kwa mfano, udhaifu wa majungu umejitokeza kwa kiasi kikubwa katika silika ya sangwini, lakini kwa kiasi kidogo kwa koleriki. Kwa hiyo, watu wa kundi la sangwini wana majungu sana ukilinganisha na koleriki. Kwa upande mwingine, alama XX ina maana kuwa uwezo huo haupo kabisa katika silika husika, ilihali alama X ina maana kuwa siyo kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, uchangamfu haupo kabisa kwa melankoli, lakini kwa flegmatiki haupo kwa kiasi kidogo. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa melankoli siyo watu wachangamfu.

Baada ya kutambua aina za silika kwa jumla, na sifa za kila silika, sehemu inayofuata inajadili aina za silika za wahusika wakuu katika riwaya teule. Kwa mujibu wa Ekstrand (h.t), kila mtu ana chembechembe za aina nne za silika, ingawa moja hujitokeza zaidi na kufuatiwa na nyingine. Kutokana na ujitokezaji huo wa aina mojawapo ya silika, ndipo tunaweza kusema kuwa mtu fulani ana silika fulani. Hili pia linajitokeza kwa wahusika, ambao ni wawakilishi wa binadamu wa kawaida. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, kila mhusika ana silika yake ambayo humtofautisha na mhusika mwingine.

### 4.3.2 Aina za Silika za Wahusika Wakuu katika Riwaya Teule

Lengo la mjadala wa sehemu hii ni kuwasilisha na kujadili data zinazohusu aina za silika za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto katika riwaya teule. Hoja kuu ya sehemu hii ni kuthibitisha kuwa kila mhusika mkuu katika riwaya husika ana silika yake inayomtofautisha na mhusika mwingine wa riwaya hiyo. Hata hivyo, ili kuielewa zaidi sehemu hii na kuleta muwala, aina za silika kwa jumla zimebainishwa. Kwa hiyo, sehemu hii ina muumano na sehemu iliyotangulia, kwa sababu utendaji ndio unaotusaidia kujua silika ya mtu.

Mlaga (2017) anasema kuwa wahusika ni kipengele muhimu cha kimuundo kutokana na sifa zao kwa namna walivyoumbwa. Umbo hilo lina nafasi kubwa katika muundo wa kazi nzima ya Fasihi. Katika riwaya ya *Safari ya Prospa* kuna wahusika wakuu wawili, wa kike na wa kiume. Mwandishi amewachora wahusika hawa kwa namna ambayo inatufundisha kuwa watoto wadogo wasidharauliwe na wapewe nafasi katika

maamuzi. Utafiti umebaini kuwa wakati anaandika kitabu hiki, mwandishi alizama katika jamii kwa kuangalia shida wazipatazo watoto. Matukio ya watoto wa mitaani aliyashuhudia mwenyewe na kuyaweka katika maandishi. Hivyo, kwa kuona hayo, mtoto atavutiwa kusoma kitabu hiki. Zaidi, utafiti ulibaini kuwa mhusika mkuu ni Prospa, kwa sababu ndiye anayekwenda kumtafuta mpwa wake, lakini kazi hiyo asingeweza kuifanya peke yake, hivyo akaona aambatane na Sara. Kutokana na umuhimu wa Sara katika kuyasukuma mbele maudhui yaliyokusudiwa, anakuwa mhusika mkuu wa pili. Kwa hiyo, Sara anakuwa mshauri wa Prospa katika mambo mengi na wanashirikiana bega kwa bega.

Pamoja na sifa hizi za wahusika, kila mmoja ana silika yake ambayo inamtambulisha namna alivyo na kumtofautisha na mhusika mwingine wa riwaya hiyo. Zifuatazo ni silika za wahusika hao:

#### 4.3.2.1 Silika ya Prospa

Prospa ni mhusika ambaye alikuwa na jukumu la kucheza na Merisho mara zote alipokuwa nyumbani. Kwa hiyo, baada ya kugundua kuwa Merisho amepotea, alipata wazo la kufanya upelelezi kwa kuwa majibu ya polisi hayakumridhisha. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa mhusika huyu ana silika ya melankoli. Kundi hili hujulikana kama wafikiriaji wa ndani. Ni wazuri katika kushughulikia matatizo magumu kwa ajili ya wengine. Mwandishi amempa sifa ambazo zinamweka katika kundi hili. Prospa ni mtu mwenye uwezo mkubwa kiakili, anawaza kwa kina na kupata ufumbuzi kwa haraka. Mwandishi anaeleza kuwa baada ya Merisho kupotea na kutoa taarifa polisi bila mafanikio, usiku ule aliwaza sana. Prospa alikata shauri kufanya uchunguzi wake mwenyewe. Uchunguzi huo alipanga uwe wa matendo zaidi kuliko maneno. Aliamua kumtafuta Merisho hadi ampate (uk. 15). Huu ni uwezo mkubwa kiakili, hasa ikilinganishwa na umri wake. Pia, Prospa wakati anaongea na Mustafa, alionesha uwezo mkubwa kiakili alipomwambia kuwa ameamua kufanya uchunguzi wake mwenyewe na kumwomba amsaidie. Palepale, alianza kumhoji Mustafa maswali na mahojiano yao yalikuwa kama ifuatavyo:

"Hebu niambie Mustafa, huyo mwanamke alifananaje usoni? Ulimwona vizuri?"
"Sikumtazama, lakini alikuwa kama bibi hivi. Mzee kidogo."
Mustafa akaendelea, "Kaja vile, kupitia barabara ya miguu. Aliuliza watoto pale, kwa Josefina Ringo ni wapi? Mtoto mmoja akamuonesha kwa kidole. Mtoto mwingine akamuita Merisho."
"Ehe"
"Sijui alimwambia Merisho nini, lakini huyo mama na Merisho waliondoka pamoja."
"Ulisikia Merisho akiniita?"
"Hapana. We ulisikia akikuita?"
Prospa hakujibu. Alimshika Mustafa mkono wakatembea kwenda mbali na nyumbani kwao, mbali na watoto wengine, na kumueleza Mustafa haja yake ya kwenda Darisalam (uk. 16-17).

Imebainika kuwa lengo la Prospa kumhoji Mustafa ni kupata taarifa ambazo zingemsaidia katika kuanza uchunguzi wake. Pia, kitendo cha kumshika mkono Mustafa na kumpeleka mbali na nyumbani, na watoto wenzake ili amwambie haja yake ni akili ya hali ya juu, kwa sababu watoto wana tabia ya kuropoka kwa sauti ya juu. Kama wangesikia, ingekuwa shida kwa Prospa. Huenda asingepata kile alichokitaka. Hili linatibitishwa na nafsi ya pili ya ki-Freud inayotokana na Nadharia ya Saikochanganuzi. Hapa, Prospa amesukumwa na nafsi hiyo inayoongoza maamuzi ya busara. Shima (2020) anaeleza kuwa Prospa ni kijana mwerevu mwenye maamuzi ya busara ambaye pia anafanya maamuzi ya haraka. Alisisitiza kuwa, mara zote anapoamua jambo, hataki kurudishwa nyuma.[7] Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, jambo alilolizungumza Shima (khj) lina ukweli kutokana na data zilizopatikana.

Mwandishi anaendelea kusawiri uwezo mkubwa wa kiakili aliokuwa nao Prospa kutokana na uamuzi anaoufanya. Jambo hili linasisitizwa na Masek na Yamini (2011) wanaposema kuwa watu wenye silika ya melankoli wana fikra za kina ambazo ni pamoja na ujuzi katika vipengele vya kuchanganua hoja, kuhukumu au kutathmini, na kufanya maamuzi au kutatua matatizo. Mwandishi anatuonesha kuwa Prospa alipofika Same, muda ulikuwa umeenda sana na njaa ilikuwa inamuuma na kuamua kula. Anasema:

[7] Mahojiano kati ya mtafiti na Getruda Shima yalifanyika katika ofisi ya mtafitiwa iliyokuwepo katika jengo la taaluma katika ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii, Chuo Kikuu cha Dodoma, mnamo tarehe 16/06/2020. Shima alikuwa ni Mhadhiri Msaidizi katika Chuo hicho na mtafiti wa Fasihi ya watoto.

> Baada ya kula ugali na maharage, chakula kilichokuwa cha bei nafuu kuliko vingine, Prospa alitembea tena mjini Same. Alitembea tu bila kujua wapi alikokwenda. Alipopita barabarani aliona vijana wa umri wake wakicheza hapa na pale. Aliliona duka moja lililokuwa na baraza kubwa, akajiambia kwamba atalala pale. Mwanga wa taa ulimulika kila mahali, lakini hakujali. Prospa aliendelea kutembea akingoja watu wapungue barabarani, waingie majumbani mwao. Hakuwa na saa, kwani usiku na mchana ndio ulioelekeza mwenendo wa safari yake (uk. 47).

Kwa mujibu wa Nadharia ya Saikochanganuzi kupitia msingi wa kwanza unaosisitiza umuhimu wa mahitaji, Prospa alipata chakula na kushiba, hivyo, alikuwa anahitaji sehemu tu ya kulala. Mwandishi anaonesha kuwa Prospa alipata mahali pa kulala, na alilala, anaposema:

> Prospa alirudi kwenye mapipa ya lami, akakaa. Alisema, “Merisho, Merisho, tutaonana eh.” Alijaribu kuongea, lakini hata mambo ya kuongea yalikwisha kichwani mwake. Wakati mwingine akili yake ilikataa kufanya kile alichotaka kufanya. Alijisikia amechoka kupita kiasi. Aliona nafasi katikati ya mapipa mawili iliyofichika pande tatu. Aliingia kwenye nafasi hiyo, akaweka mkoba wake chini, mwishoni mwa pembe iliyofichika akajilaza kwenye vumbi. Aliweka kichwa chake juu ya mkoba akautumia kama mto. Palikuwa na joto zuri. Muda si mrefu, Prospa alilala fofofo (uk. 35).

Dondoo la hapo juu linatuonesha uwezo mkubwa wa kiakili aliokuwa nao Prospa, pamoja na magumu aliyokuwa anayapitia katika safari yake. Prospa alijipumzisha katikati ya mapipa mawili, sehemu ambayo aliona itamfaa kwa usiku ule kwa kuwa alikuwa mgeni eneo hilo.

Imebainika kuwa Prospa ana upembuzi yakinifu anapotaka kufanya jambo. Hii ni sifa nyingine ya watu wa kundi la melankoli. Hafanyi jambo kwa kukurupuka, hufanya upembuzi wa kina kabla hajaamua kulifanya. Hii inatokana na akili nyingi alizokuwa nazo. Mwandishi anathibitisha hilo, pale Prospa alipokuwa katika stendi ya mabasi mjini Moshi, ambapo njaa ilikuwa inamuuma na alikuwa na hamu ya chokoleti. Alipoulizia, alishtuka kuona inauzwa bei kubwa. Baada ya kufanya upembuzi wa kina, aliamua kununua biskuti. Mwandishi anasema:

> "Prospa alitamani sana chokoleti lakini aligundua kwamba biskuti ni bei nafuu. Pia, biskuti ni nyingi kwenye kasha kuliko chokoleti. Alitoa noti ya shilingi mia mfukoni, akampa mvulana, halafu akachagua boksi la biskuti" (uk. 24).

Nukuu ya hapo juu inatuthibitishia upembuzi yakinifu aliokuwanao. Alijaribu kufanya ulinganisho wa vitu viwili kutokana na wingi na gharama zake, hivyo alifanya uamuzi sahihi kununua biskuti. Kutokana na msingi wa kwanza wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu mahitaji, Prospa alihitaji chakula ili aweze kuendelea na safari yake. Iwapo asingekidhi hitaji hili, huenda asingeweza kusafiri, kwa sababu njaa ingemuuma sana. Katika mazingira ya kawaida, mtu akiwa na njaa kwa kiasi kikubwa, hawezi kufanya kitu chochote kwa sababu viungo vya mwili vinategemeana. Kwa mfano, mwanafunzi akiwa na njaa, ni vigumu kumsikiliza mwalimu darasani.

Mwandishi anaendelea kusisitiza upembuzi yakinifu wa Prospa katika ukurasa wa 77, pale Prospa na Sara walipokuwa ndani ya meli juu ya maji wakielekea Zanzibar. Anafafanua:

> Mawazo ya Prospa yalikuwa juu ya maajabu ya bahari. Je bahari imetoka wapi? Ina mwisho? Na kama ina mwisho, ukoje na uko wapi? Haya mawimbi yanasababishwa na kitu gani? Ni kwanini bahari inaonekana ina rangi ya kijani au buluu, ambapo maji yenyewe hayana rangi hizo? Prospa aliwaza sana. Bahari inazungukaje dunia? Maji yote haya yalitoka na yanaendelea kutoka wapi? Walikuwa wamefundishwa shuleni kwamba maji ya bahari yanatoka kwenye mito. Lakini kweli inawezekana maji yote haya kutoka kwenye mito peke yake? (uk. 77-78).

Utafiti uliofanyika umebaini kuwa haya ni mawazo yenye upembuzi wa hali ya juu ambayo Prospa alikuwa akiyafikiria alipokuwa safarini kuelekea Zanzibar. Jambo hili linatiliwa mkazo na Lema (2020) kwa kusema kuwa tafakuri ya Prospa ilikuwa ya hali ya juu ambayo mara nyingi hutokea kwa watu wanaosafiri kwa njia ya maji kwa mara ya kwanza.[8]

Sifa nyingine ya watu wa kundi la melankoli ni kuondoa machungu wanapoumizwa kwa machozi, yaani hulia haraka. Imebainika kuwa Prospa aliumizwa sana na suala

[8]Mahojiano baina ya mtafiti na Elieshi Lema yalifanyika Februari 17, 2020 ofisini kwa mwandishi katika eneo la Africa-sana jijini Dar es Salaam. Lema ni Mkurugenzi wa kampuni ya uchapishaji na ni mwandishi wa kazi mbalimbali za Fasihi.

la kupotea kwa mpwa wake. Baada ya kufika Zanzibar na kupokelewa na wenyeji wao, Prospa hakuona dalili ya kuwapo kwa Merisho. Jambo hili lilimpa mawazo mengi ambayo yalimfanya asikie sauti ya Merisho akilia. Mawazo haya yalisababisha asikie kitu kimemkaba kooni. Mwandishi anafafanua jambo hili kwa kusema:

> Labda Merisho amefariki? Hapana. Haiwezekani, Prospa alijiambia haraka kama vile kufukuza wazo hilo. Alisikia kitu kimembana kooni. Alisikia uchungu. Machozi yalimjaa machoni, yakadondoka yenyewe. Alifuta machozi haraka. Hakutaka watoto waliokuwa wanacheza wamuone analia. Dada Josefina alishamwambia kwamba wanaume hawalii hovyo hovyo. Lakini alijisikia vizuri baada ya kulia, kwani maumivu yaliyokuwa kooni yalipungua (uk. 95).

Utafiti umebaini kwamba jambo hili limetokea kutokana na silika yake, kwani baada ya kulia, machungu yalipungua na akapata nguvu zaidi ya kumtafuta ndugu yake. Katika mazingira ya kawaida, inaaminika kwamba mtu anapopatwa na hasira au jambo lolote lenye uchungu, akilia, uchungu huo hupungua. Wengine hupunguza uchungu kwa kuwasimulia watu wengine yale yaliyowasibu katika maisha yao.

Mwandishi pia anaeleza kuwa Prospa alipokuwa anaendelea na harakati za kumtafuta mpwa wake alipitia changamoto nyingi, lakini aliumia sana pale kaka yake Petro alipomwambia, “Ukitoka Zanzibar urudi Moshi” wakati Merisho alikuwa bado hajapatikana. Prospa alikuwa na mawazo mengi sana, hakujua aende wapi ili aweze kumpata Merisho. Mwandishi anasema:

> Prospa aliwaza kwa muda mrefu, lakini mawazo yake yalizunguka mahali pamoja tu: “Niende wapi? Niende wapi? Niende wapi? Alisikia kitu kinamkaba kooni. Alisikia uchungu mkubwa. Alisikia joto kila mahala mwilini mwake, akahisi kifua chake kimevimba. Kwikwi za kilio zilimtoka kwa nguvu, zikasababisha maumivu makali kooni na kifuani mwake. Prospa alilia akapiga kelele kwa uchungu. Kwikwi zilimkaba akawa kama anapoteza pumzi. Sara alikuja akikimbia aliposikia kelele za Prospa. Alipofika alimtazama Prospa kwa mshangao (uk. 108-109).

Ni dhahiri kuwa Prospa alikuwa na uchungu mwingi, lakini uliondolewa na kilio. Pamoja na Sara kumbembeleza na kumwuliza kinachomliza, Prospa alibaki kimya, hali iliyomtisha Sara. Kwa busara aliyokuwa nayo Sara, ilibidi akae pembeni. Jambo

hili lilisaidia, kwani baadaye Prospa alipitiwa na usingizi na baada ya kuamka alikuwa na nguvu mpya. Kulingana na msingi wa pili wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaosisitiza hisia za matamanio, Prospa aliumizwa na matamanio yake ya kumwona Merisho kwa kuwa alikuwa hajakidhi haja hiyo.

Sifa nyingine ya melankoli ni kujali wengine, hasa wanapokuwa na shida. Utafiti umebaini kuwa Prospa alionesha kujali alipopotea mtoto wa dada yake. Alijitahidi kufanya uchunguzi wa awali kwa kuwahoji marafiki zake na watoto waliokuwa wakicheza na Merisho. Alimhurumia sana dada yake. Mwandishi anasema:

> Usiku Prospa alimsikia dada yake Josefina akilia chumbani. Prospa alijisikia uchungu. Alijiona kama yeye ndio mwenye hatia. Asingekwenda kucheza mpira uwanjani Merisho asingeibwa (uk. 15).

Kwa kawaida, watoto huwa wanacheza katika mazingira ya nyumbani au nje ya nyumba, lakini kutokana na silika yake, Prospa alijihisi mkosaji sana. Baada ya mawazo ya muda mrefu, Prospa alikata shauri la kufanya uchunguzi wake mwenyewe utakaokuwa wa matendo kuliko wa askari. Kutokana na msingi wa pili wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu matamanio, Prospa alisukumwa na matamanio yake ya kumtafuta Merisho hadi ampate. Kwa hiyo, ilikuwa ni lazima Merisho apatikane ili Prospa akidhi matamanio yake.

Utafiti uliofanyika umebaini kuwa Prospa alionesha kujali pale alipokutana na Sara. Ijapokuwa hakumfahamu msichana yule, na alikutana naye kwa mara ya kwanza, Prospa aliweza kumsimulia kuhusu safari yake na alikubali kuambatana naye. Mwandishi anafafanua kuwa baada ya Sara kumwambia Prospa anataka kwenda naye Dar es salaam, Prospa aliamua kumwambia kuwa anakwenda kumtafuta mtoto wa dada yake aliyeibwa huko TPC. Sara akamwambia Prospa kuwa anamfahamu huyo mtoto, hivyo, atamsaidia kumtafuta. Pamoja na wasiwasi na kutomwamini msichana huyo, Prospa hakumkatalia (uk. 48-49). Hivyo, Sara alimwomba Prospa amsubiri ili aende nyumbani kuchukua nguo na kumsisitiza kuwa asiondoke, na endapo angeondoka angempata tu. Prospa alichunguza wema na ubaya wa kuongozana na Sara, akaona ni busara kumsubiri, kwani kidole kimoja hakivunji chawa.

Vilevile, utafiti umebaini kuwa watu wa kundi la melankoli pia wana huruma na hawapendi kuona wengine wanaonewa. Prospa alikuwa na huruma, hasa baada ya kuona jicho la Sara. Baada ya Prospa na Sara kushushwa Makanya na msamaria aliyewapa lifti, walianza kutembea huku wakitaniana na kucheza. Maongezi yao yalikuwa kama ifuatavyo:

> Sara: Unajua? Jicho langu linaona kwa ndani.
> Prospa: Uliumizwa na nini?
> Sara: Thijui. Niliugua thana nilipokuwa mdogo. Lakini thatha naona kila kitu ndani.
> Prospa: (alinyamaza, akamtazama kwa huruma. Alichukua ile noti ya shilingi mia tano waliyopewa, akampa Sara)
> Sara: Thitaki hela.
> Prospa: Kwanini?
> Sara: Edithon aligundua umeme. Unajua?"
> Prospa: (alirudisha hela mfukoni) we hujui chochote.
> Sara: (Alicheka sana). Edithoni aligundua umeme na Prothpa aligundua ujinga, halafu akapotetha mtoto, akajamba *pyu*, *pyu*." (Aliendelea kucheka)
> Prospa: (Alichota mchanga chini akamtupia Sara) Mie sitaki utani.
> Sara: "Utaniita Edithoni?"
> (Prospa alikataa. Sara alionesha kusikitika)
> Prospa: "Mambo ya Edison uliyajulia wapi?"
> Sara: "Nilisoma kwenye kitabu."
> Prospa: Mwongo we hujui kusoma Kiingereza. Mimi najua, lakini sijasoma mambo ya Edison"
> Sara: "Hebu, hebu Prothpa funga jicho lako moja. Unaona mwanga?"
> Prospa: "Ndiyo."
> Sara: "Nikifunga jicho langu moja, naona githa. Kwa hiyo thilifungi mpaka ninapolala. Hili linaona kila kitu, na hili linaona kwa ndani, linaona ndoto."
> Prospa: (alimwonea huruma) "Sasa tufanye hivi; ukinisaidia mpaka Merisho apatikane, nitakuita Edison siku zote. Sawa?"
> Sara: "Sawa" (uk. 53-54).

Dondoo la hapo juu linatudhihirishia namna Prospa alivyoonesha huruma kwa Sara kutokana na jicho lake. Alimpa sharti la kuomba lifti ili amuite Edison kwa kuwa Sara alipenda kuitwa hivyo. Lengo la Prospa lilikuwa kumridhisha Sara ili awe na furaha.

Pia, imebainika kuwa katika harakati za kumtafuta Merisho, Prospa na Sara walifika Zanzibar baada ya kuambiwa huenda mtoto huyo yuko huko. Walipokelewa vizuri na wenyeji wao na wakajitambulisha na kueleza walikotokea na kilichowaleta.

Prospa alieleza uongo ambao alishaupanga ili ampate Merisho. Alipoona mwenyeji wao amefurahia maelezo hayo, Prospa alijisikia huruma sana kutokana na maelezo kuwa ya uongo. Mwandishi anasema:

> Kulitokea kimya cha sekunde chache kati yao, halafu Bibi Fatuma alisema, "Allah Wakbal! Mzee Mohamed, mwanetu ana mtoto. Allah mkubwa. Wasikia Mohamed, Allah kasikia dua yangu." Bibi Fatuma alitembea huku na kule akiwa ameingiwa na nguvu za aina fulani… Prospa alimtazama, akamwonea huruma. Alimpenda. Alijisikia vibaya sana kwa kumdanganya. Lakini alijua kwamba bila kufanya hivyo, hawezi kumpata Merisho (uk. 91).

Kutokana na maelezo ya Prospa, Bibi Fatuma alifurahi sana na kumshukuru Mungu kusikia mwanawe ana mtoto, kwani kilikuwa kilio chake cha muda mrefu. Pia, aliona kuwa vijembe alivyokuwa anapewa huenda vikaisha kutokana na habari hiyo. Hali hii ilimfanya Prospa ajisikie huruma kwa kumdanganya. Nafsi ya kimaadili ilimsuta, lakini hakuwa na namna, kwani ilibidi Merisho apatikane kwa namna yoyote ile.

Suala la huruma pia linajitokeza pale ambapo Prospa alionesha huruma juu ya Sara kutopata kifungua kinywa. Hii inajitokeza pale Prospa alipokuwa anakula pamoja na watoto wengine waliokutana mtaani huko Dar es Salaam. Alijiuliza kama Sara atakuwa ameshapata chai. Marafiki zake walimwambia aachane naye, lakini ilimbidi aweke maandazi mawili katika kila mfuko wa kaptula yake ili ampelekee. Utafiti unaamini kuwa jambo hili lilitokana na huruma yake kwa Sara. Prospa alimtafuta Sara kutokana na msingi wa kwanza wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaosisitiza umuhimu wa mahitaji kwa binadamu, ni dhahiri kuwa alitaka Sara apate hitaji hilo. Prospa aliamini kama Sara atapata chai ataweza kuishi vizuri na kufanya kazi zake inavyostahiki. Baada ya kumaliza kula waliondoka kuelekea mitaani. Wale watoto wa mtaani walikuwa wakimfundisha Prospa njia mbalimbali za kupita kwa imani kuwa mtu akizoea njia moja unaweza kupata majanga. Hata hivyo, mawazo ya Prospa yalikuwa kwa Sara tu. Alimwonea huruma sana. Mwandishi anasema:

> Prospa alimwambia Tofa, "Tumpelekee Sara maandazi" Tofa alisema "Achana na huyo msichana bwana. Wana kazi zao hao. Wanapata chakula hukohuko." "Sara ni dada yangu. Alinisindikiza kuja huku Darisalam kumtafuta Merisho. Nimeenda nae mpaka Zanzibar, siwezi kumsahau" Prospa alisema huku akilalamika.

> Tofa na Mansa waliondoka na kumwacha Prospa akilalamika. “Shauri yake bwana,” alimsikia Mansa akisema huku wakiwa wanatembea haraka. Moyo wa Prospa ulimsukuma kumtafuta Sara. Alitaka kufahamu alipo hata kama atakuwa amepata chakula kama walivyosema Mansa na Tofa… (uk. 119-121).

Maongezi haya yakichunguzwa kwa makini, yanaonesha kuwa Prospa ni mtu mwenye huruma sana. Anaguswa sana na matatizo ya wengine, na ana upendo wa dhati. Nafsi ya kiwango cha ukomavu ilimuongoza sana Prospa kufanya yote haya. Juhudi za kumtafuta dada yake Sara ziligonga mwamba baada ya kuzunguka mitaani bila mafanikio.

Sifa nyingine ya silika ya melankoli iliyobainika katika utafiti uliofanyika ni kujitolea kwa haraka katika mambo ya wengine. Mwandishi anatanabahisha kuwa Prospa alijitolea kufanya upelelezi binafsi wa kumtafuta mpwa wake. Mtafiti anaona kuwa hili ni jukumu kubwa sana ikilinganishwa na umri wake, lakini silika yake ndiyo iliyomsukuma kufanya hivyo. Katika safari yake ya kumtafuta Merisho, alikumbana na changamoto nyingi, lakini alikabiliana nazo ili kulifikia lengo lake. Lema (khj) anasema kuwa:

> Prospa alijitolea kuhakikisha anampata Merisho kwa sababu hakuwaamini askari. Wakati mwingine alikatishwa tamaa na watu mbalimbali, pamoja na mazingira, lakini hakuthubutu kuliacha zoezi lake. Alitaka kuionesha jamii kuwa suala la upelelezi siyo lazima lifanywe na polisi.

Ithibati ya hili pia, inaoneshwa pale kaka yake Prospa aliyeitwa Petro alipomwambia kuwa akitoka Zanzibar asirudi tena kwake, kwa sababu ameshatumia hela nyingi kwa ajili ya chakula chao. Aliwashauri warudi Moshi. Prospa alipingana na hili katika mawazo yake. Mwandishi anafafanua namna Prospa alivyokuwa anawaza:

> Prospa aliendelea kujilaza kwenye benchi ndefu. Hakuwa na usingizi. Alikuwa anawaza: Manzese, Merisho hayupo, wala kaka Petro hajui alipo. Zanzibar tumekwenda, Merisho hayupo. Sasa twende wapi? Labda turudi Manzese, tuulizie njia mpaka tufike kwa kaka Petro, lakini tukafanye nini? Tutamkuta kaka Petro? Halafu siku tuliyoondoka aliniambia nisirudi kwake. Alinieleza kwamba ameshatumia pesa yake nyingi kwa chakula na nauli, kwa hiyo tukitoka Zanzibar, tuende moja kwa moja Moshi. Najua tukienda Manzese hatutamkuta Petro (uk. 108).

Mawazo haya ya Prospa yalikuwa yanazunguka tu mahali pamoja. Swali kubwa alilokuwa anajiuliza, ni kuwa, je, aende wapi? Nafsi yake ilimsuta, kwa sababu alijitolea kwa hali na mali kuhakikisha kuwa anampata Merisho. Maneno ya Petro yalianza kumkatisha tamaa. Kutokana na msingi wa Nadharia ya Saikochanganuzi, matamanio ya mtu ni lazima yatimizwe ndipo nafsi itulie. Hii ni dhahiri kuwa Prospa alijitolea kumtafuta Merisho hadi ampate ili atimize matamanio yake.

Watu wa kundi la melankoli, akiwamo Prospa, hawapendi utani au kuchekacheka. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa Prospa hakupenda utani na namna yoyote, na mara zote alipoona mtu anamfanyia utani alikemea tabia hiyo. Yeye alikuwa mtu wa malengo zaidi, hivyo, alisimamia malengo hayo. Mwandishi analionesha hili pale Prospa alipokutana na Sara na kumwomba wakanywe supu. Anasema:

> Waliingia ndani ya *Same Guest & Bar*, msichana akapitiliza akaenda jikoni. Aliporudi alikuwa na bakuli mbili za supu. Walikaa wakanywa. Supu ilikuwa na pilipili nyingi iliyomfanya Prospa akohoe hadi kutoa machozi. Msichana alimcheka sana, akapigapiga meza kwa furaha akisema, "We mtoto kumbe, we bado mtoto mdogo tu." Prospa alikasirika, akaacha supu bila kuimaliza ingawa ilikuwa tamu sana (uk. 49).

Hapa inaonesha jinsi gani Prospa alikuwa hapendi utani. Ndiyo maana alidiriki kuiacha supu ambayo ilikuwa tamu, na isitoshe, alikuwa na njaa. Lema (2020) anafafanua kuwa huyu ni mhusika asiyependa utani, na ana msimamo katika kile anachokiamini.

Sara hakuchoka kumtania Prospa, ijapokuwa aliona ni mtu wa kukasirika anapotaniwa. Sara alitoa ahadi kwa Prospa kuwa ataomba lifti ya kwenda Dar es Salaam. Hata hivyo, Prospa alishangaa sana kuona wanatembea. Baada ya muda, Sara alianza kukimbia, Prospa naye alijikuta anakimbia kumfuata, lakini hakuweza kushindana naye. Alipomfikia akamkumbusha kuwa alisema ataomba lifti. Badala ya kujibu, Sara alianza kucheka na kuchepuka pale walipokuwa huku akiimba:

> Prothpa Prothpa,
> Mpenda lifti,
> Kiuno chake kama kiti.
> Prospa alikasirika. Alipiga miguu chini akisema, "Sara, Sara, mbaya, mbaya. Sitaki unifuate." Lakini Sara aliendelea kuimba na kucheka na kwenda mbali zaidi (uk. 51)

Kitendo cha Sara kuchekacheka kilimkasirisha sana Prospa. Alimchukia Sara, lakini nafsi ya kiwango cha kati ilimsukuma, hakuwa na namna, ilibidi amfuate kule alikokimbilia, kwa sababu aliona ni mtu muhimu sana katika safari yake. Hata hivyo, Sara alizidisha utani kwa Prospa, ijapokuwa yeye hakupenda kutaniwa. Mwandishi anasema:

> …Prospa alirudisha hela mfukoni, halafu akasema, "We hujui chochote.
> Sara alicheka sana, halafu alisema, "Edithon aligundua umeme, na Prothpa aligundua ujinga, halafu akapotetha mtoto, akajamba *pfu*, *pfu*" Sara aliendelea kucheka.
> Prospa alichota mchanga chini akamtupia Sara, akisema "Sara, mie sitaki utani."
> Sara aliuliza, "Utaniita Edithon?"
> Prospa alikataa.
> Sara alionesha kusikitika… (uk.53).

Dondoo hilo linashadidia na kudokeza kuwa Prospa alichukizwa na utani mpaka ikabidi amwambie Sara. Kutokana na silika yake, Sara hakuacha utani kwa sababu yeye aliufurahia.

Utani wa Sara kwa Prospa haukukoma. Utafiti umebaini kuwa Sara aliyafanya haya yote kutokana na silika yake; anapenda sana kuongea bila kujali amemkwaza mtu au la. Mara zote alijua Prospa hukasirika akitaniwa au kufanyiwa masihara. Baada ya kwenda kwa Petro na kulala huko, siku iliyofuata waliamka na kukuta chai na maandazi imeandaliwa. Walikunywa chai, kisha Prospa akarudi kitandani na kukaa kwa sababu kichwa kilikuwa kinamuuma. Sara alimbeza kuwa kutokana na ulafi wake ndiyo maana anaumwa. Prospa alikaa kimya na kumwangalia tu. Lakini vitimbi vya Sara havikuisha, mwandishi anasema:

> "Twende," Sara alisema. "Twende wapi?" Prospa aliuliza. "We twende utaona mwenyewe," Sara alisema. "Tupange kwanza huku ni Darisalam, usilete mchezo," Prospa alisema. Sara alifungua mlango akaondoka. "Sara, Sara njoo kwanza. We Sara…" Prospa alimwita. Alijua kwamba Sara ni mkaidi, alijua kwamba hatarudi. Alikasirika. Kwanini hasikii huyu? Kichwa chake kibovu? (uk. 67-68)

Utafiti umebaini kuwa Sara hakumwonea huruma Prospa, ijapokuwa alimwambia anaumwa na kichwa. Hivyo, Prospa alichepuka kitandani na kumfuata Sara haraka

na kumkuta karibu anakata kona kuingia uchochoroni. Prospa alikuwa na wasiwasi kuwa huenda Sara angepotea, ndiyo maana aliinuka na kumfuata, ijapokuwa alikuwa anaumwa kichwa.

Hivyo basi, mtafiti anaamini kuwa silika ya Prospa ilimfanya aishi vizuri na Sara, na kushirikiana naye. Jambo hili lilimpa wepesi sana katika maisha yake, hususani katika suala la kumtafuta Merisho hadi kumpata. Pia, aliweza kuishi vizuri na watoto wa mtaani aliokutana nao Dar es Salaam.

#### 4.3.2.2 Silika ya Sara

Utafiti uliofanyika umebaini kuwa Sara ana silika ya sangwini. Watu wa kundi hili wana uwezo wa kawaida kiakili. Mwandishi amempa matendo na maneno yanayoendana na silika hii. Tangu mwanzo wa masimulizi, Sara amekuwa akionesha matendo ambayo yalisaidia kubaini silika yake. Zifuatazo ni sifa za silika ya Sara zinazomweka katika kundi hili:

Sara ni mchangamfu sana na mahali popote hujitokeza. Kwa mujibu wa Ponera na Kasiga (2019), watu wenye kionjo cha usangwini huwa na uchangamfu, kwa sababu damu zao zina kiwango kikubwa cha hewa. Utafiti uliofanyika umedhihirisha uchangamfu wa Sara tangu mwanzo hadi mwisho wa masimulizi ya riwaya hii. Mwandishi anaeleza kuwa Prospa alipofika Same alikutana na msichana ambaye alikuwa amejifunga kitenge kifuani juu ya matiti. Alikuwa amebeba kichwa cha ngombe aliyechinjwa ambacho kilikuwa kinachuruzika damu. Prospa alishtuka na kutaka kukimbia. Mwandishi anasema:

> Msichana alisimama na kumwangalia Prospa, halafu alicheka sana. “Mungu wangu,” Prospa alizidi kushangaa akionesha uso wa kustaajabu na hata kuogopa. Msichana akiwa na sura ya ucheshi, aliuliza, “Ee nini?” Prospa hakujibu. Aliendelea kustaajabia msichana ambaye jicho lake la kushoto lilikuwa bovu…Msichana alisema,“Twende tukanywe supu”. Prospa alitingisha kichwa kukubali lakini hakuondoka kumfuata. Waliingia ndani ya Same *Guest* & *Bar*, msichana akapitiliza akaenda jikoni. Aliporudi alikuwa na bakuli mbili za supu. Supu ilikuwa na pilipili nyingi iliyomfanya Prospa akohoe hadi kutoa machozi. Msichana alimcheka sana, akapigapiga meza kwa furaha akisema, “We mtoto kumbe, we bado mtoto mdogo tu” (uk. 48-49).

Dondoo hili linatuthibitishia jinsi Sara alivyomchangamkia Prospa, ijapokuwa ilikuwa ni mara ya kwanza kuonana. Kwa kawaida, mtu wa silika ya sangwini huwa hajifichi kutokana na ucheshi wake. Anajitokeza popote alipo hata kama kuna kundi kubwa la watu. Pia, mwandishi anaonesha ucheshi wa Sara pale walipokutana na Petro walipofika Dar es Salaam. Anasema:

> Petro alipomuona Sara alisimama na kumtazama kwa mshangao. Akamuuliza Prospa "Nani huyu?" kabla aliyeulizwa swali hajajibu, Sara alimtazama Petro na kusema, "Mimi naitwa Thara Edithon. Wewe unaitwa nani?" lakini Petro hakumjibu, alimwangalia Prospa na kumuuliza kwa mara ya pili, "Nani huyu?" (uk.60).

Maongezi hapo juu yanatuthibitishia kuwa Sara hakuulizwa swali, lakini alijibu. Pia, hakujali kama Petro atakasirika au la. Kutokana na ucheshi wake, Sara aliweza kuzoeana na kila mtu kwa urahisi sana, hata kama mtu hataki, atajikuta anampenda tu. Mambo yote haya yalisukumwa na nafsi ya kiwango cha ukomavu ambayo huchunguza uadilifu wa tendo kabla ya kulitenda. Nafsi ya Sara ilichunguza na kugundua kuwa kuchangamkia watu siyo kinyume cha maadili.

Kwa upande wa data za uwandani, mwanafunzi CKDOE7 anatoa ithibati yake kuhusu uchangamfu wa sangwini. Anasema:

> Watu wenye silika ya sangwini ni wachangamfu sana, lakini wana fujo. Nilipokuwa sekondari, kuna watu wawili hao wakikosekana darasani tunahisi tumepwaya. Lakini wakati mwingine wanatuponza tunachapwa viboko kwa sababu ya fujo zao. Halafu ni rafiki wa kila mtu, hawachagui wala hawabagui.

Mwanafunzi huyo anashadidia suala la uchangamfu kwa watu wenye silika ya sangwini. Anatolea mfano wa wenzake aliokuwa akisoma nao. Ni dhahiri kuwa watu wenye sifa hizi wapo kila mahali, lakini watu hawawatambui kutokana na kutokujua aina za silika.

Sifa nyingine ya sangwini iliyobainishwa ni kupenda kusaidia watu. Watu wa kundi hili, hata kama wana uwezo mdogo, hupenda sana kutoa msaada kwa watu hata kama hamfahamu. Mwandishi anamsawiri Sara kwa kuonesha msaada mkubwa anaoutoa kwa Prospa, ijapokuwa hakumfahamu kabla na ndiyo walikuwa wamekutana kwa mara ya kwanza. Baada ya kukutana, Prospa alimweleza kuwa anakwenda Dar es

Salaam kumtafuta mtoto wa dada yake aliyeibwa nyumbani kwao TPC. Sara, bila kusita, alisema kuwa anamfahamu huyo mtoto na kumwahidi Prospa kuwa atamsaidia kumtafuta. Uamuzi huu unasukumwa na nafsi ya kiwango cha kati ambayo inampa utashi wa kufanya jambo fulani, nalo ni kumsaidia Prospa. Katika mazingira ya kawaida, mtu hawezi kuondoka na mtu asiyemfahamu. Hata hivyo, Sara aliweza kwa sababu silika yake ilimsukuma kusaidia. Msichana huyu alifanya maamuzi ya haraka ili kuambatana na Prospa. Mwandishi anasema:

> Msichana alisema "Thikia, mimi nitakwenda nyumbani kuchukua nguo. Ningoje hapa. Uthiondoke. Ukiondoka nitakupata tu." Alicheka kwa furaha. Jicho lake la kulia liling'aa. Aliondoka pale akikimbia kuelekea kilimani. Prospa aliduwaa. "Msichana huyu ni mchawi, au ni mtoto wa mchawi." Prospa aliwaza. "Sura yake inatisha lakini yeye mwenyewe hatishi. Na kwanini sikukataa au sikukimbia aliposema kwamba anataka kuja na mimi Darisalam? Itakuwaje afahamu Merisho alipo bila kumfahamu hata kidogo?" Prospa aliamua kungoja aone mwisho wa maajabu ya huyu msichana mwenye sura ya ajabu (uk. 48-49).

Utafiti umebaini kuwa Sara alikuwa msaada mkubwa sana kwa Prospa tangu walipokutana Same, walipofika Dar es Salaam, hata walipokwenda Zanzibar. Kwa mfano, mwandishi anasema kuwa walipofika Zanzibar walikuwa wanawaza namna ya kufika Chuini. Walimtafuta mtu wa kumwuliza bila mafanikio. Sara aliwaza namna ya kumsaidia Prospa, mwandishi anasema:

> Bila kuzungumza zaidi, Sara alitema mate kwenye kiganja chake cha mkono wa kushoto. Alichapa yale mate kwa kidole kimoja cha kulia, *chap*. yakaruka majumba yaliyo upande wa pili wa barabara ya Forodhani. Sara alisema, "Chuini iko upande huu." Unajuaje?" prospa alimuuliza. Najua," Sara alisema (uk. 79).

Dondoo hili linaonesha namna Sara alivyojitahidi kumsaidia Prospa kufika Chuini. Prospa aliamini kuwa kwa kufanya hivyo wanaweza kujua upande ilipo Chuini. Hata hivyo, suala hili lilikuwa ni kujifariji tu, kwani hakuna uhusiano wowote wa kutema mate na kuangalia muelekeo wake ili ujue sehemu husika ilipo. Sara alifanya hivi ili amsaidie Prospa, ambaye alionekana kutanzika kutokana na kupotea Merisho.

Utafiti ulibaini msaada mkubwa wa Sara kwa wenzake katika kufanikisha kumpata Merisho walipofika kwa mjomba Feliksi, Masaki. Katika mipango yao, Mansa[9] alimwambia Sara aongee na Uzuri (dada wa nyumbani kwa mzee Feliksi) ili afahamu kwa rafiki yake mpenzi anayefanya kazi kwa mzee Mathayo, wakidhani kwamba huyo ndiye atakuwa baba yake Merisho. Ijapokuwa Uzuri hakumpenda Sara, lakini imebainika kuwa kutokana na silika yake Sara, aliweza kumsemesha hadi wakawa marafiki na Uzuri akafunguka[10] kila kitu kuhusu mzee Mathayo, bila kujua anampa maelekezo ya kumpata Merisho (uk. 140-145). Jambo hili linathibitishwa na CKDOE6 (2020)[11] anaposema:

> Watu wenye silika ya sangwini wana sifa kubwa ya kusaidia watu hata kama hamfahamu. Mara zote huguswa na matatizo ya watu wengine. Kwa mfano, kuna watu wanawasaidia wenzao hela za chakula au wanakula nao. Yaani, kwa mwanafunzi kufanya hivi ni nadra sana.

Mwanafunzi huyo alikuwa akishadidia suala la sangwini kusaidia watu wengine. Ni Dhahiri kuwa siyo wanafunzi wote wanaoweza kusaidia wenzao wanapokuwa na shida labda awe rafiki yake wa karibu sana. Hata hivyo, kwa sangwini yote yanawezekana.

Sifa nyingine ya watu wa kundi la usangwini, akiwemo Sara, ni kutokuwa na aibu kwa watu wasiowafahamu. Kwa mujibu wa Asamoah (2018), sangwini wengi huwa ni waigizaji kutokana na kutokuwa na aibu, kwa sababu anaweza kusimama mbele ya kundi kubwa la watu na kuzungumza nao. Wengine huwa wanasiasa na wasanii wa fani mbalimbali. Katika masimulizi yote, Sara anakutana na watu mbalimbali asiowafahamu, lakini anapata uwezo wa kuwazoea bila aibu. Utafiti uliofanyika ulibaini kuwa hali hii pia ilitokana na ucheshi wake, hivyo, inakuwa rahisi. Anaingia kwa mtu yeyote na kumzoea. Haya yanadhihirika ukurasa wa 47-54 alipokutana na Prospa, ukurasa wa 58-65 walipokutana na Petro, ukurasa wa 84-87 walipokuwa kwenye magofu Zanzibar, ukurasa wa 92-102 nyumbani kwa bibi Fatuma, na

---

[9]Huyu ni kijana wa kiume ambaye alikuwa kiongozi wa watoto wa mtaani, maarufu kama changudoo. Kijana huyu na wenzake walikutana na Sara na Prospa katika bustani waliyokuwa wamepumzika na kuwaamuru waungane nao. Baadaye, anakuwa msaada mkubwa katika kufanikisha kumpata Merisho.
[10]Kueleza kwa undani mambo yote unayoyafahamu kuhusu mtu, kitu au mahali.
[11] Majadiliano ya vikundi lengwa yaliyofanyika tarehe 14/06/2020 katika Chuo Kikuu cha Dodoma Koleji ya Elimu. Huyu ni mwanafunzi anayesoma Shahada ya Awali ya Ualimu wa Elimu ya Awali (BED. ECE).

ukurasa wa 141-145 alipokutana na Uzuri. Katika sehemu zote hizi, Sara hakuonesha aibu kwa watu hao, aliweza kuongea nao kwa undani na kutafuta kile anachokitaka, ambacho alikuja kukipata kwa kusaidiana na wenzake.

Sifa nyingine ni kujipatia marafiki wengi kutokana na porojo zao. Sara anajipatia marafiki wengi kwa muda mfupi kutokana na silika yake. Haya yanathibitishwa na Ponera na Kasiga (2019) wanaoelezea namna Willy Gamba (msangwini) anavyojenga urafiki na wanawake mbalimbali kama vile Veronika Amadu, Zabibu Abeid, na Khadija. Utafiti umebaini kuwa baada ya Sara kukutana na Prospa, na kumwomba waende wote Dar es salaam, walijenga urafiki wa haraka, wakawa kitu kimoja. Walitembea pamoja, kuimba, na hata kucheza kwa pamoja. Mwandishi anaeleza:

> Baada ya Sara na Prospa kuzurura pale Makanya wakingoja magari ya usiku yanayoenda Darisalam, hatimaye waliona gari kubwa kwa mbali wakawa na matumaini. Gari hilo lilisimama kabla halijafika walipokuwa wamejificha. Sara alimuita Prospa wakakimbia wakiwa wameshikana mikono. “Twende thatha. Twende tukajaribu,” Sara alimwambia Prospa kwa sauti ya chini. Walikimbia wakiwa wameinama ndani ya shamba la mkonge hadi walipofika sambamba na lile gari (uk. 52-54).

Dondoo la hapo juu linaonesha namna Sara alivyojenga urafiki na Prospa kwa haraka na ukaimarika. Ikumbukwe kwamba, watoto hawa kwa kipindi hiki ilikuwa ni siku moja tu tangu wafahamiane. Sara alijenga urafiki kutokana na sifa ya silika yake ya sangwini.

Pia, walipofika nyumbani kwa mzee Feliksi, Sara alijenga urafiki na dada Uzuri ili apate taarifa anazozitaka. Ijapokuwa Uzuri hakumpenda Sara, lakini silika yake ilimsaidia. Mwandishi anasimulia:

> Uzuri aliuliza. “Unasemaje?”
> “Wewe ni mthuri kama udi,” Sara alirudia.
> Uzuri alicheka. Alirudia tena kuchambua mchicha, lakini kicheko kilimbana akaanza kucheka tena. “Mtoto we, una mambo,” alisema. (uk. 141).

Kutokana na maongezi hayo katika dondoo, urafiki wao ulijengeka. Wakawa kitu kimoja, walicheka pamoja, walisukana, na walilala pamoja. Aiello (2015)

anamwelezea Sara kuwa ana uwezo wa kujenga urafiki na watu mbalimbali bila kujali ubaguzi wa kijinsia, maumbile yake, kutoaminiwa na mjomba Feliksi, pamoja na watoto wengine wa mitaani. Kutokana na msingi wa pili wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaoeleza kuwa nafasi kubwa ya maisha huchukuliwa na matamanio, nafsi ya Sara ilitamani kukamilisha matamanio yake ya kuwa na marafiki wengi, kwani marafiki ni hazina katika maisha. Pia, kupitia marafiki alipata taarifa, pamoja na kujifunza mambo mbalimbali.

Sifa nyingine ya Sara inayomweka katika kundi la sangwini ni kujiamini na kuaminika. Utafiti uligundua kuwa Sara anajiamini sana anapofanya jambo, na wenzake wanamwamini pia. Mwandishi anasimulia kwamba baada ya Sara kukutana na Prospa, walikuwa marafiki, na Prospa akamweleza kuwa anaenda kumtafuta mpwa wake Dar es Salaam. Sara aliomba kuambatana na Prospa ili amsaidie kumtafuta ndugu yake huyo. Sara alitoa ahadi ambayo Prospa aliiamini. Mwandishi anasema:

> Walipotoka nje Prospa alisema, "Sina nauli."
> "Huna nauli Same ulifikaje?" Msichana aliuliza.
> Kabla Prospa hajajibu, msichana alisema "Bathi wathiwathi ondoa. Mimi Edithoni mthichana mthuri nitaomba lifti." Alijigeuza na kujipinda kwa maringo.
> "Unaitwa Edison?" Prospa aliuza.
> "Kumbe hujui? Jina langu Thara Edithon. Mtoto wa mfalme."
> "Edison ni jina la kiume," Prospa alisema. "Na siku hizi hakuna mfalme."
> Sara alicheka sana, akaondoka akikimbia huku akicheza na kusema, "Nani kathema, nani kathema…"
> Prospa alipomfikia Sara, alimwambia, "Ulisema utaomba lifti."
> Sara alicheka, akachepuka pale akiimba;
> "Prothpa Prothpa,
> Mpenda lifti,
> Kiuno chake kama kiti" (uk. 50-51).

Kutokana na dondoo hili, Prospa alimwamini Sara kuwa ataomba lifti baada ya kuahidi hivyo. Sara alitimiza jambo hilo. Baada ya magari mengi kuwapita kwa muda mrefu, moja lilisimama, akaomba lifti kwa kumweleza mwenye gari kuwa yeye na mdogo wake wanatembea kwenda Dar es Salaam. Ijapokuwa mwenye gari aliwatilia mashaka, lakini aliwapa lifti hadi sehemu iliyoitwa Makanya. Jambo hili liliongeza uaminifu wa Prospa kwa Sara.

Sehemu nyingine iliyobainika kuwa Sara anaonesha kujiamini ni wakati Petro amewaletea taarifa kuhusu ndugu wa Mohamedi. Siku hiyo Petro alirudi nyumbani akiwa na mawazo mengi, akawaambia Prospa na mwenzake kuwa ana habari ya kuwaeleza. Watoto wale walikuwa na shauku ya kuijua habari hiyo. Baada ya kuwaeleza, Sara aliongea kwa kujiamini na kusema:

> "Mimi nitakuwa mfanyakathi wa nyumbani kwake Mohamed. Prospa atakuwa kaka yake Merisho. Tutathema tumetumwa kuja kumthalimia mtoto." Petro na Prospa walicheka. Walicheka sana. "Ngoja, ngoja" Sara aliendelea. Tutathema kwamba Mohamed ni baba yake Merisho." "Acha utani wa kijinga," Petro alisema. "Thio utani," Sara alisema. "Ndugu yake akijua kwamba Merisho ni mtoto wa Mohamed, atatuambia alipo. Wewe huoni… (uk. 64-65).

Dondoo hili linaonesha namna Sara alivyokuwa anapanga mipango yake kwa kujiamini na kuamini kile anachokisema, ijapokuwa Petro aliona kama anafanya masihara. Nia yake ilikuwa ni kuhakikisha Merisho anapatikana. Lakini walishindwa kuafikiana, kwa sababu Petro alitaka wakachukue polisi, ilihali Prospa hakutaka kabisa kuwahusisha polisi.

Kwa upande mwingine, wenzake walimwamini sana, hasa pale walipokuwa nyumbani kwa mjomba wake Prospa, mzee Feliksi. Wakati wanapanga mipango yao ya namna ya kujua anapoishi mzee Mathayo, ambaye walihisi ndipo alipo Merisho. Waliona ipo haja Sara aletwe ili asaidie. Walihofia kama ataletwa msichana mwingine haitasaidia, kwa sababu walimwamini Sara. Mwandishi anasema:

> "Tunamhitaji Sara aje aongee na Uzuri mpaka amwoneshe kwa mzee Mathayo."
> "Ndiyo. Sara anaweza sana, "Prospa alisema. Alifurahi kujua kwamba inawezekana akaonana tena na Sara.
> Tofa alisema, "Muda tulionao ni mdogo. Prospa na mjomba wake watakwenda Moshi keshokutwa kabla hatujahakikisha mambo yetu."
> Mansa alisema, "Lazima tumpate Merisho, kwa bidii yetu wenyewe. Sasa majadiliano yaishe. Tofa we nenda ukamlete Sara. Ondoka na Prospa. mweleze dada yao kwamba tunamhitaji Sara leo hii. Mwambie kwamba ni lazima Sara na siyo msichana mwingine…" (uk. 138).

Prospa alikubaliana na Mansa kutokana na uwezo aliokuwanao Sara. Hivyo, walimwagiza Tofa aende kumleta Sara. Lema (2020) anaeleza kuwa, pamoja na

matatizo wanayopitia watoto wa mitaani, lakini wanaonesha uwezo mkubwa wa kufanya mambo kuliko watu wanavyotarajia. Ndiyo maana wahusika wake wanafanya kazi ya kipelelezi bila kusaidiwa na polisi. Anazidi kufafanua kuwa walipoona Uzuri siyo chaguo sahihi katika upelelezi wao, ilibidi wamlete Sara ambaye waliamini kuwa anaiweza kazi hiyo. Mtafiti anaona kuwa maongezi yao yanathibitisha ni jinsi gani walimwamini Sara katika jitihada zao za kumtafuta Merisho.

Sehemu nyingine inayotoa ithibati ya kuaminiwa Sara ni baada ya mipango yote kukamilika. Ijapokuwa wote walikuwa hawaaminiani kwa kuona kuwa huenda wakatokea wasaliti, mwishowe walimwamini Sara. Baada ya kuona Sara anacheka sana na Uzuri, walimwita na kumhoji maswali mbalimbali kujua wanaongea nini. Sara alipochoshwa na maswali yao, aliwaambia waende mjini warudi baadaye. Kutokana na kumwamini, wote walifurahia wazo hilo, na mara moja waliondoka bila ubishi. Walipokuwa njiani, wengine walionesha wasiwasi wao juu ya Sara kuwa huenda atamwambia Uzuri kila kitu, lakini Prospa aliwahakikishia uaminifu wa Sara. Mwandishi anasema:

> Walipokuwa njiani Mansa alisema, "Simwamini Sara, yule anaweza kumwambia Uzuri kila kitu, halafu kazi yetu itakuwa bure." Prospa alisema, "Sara hasemi. Sara ni mjanja yule, hawezi kusema kitu." Tofa alisema, "huwezi kumwamini msichana kabisa. Anaweza akajisahau. Sijui wakoje hao." Prospa alisema, "Sara ndiye aliyetusaidia kutafuta nyumba ya mzee Mathayo. Mbona mpaka sasa hakusema chochote kwa Uzuri? Sara ana akili kweli yule. Nilitoka naye tangu Same huko, nimekwenda naye Zanzibar, mpaka sasa ninaye… Sara hatapayuka. Nyie mtaona tu. Hawezi kupayuka yule." (uk. 149-150).

Nukuu hiyo inatuthibitishia namna Sara alivyoaminika. Haya yote yanafanyika kutokana na matamanio ya Sara kutaka kumpata Merisho ili amridhishe Prospa. Kwa upande wa wale waliokuwa na wasiwasi naye, walielezwa sababu za kuaminika, hivyo, wakakubaliana kwa pamoja. Kumwamini huku kuliwasaidia kupatikana kwa Merisho kwa urahisi bila kumwaga damu, na bila msaada wa askari.

Sifa nyingine iliyobainika kumweka Sara katika kundi hili ni kuwa na maamuzi ya haraka. Sara alifanya uamuzi wa haraka kuambatana na Prospa ili kukamilisha matamanio yake ya kwenda Dar es Salaam. Alisema, "Na mimi nataka kwenda

Darithalam, twende wote. Thiku thote natamani kwenda kutembea Darithalam. Nataka nithome univethiti" (uk. 48). Hali hii ilimshangaza Prospa, hakumwamini Sara, lakini ghafla akamwambia kuwa anakwenda nyumbani kuchukua nguo, hivyo, amngoje, asiondoke. Aliporudi, alikuwa ameshikilia kifurushi kidogo. Prospa akataka kujua alichobeba, akamwambia ni kitenge; hivyo, alimwamuru aweke kwenye mfuko. Ijapokuwa Prospa alisita, akihofia huenda msichana huyu amebeba vitu vya uchawi, lakini msichana alifanya haraka. Mwandishi anasema:

> Msichana hakuwa na subra. Alisema, "Agh, hebu," akachukua mkoba wa Prospa aliokuwa ameuning'iniza begani, akafungua zipu, akaweka kitenge chake bila kutazama ndani. Alifunga zipu, akaning'iniza mkoba begani mwa Prospa (uk. 49).

Katika dondoo hilo, tunaamini kuwa huu ni uamuzi wa haraka ambao ulimwacha Prospa akiwa ameduwaa. Hakuwa na namna ya kukataa, kwani tayari kitenge kilikuwa ndani ya mkoba wake. Uamuzi mwingine wa haraka alioufanya ni wakati wanafikiria namna gani wataweza kuondoka kwenda kwa mzee Mathayo. Mwandishi anasema kuwa Sara, kwa haraka, alisimama nje ya mlango wa chumba na kuita kwa sauti:

> "Tofa, Tofa e, tafadhali mthaidie dada Uthuri kuosha vyombo. Mimi naandika barua Prothpa aende nayo." Tofa alijibu, "Haya" lakini Uzuri alimwambia siyo kitu, aandike tu barua yake. Kabla Uzuri hajarudi jikoni, wote watatu, Sara, Prospa na Mansa walitoroka upesiupesi kwa kupitia jikoni. Walipofika nje, Mansa alizunguka nyuma akamwendea Mateo na kumwambia, "Ni sisi tunafunga geti mzee, usiwe na wasiwasi, tunakwenda dukani mara moja." Baada ya kumtoa hofu mzee Mateo walikimbia bila kutoa kelele hata kidogo hadi walipofika nje ya geti. Sara alisema, "Mimi nitarudi mara moja nimthaidie Tofa, mthee athithtuke" (uk. 157).

Kutokana na dondoo hili, ni dhahiri kuwa yote haya yalifanyika kutokana na Sara kufanya uamuzi wa haraka ambao ulisukumwa na matamanio yake ya kutaka kumpata Merisho. Uamuzi wake ulisaidia kutoka nje ya uzio wa nyumba bila ya kujulikana lengo lao.

Sara pia amebainika kuwa na sifa ya kupendwa na kupendeka kwa haraka. Hii ni sifa nyingine ya watu wenye silika ya sangwini, kama asemavyo CKDOE2 (2020) kwamba:

> Sangwini ana tabia ya kupendwa kwa sababu ya uchangamfu wake. Anapopendwa hupendeka, pia wanapenda kupendwa na kila mtu ndiyo maana huwa nadhifu. Wakati mwingine hudiriki kujisifu au kusifia watu wengine ili wawapende.

Ithibati hii inalingana na data za maktabani zitokazo katika riwaya teule. Mathalani, baada ya Sara kumuomba Prospa waende wote Dar es Salaam, Prospa alisema kuwa hana nauli, jambo ambalo lilimshangaza Sara, ambaye alimwuliza alifikaje Same. Ili kumshawishi zaidi Prospa ampende na kuondoka naye, Sara alisema:

> "Bathi wathiwathi ondoa. Mimi Edithoni mthichana mthuri nitaomba lift." Alijigeuza na kujipinda kwa maringo.
> "Unaitwa Edison?" Prospa aliuliza
> "Ee, kumbe hujui? Jina langu Thara Edithon. Mtoto wa mfalme."
> "Edison ni jina la kiume," Prospa alisema. "Na siku hizi hakuna mfalme."
> Sara alicheka sana, akaondoka akikimbia huku akicheka na kusema, "Nani kathema, nani kathema."
> Prospa alisimama alipokuwa. Alisema, Yesu Ruwa, huyu Sara ni kichaa. Zilikwisha fyatuka."
> Sara alikwishafika mbali. Alisimama na kugeuka. Alimwita Prospa kwa nguvu. Njoo, kimbia. Njoo nikuambie thiri."
> Prospa, bila kusita, alimkimbilia Sara. Sara alimpokea kwa kumshika mkono. Akamvuta na kukimbia naye wakifuata barabara…Sara alisimama ghafla akamgeukia Prospa na kumuuliza kwa sauti laini, "Prospa, hebu thema, unanipenda…" (uk. 50-51).

Utafiti uliofanyika ulibaini kuwa mazungumzo hayo yaliyonukuliwa yalifanyika ili Sara ahakikishe kuwa Prospa anampenda. Hata hivyo, alipoona Prospa hamwelezi kama anampenda, aliamua kumwuliza ili apate uhakika. Hili pia linadhihirika alipokutana na Uzuri. Alijitahidi kumsifia Uzuri ili ampende, wawe marafiki, na apate taarifa anazozihitaji. Mwandishi anafafanua:

> "Sara wewe unafanya nini hapa? Nenda ukakae na hao wazururaji wenzako." Sara alitabasamu. Mlango wa mazungumzo umefunguka, alijiambia kimoyomoyo. Uzuri alimtazama, alivutiwa na tabasamu, na hapohapo kabla ya Uzuri hajasema lolote, Sara alisema, "Wewe ni mthuri kama udi."
> Uzuri aliuliza, "Unasemaje?"
> "We ni mthuri kama udi," Sara alirudia.
> Uzuri alicheka. Alirudia tena kuchambua mchicha, lakini kicheko kilimbana akaanza kucheka tena. "Mtoto we, una mambo," alisema.
> "Unacheka hekaheka," Sara alimwahi, akiwa naye anacheka.

> "He! Hivi kuzurura mjini kwenye jua kunalainisha ubongo?" Uzuri alisema. Hali ya raha ilimrudia. Alianza kuvutiwa na huyu msichana (uk. 141-143).

Utafiti ulibaini kuwa haya yote yaliwezekana kutokana na silika ya sangwini iliyosukuma matamanio yake. Kwa vyovyote vile, mtu hawezi kukaa na mtu mwingine wa silika hii asimpende. Hata kama hatampenda yeye, basi atapenda maongezi yake na vituko vyake. Jambo hili linathibitishwa na Ponera na Kasiga (2019) kwa kumtumia mhusika Willy Gamba. Wanasema kuwa mhusika wa kisangwini hupendwa au kupendeka kwa urahisi, hususani na wanawake. Kwa hiyo, Sara alifanikiwa kumchota Uzuri na alichoteka, akampenda, wakafanya kazi pamoja, na kumweleza mambo mengi kuhusu kazi yake na maisha ya pale nyumbani.

Sifa nyingine ya sangwini ni kuwa na maono ya haraka na ubunifu katika kutatua jambo. Utafiti umebaini kuwa kutokana na silika yake, Sara aliweza kutatua mambo mbalimbali ambayo kwa wenzake yalionekana yana ugumu. Kwa mfano, baada ya kuomba lifti kwa msamaria mwema, msamaria huyo alitaka kujua kama wametoroka nyumbani. Sara alipata maono ya haraka na kumfinya Prospa ili asizungumze, kwa sababu alihisi ataharibu mipango. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

> Magari mengi yaliwapita kwa kasi yakitimua vumbi. Baada ya kujaribu kwa muda mrefu, mtu mmoja alisimamisha gari lake. Sara alimshika Prospa kwa nguvu na kumwambia, "Acha niombe mimi. Uthitheme kitu."
> "Usipopata utaniona," Prospa alimtishia.
> Sara alimwambia mwenye gari, "Baba tunatembea mimi na mdogo wangu kwenda Darithalam. Tuthaidie."
> "Mnatembea? Mmetoroka nyumbani?" Mwenye gari aliuliza.
> Mkono mmoja wa Sara ulimfinya Prospa asije akasema kitu.
> Sara alisema, "Hapana baba. Baba yetu yupo Darithalam, thatha mama ametukimbia, amemfuata baba. Nyumbani hakuna chakula"… (uk. 51-52).

Akili ya Sara hufanya kazi kwa haraka sana anapotaka kutatua jambo fulani. Kulingana na Nadharia ya Saikochanganuzi, inadhihirika kuwa nafsi ya kiwango cha kati ilimsukuma kufanya maamuzi ya busara. Ushawishi wa Sara ulimfanya yule msamaria mwema awaamuru waingie ndani ya gari na safari ikaanza ijapokuwa haikuwafikisha hadi Dar es Salaam.

Pia, imebainika kuwa Sara aliwaamuru watoto wenzake waondoke eneo la nyumbani baada ya kuona wanamwuliza maswali mengi. Watoto hao walipanga kwenda kwa Mchau kumtafuta Merisho baada ya Uzuri kumdokeza Sara kwamba katika nyumba hiyo kuna mtoto amefichwa. Baada ya mipango yao, kila mtu alikuwa anawaza, lakini walionekana kutokumwamini Sara, kwa sababu alikuwa karibu sana na Uzuri. Walihofia kuwa atatoa siri. Hivyo basi, Sara alifanya maamuzi ya haraka ya kuwashauri waondoke eneo la nyumbani. Mwandishi anasema:

> Wote walilindana isipokuwa Sara aliyekuwa na Uzuri. Wote walikuwa na wasiwasi mkubwa sana juu ya Sara. Kila mara mmoja wao alimwita Sara na kumuuliza swali: "Je, vipi, mnafanya nini huko ndani?" au, "Je, Sara, chakula tayari?" au, "Sara, mbona mnacheka sana na Uzuri? Mnaongea nini?" Ilipofika saa tano, Sara alichoka kuulizwa maswali. Aliwaambia, "Nyie thatha mtanipa taabu. Nendeni mjini mrudi thaa kumi." Wote walifurahia wazo la kwenda mjini. Walipata jambo la kufanya. Mara moja waliondoka bila ubishi … (uk. 149).

Kwa hiyo, hapo imebainika kuwa Sara alifanya uamuzi wa haraka ambao ulisaidia kuwaondoa wenzake, na waliporudi, akili zao zilikuwa zimetulia. Tunaamini kuwa ni uamuzi wa haraka, kwa sababu hakuna aliyeutarajia katika kipindi hicho. Lengo la vijana wale lilikuwa wakae na Sara na kumwuliza maswali ili asipate muda mwingi wa kuwa na Uzuri. Kutokana na Nadharia ya Saikochanganuzi, matamanio ya nafsi yake ndiyo yaliyomsukuma kufanya uamuzi huo kwa haraka kwa kuchunguza wema na ubaya wa akina Prospa kuwepo au kutokuwepo eneo hilo. Kwa hiyo, aligundua kuwa ni vibaya wao kuwepo na kuendelea kuulizwa maswali, na ni vema wakaondoka ili muda uende.

Kwa jumla, hizo ndizo silika za wahusika wakuu katika riwaya ya *Safari ya Prospa*. Silika zao zinatofautiana. Hivyo, zinawafanya waweze kuishi pamoja bila mafarakano. Pia, maelewano yanapokosekana, imekuwa rahisi kusawazisha tofauti zao. Sara ni msondani, wakati Prospa ni mndani. Jambo hili linawasaidia katika safari yao ya kumtafuta Merisho, na hatimaye kumpata.

#### 4.3.2.3 Silika ya Mbumi

Katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* mwandishi amempa Mbumi sifa na matendo ambayo utafiti umebaini kuwa yanamweka katika silika ya koleriki. Silika hii ni ya

watu ambao hisia zao zipo nje, lakini hutofautiana na sangwini, kwani wao zipo nje kwa kiasi kikubwa sana. Tumekwishaeleza katika sehemu zilizotangulia kuwa hakuna mtu mwenye silika moja, bali tunaangalia ni ipi inajitokeza zaidi. Hivyo basi, sifa zilizobainika na kumweka Mbumi katika kundi hili ni zifuatazo:

Sifa ya kwanza ni ujasiri katika mambo anayoyafanya. Imezoeleka kuwa katika riwaya nyingi mwanamke au mtoto wa kike husawiriwa kwa kuoneshwa kuwa ni kiumbe dhaifu na kisicho na maamuzi, bali, kila kitu huamuliwa na mwanaume. Mathalani, Moh'd (2017) amemsawiri mwanamke kama mtawa. Ametolea mfano wa Maimuna anayetawishwa na baba yake, mzee Maksuud, na kunyimwa haki na uhuru. Tofauti na riwaya nyingine, katika riwaya hii, mwanamke amepewa sifa za ujasiri ambazo wakati mwingine huwashinda hata wanaume. Mwandishi aliamua kwenda kinyume na kaida zilizozoeleka za kumkweza mwanaume na kumtweza mwanamke. Mwandishi anaungana na Bakize na Senkoro (2019) ambao walimsawiri mtoto wa kike kama shujaa wa riwaya za kihistoria. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa kuanzia mwanzo hadi mwisho wa riwaya hii, Mbumi ameonekana ni jasiri asiyekata tamaa. Kwa mfano, mwanzoni mwa hadithi, mwandishi anatanabahisha ujasiri wa Mbumi kwa kusema:

> Mbumi alianza kutembea gizani kuelekea mlangoni. Hajafika kizingitini akasikia Chulu akiita, "Bibi!" "Sio bibi, ni mimi Mbumi," dada yake aliitikia. "Umevisikia hivyo vishindo?" "Ndiyo; nakwenda kuangalia." Alimsikia Chulu akiteremka kitandani. Punde wote wawili walikuwa mlangoni. Chulu alikuwa ameshika mkuki aliouacha baba yake. Mbumi alizoa mundu hapo sebuleni, akaukamata imara kwa mkono wa kulia. Walitoka nje. Kulikuwa bado hakujapambazuka, japo dalili za wekundu wa mapambazuko zilikuwa zinaanza kuonekana mbali sana mashariki (uk. 7).

Dondoo hili linatuthibitishia kuwa kutokana na ujasiri aliokuwa nao Mbumi, alikuwa wa kwanza kutoka nje bila woga ili kuangalia kinachotokea. Pacha wake alisikia, lakini alikuwa bado yupo kitandani, huenda aliogopa kutoka peke yake. Kwa muktadha wa utafiti uliofanyika, maelezo katika dondoo hili yana maana kuwa mwanamke yuko mstari wa mbele kukabiliana na hatari yoyote inayoweza kutokea. Ithibati nyingine inapatikana katika ukurasa wa 11-13 walipomsaidia majeruhi aliyepigwa risasi. Mbumi alimfunga jeraha lililokuwa linavuja damu. Alidiriki

kuchana kipande cha nguo yake kutoka katika shuka aliyojifunika na kumfunga kidonda chake kilichokuwa kinavuja damu.

Mwandishi anazidi kusawiri ujasiri wa Mbumi pale walipokaa mianzini kumsubiri Mpunza ambaye alikwenda kwa Munzagila, Iringa, kupeleka habari juu ya kuonekana kwa maadui. Baada ya kupata chakula, walijipumzisha baina ya mianzi. Imebainika kuwa Mbumi hakuridhishwa na hali hii ya kukaa ilihali wao ni vijana ambao wametumwa kuitumikia nchi yao. Hivyo basi, aliamua kutoa wazo:

> "Kwanini tunaketi hapa kama mitungi?"
> "Unataka tufanye nini?" Chulu alimjibu.
> "Tunakuwa kama si wanasokomoko?"
> "Eh?"
> "Kwanini tusitoke hapa mianzini tukaenda huko kilimani kuangalia adui anafanya nini?"
> "Ni wazo zuri," Chulu alimwitikia. Waliondoka taratibu, kimyakimya, mle mianzini … walinyatianyatia kimyakimya, wakavuka kijito cha Lugalo, wakaanza kupanda kilima ng'ambo ya pili kuelekea kule walikowaona maadui alasiri ile. Walipanda kwa taabu kizani, mara kwa mara walijikwaa kwenye majabali au kukwaruzwa na vichaka vyenye miiba … (uk. 63).

Nukuu ya hapo juu inatuthibitishia kuwa, pamoja na giza lililokuwapo nje, na mazingira ya pori, Mbumi hakuona taabu kwa sababu ya ujasiri aliokuwa nao. Chulu alikuwa anafuata tu kile asemacho pacha wake, na iwapo asingesema, huenda angeendelea kupumzika na wasingejua wapi walipo maadui na kile wanachokifanya. Kulingana na Nadharia ya Saikochanganuzi inayojibainisha kwa dhana ya nafsi kuibua silika zilibanwa kutoka katika ung'amuzibwete kuingia katika hali ya umaizi, hivyo, fikra hii inatuelekeza katika hoja ya kuwa nafsi ya Mbumi iliibua hisia hizo kwa kuona kukaa mianzini ni kupoteza muda.

Sehemu nyingine inayodhihirisha ujasiri wa Mbumi ni pale ambapo Chulu alikutana na adui na kumwamrisha asimame. Chulu hakusimama, ila alikimbia kurudi juu ya kilima walipokuwa na dada yake. Alipofika pale walipokuwa na dada yake, akamwamuru dada yake akimbie kwa sababu adui anakuja, akamrushia Mkuki-wa-Mianzi, Mbumi akaudaka. Pamoja na kusisitizwa na kaka yake kukimbia, Mbumi hakukimbia kutokana na silika yake. Mwandishi anasema:

> Mbumi hakukimbia. Aliinama ghafla, akaokota jiwe kubwa, akalitupa kwa nguvu zake zote kuelekea kule alikokuwa adui. Hakujua kama jiwe hilo litampata mtu huyo au la, ila alisikia kishindo cha mtu aliyeanguka. Kisha, pakawa kimya. Alianza kukimbia kuelekea upande wao huku akimhimiza Chulu, "Twende! Twende haraka!" (uk. 64-65).

Imebainika kuwa kutokimbia kwa Mbumi na kudiriki kurusha jiwe, ni ujasiri mkubwa. Kama angekuwa goigoi angeweza kutimua mbio ili kuokoa roho yake. Chulu, pamoja na kumhimiza dada yake akimbie, alikamatwa kwa sababu alipunguza mwendo baada ya kuona kimya kimetawala akijua kuwa adui yule ameshauawa, kumbe jiwe la Mbumi lilimpata tu jichoni, na hivyo, kumuongezea hasira. Matukio yote baada ya Chulu kukamatwa yanadhihirisha ushujaa aliokuwa nao Mbumi. Hakukaa chini na kuanza kulia, bali alikimbia peke yake ili apeleke taarifa kwa Munzagila kuhusu kukamatwa kwa Chulu. Suala hili linatiliwa mkazo na Lyimo (2020) anaposema kuwa:

> Mbumi alikuwa jasiri ambaye alimhamasisha ndugu yake kufuata yale anayoyafanya. Kitendo cha kurusha jiwe gizani ni bahati aliyokuwa nayo iliyotokana na shabaha walizojifunza katika mafunzo ya wanasokomoko. Mbumi amekuwa mfano wa kuigwa kwa jamii yake na kwa wasomaji ambao humdharau mtoto wa kike na kumkweza mtoto wa kiume.[12]

Pamoja na hayo, tukio la Chulu kukamatwa lilizidisha ujasiri wa Mbumi, kwani alijihisi kuwa ni mtu anayetegemewa na ndugu yake, pamoja na nchi yake. Ari ya kumkomboa ndugu yake iliongezeka, ingawa alikuwa ameshatoa taarifa kwa Munzagila na kuahidiwa kuwa Chulu atapatikana tena akiwa salama salimini. Hivyo, usiku huohuo alitoroka ili kutimiza azma yake ya kumwokoa pacha wake. Huko nje kiza kilikuwa totoro, lakini hakujali. Macho hayakuwa na msaada, hivyo, alitumia zaidi masikio. Alisikia sauti za wadudu na wanyama tu. Aliendelea na safari yake kwa kupanda na kuteremka kwenye vilima, na mara chache alijikwaa, lakini hakukata tamaa. Alipofika katika mianzi, aliingia ili atafakari namna ya kumwokoa Chulu. Mulokozi (khj) anasema kuwa mazingira ya kiutamaduni na kihistoria yalimkuza mhusika mtoto na kumfanya kuwa jasiri, ingawa alikuwa bado mdogo. Kwa hakika, Mbumi alikuzwa na mazingira haya. Mwandishi anafafanua:

---

[12]Mahojiano kati ya mtafiti na Dkt Lyimo yalifanyika ofisini kwake katika jengo la TATAKI - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mnano tarehe 17/6/2020. Dkt Lyimo alikuwa ni Mkuu wa Idara ya IFAMU na mtaalamu wa Fasihi ya watoto.

> Mbumi aliulaza Mkuki-wa-Mianzi mapajani kwake, akakishikilia barabara kisu chake, akaketi vizuri huku amejiegemeza kwenye mwanzi mnene na kuwaza juu ya maisha na mapambano na mauti. Wakati huu hakuwa kigori wala mtoto tena; alikuwa yu mtu mzima, askari mkali, mjanja na jasiri. Alikuwa Mwanasokomoko. Hakuogopa kifo (uk. 78-80).

Maelezo hayo yanaonesha kuwa Mbumi alikuwa tayari kwa lolote kutokana na ujasiri wake. Vitendo vya kuuweka mkuki mapajani mwake na kukishikilia kisu, kwa mujibu wa utafiti wetu, ni cha kijasiri. Mambo hayo yamezoeleka zaidi kwa wanaume kama Bakize na Senkoro (2019) wanavyosema katika andiko lao kuwa suala la mkuki kubebwa na msichana linaleta mkanganyiko, kwa sababu imezoeleka kuwa mkuki unabebwa na wanaume. Wanaongeza kuwa katika riwaya za watoto za kihistoria, ikiwamo inayoshughulikiwa na mtafiti, mtoto wa kike amechorwa kama shujaa anayeweza kupambana na kukabiliana na kila hali kama ilivyo kwa mtoto wa kiume. Nafsi yake iliibua silika zilizohifadhiwa kutoka ung'amuzibwete kuingia katika hali ya umaizi. Mbumi hakuogopa kifo na alikuwa ameshajitoa muhanga kwa lolote ili mradi amwokoe ndugu yake.

Mwandishi anamsawiri Mbumi akiwa na juhudi za kumtafuta pacha wake baada ya kuona kuwa kumetulia kabisa na kuhisi kuwa hata askari wa doria watakuwa wamepumzika. Alitembea hadi kwenye uwanda wenye mianzi iliyoshikamana ambapo aliwaona maadui mchana uliopita. Baada ya kufika eneo hilo, alitoa mlio kama paka mwitu ambao walifundishwa katika mafunzo ya Wanasokomoko ili kumwarifu Chulu kuwa anakuja kumwokoa. Kisha, alianza kutembea miongoni mwa maadui. Mwandishi anasema:

> Mbumi alianza kutembea taratibu miongoni mwa maadui waliolala kwa miguu na mikono kama chui kwenye mawindo, akimkagua kila askari. Alipoona askari huyo amejitingisha alitulia kimya kama maiti. Askari huyo alifumbua macho na kumuona Mbumi. Hakushtuka; alijua kuwa katika msafara wao walikuwamo wanawake na wasichana kadha, maana askari Waafrika waliruhusiwa kwenda vitani na wenzi wao iwapo walitaka. Mbumi alisubiri hadi askari huyo arejee usingizini kabla ya kuendelea na ukaguzi wake (uk. 84).

Imebainika kuwa kitendo cha Mbumi kutembea miongoni mwa maadui ni cha kijasiri sana, ambacho ni watu wachache wanakiweza, tena wale ambao wamejitoa

muhanga kwelikweli. Kutokana na msingi wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaosisitiza haja ya kukidhi matamanio ya mtu, Mbumi alifanya yote hayo ili kukidhi matamanio yake ya kumwokoa ndugu yake. Katika mazingira kama hayo, ilikuwa ni hatari kwasababu kutokana na giza angeweza kumkanyaga askari yeyote, na ikawa rahisi kushtuka na kuweza kumgundua.

Utafiti pia umebaini kitendo kingine cha kijasiri alichosawiriwa Mbumi pale walipowaona maadui wanakuja upande wao wakati vita inaendelea. Chulu alionesha kushtuka na kumwuliza dada yake nini wafanye au wakimbie? Mbumi hakukubaliana na wazo la Chulu, kwani kukimbia haikuwa sahihi, kwa kuwa kwa wakati huo watu wote walikuwa wakipigana, hivyo, alimshauri wapigane kufa na kupona. Chulu bado alikuwa na wasiwasi na kumwuliza watafanyaje? Mbumi alitoa ushauri ambao ulibainika kuwa wa kijasiri, alisema:

> "Twendeni kule juu kilimani tukawasaidie wenzetu." Mbumi aliongoza njia kupitia mianzini na vichakani bila kuonekana, hadi wakakizunguka kile kilima mpaka upande wa pili kulikokuwa na askari wengi kiasi. Mbumi alianza kupanda kilima huku Chulu akimfuata. Walifika juu ya kilima ambapo palikuwa na chungu kubwa ya mawe. Mbumi alisogelea chungu hiyo ya mawe, akachagua jiwe moja na kulisukuma kwa nguvu zake zote kuelekea kule walikokuwako maadui. Jiwe hilo lilibiringika kama mpira kwenye mteremko mkali wa kilima, likijigonga kwenye majabali na kuruka juu ya vichaka kwa mvumo na vishindo. Kabla halijafika chini ya kilima, Mbumi alikuwa ameshaporomosha mawe mengine kama matano, yakawa yanafuatana kwa vishindo mithili ya vipande vya jabali lililolipuliwa kwa baruti (uk. 104).

Mwandishi anasimulia kuwa wakati Mbumi anafanya yote haya, Chulu alikuwa akimtazama na kushangaa vitimbi vya dada yake, lakini alipomwelewa, ilibidi aungane naye na kumsifu kuwa ana akili sana. Mbumi alimtahadharisha ndugu yake asisimame sana ili maadui wasimwone. Kitendo hiki cha Mbumi ni cha kijasiri sana kikilinganishwa na umri aliokuwa nao, kwani alikuwa na uwezo wa kukimbia kama kaka yake alivyomshauri awali. Ithibati nyingine ya ujasiri wa Mbumi inatolewa na CKDOE4 (2020) anapotaja sifa za koleriki kwa kusema kuwa ni watu jasiri sana wasiokuwa na hofu na mtu yeyote. Sifa hii imemsadifu Mbumi ambaye hakuogopa hata maadui.

Sifa nyingine ya watu wa silika ya koleriki ni kufanya maamuzi yakini. Utafiti umebaini kuwa watu wa silika ya koleriki wana maamuzi ya haraka na sahihi, na mara nyingi wanapofanya maamuzi hayo, hawakosei. Katika masimulizi, Mbumi anaonekana ni mtu wa maamuzi hasa, na mara zote anapoamua, kinachofuata ni utekelezaji tu. Baada ya kusikia vishindo nje ya nyumba yao, Mbumi alizinduka kutoka usingizini na kuketi kitandani. Maamuzi ya awali kuyafanya ilikuwa ni kumwamsha bibi yake. Mwandishi anasema:

> Hakukawia zaidi. Aliruka kutoka kitandani, akamshika bibi na kumtikisa huku akisema kwa sauti ndogo, "Bibi amka! Kuna radi." Bibi aliamka na kuketi kitandani, akauliza kwa sauti ya usingizi, "Radi gani?" "Nasikia mishindo; labda kuna tufani yenye ngurumo!" Hakutaka kumweleza bibi kuwa alikuwa amesikia mishindo ya bunduki. "Kuna nini?" Bibi alimaka huku akijizoazoa kitandani. Alisikiliza. "Labda ni vita! La haula! Mahoka wapishe mbali! Mateso tuliyopata hayajatosha tu?" Bibi, ambaye sasa alikuwa yu macho kabisa, alilalama huku akirusha mikono yake iliyokaza misuli (uk. 4).

Dondoo hili linatuthibitishia kuwa maamuzi ya Mbumi yalikuwa sahihi, kwani kama angemwacha bibi, huenda angekuja kulaumiwa baadaye, au lolote lingeweza kumtokea. Jambo hili linaungwa mkono na Spinelli (2018) anaposema kuwa watu wenye silika ya koleriki huwa na uamuzi wa haraka usiokuwa na chembe ya woga au wasiwasi. Nafsi ya kiwango cha ukomavu ilimsukuma kufanya hivyo baada ya kuchunguza wema na ubaya wa kumwamsha bibi yake. Kwa hiyo, Mbumi alipoona bibi ameamka kabisa alifanya maamuzi ya kutoka nje kwenda kushuhudia nini kinachotokea.

Utafiti pia umebaini maamuzi mengine yakini aliyoyafanya ambayo ni kwenda kutoa taarifa kwa Munzagila juu ya kukamatwa kwa Chulu. Mbumi alifahamu kuwa maisha ya ndugu yake yalikuwa hatarini na yalimtegemea yeye. Hivyo, hakuona sababu yoyote ya kupoteza muda. Mwandishi anatanabahisha:

> Aliteremka kilima mbio mbio, akaacha njia ya kushoto ya kurejea mianzini, akafuata njia ya kulia iliyoelekea kijiji cha Viwengi ambacho alihisi kilikuwa karibu. Hapakuwa na wasaa wa kupitia tena mianzini kuchukua mizigo yao. Potelea mbali! Vitu walivyoviacha huko vitafuatwa baadaye hatari ikishapita. Alikaza mwendo. Ingawa baridi ilikuwa kali, lakini jasho lilikuwa likimtoka mwili wote. Alikuwa akihema, lakini dharura ile

> ilimfanya asihisi uchovu. Kichwani alikuwa akiwafikiria watu wale aliowaona… (uk. 66).

Nukuu ya hapo juu inatuthibitishia maamuzi yakini yaliyofanywa na Mbumi. Inaonesha kuwa Mbumi hakujali mizigo waliyoiacha mianzi kutokana na umuhimu wa taarifa alizotaka kuziwasilisha. Hata hivyo, hakuhisi uchovu, licha ya kukimbia sana. Mbumi aliendelea kukimbia akiwa peke yake hadi alipofika kijiji cha Viwengi na kuoneshwa nyumbani kwa Munzagila, kisha akatimiza azma yake ya kuwaarifu kuhusu kukamatwa kwa Chulu na wageni aliowaona. Matamanio yake yalikuwa ni kumwokoa ndugu yake ili waendelee na mapambano.

Si hayo tu, imebainika pia kuwa Mbumi alifanya uamuzi wa kutoroka nyumbani kwa Munzagila alipokuwa amekaribishwa na kuambiwa apumzike hadi siku itakayofuata. Wazo lake lilikuwa moja tu, kumkomboa ndugu yake kutoka katika mikono ya maadui. Dhamira yake muda wote ilikuwa ikimwambia kuwa hatma ya uhai wa Chulu na nchi yake kwa jumla ipo mikononi mwake. Nafsi ya kiwango cha kati ilimwongoza kutoroka kwa kuona kuwa Munzagila anachelewa. Hivyo, hakujali lolote katika kutimiza azma hiyo. Tukio lenyewe ni hili:

> Baada ya kula, Mbumi akiwa na Mkuki-wa-Mianzi alitoka nje bila kuaga. Aliwapita kwa taabu, akichelea kuwakanyaga, wasichana na wanawake waliokuwa wamelala ndani na nje ya nyumba. Nje ya uzio alikuta wanaume wengi wenye silaha wameketi wakisubiri amri ya kwenda Lugalo kupambana na maadui. Aliwapita kwa mbali gizani, akaingia kwenye njia kuu na kuanza kupiga mbio kuelekea Lugalo (uk. 77).

Mbumi aliweza kukimbia katika usiku wa giza nene kiasi kwamba hata alipoona visiki na vichaka alihisi kuwa ni mazimwi au wanyama wakali. Mwandishi anasema kuwa, mara kwa mara, alijikwaa na kuanguka na kuinuka tena, lakini hakujali, kwa sababu nia yake ilikuwa ni moja tu. Hatimaye, alifika sehemu aliyotarajia na kutimiza azma yake ya kumwokoa Chulu.

Maamuzi mengine yamebainika katika ukurasa wa 104. Baada ya kuona maadui wanaelekea upande wao, hakukimbia. Mbumi alimwambia ndugu yake wapigane kufa na kupona na alipanda kilimani na kuanza kuporomosha mawe kuelekea upande walipo maadui. Jambo hilo lilifanikiwa, kwani mawe yale yaliwapiga na kuwachanganya sana maadui, wakawa wanakimbia na kurusha risasi ovyoovyo.

Sifa nyingine ya koleriki ni kutopenda kudharauliwa. Utafiti umebaini kuwa Mbumi hakupenda kudharauliwa na mtu yeyote kwa kigezo cha umri wala jinsia. Kwa mujibu wa dhana ya Nadharia ya Saikochanganuzi, Mbumi aliibua hisia zilizohifadhiwa kutoka katika ung'amuzibwete kuingia katika hali ya umaizi. Alijitambua na kutambua kuwa jinsia yake sio sababu ya yeye kudharauliwa. Mtafiti anaamini kuwa katika jamii anayoishi Mbumi wanawake hudharauliwa, kwa hiyo hali hii ilijificha katika ung'amuzibwete, lakini alipoaminiwa ilijitokeza katika ung'amuzi au umaizi. Mathalani, kutokana na udogo wake na jinsia yake watu wengi walimdharau kwa kumwona kuwa hawezi kufanya kitu. Jambo hili lilimuudhi sana Mbumi, na hakusita kulikemea kila lilipotokea. Jambo hili linathibitika baada ya kufika kwa Mutwa. Mbumi na Chulu walieleza kilichowapeleka, ijapokuwa kuonekana tu kwa Mkuki-wa-Mianzi, kuliashiria ujumbe mzito. Walieleza kwa kupokezana, lakini maelezo ya ufasaha ya Mbumi yaliwashangaza wengi; hawakutarajia binti kama yeye kutoa maelezo hayo. Mwandishi anasema:

> Mutwa aliuliza maswali machache ambayo yalijibiwa na Mbumi na Chulu kadiri walivyoweza. Maswali hayo zaidi yalihusu hali ya maadui, silaha zao na mipango ya mapambano ya wana-Kwailoza. Majibu ya ufasaha ya Mbumi yalifanya baraza zima limkodolee macho kwa mshangao. Hatimaye mzee mmoja aliuliza, "Wewe binti unajuaje mambo hayo? Wewe ni askari? Umepigana vita?" "Nimeona na nimepigana," Mbumi alijibu kwa ufupi. "Kweli enzi mpya zaja," yule mzee aliongezea. "Tayari zimeanza," Mbumi alijibu. "Ndiyo maana tupo hapa." (uk. 43).

Maelezo katika dondoo hili yanadhihirisha kuwa mzee huyo alimdharau Mbumi kutokana na usichana na udogo wake, lakini Mbumi alimpa majibu yenye uhakika. Katika jamii zetu, mara nyingi wanawake hudharauliwa kutokana na mfumo dume, lakini wanawake wanaweza kufanya mambo makubwa kuliko hata wanayoyafanya wanaume ikiwa tu watapewa fursa ya kufanya mambo hayo. Mathalani, katika siku za hivi karibuni wanawake wanafanya kazi ngumu, ambazo hapo awali walikuwa wanafanya wanaume pekee. Kwa mfano, kuendesha magari, mabasi ya abiria, malori, kufanya kazi migodini na ujenzi wa nyumba.

Kwa upande mwingine, Chulu naye alionesha dharau kwa dada yake kutokana na kuwa msichana. Yeye, Chulu, aliamini kuwa si rahisi kwa mwanaume kukamatwa, lakini mwanamke anaweza kukamatwa na maadui. Hili huenda aliliamini kutokana

na mfumo dume ambao aliuishi. Hali hii ilimchukiza sana Mbumi ambaye alikuwa ameshajipambanua miongoni mwa mashujaa wa kutegemewa. Haya yalitokea wakati wanajadiliana na Mpunza kuhusu kukutana na maadui. Mwandishi anaeleza:

> "Mimi sitashangaa kama tukikutana nao," Mbumi alitamka. "Ila tuna ujumbe muhimu kwenda kwa Mundewa. Wakitukamata ndio mwisho wa safari."
> "Safari ya masafa au safari ya maisha?" Chulu alimhoji.
> "Zote."
> "Kukamatwa si rahisi," Chulu alisema kwa kujiamini. "Hasa sisi wanaume…"
> "Lakini inaweza kutokea," Mpunza alitahadharisha.
> "Kwa hiyo mimi mwanamke ndiye nitakamatwa, siyo? Wewe Chulu vipi?"
> "Samahani dada, nilikuwa natania tu."
> Mbumi aliendelea, "Ikibidi afadhali tufe kuliko kufichua siri ya nchi." (uk. 51-52)

Kupitia nukuu hii, inabainika kuwa Mbumi hakupenda kudharauliwa. Chulu alimdharau dada yake kutokana na kauli yake kwamba wanaume hawawezi kukamatwa na maadui. Hata hivyo, kutokana na utashi na matamanio yake, Chulu alisukumwa kuomba msamaha, kwa sababu haja yao ya kuikomboa Usagara na Wasagara ilikuwa haijatimia. Kwa kuwa Mbumi hakuwa na kisirani, alimsamehe, na jambo hilo liliishia hapohapo.

Utafiti pia umebaini namna Mbumi alivyochukia kudharauliwa pale walipokutana na askari wa doria ambaye aliwakamata akijua ni maadui. Bahati nzuri, Mpunza alijitokeza akiwa na sauti ya furaha akitokea kwenye doria ya upande mwingine. Yule askari aliwaachia baada ya kugundua kuwa ni wenzao, lakini akatoa onyo. Mwandishi anasema:

> "Nisiwaone upande huu tena, watoto; kuanzia sasa huu ni uwanja wa mapambano," yule askari mrefu alisema.
> "Hakuna watoto hapa." Mbumi alimwitikia.
> "Kumbe," yule askari alifoka. "Naona mna midomo! Si kosa lenu; hamjui msemalo wala mtendalo!" Alimalizia na kutema mate chini kwa hasira.
> "Tunajua kuwa mapambano tumeshayaanza sisi!" Mbumi alimwarifu. "Twendeni!" waliongozana na Mpunza kuelekea mianzini (uk. 90).

Dondoo hili linabainisha namna ambavyo Mbumi alichukia kuitwa mtoto. Aliona ni dharau kubwa kwa kuwa hata wao walikuja kwa ajili ya kupambana kuikomboa nchi yao. Nafsi ya kiwango cha kati ilimwongoza Mbumi kujua kipi ni kibaya na kipi ni kizuri. Kuitwa mtoto ilihali alikwenda kupambana aliona ni kitu kibaya sana. Pia, kitendo cha askari kufoka na kutema mate chini ilikuwa ni dharau kubwa sana kwake. Jambo hili pia linatiliwa ithibati na Lyimo (2020) alipofanya mahojiano na mtafiti. Mtaalamu huyu anabainisha kuwa Mbumi ni kiigizo cha ukombozi wa mwanamke dhidi ya dharau za wanaume. Anaongeza kuwa siku zote mwanamke au mtoto wa kike, akijitambua, atapiga vita watu wote wanaomdharau mwanamke.

Sifa nyingine zilizobainika kumweka Mbumi katika silika ya koleriki ni kutazama vitu kitunduizi. Katika safari yao ya kuelekea kwa Mutwa Mukwava walipita maeneo mengi na walivutiwa sana na mazingira hayo. Kwa mfano, masimulizi yanaeleza kuwa katika siku ya nne, wakati wanavuka mpaka wa Usagara na kuingia Uheheni, walivutiwa sana na mianzi. Waliona mianzi mingi sana ya kijani na ya manjano iliyokuwa ikipepea taratibu katika upepo mwanana wa asubuhi. Mianzi hiyo ilikuwa mirefu, yenye afya, yenye majani mazuri ya kijani yaliyokuwa yakichezacheza kufuata mwendo wa upepo. Mandhari hayo yalivutia sana na kusababisha Mbumi kuyatazama kwa tuo. Mwandishi anasema:

> Mbumi alimaka kwa mshangao, “Chulu unaiona hiyo ngoma ya mianzi?” “Ngoma?” Chulu aliuliza kwa mshangao. “Siioni.” “Huioni hiyo mianzi inavyocheza vizuri kwa madaha? Utadhani ngoma yetu ya rika ya dighubi?” Chulu ambaye hakuwa makini kwa uchunguzi kama mwenzake, sasa aliitazama mianzi hiyo kwa kituo na kusema bila kumtazama mwenzie, “Kweli inapendeza. Utadhani mkwajungoma!” (uk. 32-33).

Maelezo hayo yanadhihirisha namna Mbumi alivyoyatazama mazingira hayo kwa utunduizi kiasi cha kung’aka kwa mshangao. Mbumi alivutiwa na mazingira hayo kutokana na silika yake ya koleriki.

Mazingira mengine ambayo Mbumi aliyatazama kitunduizi ni ngome ya Lipuli. Katika safari yao baada ya kuvuka vilima kadha, walifika juu ya safu ya milima iliyozunguka mbuga pana sana ya kipenyo cha zaidi ya kilomita kumi. Munzagila akawahabarisha kuwa hiyo ni ngome ya Lipuli au Kalenga. Mwandishi anafafanua namna ngome hiyo ilivyo:

> Kutoka pale walipokuwa waliweza kuiona vizuri hiyo Lipuli au ngome ya Kalenga. Waliona kuwa Kalenga ilikuwa mji mkubwa ulioshikamana vizuri na kuzungushiwa kuta mbili: ukuta wa nje ulijengwa kwa magogo yenye miiba na ambao muda wote ulikuwa ukilindwa na mamia ya askari wenye mikuki na magobori; na ukuta wa ndani uliokuwa umejengwa kwa mawe makubwa… Kwa muda Chulu, Mbumi na Mpunza walisimama kilimani wakiyafurahia na kuyastaajabia mandhari yale ya Kalenga. Punde Munzagila aliwaashiria waendelee na safari. Waliteremka kwa haraka kuelekea chini mbugani (uk. 36-37).

Katika nukuu ya hapo juu tunaona kuwa wote walifurahia mazingira hayo lakini kutokana na silika ya Mbumi, yeye aliyatazama kitunduizi. Mara zote alikuwa akiyafurahia mazingira kama hayo na kusahau kama yupo safarini na wenzake.

Utafiti umebaini mazingira mengine ni ya bonde la Lugalo lililofunikwa na majani mengi marefu ya aina ya matete na mabingubingu yaliyokuwa yakipepea taratibu kufuata upepo. Mazingira haya aliyachunguza na kusababisha wasimame. Mwandishi anasema:

> Walisimama kwa muda mrefu wakiangalia bonde hilo pana la Lugalo. Walivutiwa na upana na utulivu wake. Walivutiwa na vijia vya miguu vilivyoteremkia humo bondeni kutoka ng'ambo zote mbili. Walivutiwa na vichaka vyeusi vilivyofunika magenge na miteremko iliyolizunguka bonde hilo; walivutiwa pia na nyasi ndefu na matete yaliyofunika kingo za mto wa Lugalo uliokuwa ukitiririka taratibu huko bondeni. Kila walichokiona hapo kilivutia. Hata ndege wa angani… Mbumi na Chulu walivutiwa na mambo yote kwasababu yalionesha ujana, uhai na matumaini (uk. 56).

Katika dondoo hilo hapo juu ni dhahiri kuwa wote walivutiwa na mazingira hayo, lakini kwa upande wa Mbumi ilikuwa tofauti kutokana na silika yake. Mbumi alitazama kitunduizi zaidi. Hii ndiyo silika ya watu walio katika kundi la koleriki, mara nyingi wanapokuwa katika mazingira yao hutumia muda mwingi kuangalia mazingira hayo na kuyachunguza kwa undani kutokana na kuvutia kwake. Pia, wanapoamua kutoka kwa ajili ya matembezi hupendelea mazingira yanayovutia.

Vilevile, ni watu ambao wanafaa kuwa viongozi kwa asili. Kiongozi kwa mnasaba wa utafiti huu ni yule anayeanzisha jambo, au anayefanya mambo mbalimbali kwa ajili ya wengine. Pia, siyo watu wanaojilimbikizia mali. Mathalani, wakati wa kujiandaa na safari yao, Mbumi alibeba mizigo mbalimbali, ikiwemo vyakula.

Alijitahidi kubeba kila kitu ambacho kingehitajika njiani. Bibi yao aliwaongezea vyakula zaidi, lakini Mbumi alimkatalia kutokana na sifa ya silika yake ya uongozi. Kwa kawaida, kiongozi huwajali na wengine. Hii inasimuliwa katika ukurasa wa 26 mwandishi anaposema:

> "Bibi!" Mbumi alimkatisha. "Vinatosha hivyo! Wewe utakula nini tukichukua kila kitu? Kwanza vizito, hatuwezi kuvibeba vyote. Tulivyochukua vinatosha," alimalizia huku akishindilia kapu lake, lililokuwa tayari limejaa makorokoro mengine.

Dondoo hilo linaonesha namna kiongozi anavyotakiwa kuwa. Si mtu wa kujilimbikizia vitu, na hujali watu wengine. Laiti kama Mbumi angekuwa mbinafsi, angebeba kila kitu alichopewa.

Sehemu nyingine inayotoa ithibati ya uongozi ni pale walipokuwa na haja ya kupata moto baada ya kujikuta porini na jua limezama. Mbumi alifanya matayarisho yote ya kuwasha moto, lakini Chulu alicheka sana na kumshangaa dada yake kwamba atawasha moto na nini. Kutokana na sifa ya silika yake ya uongozi, Mbumi hakuwa na wasiwasi, kwa sababu alijua lazima moto utawaka. Haya yanabainishwa kama ifuatavyo:

> Mbumi hakusema neno. Aliinuka, akachukua kapu lake, akalifungua, akatoa kipande cha ubao kilichokuwa na tundu katikati, akakiweka mbele yake. Halafu akachukua ujiti mwembamba, akauchomeka katika kibao kile na kuanza kupekecha. Chulu alimtazama Mbumi kwa mshangao, halafu akasema kwa kufahamikiwa, "Ala, kumbe umeleta ulindi na wimbombo? Ulikumbukaje?"
> "Wewe ulifikiri kapu lote hili nimebeba nini?"
> "Manukato na mapambo tu."
> "Basi umekosea. Kila kitu kina wakati wake. Kuna wakati wa utoto na wakati wa utu uzima. Kuna wakati wa kujipamba na wakati wa kujipambua…" (uk. 30-32).

Kwa hiyo, katika dondoo hilo inabainika kwamba Chulu hakutarajia kuwa angeweza kubeba vitu vyote hivyo. Kwa kuwa hulka ya wanawake walio wengi ni kujipamba, alidhani kuwa amebeba mapambo na manukato pekee. Hata hivyo, kama kiongozi, tangu awali walipokuwa wanatoka nyumbani, Mbumi alijua katika safari yao ni lazima watahitaji moto.

Aidha, watu wa silika ya koleriki huwa na sifa ya kuthubutu. Watu wa silika hii huthubutu kulifanya jambo hata liwe gumu kiasi gani, na mara nyingi matokeo yake huwa chanya. Kutokana na kuthubutu, wengi huishia kuwa matajiri au kupata heshima kubwa katika jamii. Kwa mujibu wa Mudhihiri (2019) ndani ya kuthubutu mwanadamu hubeba dhamira ya kumiliki ulimwengu na kunufaika katika mahitaji yake. Utafiti umebaini kuwa Mbumi alithubutu kutoka nje aliposikia ngurumo na mishindo ya bunduki (uk. 4-5). Pia alithubutu kuondoka bila kuaga katika boma la Munzagila ili aende kumwokoa ndugu yake, ambaye alikuwa ametekwa na mwisho kumkomboa. Mwandishi anafafanua:

> Baada ya kula, Mbumi akiwa na Mkuki-wa-Mianzi alitoka nje bila kuaga. Aliwapita kwa taabu, akichelea kuwakanyaga, wasichana na wanawake waliokuwa wamelala ndani na nje ya nyumba. Nje ya uzio alikuta wanaume wengi wenye silaha wameketi wakisubiri amri ya kwenda Lugalo kupambana na maadui. Aliwapita kwa mbali gizani, akaingia kwenye njia kuu na kuanza kupiga mbio kuelekea Lugalo… (uk.77).

Masimulizi tangu mwanzo hadi mwisho, yanaonesha kuwa Mbumi alithubutu kuipigania nchi yake kwa kupeleka ujumbe wa siri kwa Mukwava, ijapokuwa safari ilikuwa ndefu, yenye hatari, naye alikuwa na umri mdogo. Kutokana na msingi wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu matamanio, Mbumi alithubutu na kufanya jitihada ili kukamilisha matamanio yake ya kuikomboa nchi yake.

#### 4.3.2.4 Silika ya Chulu

Huyu ni pacha wa kiume ambaye imebainika kuwa mwandishi amemchora na kumpa sifa na matendo yanayomweka katika silika ya melankoli. Silika hii ipo katika kundi la wandani ambao wana uwezo mkubwa kiakili. Sifa za silika hii zinazobainika kwa mhusika huyu ni kama zifuatazo:

Sifa ya kufuata sheria na taratibu ambazo zinaweza kuwa za nchi au za jamii fulani ambazo hutofautiana na jamii nyingine. Taratibu hizi zinaweza kuwa mila na desturi za jamii husika. Utafiti umebaini kuwa katika jamii ya Chulu kuna kazi ambazo hufanywa na wanawake, na nyingine za wanaume. Mtoto anapozaliwa huzikuta, hivyo naye anapokua anaendelea kuzitumia. Katika siku ya nne ya safari yao, Chulu na Mbumi walijikuta wapo porini na jua limezama. Hivyo, ilibidi wapumzike hadi

kupambazuke. Ili kujilinda na wanyama wakali, ilibidi wawashe moto, lakini Chulu aliweka pingamizi juu ya kumsaidia dada yake kutafuta kuni. Mwandishi anafafanua:

> Mbumi alianza kukusanya kuni kavu kutoka katika vichaka vilivyokuwa karibu. Chulu alibaki chini ya mti amejiegemeza kwenye mkuki wake aliousimika ardhini. "Hunisaidii Chulu?" Mbumi alisema.
> "Mwanamume kuchanja kuni si mila yetu," Chulu alisema.
> "Mambo ya mila yangesubiri tumalize matatizo kwanza; hatuna muda," Mbumi alisema. "Hebu kanisaidie kukata tawi hilo hapo kwenye kichaka kile" (uk. 29-30).

Katika dondoo hilo imebainika kuwa taratibu ambazo Chulu alikuwa anazifuata ni za mfumo dume, kwa kuwa zilibagua kazi za wanawake na wanaume. Kutokana na mazingira waliyokuwa nayo, Chulu hakutakiwa kufuata taratibu hizo, kwani ni kipindi ambacho kilihitaji ushirikiano wa hali ya juu. Pia, sehemu waliyokuwapo ilikuwa porini na giza lilikuwa limeanza kuwanyemelea. Kutokana na Nadharia ya Saikochanganuzi nafsi ya kiwango cha msingi, ambayo ni nafsi ya kisilika na matamanio bila urazini, hali ya unyama, kitovu cha misukumo ya kisilika kama ushari na ashiki dhidi ya dhamiri ilimsukuma Chulu katika shari ya kukataa kumsaidia dada yake.

Sehemu nyingine inayobainisha kuwa Chulu alikuwa mtu wa kufuata sheria na taratibu ni pale walipokubaliana kulala kwa zamu walipokuwa porini. Makubaliano hayo yalimtaka aliyepo macho kuhakikisha kuwa moto hauzimiki kwa kuuchochea na kuongeza kuni. Alitangulia Mbumi, kisha ikafuata zamu ya Chulu. Toka walipoianza safari yao, Chulu alikuwa amebeba mkuki, hivyo, ilipofika muda wake wa kulala, hakutaka kupokelewa mkuki huo. Masimulizi yanafafanua:

> Moto uliwaka usiku kucha. Walipokezana kulala na kuchochea moto hadi asubuhi. Zamu ya Chulu ya kulala ilipofika, alikwenda kulala akiwa ameushikilia mkuki wake. Mbumi alimshauri ampokee huo mkuki, lakini Chulu alikataa na kusema kuwa ni muhali kabisa kwa mwanamke kushika mkuki. Alimshauri ashikilie kisu chake tu. Mara mbili tatu mafisi na wanyama wengine wa pori waliwasogelea kwa udadisi, lakini hawakuja karibu sana kwa kuogopa moto (uk. 32).

Utafiti umebaini kuwa huo ndio ulikuwa msimamo wa Chulu mara zote anapoona mila na taratibu zinataka kubanangwa. Haya yalikuwa maamuzi ya busara, lakini kutokana na mazingira waliyokuwa nayo alitakiwa atupilie mbali mila hizo potofu.

Sifa nyingine ya melankoli ni uvumilivu. Watu wa kundi hili kwa mujibu wa utafiti uliofanyika ni wavumilivu sana, hata wanapokumbwa na mikasa mbalimbali. Uvumilivu huwafanya kuwa na mwisho mzuri. Chulu alivumilia sana kutoka mwanzo hadi mwisho wa safari yao. Pamoja na umbali mkubwa wa kutembea, lakini bado alikuwa imara kuliendea lile waliloagizwa. Walitembea kwa zaidi ya siku tano. Mwandishi anatanabaisha:

> Kwa siku tatu za kwanza hali ilikuwa hivyo. Bali siku ya nne walijikuta bado wapo porini saa za magharibi. Hapakuwa na kijiji chochote karibu. Ilibidi wasimamishe safari yao na kupiga kambi chini ya mti mkubwa wa mgudu … Siku ya tano walianza kuona mabadiliko makubwa zaidi. Milima iliongezeka, baridi iliongezeka, ukungu ulitanda kila asubuhi, na umande baridi ulilowanisha miguu yao … siku ya sita walilala katika kijiji cha Iringa, karibu na Kalenga … siku iliyofuata, Chulu na Mbumi walijidamka, wakavaa nguo zao nzuri na kuanza safari kuelekea Kalenga … (uk. 29-35).

Huu ni uvumilivu wa hali ya juu kutembea siku sita katika misitu na vichaka vikubwa, milima na mabonde yenye baridi na umande mwingi.

Utafiti pia umedhihirisha uvumilivu aliokuwa nao Chulu mara baada ya kuokolewa na dada yake kutoka katika mikono ya maadui. Hali aliyomkuta nayo ilionesha kuwa alikuwa ameadhibiwa sana na maadui hao. Kwa hiyo, baada ya kuondoka pale, Chulu alikuwa anajisikia maumivu makali sana, lakini alivumilia, kwani aliona ni bora hayo maumivu kuliko kuendelea kuwa mikononi mwa maadui. Hili linadhihirika mwandishi anaposema:

> Sasa ikabakia kuondoka mahali pale bila kuonekana. Hawangeweza kuongea wala kushauriana. Mbumi aligeuka na kuanza kuondoka taratibu, akitembea kwa mikono na miguu. Chulu alimfuata nyuma kwa mwendo huohuo wa nyatunyatu. Mikono na miguu yake ilikuwa imekufa ganzi, lakini alijikaza. Maungo yalikuwa yanamuuma na kichwa kinamuwanga kutokana na kipigo alichokipata jioni ile kutoka kwa watekaji wake, lakini alivumilia. Alifurahi kuponyoka mahali pale pa hatari (uk. 87).

Kwa hiyo, Chulu alijikaza na kuvumilia kutokana na kuponyoka katika mikono ya watekaji wake. Nafsi ya kiwango cha kati ilimsukuma kuvumilia ili matamanio yake ya kutoka katika mikono ya watekaji yaweze kutimia.

Sifa nyingine ya melankoli ni wepesi wa kuomba msamaha pale wanapokosea. Kwa kuwa watu hawa wanapenda sana suluhu na amani itawale, wanakuwa wepesi sana kuomba msamaha. Chulu baada ya kugundua kuwa amemkosea dada yake kwa kumdharau, aliomba msamaha ili waendelee na mapambano dhidi ya maadui. Mwandishi anasema:

> "Mimi sitashangaa kama tukikutana nao," Mbumi alitamka. "Ila tuna ujumbe muhimu kwenda kwa Mundewa. Wakitukamata ndio mwisho wa safari."
> "Safari ya masafa au safari ya maisha?" Chulu alimhoji.
> "Zote."
> "Kukamatwa si rahisi," Chulu alisema kwa kujiamini. "Hasa sisi wanaume…"
> "Lakini inaweza kutokea," Mpunza alitahadharisha.
> "Kwa hiyo mimi mwanamke ndiye nitakamatwa, siyo? Wewe Chulu vipi?"
> "Samahani dada, nilikuwa natania tu."
> Mbumi aliendelea, "Ikibidi afadhali tufe kuliko kufichua siri ya nchi" (uk.51-52).

Kutokana na nukuu hiyo, utafiti uliofanyika umebaini kuwa Mbumi hakupenda kudharauliwa na Chulu, hivyo, Chulu aliomba msamaha mara alipogundua amemkosea dada yake. Utashi na matamanio yake ndiyo vilimsukuma kuomba msamaha. Haja yake ya kuikomboa Usagara na Wasagara ilikuwa haijatimia. Kwa kuwa Mbumi hakuwa na kisirani, alimsamehe, na jambo hilo liliishia hapohapo.

Utafiti umebaini kuwa watu wa kundi hili pia hupenda kujitolea. Sifa hii inadhihirika kwa Chulu, kwani alijitolea kufa na kupona kuitetea nchi yake. Pamoja na umri aliokuwa nao kuwa ni mdogo, hakuonesha woga hata pale walipopewa maagizo mazito na viongozi mbalimbali. Baada ya kufika nyumbani kwa Mundewa na kuripoti katika kikosi cha Wanasokomoko, Chulu na Mbumi waliambiwa kuwa wanaitwa Ikulu kwa Mundewa. Walipofika, aliwapa maagizo aliyowaitia, nao wakakubaliana naye kwa mustakabali wa Usagara na nchi yao. Mundewa alisema:

> Tumewaiteni ninyi kwa sababu tunafikiri, baada ya safari yenu ya Bagamoyo, mnao uzoefu wa kutosha kuliko wanasokomoko wengine. Aidha, yule Mutandisi kwa matakwa ya mahoka aliwakabidhi mikoba. Wa aidha, Mwanyenza, mjumbe wa Mutwa, bado anaumwa sana, hawezi kufuatana nanyi. Itabidi aendelee na matibabu. Nyinyi bado ni watoto wadogo lakini wenye upeo na uzoefu wa kiutu-uzima… "Sisi tupo tayari kutekeleza yote unayotaka, Mheshimiwa," Chulu alisema (uk. 21).

Kutokana na silika yake, Chulu alikuwa mwepesi sana katika kujitolea. Aliweza kuchunguza uadilifu wa tendo, wema na ubaya wake kabla ya kulitenda. Muda wote alikuwa na utayari wa kupambana na maadui, licha ya umri wake kuwa mdogo.

Pamoja na sifa hizo, Chulu pia ameonesha udhaifu kutokana na silika yake. Mwandishi anamsawiri kuwa muoga katika kuanzisha jambo. Linapotokea jambo la haraka au la hatari, watu wenye silika hii huwa wazito na waoga kulikabili. Hata baada ya kusikia vishindo nje ya nyumba yao, aliendelea kubaki kitandani akisubiri kama kuna mtu atatoka ili na yeye atoke. Mwandishi anafafanua hili kwa kusema:

> Mbumi alianza kutembea gizani kuelekea mlangoni. Hajafika kizingitini akasikia Chulu akiita, "Bibi!"
> "Siyo bibi, ni mimi Mbumi," dada yake aliitikia.
> "Umevisikia hivyo vishindo?"
> "Ndiyo; nakwenda kuangalia."
> Alimsikia Chulu akiteremka kitandani. Punde wote wawili walikuwa mlangoni. Chulu alikuwa ameshika mkuki aliouacha marehemu baba yake. Mbumi alizoa mundu hapo sebuleni, akaukamata imara kwa mkono wa kulia (uk. 5).

Dondoo hili linaonesha kuwa Chulu aliweza kutoka mara tu baada ya kusikia dada yake anatoka. Nafsi ya kiwango cha msingi ilimsukuma kubaki kitandani hadi alipomsikia dada yake anatoka. Chulu alivisikia vishindo vyote, lakini kutokana na silika yake, hakutaka kutoka. Katika mazingira ya kawaida, inaaminika kuwa wanaume siyo waoga, lakini Chulu na wengine wenye silika hii huathiriwa sana na uoga.

Vilevile, utafiti umebaini kuwa Chulu alionesha uoga baada ya kuwaona maadui wanakuja upande wao wakati vita inaendelea. Huu ni udhaifu kwake, kwani mara nyingi amekuwa akifuata kila anachosema dada yake. Kwa mfano, alionesha kushtuka na kumwuliza dada yake wafanye nini, au wakimbie? Mbumi

hakukubaliana na wazo la Chulu, kwani kukimbia haikuwa sahihi kwa kuwa, kwa wakati huo, watu wote walikuwa wakipigana. Hivyo, alimshauri wapigane kufa na kupona. Chulu alionekana kuchanganyikiwa asijue la kufanya. Mbumi alitoa ushauri wapande juu ya kilima, ijapokuwa Chulu hakujua kwanini. Mwandishi anasema:

> Mbumi alianza kupanda kilima huku Chulu akimfuata. Walifika juu ya kilima ambapo palikuwa na chungu kubwa ya mawe. Mbumi alisogelea chungu hiyo ya mawe, akachagua jiwe moja na kulisukuma kwa nguvu zake zote kuelekea kule walikokuwako maadui. Jiwe hilo lilibiringika kama mpira kwenye mteremko mkali wa kilima, likijigonga kwenye majabali na kuruka juu ya vichaka kwa mvumo na vishindo. Kabla halijafika chini ya kilima Mbumi alikuwa ameshaporomosha mawe mengine kama matano, yakawa yanafuatana kwa vishindo mithili ya vipande vya jabali lililolipuliwa kwa baruti (uk. 104).

Utafiti umebaini kuwa katika zoezi hili, Chulu alikuwa anamshangaa dada yake kwa sababu ya uoga wake. Hakuelewa alichodhamiria, lakini alipogundua lengo lake, ilibidi aweke uoga kando na kuungana na dada yake katika zoezi la kuporomosha mawe. Suala hili limetiliwa ithibati na Sanga (2015) anapodhihaki uoga kwa kusema kuwa wanajamii wawe na ujasiri wa kukabiliana na mambo magumu yanayowakabili. Anatolea mfano wimbo wa wagosi wa Kaya unaoitwa "*Traffic*" kuwaasa askari wa usalama barabarani ambao huogopa baadhi ya magari kwa kuhofia kuwa ni ya wakubwa, marafiki, au ya watu wenye pesa, ilihali yana makosa na yanatembea barabarani. Kwa jumla, watu kama Chulu wanahitajika katika maisha ili dunia iwe mahali salama pa kuishi. Wakati mwingine, uoga unaweza kuwa msaada kwa kuchukua tahadhari kabla ya kuliendea jambo kwa pupa.

Hivyo basi, kutokana na kutofautiana kwa silika zao, kumesaidia kuwafanya wahusika hawa waweze kufanya kazi kwa pamoja bila kukwazana kwa kiasi kikubwa, na aliyemkwaza mwenzake, alimuomba msamaha na kuendelea na safari yao. Ijapokuwa Chulu alionesha uoga katika baadhi ya matukio, hili halikuathiri safari yao, kwani Mbumi alimpa moyo ili kuondoa uoga huo; na hivyo, kutoa hamasa ya kuendelea na safari. Kwa hiyo, utafiti umebaini kuwa utofauti wa silika za wahusika hao umesaidia sana katika kufikia lengo la kufikisha ujumbe waliotumwa.

### 4.3.3 Hitimisho

Kwa jumla, sehemu hii imefafanua silika za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto katika riwaya ya *Safari ya Prospa* na *Ngoma ya Mianzi*. Imebainika kuwa kila mhusika ana silika yake inayomtofautisha na mhusika mwingine. Pia, pamoja na wahusika Mbumi na Chulu kuwa mapacha, silika zao ni tofauti. Kwa hiyo, silika ni jambo la muhimu katika kuwajua watu na tabia zao ili kuweza kuishi bila misuguano na mifarakano. Sehemu inayofuata inatathimini uhusiano baina ya utendaji wa wahusika wakuu na sifa za silika zao.

## 4.4 Uhusiano Baina ya Utendaji wa Wahusika Wakuu na Sifa za Aina za Silika

Mjadala wa sehemu hii unalenga kutathimini uhusiano baina ya utendaji wa wahusika wakuu na sifa za aina za silika zao. Hoja kuu ni kuonesha uhusiano uliopo baina ya utendaji na sifa za aina za silika zilizojadiliwa katika sehemu zilizotangulia. Ili kubaini silika ya mhusika, ni lazima atende. Matendo ndiyo husaidia kubaini silika ya mhusika huyo. Sehemu hii ina vijisehemu viwili: Uhusiano wa utendaji na sifa za aina za silika katika riwaya ya *Safari ya Prospa* na uhusiano wa utendaji na sifa za aina za silika katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi*. Sehemu zilizotangulia zimetuweka wazi kuhusu aina za silika za kila mhusika na utendaji wake. Katika uchambuzi, tumeona kuwa kila silika ina sifa zake na kila mhusika ana silika yake. Kwa kawaida, mwandishi huumba wahusika kutokana na kile alichodhamiria kuiambia jamii, na hivyo, huwavika tabia na matendo mbalimbali. Matendo ya mhusika huthibitisha silika aliyonayo. Hapa ndipo tunapopata uhusiano huo. Mulokozi (khj) anatanabahisha kuwa kazi ya mwandishi ni kuandika tu bila kujua kuwa mhusika fulani atakuwa na silika gani. Ni wajibu wa wahakiki na watafiti kulijua hilo. Pia, anasisitiza kuwa kazi za kifasihi hueleweka kwa namna za kuachana kutoka kwa mhakiki mmoja hadi mwingine. Hata hivyo, waandishi wote wa riwaya hizi walikubaliana kuwa kuna uhusiano mkubwa kati ya utendaji wa wahusika wakuu na sifa za aina za silika, kwa sababu wahusika ni wawakilishi wa binadamu waliopo katika jamii. Ifuatayo ni tathimini ya uhusika huo:

### 4.4.1 Uhusiano Baina ya Utendaji na Sifa za Aina za Silika katika *Safari ya Prospa*

Kama tulivyofafanua katika sehemu zilizotangulia, utendaji katika riwaya hii umetumia mitindo mbalimbali kama vile kuhoji, kushauri, na kutoa taarifa. Utafiti

umebaini kuwa katika riwaya, watendaji wanakuwa na pande mbili zinazogongana na kusukuma mbele hadithi, hatimaye, kufika kileleni, ambapo ujumbe unakuwa umefika. Pande hizo hugongana kutokana na jambo linalowasilishwa. Mathalani, suala la ukombozi wa mwanamke, wapo wanaoamini utaletwa na wanaume. Kwa upande mwingine, wanaamini utaletwa kwa ushirikiano baina ya wanawake na wanaume. Kwa hiyo, utendaji huu ni wa wahusika ndani ya hadithi, lakini hurejelea watu waliopo katika ulimwengu wa hadithi. Wahusika huwa wanahusiana, wanatenda na kusababisha au kuibua mambo fulani. Wahusika hutenda kutokana na silika zao. Kwa hiyo, hata migogoro inayojitokeza, huibuliwa kutokana na silika hizo. Silika ya mhusika hutambulika kwa kutenda. Hivyo, matendo ndiyo huakisi silika ya mtu. Hii ni kwa sababu, silika ni jambo dhahania. Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, tathimini ya uhusiano uliopo kati ya utendaji wa wahusika wakuu na sifa za aina za silika katika riwaya ya *Safari ya Prospa* ni kama ifuatayo:

Sifa ya silika ya Sara ya kuongea na kufanya utani na kila mtu ina uhusiano na utendaji wa kuhoji. Sifa hii imetokana na silika yake ya sangwini. Mara nyingi amekuwa akikutana na watu mbalimbali na kuongea nao bila aibu. Mathalani, alizoeana na Prospa na alipenda kumsemesha na kumtania. Utafiti umebaini kuwa alipenda kusikilizwa kila alipoongea. Ijapokuwa Prospa alistaajabu kutokana na muonekano wa Sara, lakini haikuwa kigezo cha yeye kushindwa kumsemesha na kumzoea. Mwandishi anasema:

> "…mimi Edithon mthichana mthuri nitaomba lift." Alijigeuza na kujipinda kwa maringo.
> "Unaitwa Edison?" Prospa aliuliza.
> "Ee kumbe hujui? Jina langu Thara Edithon. Mtoto wa mfalme."
> "Edison ni jina la kiume, Prospa alisema. "Na siku hizi hakuna mfalme,"
> Sara alicheka sana, akaondoka akikimbia huku akicheza na kusema, "Nani kathema, nani kathema."
> Prospa alisimama alipokuwa. Alisema, "Yesu Ruwa, huyu Sara ni kichaa. Zilikwisha fyatuka."
> Sara alikwishafika mbali. Alisimama na kugeuka. Alimwita Prospa kwa nguvu. "Njoo nikuambie thiri."
> Prospa, bila kusita, alimkimbilia Sara. Sara alimpokea kwa kumshika mkono. Akamvuta na kukimbia naye kwa kufuata barabara.
> Prospa hakupenda kuvutwa, alisema kwa hasira, "Sara mi sitaki."
> "Niite Edithon," Sara aliamuru.

> "Sitaki," Prospa alijibu.
> "Niite Edithon na wewe nikuite Maiko." Sara aling'ang'ania.
> "Sitaki, jina langu ni Prospa. Sitaki kuitwa Maiko." (uk. 50).

Dondoo hili linathibitisha kuwa Sara alifanya yote hayo ili kuwa karibu na Prospa. Sara alifaulu kuwa karibu na Prospa na kuandamana naye katika safari yake. Alidiriki kujipa jina la Edison na kumpa Prospa jina la Maiko ili kuwa karibu zaidi. Hii yote ilitokana na sifa za silika yake ya sangwini ya kupenda kuzungumza. Katika mazingira ya kawaida, imezoeleka kuwa ni mzazi pekee ndiye mwenye uwezo wa kumpa mtoto wake jina. Kutokana na nafsi tatu za ki-Freudi za Nadharia ya Saikochanganuzi, lugha ya Sara iliakisi michakato ya akilini iliyojibainisha katika misemo na usemaji wake.

Uhusiano mwingine unadhihirika pale Sara na Prospa walipofika nyumbani kwa Petro. Petro aliwaonesha sehemu ya kulala na kuwaandalia chai ya asubuhi. Hata hivyo, kutokana na njaa waliyokuwa nayo, walivamia na kuanza kula hata kabla ya kupiga mswaki. Katika mazingira ya kawaida, mtu akilala bila kula akiamka asubuhi huwa na njaa kali. Baada ya kushiba, Sara alipata nguvu. Hivyo, alimwuliza Prospa kuhusu mipango yao iliyowaleta Dar es salaam. Mwandishi anasema:

> "Thatha leo vipi?" Sara aliuliza.
> Prospa alimtazama Sara bila kumjibu. Alikuwa anatafuna andazi na kunywa chai mfululizo bila kujipa nafasi ya kuongea. Alitafuna haraka haraka kama vile anachelewa kufanya jambo jingine muhimu.
> Sara aliendelea kusema, "Unakumbuka? Mimi leo nitakuwa mfanyakathi wa Mohamed. Wewe utakuwa nani Prothpa?"
> "Polisi." Prospa alisema huku akimeza chai.
> "Halafu utafanya nini?" Sara aliuliza.
> "Wewe ndiye unafahamu kila kitu. Niambie nitafanya nini," Prospa alisema. Sara alikuwa bado hajamaliza chai wala maandazi. Prospa alimtazama kwa macho ya uchu.
> Sara alisema, "Thikupi. Thikupi hata ukilia."
> Prospa hakusema kitu lakini aliendelea kumtazama Sara anavyoweka andazi mdomoni, anavyotafuna polepole, anavyomeza.
> Sara alijifanya kama haoni hamu ya Prospa, alisema, "Prospa utakuwa nani? Leo lathima tumpate Merisho."… (uk. 66-67).

Nukuu ya hapo juu inatuthibitishia kuwa pamoja na kuwa Sara alikuwa na njaa, hakusahau wajibu wao. Alisisitiza umuhimu wa Merisho kupatikana kwa kuwa ndiyo

lengo lililowapeleka Dar es Salaam. Sara aliyafanya yote haya kutokana na sifa za silika yake ya sangwini ya kupenda kuzungumza. Ijapokuwa yeye ni msindikizaji, alijikuta anapanga mambo mengi kuliko Prospa. Kutokana na msingi wa kwanza wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu mahitaji ambayo yakikamilishwa, humfanya mtu aishi vizuri, Sara na Prospa walipata mahitaji hayo (chakula na malazi) yaliyowasaidia kupata nguvu na akili ya kupanga namna ya kumpata Merisho.

Sehemu nyingine inayothibitisha uhusiano huu ni pale walipofika Zanzibar katika kasri ya Sultani Barghash. Walikutana na mzee ambaye aliwapa historia ya eneo hilo. Ijapokuwa walikuwa wawili, lakini Sara ndiye alikuwa akiuliza sana maswali kutokana na sifa za silika yake ya sangwini. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa Sara alitaka kupata ufahamu zaidi na kuwa karibu na jamii hiyo. Mwandishi anatanabahisha kwa kusema:

> Sara aliuliza, “Masuria ni nani?”
> Mzee alitabasamu tena. Alipendeza alipotabasamu. Macho yake yaliangalia juu kama vile kutafuta mwanga. Prospa na Sara walimtazama. Kimya. Halafu Sara akifikiria labda amesahau swali, alianza tena, “Masuri…”
> Mzee aliinua mkono wake kama kumkanya. Alisema, “Masuria wa Sultan Barghash walikuwa wanawake warembo aliowapenda yeye. Alikuwa nao tisini na tisa. Wote warembo. Wote walipendwa.”
> Sara aliuliza tena, “Alitoka wapi huyu mtu?”
> “Na hao warembo wake walikuwa Waarabu?” Prospa aliuliza.
> Sara alimtazama Prospa akatabasamu. Halafu akauliza haraka. “Wote walikuwa wathuri kabisa?”
> Mzee alicheka kwa furaha. Swali lilimtekenya, likamjaza furaha. “Masulia wa Sultani? Lahaula!” (uk. 85).

Kupitia dondoo hili, ni dhahiri kuwa kutokana na nafsi ya kiwango cha kati ya Nadharia ya Saikochanganuzi, utashi wa Sara ndio ulisababisha kuuliza yote hayo kwa lengo la kuifahamu zaidi jamii ya Sultan Barghash. Hata hivyo, mzee huyo alifurahia maswali na uchangamfu wake, hivyo alijikuta akijibu kila swali. Kwa hali hii, Sara alifaulu kumhoji maswali mengi kutokana na silika yake ya sangwini.

Sehemu nyingine inayoonesha uhusiano huu ni pale Sara na Prospa walipokutana na watoto wa mitaani, maarufu kama changudoa. Kutokana na maongezi yao, yaliyoonesha ukali na chuki, Prospa aliwaambia kuwa Sara ni dada yake, na ni bubu. Prospa alitaka kumlinda Sara dhidi ya watoto hao walioonekana kuwa na roho

mbaya kutokana na namna walivyoongea. Hata hivyo, ilibainika kuwa, kutokana na sifa za silika yake na kutaka kuamiliana na watu mbalimbali, Sara alishindwa kujizuia na kujikuta anazungumza. Mwandishi anatanabaisha:

> Prospa alisema, "Huyu ni Sara. Huyu Sara ni dada yangu, ni mdogo wangu. Sara ni bubu, hawezi kuongea."
> "Mlifika lini mjini hapa?" Mvulana mwingine aliuliza.
> "Jana. Leo." Prospa alijibu. Tunamtafuta Merisho. Merisho ni mpwa wangu, alipotea kule TPC. Unafahamu mahali panapoitwa TPC? Kile kiwanda cha sukari? Sasa Merisho hayuko, Moshi, wala Manzese, wala hayuko Zanzibar, tumeshatoka huko." Prospa aliongea kwa haraka. Kitu kilimsukuma kuwaeleza wavulana hawa hadithi ya safari yao. Alitaka wamwonee huruma, wasiwaumize.
> Thithi tumeibiwa vitu vyetu vyote. Hatuna petha. Thithi ni mathkini." Sara alisema (uk. 112).

Kupitia nukuu hii, inathibitika kuwa Sara alisahau kwamba alitambulishwa kuwa yeye ni bubu, hivyo alisababisha wavulana wale kuangua kicheko mara baada ya kuona na kusikia bubu anaongea. Imebainika kuwa matendo haya yalitokana na sifa za silika yake ya sangwini ya uchangamfu na kutaka kuongea na kila mtu. Hata hivyo, kutokana na maongezi yao, walifungua ukurasa mpya na kuwa kitu kimoja na kutengeneza uhusiano wenye lengo moja, kumtafuta Merisho. Lengo hilo lilifanikiwa baadaye kutokana na umoja wao.

Sifa ya silika ya Sara ya uchangamfu na kupenda kuongea imebainika alipokutana na Uzuri. Uzuri hakumpenda kwa sababu ni mtoto wa mitaani. Hata hivyo, Sara alitumia sifa za silika yake kuhakikisha anazungumza na kuwa karibu naye, ili apate anachohitaji. Mathalani, baada ya ukimya kutawala pale jikoni, Uzuri aliamua kumwambia Sara atoke ili akakae na wenzake, jambo ambalo kwa Sara lilikuwa ufunguo wa mlango wa mazungumzo. Walizungumza mambo mengi yahusuyo maisha yao na familia kwa jumla. Ili kumchota zaidi Uzuri, Sara alimwimbia na kumsifu. Mwandishi anaonesha wimbo huu kwa kusema:

> "*Aa, dada Uthuri, mthuri*
> *Ndugu hao ni vurugu*
> *Ukicheka da Uthuri*
> *Jicho langu litapona.*"
> Sara aliimba kwa sauti nyororo.
> Hm, wimbo gani huo! Wanitapeli tu. Mungu, sijui wamekutoa wapi," alisema Uzuri akiwa kama analalamika. Hata hivyo,

> alicheka na kusema, "Kuna vichaa duniani jamani. Kweli." (uk. 143).

Nukuu hii inaonesha kuwa kutokana na uimbaji wake na namna alivyomsifia Uzuri, Sara alijikuta yupo karibu sana na Uzuri, na upendo ulichipua kati yao. Ukaribu huu ulisaidia kupata taarifa alizozihitaji ambazo zilisaidia kupatikana kwa Merisho. Kutokana na dhana ya Nadharia ya Saikochanganuzi inayohusu lugha kuakisi michakato ya akilini inayojibainisha katika ndoto, misemo, na usemaji, lugha ya Sara iliakisi michakato ya akilini iliyojibainisha katika misemo na usemaji wake.

Utendaji mwingine wa Sara ni ushawishi. Imebainika kuwa Sara hutumia utendaji huu katika kujipatia marafiki na vitu mbalimbali katika jamii. Mathalani, baada ya Prospa kuamka pale Same, alikwenda katika bomba lililokuwa karibu, na kunawa uso ili atafute sehemu ya kupata kifungua kinywa. Ghafla alikutana na Sara ambaye alimstaajabisha kutokana na muonekano wake, hususani jicho lake. Sara hakujali hilo, alitumia silaha yake ya ushawishi kuamiliana na Prospa na kumtaka wakanywe supu. Mwandishi anasema:

> Msichana alisema, "Twende tukanywe thupu."
> Prospa alitingisha kichwa kukubali lakini hakuondoka kumfuata. Alimtazama hadi alipoingia ndani ya Same *Guest and Bar*. Msichana alirudi mara moja, akanawa uso wake palepale aliponawa Prospa, halafu akamfuata na kumshika mkono. Prospa aliogopa.
> Msichana alimwambia, "Twende kwetu."
> "Siwezi nakwenda Darisalam," Prospa alimjibu.
> "Kweli? Na mimi nataka kwenda Darithalam. Nataka nithome univethiti."
> Nakwenda kumtafuta mtoto wa dada yangu aliyeibiwa nyumbani kule TPC," Prospa alimwambia.
> Msichana alimtazama Prospa kwa makini. Jicho lake bovu lilionekana kama linaelea tu kwenye tundu lake bila kupepesuka. Mara alisema, "Bathi, nafahamu huyo mtoto alipo. Nitakusaidia kumtafuta."
> Prospa alikuwa na wasiwasi. Hakumwamini huyu msichana, lakini hakumkatalia (uk. 48-49).

Kutokana na maongezi haya yaliyonukuliwa, utafiti umebaini kuwa Sara alijitahidi kwa maneno na vitendo hadi akamshawishi Prospa, akakubali kwenda kunywa supu. Kutokana na nafsi za ki-Freud za Nadharia ya Saikochanganuzi inayohusu michakato ya akilini, usemaji wa Sara ulibainisha michakato iliyopo akilini mwake. Ukaribu

wao uliimarika na kuwa na lengo moja tu, kumtafuta Merisho. Hivyo, baadaye waliondoka pamoja kuelekea Dar es salaam ili kutimiza lengo hilo. Katika kuthibitisha umoja wao, mara zote Sara alikuwa akimshauri Prospa pale anapokwama kufanya jambo. Mathalani, walipoanza safari ya kwenda Dar es Salaam, wakiwa hawajui wataenda kwa usafiri gani, Sara alimwambia Prospa kuwa yeye ataomba lifti itakayowafikisha huko wanakotaka kwenda. Utendaji wa kushawishi katika sehemu iliyopita imebainisha uhusiano huu ambapo Sara alimshawishi dereva awape lifti na alifanikiwa (uk. 50-52).

Uhusiano mwingine umetokana na sifa ya silika ya Sara ya kutokuwa na aibu kwa watu asiowafahamu. Hii ni sifa nyingine ambayo utafiti unaamini kuwa ilimfanya awe karibu na jamii yoyote anayokutana nayo. Sara aliweza kuzungumza na kuwaamini watu ambao hawafahamu. Jambo hili lilimfanya naye pia aaminiwe na watu hao. Kwa mfano, aliweza kuongozana na Prospa na kuzungumza naye mambo mengi ambayo ni nadra kuyazungumza kwa mtu asiyefahamika. Sara aliondoka na Prospa hadi Dar es Salaam kwenda kumtafuta Merisho. Pia tunaoneshwa kuwa Sara hakuwa na aibu kwa Uzuri, kwa mama wa Zanzibar na kwa watoto wenzake wa mitaani maarufu kama changudoo. Mathalani, walipokuwa Zanzibar Sara hakuonesha aibu kwa mama aliyekuwa naye nje, aliyekuwa akifuatilia habari za kuwapo kwa mjukuu wa mke mwenzake. Mwandishi anasema:

> Sara alimkazia mtoto macho. Alikuwa bado anajaribu kupata titi. Alishindwa, akalia kwa nguvu zaidi.
> Sara alimwambia Bibi Tatu, “Mtoto ana njaa.”
> “Hamna lolote,” Bibi Tatu alisema, lakini akatoa titi ndani ya kanga mtoto akaliinua mwenyewe, akaanza kunyonya.
> “Wewe ni mtoto, huwezi kufahamu, lakini mimi najua. Kuna uongo tu mahali. Bibi Sofia hana mtoto,” Bibi Tatu alisema. Sara alimwangalia sana Tatu alimwona kama amekasirika, akataka kumuuliza kuwa kakasirishwa na nini (uk. 92-93).

Nukuu hii inabainisha kuwa Sara alimtathimini Bi Tatu na kuona kuwa amekasirika, hivyo, haikuwa busara kuendelea kumwuliza maswali. Kutokana na tabia hii Sara aliweza kuongea na kila mtu na kupata kile alichokihitaji kwa wakati muafaka.

Hali kadhalika, Sara alitengeneza marafiki kwa haraka sana kutokana na ucheshi wake na kukubalika kwake kwa jamii. Kwa mujibu wa Ponera na Kasiga (2019),

masangwini husaka, hutengeneza na kulinda marafiki ili wasipotee. Mwandishi anaonesha jinsi alivyotengeneza urafiki na Prospa, changudoo, Uzuri na Bibi Fatuma kule Zanzibar. Pia, alijitahidi sana kuulinda urafiki huo kwa uwezo wake wote. Kupitia marafiki hao aliweza kujifunza mambo mengi. Kwa mfano, imebainika kuwa walipokuwa Zanzibar alikuwa karibu sana na Bibi Fatuma na akajifunza mambo mengi. Mwandishi anasema:

> Sara alijifunza kuweka ukili rangi. Bibi Fatuma alimweleza kwamba hana pesa za kununua rangi za ukili kutoka mjini, kwa hiyo hujitengenezea rangi yeye mwenyewe. Walitembea shambani na bibi Fatuma, akamwonesha mti wa mdaa, akamfundisha jinsi ya kutoa vipande vya gamba lake. Alimwonesha pia mmea unaoitwa manjano, jamii ya tangawizi na binzari, akamwonesha jinsi ya kupata mizizi yake… Bibi Fatuma alimwonesha jinsi ya kuchemsha ukili hadi ukolee rangi. Halafu alijifunza kusuka mkeka wa kuchanganya rangi tofauti (uk. 101).

Kutokana na kutengeneza urafiki na kuwa sehemu ya familia, utafiti umebaini kuwa Sara alipata habari nyingi ambazo zilimsaidia katika kumpata Merisho, ambaye aliibwa nyumbani kwao TPC Moshi. Pia, alipata ujuzi wa mambo mbalimbali yaliyomsaidia katika maisha yake.

Kwa jumla, matendo haya ya Sara yana uhusiano mkubwa na sifa za aina za silika. Mtu akiyamakinikia matendo haya atagundua silika yake kwa urahisi zaidi. Huu ndio uhusiano uliopo. Iwapo asingefanya yote haya ingekuwa vigumu kuitambua silika yake.

Kwa upande mwingine, uhusiano wa utendaji na sifa za silika ulibainika kwa Prospa kutokana na sifa yake ya kuchanganua mambo kwa undani. Jambo lolote lililomsumbua kichwani alitumia muda mwingi kulichanganua na kulichambua ili aweze kupata suluhu. Baada ya kutoka kucheza mpira kule TPC na kugundua kuwa Merisho ametoweka, Prospa alianza kuwauliza watu mbalimbali wakiwemo watoto wenzake. Baadaye alifika kwa mama mmoja ambaye alikuwa anapalilia, naye akamwambia alimwona Merisho akiwa na mama mmoja. Utafiti umebaini kuwa Prospa bila kusita alichanganua jambo hili na kupata hisia kwamba mama huyu anaweza kujua alipo Merisho. Mwandishi anasema:

> Prospa hakuweza kujizuia tena. Alianza kulia. Kila mtu aliyekutana naye alimuuliza, “Umeshamuona Merisho?” Waliokuwa hawamfahamu Merisho waliuliza, “Ni nani huyo?”
> Prospa alijibu, “Ni mtoto wa dada. Sijui amekwenda wapi.”
> Mama mmoja aliyekuwa anapalilia bustani ya mboga alimwambia, “Mbona Merisho kapita hapa kitambo? Alikuwa amefuatana na mama mmoja aliyejitanda kitenge. Merisho alikuwa anakula andazi. Mie sikuwa na wasiwasi nilifikiri ni rafiki wa dada yako”
> “Sasa wameenda wapi?” Prospa aliuliza bila tumaini.
> Mama yule aliendelea kueleza, “Ndiyo mama alijitanda kitenge chekundu na alivaa raba za buluu kama za watoto wa shule. Balaa gani hii! Sasa kimbia haraka ukamwite mwalimu Josefina shuleni. Mtoto hawezi kutafutwa na mtoto mwenzie. Kimbia.” (uk. 5)

Katika dondoo hilo tunathibitisha kwamba Prospa baada ya kupata maelezo ya mama huyu na kufanya uchambuzi wake, alimwambia waende wote polisi ili akajieleze, kwa kuwa alihisi huenda alikuwa anamfahamu mwanamke huyo aliyepita na Merisho. Kwa hiyo, yule mama alikubaliana naye, ijapokuwa kwa shingo upande. Hata hivyo, uchambuzi wa Prospa haukufua dafu mbele ya yule mama ambaye alijitetea mbele ya askari, kisha akaruhusiwa kuondoka. Prospa alipata shauku ya kufanya uchunguzi wake mwenyewe baada ya kuchoshwa na maswali ya askari.

Uhusiano mwingine wa utendaji wa kudadisi na sifa za aina ya silika yake ya melankoli unatokana na huruma na kujali wengine. Utafiti umebaini kuwa Prospa alifanya matendo mengi ya kudadisi. Kwa kawaida, watu wa silika ya melankoli huwa na huruma pale wanapoona mtu ana shida au anaonewa. Jambo hili limewafanya wawe wadadisi na kuwa karibu na jamii inayowazunguka. Baada ya Merisho kutoweka nyumbani, Prospa alifuata hatua zote za kumtafuta maeneo aliyopendelea kucheza, alipomkosa, alimjulisha dada yake, kisha wakaenda kutoa taarifa kituoni. Baada ya kuandika maelezo, walirudi nyumbani wakiwa hawana furaha, kwani Merisho alikuwa bado hajaonekana. Nafsi ya Prospa ilikuwa inamsuta kwa kumuacha Merisho peke yake. Prospa alikuwa akifanya udadisi katika kichwa chake. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa mawazo ya Prospa yalimzidi kwa sababu alijihisi kwamba yeye ndiye mwenye hatia. Kama asingeenda kucheza Merisho asingepotea. Prospa alionesha kujali. Kwa hiyo, alikuwa sahihi kuamua kuanzisha uchunguzi wake mwenyewe, ijapokuwa alikuwa akiingilia kazi ya askari (uk. 15). Kutokana na misingi ya Nadharia ya Saikochanganuzi Prospa alisukumwa na matamanio yake ya kutaka kumpata Merisho.

Prospa pia alimuonea huruma Sara baada ya kutengwa naye na watoto wa mitaani. Sifa hii ina uhusiano na utendaji wa kudadisi. Prospa na Sara walizoeana kama kaka na dada. Prospa alijiona ana wajibu kwa Sara kwa sababu yeye ndiye aliyesababisha akaja katika jiji la Dar es Salaam. Kwa hiyo, alikuwa na haki ya kumuonea huruma na kumjali. Katika akili yake alikuwa akiwaza na kudadisi kuhusu kitakachotokea baada ya kutengwa na Sara. Hakutaka kabisa kutengwa naye. Msemaji wa changudoo anasema:

> "Sasa we Tofa, mchukue Sara, bubu anayeweza kuongea, mpeleke kwa dada yao. Yeye atajua la kumfanya. We Mansa, huyo wako. Mpe jina kama hana lake," mkubwa wao aliamuru.
> Prospa alijaribu kukataa. Alijaribu kumtoa Sara mikononi mwa Tofa. Msemaji wao alimwonesha kipande cha chupa kilichochongeka na kusema, "Ninyi hamjui jiji hili. Jiji halina huruma hili, na tukiwaacha mnaweza kuumizwa vibaya. Tumeshaamua nyie ni changudoo kuanzia sasa. Wasichana wana shughuli zao na sisi tuna zetu. Ukileta fujo tutakuumiza" (uk. 113-114)

Dondoo hilo linaonesha huruma na kujali kwa Prospa kulikotokana na silika yake ya melankoli. Hata hivyo, watoto waliokutana nao walionekana kutokuwa na huruma, na walikuwa na msimamo. Kutokana na maisha ya mitaani, watoto wa kike na wa kiume hufanya kazi mbalimbali ili wapate kipato cha kukidhi mahitaji yao ya kila siku. Kwa hiyo, haikuwa rahisi Prospa na Sara kukaa pamoja. Hili linathibitishwa na mwandishi wa riwaya hii anaposema kuwa aliwaumba wahusika wake kama watoto wa mitaani, lakini aliwatofautisha na watoto wengine wanaoishi kwa kuombaomba mitaani. Wahusika katika riwaya hii wanafanya kazi mbalimbali kama kuosha magari, kubeba mizigo na kusafisha vyombo katika hoteli ili wapate ujira.

Pia, Prospa alionekana mwenye mawazo pale alipokuwa anafanya mipango ya kutoroka ili akamtafute Merisho. Sifa hii inauhusiano na utendaji wa kudadisi. Prospa alifanya udadisi katika akili yake. Alikuwa akitanzika na namna ya kutoka eneo la TPC ambako alikuwa akifahamika. Alitaka asionekane na watu wanaomfahamu kwa sababu wangeweza kumrudisha au kumwuliza maswali mengi. Mwandishi anasema:

> Prospa alifikiri, “Nitaomba lifti za watu wanaokuja kukata majani ya ng’ombe na kuyabeba kwenye pick-up. Nitapata lifti tu. Nitasema nini? Nitasema nakwenda mjini Moshi. Hapana. Nakwenda kumsalimia bibi. Hapana. Nitasema nini? Nitasema kwamba bibi anaumwa, kwa hiyo nampelekea dawa. Nadhani mtu atanionea huruma atakaposikia kwamba bibi anaumwa.” Alikariri, “Bibi anaumwa nampelekea dawa. Bibi anaumwa …” (uk. 21).

Dondoo hili linabainisha kuwa Prospa alitanzika kuhusu namna ya kujieleza iwapo ataulizwa anapokwenda. Alijaribu kupanga uongo utakaoweza kumsaidia lakini aliona haufai. Hata hivyo, alipopata wazo la kusema kuwa bibi yake anaumwa, aliona linafaa na anaweza akaonewa huruma. Utafiti umebaini kuwa Prospa aliogopa kutokana na umri wake kwani dereva yeyote ni lazima angeuliza kabla ya kumpa lifti. Haya yote aliyafanya kutokana na silika yake ya melankoli.

Sehemu nyingine inayodhihirisha uhusiano huu ni pale Prospa alipoamua kufanya juhudi binafsi ikiwa ni pamoja na kudanganya akafanikiwa kutoroka hadi stendi ya mabasi iliyopo Moshi mjini. Katika mizunguko yake alikutana na mzee mmoja ambaye alimfahamu na kumwambia alimwona Merisho na dada wa kazi wakisafiri. Aliongeza kuwa, basi lilipokuja yule dada wa kazi na Merisho walipanda, na hakumwona mwalimu Josefina. Imebainika kuwa Prospa roho yake ilishtuka, lakini hakutaka kuonesha, hivyo alianza kufanya mchakato wa namna ya kufika Dar es Salaam, kwani tayari alipata uhakika kuwa Merisho kapelekwa huko. Mwandishi anasema:

> Sasa raha yote ilimtoka. Alihisi jua ni kali zaidi. Alijaribu kufikiria, kubuni mbinu ya kupata fedha, lakini akili ilimsaliti. Ilikataa katu kufanya kazi. Baada ya muda alikata tamaa kuondoka na basi lolote lile. Alifahamu kwamba itabidi afanye kila njia aingie ndani ya basi bila kuonekana. Prospa aliamua kufanya hivyo, ingawa hakujua angetumia mbinu gani kufanikiwa (uk. 26).

Kwa kuzingatia maelezo yaliyo katika nukuu hii, ni dhahiri kuwa kutokana na sifa ya silika yake ya kujali wengine, Prospa alipata suluhisho la kuondoka na basi lolote litakalokuja. Maamuzi haya yametokana na uhusiano wa utendaji wa kudanganya na silika yake ya kujali wengine. Kulingana na msingi wa pili wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu matamanio, Prospa alifanya juhudi zote ili matamanio ya nafsi yake, ya kumtafuta Merisho hadi ampate yatimie.

Uhusiano wa utedaji na sifa za aina ya silika yake ya kujali wengine na kuwa na mawazo mengi, pia umebainika pale aliposhushwa kwenye basi baada ya kubainika kutokuwa na nauli. Prospa hakulitarajia jambo hili, kwa sababu kitendo cha kupanda basi kilimpa matumaini ya kufika Dar es Salaam. Lema (khj) anasema kuwa kitendo cha Prospa kushushwa sehemu asiyoijua kilimshtua sana na aliona ndoto yake inafifia. Anaongeza kuwa Prospa hakukata tamaa, kwa sababu dhamira yake ilikuwa haijatimia. Katika ithibati ya hilo, mwandishi anasema:

> Prospa aliketi juu ya pipa kwa muda mrefu. Alihisi donge kavu kooni mwake. Alijaribu sana kufikiria la kufanya, lakini kila mara nafsi yake ilimwambia alishakata shauri kumtafuta Merisho hadi ampate. Agh, donge kavu kooni lilizidi kumuumiza. Alijaribu kumeza mate ili apunguze maumivu. Alijikaza. Alipoona karibu aanze kutoa kilio, alijisemea kwa sauti ya chinichini, “Sitalia, sitaogopa, sitalia, sitaogopa, sitalia, sitaogopa, sitalia, sitaogopa.” (uk. 33).

Nukuu ya hapo juu inathibitisha kuwa Prospa alikuwa anazungumza na nafsi yake ili kujifariji kila alipoona anakaribia kukata tamaa. Maneno ‘sitaogopa’ na ‘sitalia’, aliyarudiarudia kwa ajili ya kujipa moyo ili asilie, na kweli yalimsaidia kuwa imara na kutafakari hatma ya safari yake. Kutokana na msingi wa pili wa Nadharia ya Saikochanganuzi unozumngumzia matamanio, Propsa alifanya jitahada kuhakikisha anayakamilisha matamanio yake ya kumpata Merisho.

Sehemu nyingine aliyoonesha matendo ya udadisi kutokana na sifa ya silika ya kuwa na mawazo mengi ni alipokuwa ameanza safari ya kwenda Dar es Salaam. Prospa alibahatika kupanda basi, lakini alishushwa baada ya kubainika kuwa hana nauli. Hali hii ilimfanya atembee tu bila kujua anaenda wapi. Baada ya muda alianza kujisemesha kutokana na mawazo aliyokuwa nayo. Mwandishi anasema:

> “Nasikia njaa,” Prospa alijiambia. Alianza kujizungumzia kwa sauti, kwani aligundua kuwa akifanya hivyo alikuwa kama anazungumza na mtu mwingine karibu naye. “Nitakula chakula kwenye hoteli ile, halafu nitatafuta mahali pa kulala (uk. 34).

Katika dondoo hilo Prospa alikuwa anawaza, lakini ilibidi ajisemeshe kwa sauti ili kupunguza uoga aliokuwa nao katika eneo asilolifahamu. Hata hivyo, Prospa alisukumwa na nafsi yake kuhakikisha kuwa anampata Merisho, hivyo alijipa ujasiri mwenyewe.

Utafiti uliofanyika ulibaini sehemu nyingine inayoonesha uhusiano wa sifa ya kuwa na mawazo mengi na utendaji wa kudadisi ni wakati Prospa na Sara wakiwa kwenye boti kuelekea Zanzibar. Watoto hawa ilikuwa mara yao ya kwanza kupanda chombo kinachopita juu ya maji. Prospa alitulia na kuzungumza na nafsi yake na kujiuliza maswali juu ya maajabu ya bahari. Mwandishi anasema:

> Mawazo yote ya Prospa yalikuwa juu ya maajabu ya bahari. Je, bahari hii imetoka wapi? Ina mwisho? Na kama ina mwisho, ukoje na uko wapi? Haya mawimbi yanasababishwa na kitu gani? Ni kwanini bahari inaonekana ina rangi ya kijani au buluu, ambapo maji yenyewe hayana rangi hizo? Prospa aliwaza sana. Bahari inazungukaje dunia? Maji yote haya yalitoka na yanaendelea kutoka wapi? Walikuwa wamefundishwa shuleni kwamba maji ya bahari yanatoka kwenye mito. Lakini inawezekana maji yote haya kutoka kwenye mito pekee? (uk. 77).

Kupitia mazungumzo hayo, ni dhahiri kuwa Prospa alijiuliza mengi kwa njia ya udadisi, lakini hakupata majibu kwa sababu alikuwa akizungumza na nafsi yake. Jambo hili lilimfanya amsahau Merisho kwa muda na kujiona yupo katika dunia nyingine. Prospa aliwaza haya yote kutokana na sifa za silika yake ya melankoli. Kutokana na dhana ya Nadharia ya Saikochanganuzi inayosisitiza michakato ya akilini inayobainika kwa misemo au usemaji, Prospa alikuwa akizungumza mwenyewe kutokana na michakato iliyokuwa kichwani mwake. Jambo hili lilimfanya asipate majibu ya maswali yake hadi aliposhtukia anaona nchi kavu kuashiria kwamba wamekaribia Zanzibar.

Uhusiano huu unadhihirika pia baada ya Prospa na Sara kutoka Zanzibar bila Merisho. Jambo hili lilimuumiza sana Prospa na kumuongezea mawazo. Alikuwa akifikiria mahali alipo Merisho. Mwandishi anatanabahisha:

> Prospa aliendelea kujilaza kwenye benchi ndefu. Hakuwa na usingizi. Alikuwa anawaza: Manzese, Merisho hayupo, wala kaka Petro hajui alipo. Zanzibar tumekwenda, Merisho hayupo. Sasa twende wapi? Labda turudi Manzese, tuulizie njia mpaka tufike kwa kaka Petro, lakini tukafanye nini? Tutamkuta kaka Petro? Halafu siku tulivyoondoka aliniambia nisirudi kwake. Alinieleza kwamba ameshatumia pesa yake nyingi kwa chakula na nauli, kwa hiyo tukitoka Zanzibar, tuende moja kwa moja Moshi. Najua tukienda Manzese hatutamkuta Petro (uk. 108).

Katika dondoo hilo, mawazo ya Prospa yalikuwa yakizunguka tu sehemu moja. Hakuweza kupata jibu la maswali yake, kwa sababu alikuwa akizungumza peke yake. Kupotea kwa Merisho kulimuongezea sana mawazo kutokana na sifa ya silika yake ya Melankoli ya huruma.

Sehemu nyingine inayothibitisha uhusiano uliotokana na sifa ya silika ya kuwa na mawazo mengi na kujali watu wengine na utendaji wa kudadisi ni baada ya Prospa kutengwa na Sara, aliyemwamini na kumjali kama sehemu ya familia yake. Utafiti umebaini kuwa, kutokana na upendo aliokuwa nao Sara kwa Prospa, kitendo cha kutenganishwa naye kilimuathiri sana, hasa walipokuwa wanakunywa chai bila kujua kama Sara naye amekunywa. Prospa alifanya uamuzi wa kumtafuta katika maeneo mbalimbali, lakini haukufanikiwa. Mwandishi anafafanua:

> Hakuona dalili ya Sara. Sasa amekwenda wapi na yeye? Kwanini nilikubali tutenganishwe? Sasa ona, naye pia amepotea! Prospa alijilaumu. Moyo ulimsuta. Kila alipoona msichana kama Sara akitembea, alimkimbilia na halafu kukuta kuwa siyo Sara. Alizurura. Alikwenda huku na kule (uk. 120-121).

Nukuu hii inaonesha namna Prospa alivyokuwa akiidadisi na kuilaumu nafsi yake kutokana na kukubali kutenganishwa na Sara. Aliona kuwa amempoteza mtu muhimu katika safari yake ya kumtafuta Merisho. Maelezo yake yanadhihirisha uhusiano uliotokana na sifa ya aina ya silika yake ya melankoli ya kujali watu wengine.

Uhusiano mwingine wa utendaji wa kudadisi na sifa za silika yake unatokana na Prospa kujawa na mawazo mengi ya namna ya kumpata Merisho. Baada ya kufika kwa mjomba wake, Feliksi, matumaini yalianza kuonekana kutokana na mazungumzo ya Sara na Uzuri. Lakini, Prospa alikuwa bado na wasiwasi. Walipanga mipango yao ya kwenda kwa jirani wa mjomba wake, aliyesadikika kuwa na Merisho. Prospa aliapa kutorudi nyumbani endapo hatompata Merisho. Mwandishi anafafanua:

> Prospa aliingia chumbani, akakaa kwenye kitanda. “Lazima nimpate Merisho, bila hivyo siendi nyumbani,” Alijiinamia akashika kichwa chake kwa mikono yote miwili. “Mbona Mansa haji? Agh!” Prospa aliendelea kuzungumza peke yake chumbani. Prospa alisimama kutoka kitandani kwenda kuchungulia na

> kusikiliza yanayoendelea. Mara Mansa alitokea akiwa na Sara …
> (uk. 156).

Dondoo hilo hapo juu linatuonesha uhusiano wa utendaji wa kudadisi na sifa za silika ya melankoli za kuwa na mawazo mengi na kujali wengine. Kutokana na msingi wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu matamanio, Prospa alikuwa na haja ya kukamilisha matamanio yake ya kumpata Merisho. Haja hii ilimuongezea mawazo kila uchao, kubwa ni kuhakikisha Merisho anapatikana.

Kwa jumla, uhusiano wa utendaji wa wahusika wakuu na sifa za silika zao katika riwaya ya *Safari ya Prospa* ulisaidia kufanikisha safari yao ya kumtafuta Merisho. Wahusika hawa wana silika tofauti, Prospa ni melankoli, ilihali Sara ni Sangwini. Sifa za silika zao zimesaidia kuepusha kutokuelewana na kupunguza misuguano ambayo ingeweza kutokea. Sehemu ambayo ilitokea kutokuelewana mmoja alijishusha. Kwa mtazamo wa utafiti uliofanyika, kwa kiasi kikubwa, mwandishi amefaulu kutuonesha kuwa kama wahusika watakuwa na silika zinazotofautiana, ni lazima wafanikiwe katika kufikia lengo lao.

### 4.4.2 Uhusiano Baina ya Utendaji na Sifa za Aina za Silika katika *Ngoma ya Mianzi*

Ilikwishabainishwa hapo awali kwamba huwezi kujua silika ya mtu kama hajatenda jambo fulani. Kwa kupitia matendo hayo, ndipo tunapata sifa za aina za silika. Uhusiano baina ya utendaji na sifa za aina za silika katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi* unaobainishwa ni kama ifuatavyo:

Wepesi wa wahusika katika kujitolea kushiriki mambo mbalimbali katika jamii. Sifa hii ya silika ya melankoli ina uhusiano na utendaji wa kuhoji na kutaarifu. Katika uhusiano huu mhusika anaposikia jambo hujitolea kwa faida ya watu wake na nchi yake kwa jumla. Watu wa silika ya melankoli kama Chulu hutawaliwa na sifa hii ya kujitolea, hata kama anajua jambo halitafanikiwa. Ni tofauti na sangwini ambao, kabla hajajitolea, huanza kufikiria kwanza faida ya lile jambo. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa baada ya Mbumi kusikia ngurumo nje, aliamua kutoka ili kujua kinachoendelea. Chulu alijitolea kuongozana na dada yake, ijapokuwa alikuwa na usingizi. Mwandishi anafafanua:

> Alimsikia Chulu akiteremka kitandani. Punde wote wawili walikuwa mlangoni. Chulu alikuwa ameshika mkuki aliouacha marehemu baba yake. Mbumi alizoa mundu hapo sebuleni, akaukamata imara kwa mkono wa kulia. Walitoka nje. Kulikuwa bado hakujapambazuka, japo dalili za wekundu wa mapambazuko zilikuwa zimeanza kuonekana mbali sana mashariki… (uk. 5).

Dondoo hili linabainisha namna Chulu alivyoamua kujitolea kulinda usalama wa eneo lao. Kulingana na nafsi ya kiwango cha kati ya Nadharia ya Saikochanganuzi, imebainika kuwa Chulu aliona ni busara kujitolea kuongozana na dada yake, kwani kidole kimoja hakivunji chawa. Alidiriki kubeba mkuki ili kupambana na lolote litakalotokea. Mwandishi anaendelea kueleza namna alivyojitolea pamoja na Wanasokomoko wengine kwa ajili ya kuilinda nchi yao. Anasema:

> Kesho yake asubuhi na mapema, baada ya kifungua kinywa cha viazi vitamu na maziwa ya mtindi, walimuaga bibi yao, wakaenda zao mbuyuni na kuwakuta Wanasokomoko kituoni. Walikuta hali ni shwari, wenzao wamekwisha pangiwa doria na kupewa maagizo mengine na kamanda wao.
> “Mmekuja?” Kamanda aliwauliza.
> “Naam, tumekuja,” Chulu alijibu. “Mipango ni ipi?”
> “Ingawa hatujui kama kutakuwa na vita, lakini kwa tahadhari wazee na watoto watachukua mifugo na mali nyingine na kuzipeleka mafichoni. Vikosi vya wapiganaji vinaelekea kwenye sehemu zao vilikopangiwa.”
> Na Sokomoko je?”
> Wale wenye zamu watakuwa kwenye sehemu zao. Wengine watasubiri hapa kwa maagizo zaidi.”
> “Na sisi je?”
> Wewe na Mbumi mnatakiwa na Mundewa sasa hivi.”… (uk. 19-20)

Kwa hiyo, Chulu aliuliza maswali yote hayo kwa kuwa alikuwa na ari ya kujitolea ili kuikomboa nchi yake dhidi ya uvamizi wa wazungu. Kutokana na msingi wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu matamanio, Chulu alitamani kupigana vita na kupata ushindi. Ni kawaida mtu wa namna hii kuhakikisha anatimiza matamanio yake, ndipo nafsi yake itulie. Matendo haya ya Chulu ndiyo yanayotuonesha silika yake, na hivyo, kudhihirisha uhusiano baina ya utendaji na sifa za aina ya silika.

Sehemu nyingine inayobainisha uhusiano wa utendaji na sifa za silika ni kujitolea kwa Chulu kupeleka ujumbe wa siri (Mkuki-wa-Mianzi) kwa Mutwa Mukwava.

Chulu hakuwa na wasiwasi wowote kutokana na utayari aliokuwanao na jinsi walivyoaminiwa na Mundewa na wazee wengine. Masimulizi yanafafanua:

> Mundewa aliuchukua mkuki huo kutoka pale kiambazani, akamkabidhi Chulu, ambaye alisimama na kuupokea kwa heshima. "Muuchunge kama uhai wenu wenyewe."
> "Tutafanya hivyo Mundewa," Chulu na Mbumi walisema huku wakiwa wamesimama (uk. 23-24).

Nukuu hii inatudhihirishia uhusiano wa utendaji na sifa ya silika ya melankoli ya kujitolea. Hata hivyo, katika suala zima la kujitolea hasa katika kuipambania nchi, ni lazima kuwe na silaha zitakazofanikisha kupambana na adui. Watoto hawa walipokuwa wanaagwa na Mutwa, walipewa silaha mbalimbali ili ziwasaidie katika mapambano pamoja na kuusiwa kuhusu mapambano hayo. Mwandishi anasema:

> Chulu alipewa sime ya kimasai na kuusiwa kwamba sime hilo ni mwiko kushikwa na mwoga; pindi mwoga akiingia nalo vitani humgeukia na kumuua yeye mwenyewe badala ya kuwaua maadui (uk. 44).

Kutokana na kujitolea kwa Chulu, hakujali umbali wowote watakaotembea. Alionesha uvumilivu wa hali ya juu wa kuvuka milima na mabonde, mito na vijito na kukutana na masahibu mbalimbali, hatimaye lengo lao likatimia. Safari zote hizi aliongozana na dada yake na mwenyeji wao, ambaye aliteuliwa katika kijiji husika ili kuwasindikiza na kuwaelekeza njia. Masimulizi yanaonesha kuwa walipita katika bonde la Kalenga na Lugalo ambapo walifuata njia nyembamba zilizowafanya watembee kwa kuongozana kama wamepanga mstari. Katika njia hizo kulikuwa na vilima, mabonde na majabali makubwa. Safari yao iliwachukua zaidi ya siku nne, jambo ambalo linahitaji uvumilivu mkubwa sana.

Uhusiano wa utendaji wa kutaarifu na sifa za aina ya silika, pia unadhihirika kupitia uvumilivu wa Chulu pale alipokamatwa na maadui baada ya kuzidiwa mbio. Chulu alichukuliwa kama mateka na kupelekwa kambini kwa maadui. Huko aliteswa sana ili atoe siri, lakini alikuwa imara na kuvumilia maumivu yote yaliyotokana na kipigo hicho, kwani alishaapa kutotoa siri ambayo ingeiangamiza jamii yake na nchi kwa jumla. Mwandishi anasema:

> Chulu alikumbuka jinsi alivyochapwa mijeledi na Mjerumani alipowasilishwa kwake baada ya kutekwa. “Unajua Mbumi, hivi unavyoniona mgongo wote umevimba.”
> “Kwanini?”
> “Kipigo cha Mdachi. Walitaka niwape habari za siri lakini hawakupata chochote.”
> “Uliwaambiaje?”
> “Niliwaambia mimi ni mwenyeji wa kijiji cha hapa karibu na nimekuja Lugalo bondeni kugema ulanzi. Niliwaambia habari za Mukwava na nyendo zake sizijui, maana mimi ni mtoto tu, si askari.”
> “Waliamini?”
> “Yaelekea hivyo maana hawakunipiga tena. Ila askari aliyenichukua pale kwa mzungu kunileta kwenye boma la wapagazi alinitishia kuwa zile fimbo tano nilizoonjeshwa zilikuwa ni za makaribisho tu; kipigo chenyewe cha khamsa-ishirini kingekuwa kesho.”
> “Alidhani ungesubiri hapo ili uchinjwe kama kondoo wa kafara kana kwamba si mwanasokomoko?”
> “Ati!” (uk. 88).

Kupitia nukuu ya hapo juu, imebainika kuwa uvumilivu wa Chulu uliambatana na uongo kwa lengo la kutotoa siri na kuponyoka mikononi mwa adui. Chulu alifaulu kutotoa siri za jamii yake na nchi kwa jumla. Kutokana na nafsi ya pili ya Nadharia ya Saikochanganuzi ambayo ni nafsi ya utashi, urazini na tafakuri, inayoongoza maamuzi ya busara, Chulu aliona busara kuvumilia ili asitoe siri ya nchi yake. Kwa kumakinikia matendo haya ya Chulu tunaona uhusiano mkubwa baina ya utendaji na sifa za aina za silika, ambazo ndizo zinazomtofautisha mhusika mmoja na mwingine.

Kwa upande wa Mbumi, mwandishi amebainisha matendo yake ambayo ukiyajua utaelewa aina ya silika aliyonayo ya koleriki. Kwanza, Mbumi alifanya matendo ya kijasiri sana tangu mwanzo hadi mwisho wa masimulizi. Ujasiri wake kama sifa ya silika aliyokuwa nayo una uhusiano na utendaji wa kutaarifu na kuhoji. Kwa mfano, aliposikia mngurumo hakujali atakutana na nini, aliamua kutoka nje ilihali kulikuwa hakujapambazuka vizuri. Pia, hakutaka kumwambia ukweli bibi yake ili asimtie woga. Mwandishi anasema:

> Hakukawia zaidi. Aliruka kutoka kitandani, akamshika bibi na kumtikisatikisa huku akisema kwa sauti ndogo, “Bibi amka kuna radi!” Bibi aliamka na kuketi kitandani, akauliza kwa sauti ya usingizi, “Radi gani?” “Nasikia mshindo; labda kuna tufani yenye ngurumo.” Hakutaka kumweleza bibi kuwa alikuwa amesikia

> mishindo ya bunduki. "Kuna nini?" Bibi alimaka huku akijizoazoa kitandani. Alisikiliza. "Labda ni vita! La haula, mahoka mahoka wapishe mbali! Mateso tuliyopata hayakutosha tu?" Bibi ambaye sasa alikuwa yu macho kabisa, alilalama huku akirusha mikono yake iliyokaza misuli … (uk. 4).

Dondoo la hapo juu linatuonesha ujasiri wa Mbumi wa kuamka baada ya kusikia mshindo wa bunduki. Kutokana na umri wake, kama asingekuwa jasiri angeweza kuendelea kulala na kujifunika gubigubi ili asisikie mlio huo. Utafiti umebaini kuwa kitendo cha kumdanganya bibi yake ni cha kijasiri, kwani alihofia kuzua taharuki. Kitendo hicho kinadhihirisha silika yake ya koleriki.

Uhusiano mwingine unadhihirika kupitia mawazo ya kijasiri ya Mbumi pamoja na maamuzi yake. Mathalani, baada ya kukaa kwa muda mrefu katika mianzi, alitoa wazo la kutoka kuelekea kilimani ili kuona adui alikuwa anafanya nini. Ni wazo la hatari sana, lakini kutokana na silika yake ya koleriki hakuona hatari iliyomkabili. Chulu hakupinga wazo hilo, kwa sababu ya sifa ya silika yake ya kujitolea. Pia, aliamini kuwa ni kosa kwa Wamasokomoko kuwa waoga, na hivyo, aliambatana naye. Mwandishi anasema:

> Waliondoka taratibu, kimyakimya, mle mianzini. Chulu alikuwa ametangulia ameshika Mkuki-wa-Mianzi na kiunoni kaning'iniza sime yake. Mbumi alimfuata hatua chache nyuma akiwa na sime na kisu. Nje ya mianzi baridi iliyoandamana na upepo ilipenya hadi kwenye mifupa. Walinyatianyatia kimyakimya, wakavuka kijito cha Lugalo, wakaanza kupanda kilima ng'ambo ya pili kuelekea kule walikowaona maadui alasiri ile … (uk. 63).

Dondoo hilo linashadidia na kudokeza namna Mbumi alivyokuwa na mawazo ya kijasiri. Hakuogopa baridi na giza nene lililokuwapo. Alichokuwa anajali kwa wakati huo ni kuikomboa jamii yake na nchi kwa jumla. Mwandishi anasema kuwa walipofika kilimani ilibidi Chulu aende, na Mbumi amsubiri. Hata hivyo, hakufika mbali, akagundua maadui wapo karibu na wameshamwona. Chulu aligeuza mbio kuelekea upande aliokuwapo Mbumi na kumwambia akimbie. Kinyume chake, Mbumi hakufanya hivyo, bali aliokota jiwe na kulirusha kuelekea waliko maadui. Huu ni ujasiri wa hali ya juu kwani angekuwa muoga angeshakimbia kama kaka yake alivyomshauri. Mwandishi anatanabahisha:

> Mbumi hakukimbia. Aliinama ghafla, akaokota jiwe kubwa, akalitupa kwa nguvu zake zote kuelekea alikokuwa adui. Hakujua kama jiwe hilo lilimpata mtu huyo au la, ila alisikia kishindo cha mtu aliyeanguka. Kisha pakawa kimya. Alianza kukimbia kuelekea upande wao huku akimhimiza Chulu, "Twende! Twende haraka! (uk. 65).

Dondoo hili linaonesha uhusiano wa utendaji na sifa za aina ya silika kwa kurejelea ujasiri wa Mbumi. Imebainika kuwa Mbumi alifanikiwa kumpiga yule adui na kumwangusha. Kitendo cha kumwangusha adui pia kinathibitisha shabaha aliyokuwa nayo ambayo walifundishwa katika mafunzo ya Wanasokomoko. Jambo hili linashadidiwa na Mulokozi (khj) anaposema:

> Utendaji una uhusiano mkubwa na sifa za silika kwa sababu kupitia utendaji tunatambua silika hizo. Chukulia mfano wa Mbumi ambaye alikuwa binti jasiri sana, hakuogopa lolote ingawa alikuwa na umri mdogo. Katika kitabu kuna sehemu alirusha jiwe gizani ili ampige adui, kweli alifaulu, na adui akaanguka. Hata alipoambiwa akimbie na ndugu yake, hakukimbia.

Dondoo hilo linashadidia ujasiri wa Mbumi ambao una uhusiano na utendaji wa kuhoji na kushauri.

Ujasiri mwingine wa Mbumi ambao ni sifa ya silika yake ni pale Chulu alipokamatwa na maadui. Mbumi alijiona ana jukumu la kumsaidia ndugu yake na jamii yake kwa jumla kwani lengo lao halikuwa limekamilika. Kwa hiyo, alijitwisha jukumu la kupeleka taarifa kuhusu kukamatwa huko. Hapo ndipo uhusiano baina ya utendaji wa kutaarifu na sifa ya silika ya ujasiri unapodhihirika. Mwandishi anasema:

> Ingawa baridi ilikuwa kali, lakini jasho lilikuwa likimtoka mwili wote. Alikuwa akihema, lakini dharura ile ilimfanya asihisi uchovu. Kichwani alikuwa akiwafikiria watu wale aliowaona. Bila shaka walikuwa maadui, lakini je, walikuwa ni watu gani? Waarabu? La, Waarabu huvaa kanzu nyeupe na visibau na vilemba, na huwa na ndevu nyingi. Kwa kadiri alivyoweza kuona gizani, hawa walikuwa na mavazi tofauti, na hawakuwa na ndevu nyingi. Kwa hiyo hawakuwa wasaka watumwa. Walikuwa ni kina nani basi?... Mbumi aliendelea kuwaza huku akikimbia. Njia nzima alikuwa peke yake. Hakukutana na mtu hata mmoja (uk. 66-77).

Katika nukuu ya hapo juu, tunathibitisha jitihada za Mbumi za kupeleka taarifa kuhusu kukamatwa Chulu. Ijapokuwa alihema sana kutokana na kukimbia, lakini

hakuhisi uchovu kutokana na ujasiri wake. Kulingana na msingi wa tatu wa Nadharia ya Saikochanganuzi unaohusu wasiwasi, Mbumi alikuwa na wasiwasi wa kukamatwa kwa Chulu na watu aliowaona. Alikuwa akiwaza kama atafanikiwa kumkomboa ndugu yake au la.

Wahusika katika riwaya hii walitumwa kupeleka ujumbe wa mbiu ya mapambano dhidi ya wageni. Jamii yao iliwaamini kutokana na ujasiri waliokuwa nao, pamoja na kujitolea kwao. Mwanzo wa masimulizi, mwandishi anaonesha utayari wa vijana hawa mara baada ya kusikia muungurumo nje ya nyumba. Imeelezwa kuwa walitoka wakiwa na silaha za jadi. Mwandishi anasema:

> Punde wote wawili walikuwa mlangoni. Chulu alikuwa ameshika mkuki aliouacha marehemu baba yake. Mbumi alizoa mundu hapo sebuleni, akaukamata imara kwa mkono wa kulia. Walitoka nje kulikuwa bado hakujapambazuka, japo dalili za wekundu wa mapambazuko zilikuwa zimeanza kuonekana mbali sana mashariki… (uk. 5).

Nukuu hiyo inaonesha utayari waliokuwa nao, walijizatiti kukabiliana na lolote watakalokutana nalo nje. Silaha walizobeba, mkuki na mundu, ni za jadi, zilizosaidia katika kutimiza lengo la kupigania jamii yao na nchi kwa jumla. Kulingana na nafsi ya pili inayohusu utashi, urazini, na tafakuri inayoongoza maamuzi ya busara katika Nadharia ya Saikochanganuzi, watoto hawa waliongozwa na utashi wao kubeba silaha na kutoka nje ili waone kinachotokea. Ni dhahiri kuwa silaha hizo wangetumia kujihami kama wangekutana na maadui.

Ithibati nyingine iliyobainika inayoonesha uhusiano wa utendaji wa kuhoji na kutaarifu na sifa za aina za silika za kujitolea na ujasiri ni wakati Mundewa anawapa maagizo Mbumi na Chulu, ya kupeleka kwa Mukwava. Maelezo hayo yaliambatana na kukabidhiwa silaha aina ya mkuki. Yote haya yalifanyika kutokana na sifa za silika zao, kama wasingekuwa nazo, wasingekabidhiwa. Mwandishi anasema:

> Mundewa alisimama na kuuchukua ule mkuki – Mkuu – wa - Mianzi, uliokuwa umeegemezwa kiambazani karibu naye, akauinua huku akisema: "Mkuki huu unaitwa Mkuki-wa-Mianzi. Ni mkuki wa Mutwa. Alikuja nao Mutandisi. Ndio uliokuwa kitambulisho cha utume wake. Mkuki huu sasa naukabidhi rasmi kwenu. Utakuwa ndio kitambulisho chenu. Popote mtakapopita, wakiuona watajua kuwa mna ujumbe wa Mutwa na watawasaidia." (uk. 23).

Maelezo katika dondoo hili yanaonesha kuwa watoto hao walikabidhiwa mkuki kutokana na kujitolea na ujasiri wao, ambazo ni sifa za silika zao. Hata hivyo, imebainika kuwa pamoja na kuwa ni silaha, mkuki pia hutumika kama kitambulisho kwa watu wa jamii ya Wahehe. Hili limethibitishwa katika dondoo hilo na Mundewa aliposema mkuki huo ni utambulisho wa utume wa Mutwa. Sehemu nyingine inayoonesha utambulisho ni pale walipopeleka taarifa kwa Mundewa kuhusu majeruhi aliyewafia; walienda na mkuki. Walipoingia nao tu, watu wote waliutambua mkuki huo na kuhoji kutaka kujua waliupata wapi. Utafiti uliofanyika umebaini kuwa, suala la mkuki kubebwa na mwanamke ni ishara kuwa katika tukio la vita, matumizi ya silaha hayabagui jinsia ya mhusika. Ndio maana tunaona Mbumi na Chulu wakikabidhiwa mkuki kwa pamoja.

Uhusiano mwingine baina ya utendaji na sifa za aina za silika unaoneshwa pia wakati Chulu na Mbumi wakikabidhiwa zawadi mbalimbali na Mutwa. Kutokana na ujasiri na kujitolea kwao, walipewa silaha kama zawadi. Kwa mujibu wa utamaduni wa Wahehe, kijana shujaa na aliyetumwa kupeleka taarifa, huandaliwa zawadi hizo ili zimfae awapo njiani. Mwandishi anaonesha hili kwa kusema:

> Mutwa aliwapa mawaidha na maelekezo mengine, kisha akampa Mbumi zawadi ya kisu na kamba huku akisema, “Chukua kisu hiki, kikusaidie kukata majani ya kulisha ng’ombe watakaotekwa na Wahehe na Wasagara na Wakaguru pamoja katika mapambano na maadui zetu. Kamba hii ni ya kuwafungia mateka Wekundu wasitoroke.” Chulu alipewa sime la Kimasai na kuusiwa kwamba sime hilo ni mwiko kushikwa na mwoga; pindi mwoga akiingia nalo vitani humgeukia na kumuua yeye mwenyewe badala ya kuwaua maadui zake. Mbumi na Chulu walipokea zawadi hizi kwa heshima na shukrani nyingi, huku wakipiga magoti (uk. 44).

Kupitia maelezo haya ni dhahiri kuwa katika zoezi la kujitolea kupigana ni lazima wapiganaji wapewe silaha za kukabiliana na adui. Kwa kufanya hivyo, wapiganaji hupata moyo na kuwa katika mstari wa mbele katika mapigano. Bakize (2020) anasema kuwa silaha walizopewa Mbumi na Chulu ni ishara ya ushujaa wao na mafunzo waliyoyapata kama Wanasokomoko. Anaongeza kuwa kama wangekwenda kwa ajili ya jambo jingine wasingepewa zawadi hizo. Imebainika kuwa, baadaye, kila silaha ilifanya kazi yake iliyokusudiwa. Mathalani, kisu kilitumika kukatia kamba ambayo ilitumika kumfunga mateka wa Mbumi, aliyemnywesha ulanzi,

akalewa (uk. 108-109). Kwa hiyo, wahusika walifanikiwa katika matumizi ya silaha hizo walizopewa kutokana na ujasiri na kujitolea.

Kwa upande mwingine, Mbumi alitumia ulanzi kumrubuni askari wa Wadachi ambaye alikuwa na njaa. Kutokana na umbo na umri wa Mbumi, askari huyo alimwamini na kumwomba chakula. Lakini, Mbumi alimwambia kuna kinywaji kizuri kinachoburudisha, akakubali kukinywa. Baada ya muda, alilewa sana kwa sababu alikunywa kwa kiasi kikubwa kutokana na njaa aliyokuwa nayo. Mbumi aliibuka shujaa kwa kumfunga kamba na kuwa mateka wake (uk. 107-108). Kwa hiyo, uhusiano baina ya utendaji wa kutaarifu na sifa ya silika ya ujasiri umedhihirika kutokana na Mbumi kumnywesha ulanzi askari wa Kidachi ambaye alimhoji kutaka kujua ulanzi ni nini?

Pia mwandishi anatuonesha uhusiano mwingine wa utendaji wa kuhoji na sifa ya silika ya Chulu ya kufuata mila na desturi. Katika uhusiano huu wahusika hufuata mila hizo au hukumbushana kuzifuata ili kutokiuka miiko ya jamii husika. Mathalani, Chulu hakutaka kusaidiwa mkuki na dada yake kwa kuwa mila na desturi zao haziruhusu mwanamke kubeba mkuki. Pia, Chulu aligoma kumsaidia dada yake kukata kuni kwa sababu kutokana na mila zao, hizo huonekana ni kazi za wanawake (uk. 29-30). Mulokozi (2020) anasema kuwa:

> Mkuki una siri kubwa sana, ndiyo maana haushikwi na wanawake. Wakati mwingine wanaamini kuwa, iwapo mwanamke ataushika, utapungua makali au utaleta madhara ya kumjeruhi mhusika mwenyewe.

Katika dondoo hilo mwandishi wa riwaya hii ana na kudokeza kuhusiana na mila na desturi za jamii ya Wahehe, ambapo mwanamke haruhusiwi kubeba mkuki. Jambo jingine linalothibitisha uhusiano wa kiutamaduni kupitia mila na desturi, ni adabu kabla na wakati wa kula. Kwa kawaida, kila jamii ina utamaduni wake unaofuatwa kabla na wakati wa kula. Vivyo hivyo, kwa jamii ya Wasagara, pia hufuata taratibu za kijamii kama vile mkubwa kunawa kabla ya mdogo. Mwandishi anasema:

> Waliketi kwenye nyasi nyororo katika kivuli cha mianzi, wakafungua kapu lao la chakula na kutoa chakula chao. Chulu alipotaka kuchukua chakula Mbumi akamzuia, “Mbona unataka kula bila kunawa? Maji haya, nawa.” Alichukua kibuyu cha maji na

> kuanza kummiminia Mpunza mikononi kwa kuwa alikuwa amewazidi kidogo kwa umri. Kisha alimnawisha Chulu, baadaye Chulu naye akamnawisha dada yake. Walianza kula kimya kimya (uk. 58-59).

Nukuu hiyo inaonesha namna watoto walivyofuata mila na desturi. Suala la kunawa kabla ya kula, kumnawisha mkubwa kabla ya mdogo, na kula kimya, ndiyo utamaduni wa Waafrika wanaowakilishwa na Mbumi na Chulu. Katika dondoo hilo, ithibati ya utendaji na sifa za aina ya silika inatokana na ushauri wa Mbumi kwa kaka yake ambaye alikuwa muumini wa mila na desturi. Kutokana na misingi ya Nadharia ya Saikochanganuzi inayobainisha kuwa nafsi hubeba mahusiano hai yenye kudokeza ukinzano, inashabihiana na matendo ya Chulu ya kufuata mila na desturi. Hata hivyo, wakati mwingine anakengeuka kutokana na silika yake.

Jambo jingine linaloonesha uhusiano baina ya utendaji wa kuhoji na sifa za aina ya silika ya kuwa na maono ni kupitia ndoto. Katika riwaya hii, suala hili limesadifu sehemu mbalimbali. Mathalani, mwanzoni mwa masimulizi ya riwaya hii mwandishi ametuonesha namna Mbumi alivyokuwa amelala usingizi wa mang'amung'amu kwa sababu ya kuwaza safari yao ya pwani. Mbumi na Chulu walikwenda Pwani kumtafuta mama yao aliyechukuliwa na wateka watumwa. Kutokana na kadhia hiyo, Mbumi alipata maono akiwa usingizini. Mwandishi anasema:

> Alikuwa tayari ameanza kuchukuliwa polepole na usingizi alipotekwa na ndoto ya kusisimua ambayo hakupata kuiota kabla. Alijikuta akiwa katikati ya ngoma ya mtunya ambayo watu wote, wanawake kwa wanaume, wasichana kwa wavulana, walikuwa wakiicheza huku wakirukaruka na kuimba. Lakini nyimbo zao, badala ya kuwa na furaha, zilikuwa na huzuni; walicheza huku machozi yakiwatoka. Wachezaji wote walikuwa wameshika kamba. Kamba hizo mara ziliwazingira na kuanza kuwafunga miguu na mikono, wakawa wanaanguka kila walipojaribu kuinuka ili wakimbie. Punde Kamba hizo ziligeuka fimbo, zikaanza kuwapiga. Wakati huohuo ngoma zilizidi kuchanganya. Punde likaja kundi jingine la wacheza ngoma ya mbali ambayo hakuweza kuitambua kama ni dighubi au ni mkwajungoma. Mdundo wa ngoma hiyo ulikuwa hauchezeki. Wachezaji hao wapya waliwaingilia wachezaji wenyeji na kuvuruka miondoko yao. Makundi hayo mawili yakaanza kupambana. Lakini midundo ya ngoma ambayo sasa haikuwa na urari haikusita bali iliongezeka. Baadaye likapigwa goma kubwa lililotoa mshindo kama wa radi… (uk. 2-3).

Maelezo katika nukuu hii yanadhihirisha kuwa Mbumi alipata maono kupitia ndoto aliyoiota. Kuwa na maono ni sifa ya silika ya koleriki ambayo Mbumi alikuwa nayo. Kwa mtazamo wa utafiti uliofanyika, ngoma ya kwenye ndoto hiyo ilikuwa ikiashiria jambo baya, vita, ambavyo vilitaka kutokea. Kutokana na msingi wa Nadharia ya Saikochanganuzi inayoonesha namna lugha inavyoakisi michakato ya akilini inayojibainisha katika ndoto, misemo na usemaji, Mbumi alidhihirisha michakato hiyo kupitia ndoto. Hata hivyo, ule mshindo wa goma kubwa haukuwa mshindo wa ngoma kweli, bali milio ya bunduki iliyoashiria kuvamiwa. Kwa hiyo, uhusiano wa utendaji na sifa za aina ya silika umedhihirika kupitia ngoma aliyoiota Mbumi, ambayo ilikuwa ni maono kwa kile kilichokuja kutokea baadaye.

Kwa hiyo, tathimini ya uhusiano baina ya utendaji na sifa za aina za silika umebainika kwa kuwarejelea wahusika wakuu wanne kwa kuzingatia silika zao. Wahusika wawili silika zao zinafanana, ijapokuwa wapo katika riwaya tofauti. Wahusika hao ni Chulu na Prospa, ambao wana silika ya Melankoli. Wahusika waliobaki silika zao ni tofauti; Sara ana silika ya sangwini, wakati Mbumi ana silika ya koleriki. Kwa mujibu wa Cao, Sun, na Zhang (2011) wasichana na wavulana hutofautiana katika silika zao na ufanyaji wa kazi. Wanaongeza kuwa aina za silika huchangiwa na utaalamu wa baba, elimu ya mama, mfumo wa familia, uhusiano wa wazazi na watoto, na wakati mwingine umri.

Hata hivyo, katika makundi yote manne, kundi moja halijajitokeza, ambalo ni flegmatiki. Kwa mtazamo wa tasinifu hii, huenda silika hii haijajitokeza kwa sababu ni kundi lenye watu wachache ukilinganisha na makundi mengine. Kwa minajili hiyo, ni nadra kumpata mtu mwenye silika ya flegmatiki. Pia, ili kutimiza lengo la watunzi, tunaamini kuwa wahusika wanapaswa kuvikwa silika zitofautinazo ili kuepusha migogoro isiyokuwa ya lazima.

Kwa upande mwingine, wahusika wamefanikiwa katika utendaji wao kutokana na silika walizovikwa. Mathalani, Prospa na Sara wamefanikiwa kumpata Merisho ambaye alikuwa amepotea katika mazingira ya kutatanisha. Kwa kutumia sifa za silika zao, wameweza kuchangamana na watu mbalimbali, hasa changudoo ambao wamekuwa msaada mkubwa katika kumtafuta Merisho. Pia, tofauti ya silika zao ilisaidia katika kufikia lengo la mwandishi. Kwa mtazamo wa utafiti uliofanyika,

wahusika hao walishirikiana kwa karibu ili kufanikisha lengo lao kwa upande mmoja, na la mwandishi kwa upande mwingine. Palipokuwa na ugumu kwa Prospa, Sara alimtia moyo. Sara, pia alihakikisha Prospa anakuwa na furaha mara zote, pamoja na magumu waliyokuwa wanayapitia. Kuwapo kwa Sara mwenye silika tofauti na Prospa kulikuwa chachu katika safari yao ya kumtafuta Merisho, hatimaye walimpata.

Kwa upande mwingine, Mbumi na Chulu wamefanikiwa kuwasilisha ujumbe wa mbiu ya vita kwa Mukwava kutokana na kutofautiana silika zao. Kwa hiyo, utendaji uliodhihirisha silika zao umechagiza wananchi wa jamii ya Uhehe kuwa na utayari wa kukabiliana na maadui na, hatimaye, kushinda vita.

Kwa mujibu wa Larrimore (2001) watu tofauti wenye uzoefu sawa wanapotakiwa kufanya jambo moja, itagundulika kuwa kuna utofauti kwa kila mmoja. Jambo hilo linaweza kuwa la haraka na kudumu, au taratibu lakini la kudumu, au linaweza kuwa taratibu na kwa kipindi kifupi. Namna hii ya mwitikio ndiyo inayoitwa silika. Kwa hiyo, ni lazima tutambue kwamba kila mtu ni wa kipekee, hakuna watu wawili wanaofanana kwa kila kitu. Kutokana na maelezo ya Larrimore (khj), ni dhahiri kuwa Chulu na Mbumi walikuwa mapacha, lakini walitofautiana kwa kila kitu, ikiwa ni pamoja na utendaji wao na silika zao. Utafiti uliofanyika uliona kuwa, iwapo wahusika hawa wangevishwa silika tofauti na hizi, au zinazofanana, huenda lengo la mwandishi lisingetimia. Pia, watunzi wametumia wahusika wa kike na wa kiume, kwa kuwa silika zao zinatofautiana na kuweka ulingano wa jinsia.

Pamoja na hayo, waandishi wamefanikiwa kuwaumba wahusika wenye jinsia tofauti na silika tofauti, lakini wamewatwika majukumu yanayofanana. Imezoeleka katika riwaya nyingi, mtoto wa kike anadunishwa na kuonekana mtu wa nyumbani, asiyekuwa na maamuzi na anafanyiwa kila kitu na mwanaume. Waandishi hawa wameenda kinyume kwa kuwapa majukumu makubwa, ambayo mengine hata watu wakubwa wasingeweza kuyafanya. Jambo hili linatiliwa mkazo na Bakize (2021) anaposema kuwa Fasihi ya watoto ikiwasawiri vizuri watoto na kuwaonesha kuwa ni watu muhimu, tunaweza kuwa na jamii bora leo na kesho. Mtazamo wa Bakize ni kwamba watoto wanaposoma, wanaamini sana kile wanachokisoma, na hivyo, kinaweza kuwabadilisha. Kwa hiyo, anasisitiza umuhimu wa kuwa na tahadhari

katika kuwasawiri wahusika watoto, jambo ambalo waandishi wa riwaya zote mbili wamefaulu.

### 4.4.3 Hitimisho

Kwa jumla, sehemu hii imetathimini uhusiano uliopo baina ya utendaji na sifa za aina ya silika za wahusika wakuu wa riwaya teule. Maelezo na mifano iliyotolewa inathibitisha uhusiano uliopo baina ya silika na utendaji wa wahusika wakuu. Ili kubaini silika ya mhusika, ni lazima atende au azungumze jambo fulani, na silika ndiyo inayomsukuma mhusika kutenda jambo hilo. Kwa hiyo, zote zinaathiriana, kukamilishana, na kufanya dunia iwe mahali salama pa kuishi. Aidha, tofauti ya silika baina ya wahusika katika riwaya moja imesaidia kufikia malengo ya waandishi.

## 4.5 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imewasilisha na kujadili matokeo ya utafiti uliofanyika. Mjadala umefanyika kwa kurejelea malengo matatu ya utafiti. Ili kupata muwala, muhtasari wa riwaya teule ulifafanuliwa, kisha utendaji wa wahusika wakuu katika riwaya hizo umefafanuliwa. Utendaji umefafanuliwa kwa namna ya kuhoji, kushawishi, kudadisi, kuonya, kudanganya, kutaarifu, na kushauri. Sehemu ya tatu tumechambua aina ya silika na sifa zake, kisha tumebainisha aina za silika kwa kila mhusika. Imebainika kuwa kila mhusika ana silika yake inayomtofautisha na mhusika mwingine. Prospa na Chulu wana silika ya melankoli, Sara sangwini, na Mbumi Koleriki. Silika zao zimewasaidia kufanya kazi pamoja na kupunguza migongano kati yao na kufanikisha malengo ya safari zao. Prospa na Sara walifanikiwa kumpata Merisho, aliyetoweka nyumbani kwao TPC-Moshi. Kwa upande mwingine, Mbumi na Chulu walifanikiwa kufikisha ujumbe wa mbiu ya mapambano kwa Mukwava. Katika sehemu ya nne tumetathimini uhusiano baina ya utendaji wa wahusika na sifa za aina za silika zao. Imebainika kuwa upo uhusiano mkubwa, kwani huwezi kubaini silika ya mhusika kama hajatenda au hajasema jambo lolote, na silika ndiyo inayomsukuma mhusika kutenda jambo hilo. Uhusiano baina ya utendaji na sifa za aina za silika umewasaidia wahusika kutimiza malengo ya waandishi. Mwisho, muhtasari wa Sura nzima umetolewa.

Sura inayofuata inaonesha muhtasari wa tasinifu, hitimisho la jumla, na kutoa mapendekezo mbalimbali.

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inaundwa na sehemu nne ambazo ni: utangulizi, muhtasari wa tasinifu, hitimisho, na mapendekezo.

## 5.2 Muhtasari wa Tasinifu

Tasinifu hii inahusu uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Tasinifu hii ina jumla ya Sura tano, kama ifuatavyo:

Sura ya Kwanza imefafanua istilahi muhimu zilizotumika katika tasinifu hii ambazo ni silika, utendaji, wahusika, mtoto, na Fasihi ya watoto. Usuli wa tatizo la utafiti umefafanuliwa kwa kuonesha kwamba utanzu huu bado haujafanyiwa sana utafiti kutokana na kasumba ya watu, hasa wasomi, ya kuhusianisha utanzu huu na mambo ya kitoto yasiyo na maana. Utafiti uliofanyika, umedhihirisha kuwa Fasihi ya watoto ni muhimu kuliko hata ya watu wazima, kwani inahusu ujenzi wa utu wa mtu na tabia yake kwa jumla. Hii ni kwa sababu, watoto wana tabia ya kufyonza vitu akilini, vikawakaa kuliko watu wazima. Pia, silika ni muhimu katika kuzisoma na kuzielewa kazi hizi ambazo huandikwa kwa ajili ya watoto.

Kipengele kingine cha sura hii ni tamko la tatizo la utafiti. Tamko limebainisha kuwa masuala ya silika katika Fasihi ya watoto hayajachambuliwa kwa upekee wake, jambo ambalo likiachwa, litaathiri wasomaji ambao ni watoto. Pia, sura hii imebainisha malengo na maswali ya utafiti ambayo yalituongoza katika uchambuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Vilevile, manufaa ya utafiti yamejadiliwa katika mtazamo wa kijamii, kitaaluma, kifasihi, na kisera. Mwisho, mawanda ya utafiti yamefafanuliwa kwa kuonesha kuwa, ijapokuwa riwaya teule zina wahusika wengi, tasinifu hii imewaangalia wahusika wakuu tu kulingana na malengo ya utafiti uliofanyika.

Sura ya Pili imeweka wazi maandiko mbalimbali ambayo yameshabihiana na mada ya utafiti uliozaa tasinifu hii. Maandiko hayo ni tafiti tangulizi ambazo zilihusu silika, utendaji, wahusika, na Fasihi ya watoto. Baada ya kuyajadili mapitio hayo, mapengo ya utafiti yalibainika. Ilibainika kuwa wataalamu wengi wametafiti zaidi

katika Fasihi ya watu wazima kwa kuwaangalia wahusika wakuu, hasa wanawake. Pia, tafiti kuhusu silika zimefanywa zaidi katika uga wa saikolojia na sosholojia. Hivyo, ilionekana haja ya kuonesha mtagusano baina ya saikolojia na Fasihi kwa kuonesha uhusiano baina ya silika na utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Mwisho, tafiti nyingi za utendaji zimefanyika katika tamthiliya na Fasihi simulizi, na waliofanyia riwaya walijikita zaidi katika riwaya za watu wazima.

Jambo jingine lililofafanuliwa katika Sura hii, ni nadharia ya utafiti. Nadharia ya Saikochanganuzi iliyoasisiwa na mwanasaikolojia Sigmund Freud ilitumika kama kiunzi cha ufafanuzi wa mambo mbalimbali katika mjadala wa matokeo ya utafiti. Katika nadharia hii, tumeangalia namna nafsi tatu za ki-Freud zinavyomsukuma mhusika kutenda mambo mbalimbali kutokana na mahitaji ya wakati husika. Pia, imebainika kuwa matamanio ndiyo kiini cha matendo yote ya wahusika ambapo, wakati mwingine, huvunja sheria na taratibu na kuumiza wengine ili tu wakidhi matamanio yao.

Sura ya Tatu imefafanua methodolojia iliyotumika katika utafiti uliozaa tasinifu hii. Vipengele vilivyojadiliwa katika sura hii ni pamoja na: usanifu wa utafiti, mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, njia za kukusanya na kuchanganua data za utafiti, maadili ya utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, na changamoto za utafiti na utatuzi wake. Usanifu uliotumika ni uchunguzi kifani, ambao ulisaidia kuteua riwaya mbili za watoto za *Safari ya Prospa* na *Ngoma ya Mianzi* ambazo zilisomwa kwa kumakinikia silika na utendaji wa wahusika wakuu. Pia, mkabala uliotumika ni wa kitaamuli ambao hujikita katika maelezo kwa kiasi kikubwa kuliko takwimu.

Sura ya Nne imewasilisha na kujadili matokeo ya utafiti uliofanyika. Mjadala umefanyika kwa kurejelea malengo matatu ya utafiti. Ili kupata muwala, muhtasari wa riwaya teule ulitolewa. Katika sehemu ya kwanza tumefafanua utendaji wa wahusika kwa namna ya kuhoji, kushawishi, kudadisi, kudanganya, kuonya, kutaarifu, na kushauri. Katika sehemu ya pili, tumebainisha kuwa kila mhusika ana silika yake inayomtofautisha na mhusika mwingine. Prospa na Chulu wana silika ya melankoli, Sara ana silika ya sangwini, na Mbumi ana silika ya koleriki. Silika zao

zimewasaidia kufanikisha malengo ya safari zao. Prospa na Sara walifanikiwa kumpata Merisho. Kwa upande mwingine, Mbumi na Chulu walifanikiwa kufikisha ujumbe wa mbiu ya mapambano kwa Mukwava. Katika sehemu ya tatu, tumetathimini uhusiano baina ya utendaji wa wahusika na sifa za aina za silika zao. Imebainika kuwa upo uhusiano mkubwa, kwani ni vigumu kubaini silika ya mhusika kama hajatenda au hajasema jambo lolote. Kwa hiyo, silika ndiyo inayomsukuma mhusika kutenda jambo fulani.

### 5.3 Hitimisho

Hitimisho la utafiti uliochunguza uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili linafafanua mambo muhimu matatu ambayo ni: mchango wa tasinifu hii, utoshelevu wa nadharia iliyotumika katika uchanganuzi na uwasilishaji wa data, na maoni mbalimbali yaliyotokana na utafiti uliofanyika.

#### 5.3.1 Mchango Mpya wa Tasinifu

Matokeo ya utafiti uliofanyika yana mchango mpya katika taaluma ya Fasihi kama ifuatavyo:

Kwanza, yameonesha mtagusano baina ya Fasihi na saikolojia na kudhihirisha kwamba, katika taaluma, hakuna uga unaoweza kutazamwa kipwekepweke, bali nyuga zote zinategemeana, kuathiriana na kukamilishana. Fasihi haiwezi kujifungia kama kisiwa, bali huchota maarifa katika nyuga nyingine za kitaaluma na kuzitumia katika kufafanua mambo mbalimbali.

Pili, ni kupambanua suala la utendaji katika riwaya za watoto za Kiswahili. Ifahamike kuwa suala la utendaji limekuwa likiwashughulisha wahakiki wengi katika Fasihi simulizi na tamthiliya. Kupitia utafiti uliozaa tasinifu hii, suala la utendaji limefafanuliwa kwa kupitia lugha ya mazungumzo baina ya wahusika na masimulizi ya kiutendaji yanayokwenda sambamba na mazungumzo hayo. Kwa hiyo, utendaji umebainika kwa namna mbalimbali. Mathalani, katika lengo la kwanza, utendaji umefafanuliwa kwa namna ya kuhoji, kushawishi, kudanganya, kutaarifu, na kudadisi. Pia, katika lengo la tatu, utendaji huu umetumika kuhusianishwa na sifa za aina za silika za wahusika wakuu katika riwaya teule. Kupitia maandiko mbalimbali yaliyosomwa na mtafiti, utendaji wa aina hii haujawahi kufanyika mahali popote

kwa kurejelea Fasihi ya watoto ya Kiswahili. Kwa hiyo, inaaminika kuwa tasinifu hii inatoa mchango mkubwa wa kimaarifa unaohusiana na utendaji wa wahusika wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili.

Tatu, dhana ya silika imetambulishwa katika uga wa Fasihi kwa jumla na Fasihi ya watoto kwa upekee wake. Dhana hii imebainishwa kwa uchache sana katika fasihi ya watu wazima, lakini katika tahakiki na tafiti mbalimbali za Fasihi ya watoto ya Kiswahili kuna uhaba wa maandiko hayo. Kwa hiyo, tasinifu hii imeongeza utajiri wa dhana na marejeleo katika Fasihi kwa ujumla na Fasihi ya watoto kwa upekee wake.

### 5.3.2 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika

Nadharia ya Saikochanganuzi imetumika katika tasinifu hii kama ilivyofafanuliwa katika Sura ya Tatu. Nadharia hii imetumika katika kukusanya data, kuzichambua na kuziwasilisha. Kwa hiyo, imetumika kama mwega wa kuonesha utendaji wa wahusika hao, ambao hutokana na misukumo ya ndani inayotokana na matamanio yao. Matamanio ya wahusika husukumwa na nafsi tatu za ki-Freud, ambazo humfanya mhusika atende au asitende jambo fulani kutokana na miiko na makatazo ya jamii husika. Katika muktadha huu, jamii ni ile iliyoandikiwa kazi husika, ambayo mara nyingi, ndiyo atokayo mwandishi wa kazi hiyo. Inaaminika kuwa mwandishi huandika kutokana na uzoefu wa maisha yake na jamii inayomzunguka, kwa kuwa naye ni sehemu ya jamii.

Pia, nadharia imetumika kutubainishia aina za silika za wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili katika riwaya teule, ambayo yamemtofautisha mhusika mmoja na mwingine. Silika hizi zilibainika kutokana na wahusika kutenda mambo mbalimbali, ambayo yalibainika kutokana na mazungumzo baina ya wahusika na masimulizi ya kiutendaji yanayokwenda sambamba na mazungumzo hayo

Zaidi, nadharia hii imetumika katika kuonesha uhusiano baina ya utendaji na sifa za aina za silika, kwa kuwa nafsi za ki-Freud ndizo zinazosukuma wahusika kutenda, na kupitia matendo hayo, tunapata sifa za silika; na hivyo, uhusiano wake unabainika. Mtafiti anaamini kuwa nadharia hii imefanya matokeo ya utafiti kuwa thabiti na halali.

### 5.3.3 Maoni Kutokana na Utafiti Uliofanyika

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti uliofanyika, mtafiti anaona kwamba dhana ya utendaji inaweza kutumika katika riwaya kwa kuchambua mazungumzo ya wahusika na masimulizi ya mwandishi. Maoni haya hayapingani na wataalamu wanaobainisha kuwa utendaji ni lazima uwe ana kwa ana, na wale wanaosema utendaji upo katika tamthiliya na Fasihi simulizi, bali yameenda mbali kwa kuongeza utendaji katika riwaya.

Hali kadhalika, silika ni dhana muhimu katika kuzihakiki kazi za Fasihi, kwani itasaidia katika kuzisoma na kuzielewa kazi hizo. Pia, kwa kuzijua silika, jamii itapunguza migogoro isiyokuwa ya lazima, kwa sababu kila mtu atajijua na atawajua wengine, na hivyo, kiwango cha uvumilivu kitaongezeka.

## 5.4 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti uliofanyika na kuzaa tasinifu hii, tunatoa mapendekezo yafuatayo:

### 5.4.1 Mapendekezo kwa Waandishi, Wahakiki, na Wataalamu wa Fasihi

Riwaya za watoto zifanyiwe ufaraguzi ili ziweze kuigizwa katika majukwaa, kwani mambo yote yanayohitajika ili kuigiza yapo, kama vile: maleba, mandhari, wahusika, na uhusika wao. Mathalani, katika riwaya ya *Ngoma ya Mianzi,* yametajwa maleba kama kaniki, kofia zenye manyoya na tarbushi, makaptura ya kaki, lubega nyekundu na nyeusi, vilemba vyeupe, mgolole, mabangili ambayo yalivaliwa na wahusika mbalimbali. Katika *Safari ya Prospa*, ijapokuwa mwandishi hakutaja sana maleba, lakini picha zinazofafanua maelezo mbalimbali zinaonesha maleba hayo. Pia, katika suala la uigizaji, huwa kuna maelezo ya awali. Hivyo, maelezo ya kila hatua yatafafanuliwa kwa kutumia lugha ya masimulizi ya mwandishi. Kwa kufanya hivyo, riwaya hizi zitaweza kuigizwa na kuwafikia watu wengi kwa wakati mmoja. Pia, kupitia kuona na kusikia, watoto watazielewa kazi hizi, kwani milango miwili ya fahamu itatumika tofauti na wakisoma tu. Kwa hiyo, wataweza kuelewa utendaji wa wahusika ambao ndio kiini cha kujua silika zao.

### 5.4.2 Mapendekezo kwa Watafiti

Fasihi ya watoto ni uga mpana sana wenye utajiri wa mada zinazoweza kutafitiwa. Hivyo, watafiti wachangamkie uga huu na kuacha kuudharau na kuunasibisha na mambo ya kitoto, kwani una mchango mkubwa katika ukuaji wa mtoto kijamii na kisaikolojia. Kutokana na umuhimu wa Fasihi hii kwa watoto, shirika la *Room to Read*[13] limeanzisha maktaba ya mtandaoni, ambayo ina mkusanyiko wa hadithi zaidi ya mia tatu. Lengo la maktaba hii ni kuwajengea uwezo watoto kujisomea hadithi mbalimbali ili kuwajenga kisaikolojia. Kwa hiyo, kutokana na umuhimu wa suala la silika kwa wahusika wa Fasihi ya watoto ya Kiswahili, mtafiti anatoa mapendekezo kwa watafiti wengine kufanya utafiti katika riwaya nyingine za watoto na tanzu nyingine za Fasihi ya watoto kama vile tamthiliya na hadithi fupi. Pia, tafiti zinaweza kufanywa kuhusu silika za wahusika wema na wahusika wawi ili kubaini kufanana au kutofautiana kwa silika zao. Pia, kuona ni kwa namna gani silika zao zinaathiri utendaji wao katika kusukuma mbele maudhui ya hadithi husika. Mtazamo wetu ni kuwa, endapo tafiti nyingi zitafanyika, zitaongeza marejeleo kwa watafiti wengine na kuzidi kuipanua Fasihi ya watoto ya Kiswahili.

### 5.4.3 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu

Wanafunzi wazoeshwe kusoma vitabu vya ziada ili kukuza usomaji wa kifasihi. Utafiti uliofanyika uligundua kuwa wanafunzi wengi wanasoma vitabu vya kiada tu kwa ajili ya kujibia mitihani yao. Hali hii inadumaza ari ya wanafunzi kujisomea vitabu vingine vilivyoandaliwa kwa ajili yao. Pamoja na hayo, imebainika kuwa vitabu vya Mradi wa Vitabu vya Watoto havisomwi kwa mwamko kama ilivyokuwa awali. Hivyo, Wizara ya Elimu ipendekeze vitabu vya ziada vitakavyosomwa katika shule zote za sekondari ili kuleta uwiano. Vilevile, shule za sekondari zinunue nakala za vitabu vitakavyopendekezwa kwa ajili ya usomaji wa ziada, na kuwaazimisha wanafunzi ili wavisome, kisha wavirudishe kwa ajili ya kutumiwa na wengine. Ili kupima uelewa wao, inashauriwa kuwa kila aliyeazimishwa kitabu asimulie kwa ufupi kuhusu kile alichokisoma. Hili likifanyika, inaaminiwa kuwa litakuza ari ya wanafunzi kujisomea kifasihi. Sambamba na hilo, shule zote zilizokuwa na Mradi wa

---

[13] Hili ni shirika binafsi ambalo limelenga katika kuweka vitabu mtandaoni kwa ajili ya watoto kujisomea na kukuza usomaji huo. Shirika hili hutumia mtandao wa *Facebook* na *Instagram*, ambapo kuna kurasa zenye kazi hizo. Pia, hurusha matangazo yake katika kituo cha redio cha *RFA* (*Redio Free Africa*) kilichopo jijini Mwanza na chaneli za kituo cha runinga cha Azam *Media*.

Vitabu vya Watoto zitupiwe jicho kuhakikisha kuwa walimu wanasimamia usomaji wa ziada kwa wanafunzi wao.

## MAREJELEO


Abulizi, at al. (2017). Temperament in infancy and behavioral and emotional problems at age 5.5: *The Eden other-child cohort. Plos One*, *12*(2). Ilisomwatarehe 20/01/2020 katika https://doi.org/10.1371/journal.pone. 0171971.

Aiello, F. (2015). Promoting readership in African languages: Swahili books for children and youth in East Africa. *The borders of Fantasia*, 133, 82-88.

Ali, H. A. (2015). *Kutathmini usawiri wa mhusika mwanamke katika hadithi simulizi za Wapemba*. Ilisomwa tarehe 22/02/2019 katika http://repository. out.ac.tz/1194/

Ali, S. M., Islam, R., & Hamdard, J. (2007). A scientific correlation between blod groups & temperaments in Unani medicine. *Indian Journal of Traditional Knowledge*,*Vol 3*(1).

Amukowa, D. N. (2018). Mchango wa Kirikuu katika makuzi ya Fasihi ya watoto. *Mulika Journal*, *1*(1) 2018.

Asamoah, G. (2018). A synoptic account of the four human temperament. *Inter Disciplinary Research Journal of Theology, Apologetics, Natural and Social Sciences*, *1*(1&2), 67–70.

Bakhressa, S. K. (1992). *Kamusi ya matumizi na maana.* Nairobi, Kenya: Oxyford University Press.

Bakize, L. H. (2013). Changamoto zinazoikabili Fasihi ya watoto nchini Tanzania. *Kiswahili*, *76*, 61–71.

Bakize, L. H. (2015). Gender balance struggles in Tanzanian Kiswahili children's literature. *Kiswahili*, *78*, 59-66.

Bakize, L. H. (2018). Mchango wa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI) katika kukuza na kuendeleza uwanja wa Fasihi ya Kiswahili ya watoto ndani na nje ya Tanzania (2009-2016). *Mulika Journal*, *36* (1).

Bakize, L. H. (2021). Usawiri chanya wa watoto katika Fasihi ya watoto kama njia faafu ya kujenga jamii bora ya leo na kesho: Mifano kutoka vitabu teule vya watoto vya Kiswahili. *Jarida la Mnyampala*, Na. 2 (1), 83-94.

Bakize, L. H., Lyimo, E., & Ngugi, P. M. (2017). Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili ya watoto nchini Tanzania na Kenya : Mkabala linganishi. *Kiswahili*, *80* (1), 115–136.

Bakize, L. H. & Senkoro, F. E. M. K. (2019). Shujaa wa kike katika bunilizi za kihistoria za watoto katika Kiswahili. *Kiswahili*, *82*,121-137.

Bingham, J. (1970). *A content analysis of the treatment of Negro characters in children's picture books 1930-1968*. Unpublished PhD dissertation prepared for Michigan State University.

Carey, W. B. (1981). The importance of temperament-environment interaction for child health and development. In *The uncommon child* (pp. 31-55).

Chama cha Wanasheria Tanganyika (2016). *Mtoto na haki zake.* Ilisomwa tarehe 13/03/2019 katika https://tls.or.tz/publication/view/ijue-sheria-ya-mtoto-na-haki-zake/

Cohen, L., Manion, L., & Marrison, K. (2000). *Rasearch methods in education*. New York: Routledge Falmer.

Creswell, J. W. (2007). *Educational reseach: Planning, conducting and evaluating quantitative and qualitative research*. Boston: Pearson.

Creswell, J. W. (2009). *Research design: Qualitative, quantitative, and mixed methods approaches*. Los Angeles: SAGE Publications.

Crippen, M. (2012). The value of children's literature. *Oneota Reading Journal of Luther College*, *2*, 32-34.

Dawson, C. (2002). *Practical research methods*: *A User-friendly guide to mastering research*. United Kingdom: How to Books.

Ekstrand, D.W. (ht). “The Four Human Temperaments,” in *www.thetransformedsoul.com/.../the-four-human-temperaments*. Accessed on 19 August 2018.Gatwiri, J. N. (2015). *Tathmini ya hadithi za watoto katika mtandao*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Kenyatta(Haijachapishwa).

Finnegan, R (1970). Oral literature in Africa. Oxford University Press. Dar es Salaam and Nairobi.

Flaskerud, J. H. (2012). Temperament and personality: From Galen to DSM. *Mental Health Nursing*, *33*(9), 631–634. https://doi.org/DOI: 103109/ 01612840. 2011647256

Gerard, S., & Sanjay, S. (1992). Running head: Personality dimensions. *Psychology*,*3*, 54-60.

Greenlaw, M. (1970). *A study of the impact of technology on human values as reflected in modern science fiction for children*. Unpublished PhD dissertation prepared for Michigan State University.

Herman, L. (2012). Fantansia katika Fasihi ya Kiswahili ya watoto. *Kioo Cha Lugha*, *TATAKI*, 122–134.

Howart, E. (1988). Personality and individual differences. *Jornal of Research in Personality, vol 9* (1), 173-175.

Kawira, S & Kisurulia, S. (2018). Wahusika, uhusika na mtazamo katika riwaya ya Kiswahili. *University of Dar es Salaam Journals*. Ilisomwa tarehe 26/01/2019 katika journals.udsm.ac.tz.%3Eview.

Kothari, C. R. (2004). *Research methodology: Methods and techniques* (Second Rev). New Delhi: New Age International (P) Limited.

Kothari, C. R. (2009). *Research methodology methods and techniques* (Second Rev). New Delhi: New Age International (P) Limited.

Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A. (2006). *Proposal and Thesis writing: An introduction*. Nairobi: Pauliness Publications.

Lebron, A. (2013). What is Culture? *Merit Research Journals of Education and Review*. *Vol. 1* (6), pp 126-132.

Lema, E. (2004). *Safari ya Prospa*. Dar es Salaam: E & D Limited.

Lyimo, E. B. (2014). Nduni za Fasihi ya watoto: Mifano kutoka vitabu vya Fasihi ya Kiswahili ya watoto nchini Tanzania. *MULIKA*, *33*, 33–45.

Lyimo E.B. (2017). Dhima ya Mianzo na Miisho katika Nathari za Watoto: Mifano kutoka Nathari za Kiswahili Nchini Tanzania. *Kioo Cha Lugha*, *Juz. 15*, 89-105.

Madumulla, J. S. (2001). Hali ya vitabu vya watoto katika Tanzania. *Swahili Forum*, *VIII*, 171-183.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, historia na misingi ya uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Martin, M., & Bobgan, D. (1992). *Christian and the four temperaments*. Califonia: East Gate.

Masek, A., & Yamin, S. (2011). The effect of problem based learning on critical thinking ability: a theoretical and empirical review. *International Review of Social Sciences andHumanities*, *2*(1), 215-221.

Mbarouk, S. S.(2019). Uchambuzi wa riwaya ya *Kiu* kwa kutumia nadharia ya Saikolojia Changanuzi. *Eastern African Literary and Cultural Studies*. DOI :10.1080/23277408.2018.1540127.

Mbunda, M. (1992). *Misingi ya hadithi fupi*. Dar es Salaam: DUP.

Mbunda, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa Fasihi*. Dar es Salaam: East African Educational Publishers Ltd.

Mbuthia, M. (2018). The role of Kiswahili children's literature in formulating their worldview. *International Journal of Education and Research,6*(2), 129–140.

Mills, D. (2005). Model marriage. In *Parchment House* (Second Ed, Vol. 84). Ilisomwa tarehe 20/03/2019 katika http://ir.obihiro.ac.jp/ dspace/handle/ 10322/3933.

Mlacha, S. A. K. (1985). Wahusika katika riwaya za Kiswahili Tanzania (1970-1982). *Mulika,17*, 29–45.

Mlaga, W. K. (2017). *Misingi ya ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mlama, P. (2003).*Utunzi wa tamthiliya katika mazingira ya Tanzania katika makala za semina ya kimataifa ya waandishi wa Kiswahili III: Fasihi* (Chapa ya tatu). Dar es Salaam: TUKI.

Moh'd, M. O. (2017). *Ulinganishi wa tabia za wahusika wakuu na dhamira katika riwaya za Kusadikika na Utengano.* Tasinifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (Haijachapishwa).

Mudhihiri, M. (2019). *PressReader.com* - Your favorite newspapers and magazines. Ilisomwa tarehe 14/04/2019 katika https://www.pressreader.com/

Muhando, P.& Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonyesho*. Dar es Salaam: TPH.

Mulewa, A. (2011). *Wahusika katika hadithi fupi za kisasa za Kiswahili*. Ilisomwa tarehe 21/04/2019 katika http://41.89.55.71: 8080/xmlui/ handle/ 123456789/855.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mulokozi, M. M. (2018). *Ngoma ya Mianzi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Munyioki, A. M. (2018). *Utendaji wa kidrama wa riwaya ya Haini ya Adam Shafi 2003.* Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi ya Kiswahili. Chuo Kikuu cha Moi (Haijachapishwa).

Mwashota, P. & Nchimbi, F. (2016). Matapo ya nyimbo za Shisafwa. *Kiswahili*, 79, 1-14.

Nazarov, A. (2022). Kinds of temperament of human beings. *International Scientific Journal*, *Vol 3*(1) 321-324.

Ngugi, P. M. Y. (2014). Fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji ya mtoto kisaikolojia. *TATAKI*, *77*(*1*), 170–180.

Nodelman, P. & Reimer, M. (2003).*The Pleasure of children's Literture*. USA: Longman.

Okal, B. O, Ambuyo, B. A & Amukowa, D. N. (2012). The functionality of four temperaments and communication theories towards the realisation of peaceful general elections in Kenya. *Journal of Socialogical Research*. Ilisomwa tarehe 12/07/2020 katika https//dx.doi.or/10.5296/jsr.v3il.2012.

O'Quinn, J. (ed) et al (1981). African performance issue. *The Drama Review*, Vol 25. Winter. Massachusetts Institute of Technology.

Ponera, A. S. (2010). *Athari za ufutuhi katika nathari za Shaaban Robert.* Tasnifu ya Shahada ya Umahiri. Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).

Ponera, A. S. (2014). *Ufutuhi katika nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu. Chuo Kikuu cha Dodoma(Haijachapishwa).

Ponera, A. S. (2019). *Misingi ya utafiti wa kitaamuli na uandishi wa tasinifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Ponera, A. S & Kasiga, G. A (2019). Mdhihiriko wa kionjo cha usangwini kwa mhusika Willy Gamba katika riwaya ya *Njama*. *Kioo cha Lugha.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, *Juz 17*, 99-113.

Rakhmanina, L., Martina, F., & Nevan, J. (2020). The comparison study of student personality: Sanguine and Phlematic toward their English speaking ability. *Professional Journal of English Education*, *vol 3*(4), 443-452.

Robson, C. (2007). *How to do a research project: A Guide for undergraduate students*. Carton Victoria: Blackwell Publishing.

Rothbart, M. K. (2012). Early temperament and psychosocial development. In *Encyclopedia on Early Childhood Development* (2012thed., p. 12). University of Oregan, U.S.A.

Rothbart, M. K. & Bates, J. E (2007). Temperament: Social, emotional, and personality development. *Handbook of Child Psychology* vol III. Ilisomwa tarehe 22/04/2019 katika https://doi.org/10.1002/9780470147658. psy0303.

Sanga, E. S. (2015). Dhima ya nyimbo za bongo fleva zihusuzo rushwa katika kuleta mabadiliko kwa jamii. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dodoma (haijachapishwa).

Schechner, R. (2013). (3rd ed). *Performance studies*: *An introduction*. USA and Canada: Routledge.

Senkoro, F. E. M. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Shepard, J. P. (1962). The treatment of character in popular children's Fiction. *Elementary English*, *39*,672-76).

Shiner, R. L. (2012). The impact of temperament on child development: Comments on Rothbart, Eisenberg, Kagan, Schermerhorn and Bates. In *Encyclopedia on Early Childhood Development*,pp. 28–30.

Soyinka, W. (1988). *Art, dialogue and outrage: Essays on literature and culture.* Ibadan: New Horn Press.

Spinelli, M. (2018). The influence of early temperament on language development: The moderating role of maternal input. *Developmental Psychology*. Ilisomwa tarehe 18/04/2019 katika https://doi.org/10.3389/fpsyg.2018.01527.

TATAKI. (2013). *Kamusi ya Kiswahili sanifu* (Toleo la tatu). Dar es Salaam: Oxford University Press.

TUKI (2006). Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam.

Vice, S. (1990). *Ed. Psychoanalytic criticism: A reader*. London: Polity Press.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Nairobi, Kenya: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2 003). *Kichocheo cha Fasihi:simulizi na andishi*. Nairobi, Kenya: Focus Publication.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi, Kenya: Vide Muwa Publishers Limited.

Wa Thiong'o,N. (1986). *Decolinising the mind*:*The language of African theatre*. Nairobi: Heinemann Kenya.

Wen, H., Sze, N.N., Zeng, Q., and Hu, S.(2019). Effect of music listening on phsiological condition, mental workload, and driving performance with consideration of driver temperament. *International Journal of Environmental Research and Public Healthy*, *vol 16*, 6-12.

Young, P. V. (1949). *Scientific social surveys and research*. New York: Prentice Hall.

# VIAMBATISHO

## A. Zana za Ukusanyaji wa Data

Katika kijisehemu hiki tunabainisha zana mbalimbali zilizotumika katika mchakato mzima wa kukusanya data za utafiti uliozaa tasinifu hii. Zana hizo ni: mwongozo wa usaili kwa waandishi wa riwaya teule, mwongozo wa usaili kwa wataalamu wa Fasihi ya watoto, mwongozo wa majadiliano na vikundi lengwa, na mwongozo wa usomaji matini.

### A.1 Mwongozo wa Usaili kwa Waandishi wa Riwaya Teule

Ninaitwa Saumu Mkomwa, mwanafunzi wa ngazi ya Uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Ninafanya utafiti kuhusu **Uhusiano wa Silika na Utendaji wa Wahusikawa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili.** Lengo la utafiti huu ni kutaka kuchunguza silika na utendaji wa wahusika wakuu. Vitabu teule vya utafiti huu ni *Ngoma ya Mianzi* na *Safari ya Prospa*. Ninaomba unisaidie kujibu maswali yafuatayo ili kukamilisha shabaha hiyo. Majibu yake yatatumika kwa shabaha za kitaaluma tu, na si vinginevyo.

1. Mpaka sasa una vitabu vingapi vya watoto? Naomba unitajie.
2. Lengo la kutunga riwaya hii lilikuwa lipi?
3. Ni vigezo gani huwa unavizingatia unapowaumba wahusika wako?
4. Wahusika wa riwaya hii wana uhalisia gani?
5. Kwa mtazamo wako, tunapozungumzia utendaji katika riwaya tunamaanisha nini?
6. Naomba unieleze tofauti ya utendaji katika tamthiliya na katika riwaya.
7. Kuna jambo linaitwa silika ambalo ni maumbile ya msingi ambayo mtu huzaliwa nayo, na humtofautisha mtu mmoja na mwingine. Kwa kuwa wahusika huwakilisha binaadamu, Unadhani wahusika wanapoumbwa wanakuwa na silika zao?
8. Unadhani silika zina mchango wowote katika utendaji wa wahusika wakuu? Kivipi?
9. Je sifa za aina za silika zina uhusiano na utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto?
10. Una maoni gani kuhusu dhana ya silika katika Fasihi?

Asante kwa ushirikiano.

**A.2 Mwongozo wa Usaili kwa Wataalam wa Fasihi ya Watoto**

Ninaitwa Saumu Mkomwa, mwanafunzi wa ngazi ya Uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Ninafanya utafiti kuhusu **Uhusiano wa Silika na Utendaji wa Wahusika wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili.** Lengo la utafiti huu ni kutaka kuchunguza silika na utendaji wa wahusika wakuu. Vitabu teule vya utafiti huu ni *Ngoma ya Mianzi* na *Safari ya Prospa*. Ninaomba unisaidie kujibu maswali yafuatayo ili kukamilisha shabaha hiyo. Majibu yake yatatumika kwa shabaha za kitaaluma tu, na si vinginevyo.

1. Nini maana ya Fasihi ya watoto?
2. Wewe ni mtaalamu wa uga huu ambaye umejishughulisha sana na tafiti, naomba unielezee historia fupi ya Fasihi ya watoto.
3. Mojawapo ya kazi za watoto ni *Ngoma ya Mianzi na Safari ya Prospa*, unawazungumziaje wahusika wa riwaya hizi.
4. Je, wahusika hawa wana uhalisia wowote? Naomba unielezee kwa kifupi.
5. Suala la utendaji limejadiliwa sana katika tamthiliya na Fasihi simulizi. Naomba unipe maoni yako kuhusu utendaji katika riwaya.
6. Unadhani kwanini watafiti wengi wa Fasihi ya watoto hawajashughulikia wahusika?
7. Kuna mambo ambayo hutofautisha mtu mmoja na mwingine katika matendo yao, muonekano wao na tabia zao. Mambo hayo ni ya kuzaliwa nayo, huitwa silika. Kwa kuwa wahusika huwakilisha binadamu basi nao wana silika zao. Naomba unitajie aina za silika unazozifahamu na sifa zake.
8. Sifaza aina za silika zina uhusiano gani na utendaji wa wahusika wakuu wa Fasihi ya watoto kwa jumla?
9. Ni mambo gani ambayo husukuma utendaji wa wahusika katika Fasihi ya watoto?
10. Una maoni gani kuhusu dhana ya silika katika Fasihi?

Asante kwa ushirikiano.

**A.3 Mwongozo wa Majadiliano ya Vikundi Lengwa**

Ninaitwa Saumu Mkomwa mwanafunzi wa ngazi ya Uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Ninafanya utafiti kuhusu **Uhusiano wa Silika na Utendaji wa Wahusika wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili.** Lengo la utafiti huu ni kutaka kuchunguza uhusiano wa silika na utendaji wa wahusika wakuu. Vitabu teule vya utafiti huu ni *Ngoma ya Mianzi* na *Safari ya Prospa*. Ninaomba mnisaidie kujadilili mada zifuatazo ili kukamilisha shabaha hiyo. Maelezo na maoni yote yatatumika kwa shabaha za kitaaluma tu, na si vinginevyo.

**Maelekezo ya Mjadala**

Mjadala wetu utafanyika kwa dakika ishirini, ambapo kila mada itajadiliwa kwa dakika kumi. Wakati wa mjadala tutatumia simu kurekodi, kwa sababu kila neno lina thamani katika utafiti huu. Kila wazo tunaliheshimu, hivyo ninaomba wakati mmoja anazungumza wengine tumsikilize kwa makini bila kumuingilia. Pia, ninawasihi kama hujakubaliana na hoja usiipinge bila kuwa hoja nyingine. Karibuni.

**Mada kwa Wanafunzi Wanaosoma Shahada ya Awali ya Ualimu katika Elimu ya Awali (BED ECE)**

**Mada 1**.

a) Maana ya Silika/ Meaning of Temperament
b) Aina za Silika / Types of Temperament
c) Sifa za kila Aina ya Silika /Characteristics of Each Type of Temperament

**Mada 2**.

Uhusiano wa Utendajina Sifa za Aina za Silika / Relationship between Performance and Characteristics of Types of Temperament

**Mada kwa Wanafunzi Wanaosoma Fasihi ya Watoto na Ubunifu**

**Mada 1**. Sifa za Wahusika wa Fasihi ya Watoto

**Mada 2**. Utendaji wa Wahusika wa Fasihi ya Watoto

**Mada 3**:Uhusiano wa Utendaji na Sifa za Aina za Silika

**A.4 Mwongozo wa Usomaji Matini**

| **Jina la Kitabu** | **Safari ya Prospa** | | **Ngoma ya Mianzi** | |
|---|---|---|---|---|
| **Jina la Mhusika** | Prospa | Sara | Chulu | Mbumi |
| **Aina ya silika yake** | Melankoli | Sangwini | Melankoli | Koleriki |
| **Sifa za Aina ya Silika** | Uwezo mkubwa kiakili<br>Ana hisia za ndani<br>Upendo wa dhati<br>Hapendi kuona wengine wakionewa<br>Hana majungu<br>Ana ushawishi mkubwa katika mambo ya kiimani<br>Mwepesi kuomba msamaha<br>Hajiamini<br>Mwoga kuanzisha jambo | Mcheshi<br>Hujitokeza kila mahali<br>Anapenda utani<br>Mshauri<br>Anapenda starehe<br>Anapenda kujichanganya<br>Ni mtu wa watu<br>Husaka marafiki na huwatunza<br>Ana maamuzi ya haraka | Uwezo mkubwa kiakili<br>Ana hisia za ndani<br>Upendo wa dhati<br>Hapendi kuona wengine wakionewa<br>Hana majungu<br>Ana ushawishi mkubwa katika mambo ya kiimani<br>Mwepesi kuomba msamaha<br>Hajiamini<br>Mwoga kuanzisha jambo | Jasiri<br>Ushawishi<br>Hapendi kudharauliwa<br>Uthubutu<br>Anajitegemea<br>Ana maono<br>Afanyapo jambo huwaza mafanikio<br>Hutumia pesa kwa kuwekeza<br>Mtu wa vitendo kuliko maneno |
| **Utendaji wake** | Kuhoji<br>Kushawishi<br>Kudadisi<br>Kuonya<br>Kudanganya | | Kuhoji<br>Kutaarifu<br>Kushauri<br>Kudadisi | |
| **Uhusiano wa Utendaji na Sifa za Aina za Silika** | | | | |

**B. Taarifa za Watafitiwa**

| Na | Jina | Jinsi | Tahsusi | Tarehe ya Usaili/Majadiliano | Mahali |
|---|---|---|---|---|---|
| 01 | Profesa Mulinzi Mulokozi | Me | Mwandishi | 10/02/2020 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| 02 | Bw. Herman Bakize | Me | Mtaalamu wa Fasihi ya Watoto | 12/02/2020 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| 03 | Bi. Elieshi Lema | Ke | Mwandishi | 17/02/2020 | E&D Publishing House |
| 04 | Bi. Getrude Shima | Ke | Mtaalamu wa Fasihi ya Watoto | 15/06/2020 | Chuo Kikuu cha Dodoma |
| 05 | Kikundi cha Majadiliano<br><br>CKDOISJ 1<br>CKDOISJ 2<br>CKDOISJ 3<br>CKDOISJ 4<br>CKDOISJ 5<br>CKDOISJ 6<br>CKDOISJ 7<br>CKDOISJ 8<br>CKDOISJ 9<br>CKDOISJ 10 | Me<br>Me<br>Me<br>Ke<br>Ke<br>Ke<br>Me<br>Ke<br>Ke<br>Ke | Wanafunzi wa Shahada ya Awali katika Fasihi ya Kiswahili (BAKILIT) | 14/06/2020 | Chuo Kikuu cha Dodoma |
| 06 | Kikundi cha Majadiliano<br><br>CKDOE1<br>CKDOE2<br>CKDOE3<br>CKDOE4<br>CKDOE5<br>CKDOE6<br>CKDOE7<br>CKDOE8<br>CKDOE9<br>CKDOE10 | Ke<br>Ke<br>Me<br>Me<br>Me<br>Me<br>Ke<br>Ke<br>Ke<br>Me | Wanafunzi wa Shahada ya Awali ya Ualimu wa Elimu ya Awali (BED ECE) | 16/06/2020 | Chuo Kikuu cha Dodoma |
| 07 | Dkt. Edith Lyimo | Ke | Mtaalamu wa Fasihi ya Watoto | 17/06/2020 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| 08 | Bw. Golden Hinju | Me | Msimamizi wa Mradi wa Vitabu vya Watoto | 17/07/2020 | Shule ya Msingi Mbezi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 09 | Kikundi cha Majadiliano<br><br>CKDA1<br>CKDA2<br>CKDA3<br>CKDA4<br>CKDA5<br>CKDA6<br>CKDA7<br>CKDA8<br>CKDA9<br>CKDA10 | Ke<br>Me<br>Me<br>Ke<br>Me<br>Me<br>Ke<br>Ke<br>Ke<br>Ke | Wanafunzi wa Shahada ya Awali katika Kiswahili (BA Kiswahili) | 20/07/2020 | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |

**Ufunguo**:

CKDOISJ – Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki ya Insia na Sayansi za Jamii

CKDOE - Chuo Kikuu cha Dodoma, Ndaki  ya Elimu

CKDA - Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili

Bw – Bwana

Bi. – Bibi

Dkt. Daktari wa Falsafa

Me – Mwanaume

Ke - Mwanamke

## C. Vibali vya Utafiti

# CHUO KIKUU CHA DODOMA
## OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO

P.O. BOX 259
DODOMA, TANZANIA TEL: +255 (0)26 2323001 NUKUSHI: +255 (0)26 2323001

**Kumb. Na. UDOM/RP/68Vol. II/5** **Tarehe: 20 Januari, 2020**

Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
**Dar es Salaam.**

Rasi wa Ndaki,
Humanitia,
**Chuo Kikuu cha Dodoma.**

**YAH: IDHINI YA KUFANYA UTAFITI**

Dhumuni la barua hii ni kumtambulisha ndugu **Mkomwa, Saumu** ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma mwenye nambari ya usajili HD/UDOM/0488/PhD/T.2018. Mwanafunzi wetu amefikia hatua ya kufanya utafiti kama sehemu ya mafunzo katika kozi (programu) husika.

Kwa mujibu wa waraka wa Serikali wenye Kumb: Na. MPEC/R/10/1 wa tarehe 4 Julai, 1980, Makamu Mkuu wa Chuo amepewa mamlaka ya kutoa idhini ya kufanya utafiti kwa watumishi na wanafunzi wa Chuo Kikuu kwa niaba ya serikali na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Hivyo ninapenda kukuarifu kuwa nimetoa idhini ya utafiti kwa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

Aidha ninakuomba umpatie msaada wowote utakaohitaji kufikia malengo ya utafiti wake. Zaidi tunakuomba umruhusu mwanafunzi wetu kuonana na kuzungumza na viongozi na wadau wote muhimu kwa utafiti wake katika taasisi yako.

Mada ya utafiti wake ni **"Uhusiano wa Silika na Utendaji wa Wahusika wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili:** ***Uchunguzi Kifani Ngoma ya Mianzi na Safari ya Prospa."***

Kipindi cha utafiti wake ni kuanzia Februari, hadi May, 2020 na utafanyika maeneo ya Dare s Salaam- atazungumza na Wahadhili na Wataaluma wa Fasihi na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu Dar es Salaam; Dodoma- ataongea na Wahadhiri na Wataalam wa Fasihi ya Kiswahili – Chuo Kikuu cha Dodoma; kuhusiana na utafiti huo.

Kama kuna pingamizi lolote unaombwa kutushauri ipasavyo. Kwa taarifa zaidi usisite kuwasiliana nasi kupitia kurugenzi ya Utafiti, Machapisho, Ushauri na Ushirikiano wa Kitaasisi S. L. P. 251, Dodoma. Namba ya simu + (255) 262310301, Barua pepe:research@udom.ac.tz.

Wako katika ujenzi wa Taifa,

Prof. Faustine K. Bee
**MAKAMU MKUU WA CHUO**

VICE CHANCELLOR
THE UNIVERSITY OF DODOMA
P. O. BOX 259
DODOMA, TANZANIA

30/6/20
Rev
[illegible]


# CHUO KIKUU CHA DODOMA

## OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO

P.O. BOX 259
DODOMA, TANZANIA TEL: +255 (0)26 2323001 NUKUSHI: +255 (0)26 2323001


**Kumb. Na. UDOM/RP/68Vol. II/5** **Tarehe: 04 Juni, 2020**

Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
**Dar es Salaam.**

Rasi wa Ndaki,
**Chuo Kikuu cha Dodoma**

Mkurugenzi
Halmashauri ya Jiji la Dodoma
**Dodoma**

Mkurugenzi
Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo
**Dar es Salaam.**

**YAH: IDHINI YA KUFANYA UTAFITI**

Dhumuni la barua hii ni kumtambulisha ndugu **Mkomwa, Saumu** ambaye ni mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma mwenye nambari ya usajili **HD/UDOM/0488/PhD/T.2018**. Mwanafunzi wetu amefikia hatua ya kufanya utafiti kama sehemu ya mafunzo katika kozi (programu) husika.

Kwa mujibu wa waraka wa Serikali wenye Kumb: Na. MPEC/R/10/1 wa tarehe 4 Julai, 1980, Makamu Mkuu wa Chuo amepewa mamlaka ya kutoa idhini ya kufanya utafiti kwa watumishi na wanafunzi wa Chuo Kikuu kwa niaba ya serikali na Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Hivyo ninapenda kukuarifu kuwa nimetoa idhini ya utafiti kwa mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

Aidha ninakuomba umpatie msaada wowote utakaohitaji kufikia malengo ya utafiti wake. Zaidi tunakuomba umruhusu mwanafunzi wetu kuonana na kuzungumza na viongozi na wadau wote muhimu kwa utafiti wake katika taasisi yako.58

Mada ya utafiti wake ni **"Uhusiano wa Silika na Utendaji wa Wahusika wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili: *Uchunguzi Kifani Ngoma ya Mianzi na Safari ya Prospa.*"**

Kipindi cha utafiti wake ni kuanzia Juni, hadi Agosti, 2020 na utafanyika maeneo ya Dar es Salaam- atazungumza na Wahadhili na Wanafunzi wa Fasihi na Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo

Kikuu Dar es Salaam; Dodoma- ataongea na Wahadhiri na wanafunzi wa Fasihi ya Kiswahili kuhusiana na utafiti huo.

Kama kuna pingamizi lolote unaombwa kutushauri ipasavyo. Kwa taarifa zaidi usisite kuwasiliana nasi kupitia kurugenzi ya Utafiti, Machapisho, Ushauri na Ushirikiano wa Kitaasisi S. L. P. 251, Dodoma. Namba ya simu + (255) 262310301, Barua pepe:research@udom.ac.tz.

Wako katika ujenzi wa Taifa,

Prof. Faustine K. Bee
**MAKAMU MKUU WA CHUO**

VICE CHANCELLOR
THE UNIVERSITY OF DODOMA
P. O. BOX 259
DODOMA, TANZANIA

# UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM

*DIRECTORATE OF RESEARCH AND PUBLICATION*

*P.O. Box 35091 ▪ DAR ES SALAAM ▪ TANZANIA*

**General Line:** 2410500-8 Ext. 2084
**Direct Line:** 2410727
**Website**: *www.udsm.ac.tz*

**Fax:** 255 022 2410743
*255 022 2410023*
*E-mail: research@udsm.ac.tz*


Our Ref. AB3/31

5th February 2020

Director
Institute of Kiswahili
**University of Dar es Salaam**

**RE: RESEARCH CLEARANCE**

This is to introduce **Ms. Saumu Mkomwa** PhD student from University of Dodoma. Ms. Saumu is at the moment conducting data collection as part of her Studies. The title of her research is **'Uhusiano wa Siliki na Utendaji wa Wahusika wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili: Uchunguzi Kifani Ngoma ya Mianzi na Safari ya Prospa'**

This is to request you to grant the above-mentioned student any help that may enable her to achieve her study objectives. The period for which this permission has been granted is from **February to May 2020.**

Dr. Mussa I. Mgwatu
**DIRECTOR OF RESEARCH AND PUBLICATION**

cc: Vice Chancellor
cc: Deputy Vice Chancellor - Academic
cc: Deputy Vice Chancellor - Administration
cc: Deputy Vice Chancellor - Research

# CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM
## TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI
OFISI YA MKURUGENZI
S. L. P.35110 DAR ES SALAAM TANZANIA

SimuyaJumla: 255 22 2410500-8
Tawi: 2647
SimuyaTaasisi: 255 22 2410757

Barua pepe: iks@udsm.ac.tz
Tovuti: www.udsm.ac.tz


*Kumb:TATAKI/V/5/*

*Tarehe: 10/02/2020*

Ms Saumu Mkomwa
Chuo Kikuu cha Dodoma
DODOMA

YAH. KIBALI CHA KUFANYA UTAFITI KATIKA TAASISI YA TAALUMA ZA KISWAHILI

Ninafurahi kukufahamisha kuwa kibali kimetolewa ili ufanye utafiti wako wa shahada ya uzamivu katika Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mada yako ya Utafiti ikiwa:

**" Uhusiano wa Silika na Utendaji wa Wahusika wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili:Uchunguzi Kifani Ngoma ya Mianzi na Safari ya Prospa"**

Aidha unaarifiwa kuwa kibali hiki kimetolewa kwa kipindi kuanzia **Februari hadi Mei 2020** .Ni matumaini yangu kuwa utazinngatia maadili ya utafiti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ninakutakia masomo mema.

Cornel R. Zawadi

AFISA UTAWALA TATAKI

Nakala:Mkurugenzi TATAKI

Mkurugenzi Mshiriki TATAKI

Mudir , IFAMU

Mudir ,ILUKI


Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni taasisi inayojali fursa sawa inayoendeshwa bila ubaguzi katika udahili wa wanafunzi na ajira ya wafanyakazi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

***(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)***

**MKOA WA DODOMA**
Tel.: 2354817
Fax: 2354817/ 2321550

MKURUGENZI WA JIJI
S.L.P. 1249
**DODOMA**
Baruapepe: md@dodomamc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja

Kumb No. HJD/ED. 0033/167

Tarehe: **24/06/2020**

Mkomwa Saumu
Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)
**Dodoma**

## YAH: IDHINI YA KUFANYA UTAFITI

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu na pia rejea barua yako yenye kumbukumbu namba UDOM/RP/68VOL II/5 ya tarehe 04/06/2020 yenye kichwa hapo juu.

Kwa barua hii unatakiwa kufika ofisi ya Afisa Elimu Sekondari Jiji ili kuonana na uongozi.

*Asante*

***Mwl. Upendo B. Rweyemamu***
**Kny: MKURUGENZI WA JIJI**
**DODOMA**

Nakala    Mkurugenzi wa Jiji
S.L.P 1249
**Dodoma** - Aione kwenye Jalada